JAMHURI YA KENYA

Mali ya
Serikali ya Kenya
**HAKIUZWI**

# Kiswahili 1

## Mazoezi ya Lugha

### Mwongozo wa Mwalimu



KIMEIDHINISHWA
KICD
KIMEAINISHWA KWA MTAALA ULIOJIKITA KWENYE UFARISI

**Tusome Early Literacy Programme**

# Kiswahili 1

Mazoezi ya Lugha

Mwongozo wa Mwalimu

## Yaliyomo


Utangulizi ........ ii
Dibaji ........ ii
Mwongozo kwa mwalimu ........ iii
Utangulizi ........ v
Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo ........ vi
Mwongozo wa Mwalimu wa Kiswahili kwa Gredi ya 1 ........ vii
Tathmini ........ vii
Kamusi ya Kiswahili ........ viii
Michoro ya Kuashiria ........ xii
Karibu darasani 1 ........ 1
(Kipindi cha 1 hadi 5)
Mimi na wenzangu 1 ........ 8
(Kipindi cha 6 hadi 10)
Tarakimu 1 ........ 15
(Kipindi cha 11 hadi 15)
Siku za wiki 1 ........ 22
(Kipindi cha 16 hadi 20)
Familia 1 ........ 29
(Kipindi cha 21 hadi 25)
Familia 1 ........ 37
(Kipindi cha 26 hadi 30)
Mwili wangu 1 ........ 46
(Kipindi cha 31 hadi 35)
Mwili wangu 1 ........ 51
(Kipindi cha 36 hadi 40)
Usafi wa mwili 1 ........ 58
(Kipindi cha 41 hadi 45)
Usafi wa mwili 1 ........ 63
(Kipindi cha 46 hadi 50)
Marejeleo 1 ........ 68
(Kipindi cha 51 hadi 55)
Vyakula vya kiasili 1 ........ 73
(Kipindi cha 56 hadi 60)
Vyakula vya kiasili 1 ........ 78
(Kipindi cha 61 hadi 65)
Mimi na wenzangu 2 ........ 84
(Kipindi cha 66 hadi 70)
Mimi na wenzangu 2 ........ 89
(Kipindi cha 71 hadi 75)
Siku za wiki 2 ........ 94
(Kipindi cha 76 hadi 80)
Tarakimu 2 ........ 99
(Kipindi cha 81 hadi 85)
Familia 2 ........ 104
(Kipindi cha 86 hadi 90)
Familia 2 ........ 109
(Kipindi cha 91 hadi 95)
Usafi wa mwili 2 ........ 114
(Kipindi cha 96 hadi 100)
Marejeleo 2 ........ 119
(Kipindi cha 101 hadi 105)
Mwili wangu 2 ........ 124
(Kipindi cha 106 hadi 110)
Mwili wangu 2 ........ 129
(Kipindi cha 111 hadi 115)
Usafi wa mwili 3 ........ 134
(Kipindi cha 116 hadi 120)
Usafi wa mwili 3 ........ 139
(Kipindi cha 121 hadi 125)
Vyakula vya kiasili 2 ........ 144
(Kipindi cha 126 hadi 130)
Vyakula vya kiasili 2 ........ 149
(Kipindi cha 131 hadi 135)
Mimi na wenzangu 3 ........ 154
(Kipindi cha 136 hadi 140)
Tarakimu 3 ........ 159
(Kipindi cha 141 hadi 145)
Marejeleo 3 ........ 164
(Kipindi cha 146 hadi 150)



© 2021 ya RTI International kwa nchi zote isipokuwa Jamhuri ya Kenya.

RTI International ni alama na jina la kibiashara la Research Triangle institute.

Haki ya Kunakili ya Jamhuri ya Kenya inashikiliwa na wizara ya elimu Kenya.



Chapisho hili limefanikishwa kupitia kwa ufadhili kutoka kwa shirika la kimataifa na maendeleo la America (USAID) kupitia mradi wa USAID -Tusome.



Kazi hii inapatikana chini ya leseni ya Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 International (CC BY-NC-ND 4.0). Ili kuona nakala ya leseni hii, tembelea https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/ ama tuma barua kwa Creative Commons, sanduku la posta 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

**Kunukuu na kutambua kazi asili** — Ukinakili na kusambaza kazi hii tafadhali nukuu kama ifuatavyo: *Imenakiliwa kutokana na kazi asili ya RTI International na kuruhusiwa chini ya leseni ya Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 International (CC BY-NC-ND 4.0).*

**Si ya Biashara** — Usitumie kazi hii kwa nia ya biashara.

**Si ya Kuigaiga na Kusambazwa** — Usisambaze kazi hii kama utaifanyia mabadiliko kazi asili pamoja na kuichanganya na kazi nyingine, kuitumia kama msingi wa kazi nyingine au kuibadilisha kwa njia yoyote ile.

**Kazi ya Mtu wa Tatu** — Sio lazima RTI International kumiliki kila kipengele cha maudhui yaliyomo katika kazi hii. Hivyo basi, RTI international haikuhakikishii ya matumizi ya kipengele chochote cha kazi ya mtu mwingine au baadhi ya kazi yake haitakiuka haki za watu hao. Utawajibika kutokana na hatari ya kudaiwa kutokana na kuingilia haki za wengine. Ukitaka kutumia tena kipengele cha kazi hii, ni jukumu lako kuamua kama imeruhusiwa kutumia tena na kupata ruhusa kutoka kwa mwenye hati ya kunakili. Baadhi ya mifano ya vipengele hivi ni majedwali, maumbo na picha.



Kimechapishwa nchini Kenya kwa ufadhili kutoka kwa USAID (U.S. Agency for International Development) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

ISBN: 978 9966 110 09 1

Toleo la Kwanza

Kimechapishwa 2018

## Utangulizi

Serikali ya Kenya imejitolea kutoa elimu bora kama haki ya kimsingi kwa wanafunzi wote. Azma hii inaambatana na majukumu ya kitaifa na kimataifa yanayohitaji kila nchi kukimu mahitaji ya kielimu na kijamii ya raia wake. Ingawa juhudi zimefanywa kuhakikisha elimu inapatikana kwa urahisi, lengo kuu la serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu bora. Serikali ya Kenya imewekeza zaidi katika kuboresha vifaa vya kielimu, miundomsingi pamoja na wafanyakazi ili kuinua kiwango cha elimu inayotolewa katika viwango vyote vya elimu nchini. Mfumo wa elimu unaolengwa umebuniwa kutokana na matokeo ya utafiti wa kina. Kadhalika, umejumuisha mbinu zingine zinazokubalika na kutumiwa kimataifa. Msukumo uliopo katika mageuzi ya elimu unatokana na haja ya kuifanya elimu nchini Kenya kuwa kwenye kiwango cha kimataifa na kuwa ya manufaa kiuchumi katika jamii. Serikali inahakikisha kwamba kupitia elimu, wananchi watakuwa wabunifu na kupata stadi za karne ya 21 ikiwemo utafiti, kutatua matatizo, kufikiria kwa kina na kufanya kazi katika hali zote.

Vitabu vya TUSOME vimeshirikisha maadili ya mtaala mpya na vimeandikwa ili kuimarisha uwezo wa kujua kusoma na kuandika, uwezo ambao ni stadi ya kimsingi katika elimu bora. Kitabu hiki kitatumika katika Gredi ya 1 kujifunza na kufundishia Kiswahili katika mtaala mpya. Mpangilio wa kitabu hiki unatilia maanani maantiki na mikakati inayotokana na utafiti ili kukuza stadi za kusoma na kuandika. Vilevile, mpangilio huu utahakikisha kuwa wanafunzi wanapata umilisi ambao ni muhimu kwa viwango vyao.

Ninawasihi washikadau wote kuendelea kuunga mkono mageuzi yanayoshughulikiwa katika sekta ya elimu nchini Kenya ili kufikia matokeo bora.

[redacted]

Waziri wa Elimu

## Dibaji

Wizara ya Elimu imejitolea kuwapa Wakenya elimu bora kama ilivyo katika Katiba ya Kenya, ya mwaka wa 2010. Mabadiliko yanayoendelea katika elimu yanalenga kushughulikia uwepo wa elimu bora. Mipango ya utafiti kama vile Tathmini ya Kitaifa ya Ufuatiliaji wa Mafanikio ya Masomo (NASMLA) na Muungano wa Kusini na Mashariki ya Afrika wa Kufuatilia Ubora wa Elimu (SACMEQ) imeangazia mianya ambayo inafaa kushughulikiwa ili kuboresha matokeo ya elimu.

Matukio ya hivi punde katika mfumo wa elimu yanasisitiza uwezo wa kusoma na kufanya hesabu kama nguzo ya kujifunza katika darasa tangulizi. Umakinifu katika elimu umechangia hatua ambazo zimeimarisha matokeo ya kusoma na kufanya hesabu. Mradi wa kitaifa wa Tusome umeimarisha uwezo wa mwanafunzi wa kusoma na kuandika katika Gredi ya 1 na ya 2. Matokeo haya bora yamechangia kuendelezwa kwa mradi huu hadi gredi ya 3. Kitabu hiki kimeandikwa ili kuelekeza mafunzo ya Kiswahili; kiwango cha Gredi ya 1 katika mtaala mpya. Mbinu za ubunifu katika kujifunza na kufundisha pamoja na Masuala Mtambuko yameangaziwa kulingana na mtaala mpya.

Wizara ya Elimu inatambua usaidizi wa kifedha kutoka kwa shirika la usaidizi la Marekani (USAID). Kadhalika, ningependa kutoa shukrani zangu kwa washirika na washikadau wengine kwa mchango wao katika uandishi na uchapishaji wa kitabu hiki.

[redacted]

Katibu Mkuu, Elimu ya Msingi

Wizara ya Elimu.

# Mwongozo kwa mwalimu

Mwongozo huu wa mwalimu umejikita kwenye mfumo wa kufundisha wa moja kwa moja. Mbinu hii humsaidia mwalimu kufundisha wanafunzi akitumia ujuzi wa kimsingi ambao unahitajika katika kuboresha ufasaha wa kusoma, kufahamu na kuandika. Mbinu hii huzingatia hatua tatu rahisi: kuonyesha kwa mfano, maongozi kwenye mazoezi na mazoezi huru au tathmini. Kwa kutumia mbinu hii, mwalimu huweka mikakati iliyosawazishwa ya kufundishia na kuonyesha mkusanyiko wa shughuli ndani ya darasa. Mbinu hii huruhusu ubunifu wa mwalimu. Japo matayarisho ya mwalimu ni muhimu kufanikisha somo kwa kutumia mwongozo huu, mwalimu anahimizwa kubuni, kutayarisha na kutumia nyenzo za kufundishia katika kila muktadha ili kuboresha umilisi wa kimsingi unaofundishwa. Nyenzo hizi zinaweza kujumuisha vifaa halisi, vya kidijitali, picha, ramani, kamusi na kadhalika.

Matumizi ya ubao ni muhimu na yanatiliwa mkazo katika mwongozo huu. Hata hivyo, inampasa kila mwanafunzi kuwa na kitabu chake mwenyewe ili kuongeza uzoefu wake wa kusoma na kuandika. Zaidi ya hayo, kuna mazoezi kwenye kitabu cha mwanafunzi ambayo yanawahitaji wanafunzi kuyafanya pekee yao darasani. Kazi ya ziada pia imejumuishwa ili wanafunzi wafanye mazoezi wakiwa nyumbani. Lengo kuu haswa ni kuhakikisha kuwa mlezi au mzazi anashirikishwa katika jitihada za kumwezesha mwanafunzi kufaulu kimasomo. Walimu wanahimizwa kuangalia kazi ya wanafunzi ili kuhakikisha kuwa mazoezi yote yanafanywa na kutoa tathmini kwa wakati ufaao. Ni vyema kukumbuka pia kwamba walimu hawapaswi kuhisi kuwa wamezuiwa kuwapa wanafunzi kazi zingine zifaazo za ziada. Ikiwa wanahisi kuwa wanafunzi wanahitaji mazoezi zaidi, wanapaswa kutumia uamuzi wao kutoa mazoezi yanayofaa kama kazi ya ziada.

Walimu pia wanahimizwa kuchagua shughuli zitakazofanikisha uelewa wa wanafunzi wa dhana zinazofundishwa. Shughuli hizi zinajumuisha maonyesho, maigizo au maelezo kwa kutumia maneno mafupi, rahisi na yanayoeleweka.

Mwongozo huu wa mwalimu umeundwa kwa njia inayoondoa vizuizi vya ujifunzaji bora. Hivyo basi, mwongozo huu unakidhi mahitaji ya wanafunzi wote (hata wenye ulemavu) kwa kuzingatia viwango vyao vya kuelewa na changamoto zao. Wanafunzi kama hawa wanaweza kusaidiwa na walimu kwa njia kadha wa kadha. Zifuatazo ni baadhi ya njia ambazo mwalimu anaweza kutumia kuwasaidia wanafunzi wenye changamoto tofauti za kujifunza.

Namna ya kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

1. Mwalimu anapaswa kutafuta mbinu ya kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji maluum. Baadhi ya mahitaji haya ni kama vile:
   a) matatizo ya kusikia.
   b) matatizo ya kuona.
   c) udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo haraka.
   d) udhaifu wa kuwasiliana. Kwa mfano, mtoto aliye na kigugumizi na kadhalika.
   e) udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili.
   f) walio wepesi katika kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani.
2. Ni muhimu kwa mwalimu kutambua uwezo na udhaifu wa kila mwanafunzi kabla ya, wakati wa na baada ya somo. Kufanya hivi kutamwezesha kushughulikia mahitaji hayo kwa njia inayofaa ili yasiadhiri mafanikio ya somo. Mifano ya mahitaji maalumu na namna ya kuyashughulikia imetolewa katika Jedwali la 1.



Hakiuzwi

**Jedwali la 1: Mahitaji maalum ya wanafunzi na mapendekezo na namna ya kuyashughulikia**

| Mahitaji | Mapendekezo ya namna ya kuyashughulikia |
|---|---|
| a) Matatizo ya kutosikia | - Tumia lugha ya ishara inapowezekana.<br>- Mwanafunzi aketi karibu na mwalimu au mahali atakapoweza kusikia vizuri.<br>- Himiza matumizi ya vipaza sauti inapowezekana.<br>- Tumia vifaa halisi. |
| b) Matatizo ya kutoona vyema | - Mwanafunzi aketi karibu au mbali na ubao kulingana na mahitaji yake.<br>- Himiza matumizi ya breli (braille) inapofaa.<br>- Jadili na wazazi au walezi kuhusu matumizi ya miwani au vioo vya kukuza kimo cha maandishi.<br>- Epuka ama ondoa vifaa vinavyoathiri uwezo wa kuona.<br>- Mwanafunzi aketi karibu au mbali na mwangaza kulingana na mahitaji yake.<br>- Tumia vifaa halisi. |
| c) Udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo kwa haraka | - Wape wanafunzi hawa muda mwingi wa ziada kuliko wanafunzi wengine.<br>- Watengee wanafunzi hawa muda maalumu wa kurejelea waliyoyasoma baada ya somo.<br>- Gawa somo kwa hatua fupi fupi kuanzia nyepesi hadi hatua tatanishi.<br>- Wape mazoezi ya ziada.<br>- Mwalimu awakinge wanafunzi walio na udhaifu dhidi ya kudunishwa kwa njia yoyote ile. |
| d) Udhaifu wa kuwasiliana/ kigugumizi | - Wape wanafunzi muda wa kuwasilisha mawazo yao.<br>- Mwalimu aepukane na vitendo vinavyoweza kuathiri hisia au maono ya wanafunzi.<br>- Mwalimu atumie mbinu tofauti za mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi. |
| e) Udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili | - Mwanafunzi apewe muda wa ziada ili kukidhi upungufu (ulemavu) wake.<br>- Wapewe vifaa vya teknolojia ikiwezekana au vya kubuniwa kulingana na hali ya ulemavu ili kuongeza uwezo wa utenda kazi wao.<br>- Mwalimu anaweza kushauriana na wahudumu wa walemavu kwa usaidizi zaidi. |
| f) Walio wepesi katika kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani | - Wanafunzi wapewe kazi ya ziada ili watumie muda wao vyema.<br>- Wanafunzi wapewe nafasi za kukuza vipawa vyao.<br>- Wanafunzi wapewe kazi zenye changamoto zaidi ili kufanyisha akili zao zoezi na kuwapa fursa ya kutumia wepesi wao wa kuelewa. |

# Utangulizi

Mwongozo huu umeandaliwa kwa maelekezo ya wataalamu wa kimataifa na wa hapa nchini wa kusoma na wa lugha kwa kufuata mchakato uliopangwa kwa utaratibu. Kwenye warsha ya kwanza ya maafisa wa Wizara ya Elimu na ya Taasisi ya Mitaala ya Kenya, upeo na mpangilio ulibuniwa ambao umekuwa ramani ya kuendeleza mpangilio wa somo. Kwenye warsha hiyo, maamuzi yaliafikiwa kuhusu ujuzi wa kukuzwa miongoni mwa wanafunzi kwa kila muhula na shughuli maalum ambazo zingetumiwa kutimiza malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kuna jaribio la wazi la kuwa na mwendelezo wa herufi na sauti na msisitizo wa kusoma maneno magumu zaidi yenye uwiano tata kati ya herufi na sauti na kuwasilisha kwa mwanafunzi mikakati mingine ya kusoma maneno.

Matini kwenye masomo yanawiana kimandhari na silibasi ya Taasisi ya Mitaala ya Kenya na yameundwa kwa uangalifu ili mwanafunzi aelewe aina tofauti ya maandishi huku akitilia maanani misamiati ya kimandhari. Kila matini inajumuisha mifumo ya maneno na miundo husika ya lugha. Ili kuboresha ufahamu wa wanafunzi wa matini, baadhi ya mbinu za ufahamu zinazolingana na kiwango chake zimetumiwa ili kumpa mwanafunzi mbinu tofauti za kuelewa matini.

Kila mpango wa somo unajumuisha shughuli tofauti zilizopangwa ili kukuza ujuzi na ufahamu wa mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Shughuli za somo ni simulizi na za kuandika zikizingatia stadi nne za lugha (kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika). Katika masomo manne ya kwanza, wanafunzi hujifunza na kufanya mazoezi ya matumizi ya maneno, kusoma hadithi, ufahamu na sarufi. Somo la tano linazingatia marejeleo na shughuli za kutathmini zitakazosaidia mwalimu kufuatiliza maendeleo ya mwanafunzi. Mambo haya yametolewa, japo kwa muhtasari katika Jedwali la 2.



Hakiuzwi

# Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo

### (Gredi ya 1, Kipindi cha 1-22)

| Sehemu | Utangulizi 1 | Kipindi cha Mazoezi 1 | Utangulizi 2 | Kipindi cha Mazoezi 2 | Kipindi cha marejeleo (Tathmini) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli ya mwalimu na mwanafunzi** | | | | | |
| Kutazama na kujadili picha | 5 | 5 | 5 | 5 | 5 |
| **Shughuli ya mwanafunzi** | | | | | |
| kama vile: kuigiza maamkuzi; kutoa na kufuata maagizo; kutoa maelezo; kuimba nyimbo; eleza matukio; kuhesabu; kutoleana muhtasari; kusimuliana; kuambatanisha; kujaza mapengo; kuchora; kupanga; kunakili; kutunga sentensi | 25 | | 25 | | 25 |
| **Hadithi ya mwalimu** | | | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi | | 5 | | 5 | |
| Wakati wa kusoma hadithi | | 13 | | 13 | |
| Baada ya kusoma hadithi | | 7 | | 7 | |
| | **30** | **30** | **30** | **30** | **30** |

### (Gredi ya 1, Kipindi cha 23-150)

| Sehemu | Utangulizi 1 | Kipindi cha Mazoezi 1 | Utangulizi 2 | Kipindi cha Mazoezi 2 | Kipindi cha marejeleo (Tathmini) |
|---|---|---|---|---|---|
| Ufahamu wa fonimu | 3 | | 3 | | |
| Ufahamu wa herufi | 3 | 2 | 3 | 2 | **5** |
| Kusoma silabi | 3 | 2 | 3 | 2 | |
| Kusoma maneno kwa silabi | 3 | 2 | 3 | 2 | |
| Kusoma maneno marefu | | 3 | | 3 | |
| Jedwali la silabi | | | | | 10 |
| Sarufi | | 3 | | 3 | 10 |
| **Hadithi ya mwanafunzi** | | | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi | 4 | | 4 | | |
| Wakati wa kusoma hadithi | 5 | 3 | 5 | 3 | |
| Baada ya kusoma hadithi | 4 | | 4 | | |
| **Hadithi ya mwalimu** | | | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi | | 5 | | 5 | |
| Wakati wa kusoma hadithi | | 5 | | 5 | |
| Baada ya kusoma hadithi | | 5 | | 5 | |
| Kuandika/zoezi | 5 | | 5 | | 5 |
| | **30** | **30** | **30** | **30** | **30** |

| Utangulizi 1 | Kipindi cha mazoezi 1 | Utangulizi 2 | Kipindi cha mazoezi 2 | Kipindi cha marejeleo (Tathmini) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 1o |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | 32 | 33 | 34 | 35 |
| 36 | 37 | 38 | 39 | 40 |
| 41 | 42 | 43 | 44 | 45 |
| 46 | 47 | 48 | 49 | 50 |
| 51 | 52 | 53 | 54 | 55 |
| 56 | 57 | 58 | 59 | 60 |
| 61 | 62 | 63 | 64 | 65 |
| 66 | 67 | 68 | 69 | 70 |
| 71 | 72 | 73 | 74 | 75 |
| 76 | 77 | 78 | 79 | 80 |
| 81 | 82 | 83 | 84 | 85 |
| 86 | 87 | 88 | 89 | 90 |
| 91 | 92 | 93 | 94 | 95 |
| 96 | 97 | 98 | 99 | 100 |
| 101 | 102 | 103 | 104 | 105 |
| 106 | 107 | 108 | 109 | 110 |
| 111 | 112 | 113 | 114 | 115 |
| 116 | 117 | 118 | 119 | 120 |
| 121 | 122 | 123 | 124 | 125 |
| 126 | 127 | 128 | 129 | 130 |
| 131 | 132 | 133 | 134 | 135 |
| 136 | 137 | 138 | 139 | 140 |
| 141 | 142 | 143 | 144 | 145 |
| 146 | 147 | 148 | 149 | 150 |

## Tathmini

Mfumo mpya wa elimu unadhamiria kuhakikisha kuwa matokeo ya mafunzo ni ujenzi wa umilisi utakaomwezesha mwanafunzi kutumia ujuzi wake kujiendeleza. Kutokana na hayo, mwongozo huu umezingatia tathmini katika kila kipindi na mwishoni mwa kila wiki.



Hakiuzwi

| Mada | Mada ndogo | Mapendekezo ya tathmini |
|---|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | Kusikiliza kwa makini | - Tathmini matumizi ya mwanafunzi ya ishara.<br>- Uliza maswali |
| | Matamshi | - Tathmini anavyotamka maneno.<br>- Tathmini matumizi ya maneno katika mazungumzo. |
| | Msamiati | - Tathmini anavyotamka msamiati lengwa na anavyotumia msamiati huo kujieleza au kutunga sentensi na katika maandishi. |
| | Muundo wa lugha na matumizi yake | - Tathmini anavyotunga sentensi katika miktadha tofauti tofauti na ikiwa anazingatia muundo mwafaka wa lugha katika mazungumzo na katika maandishi.<br>- Unaweza kutumia maswali kupima uelewa wao wa muundo lengwa wa lugha. |
| Kusoma | Ufahamu wa jina na sauti ya herufi | - Tathmini ufahamu wake wa jina na sauti ya herufi lengwa na anavyotumia ujuzi huo kusoma maneno mapya. |
| | Kusoma maneno | - Tathmini ufasaha wake wa kusoma maneno, kucheza michezo ya maneno na mbinu anazotumia kusoma maneno mapya. |
| | Kusoma matini kwa ufasaha | - Tathmini ufasaha wao wanaposomeana wakiwa wawili wawili, katika darasa zima au akiwa peke yake.<br>- Tathmini iwapo anazingatia shadda na kiimbo wakati wa usomaji. |
| | Ufahamu | - Muulize atabiri kitakachotendeka katika hadithi kabla na wakati wa kusoma.<br>- Tathmini pia anavyosimulia hadithi aliyoisoma, anavyojibu maswali ya ufahamu au kujadili wahusika na muktadha wa matini lengwa. |
| Kuandika | Hati | - Tathmini nakala zake za maneno na sentensi au michoro hasa wakati wa imla na kuandika.<br>- Zingatia maumbo na mpangilio mwafaka wa maneno. Tumia kazi zake kujadili kuhusu hati nadhifu. |
| | Tahajia | - Tathmini ikiwa amezingatia tahajia katika maandishi yake. Unaweza kutumia kadi za herufi na kamusi katika tathmini hiyo. |
| | Uakifishaji | - Tathmini usahihi wa uakifishaji wake (herufi kubwa/ndogo, koma, kituo na kiulizi) katika maandishi na ikiwa anaweza kutambua alama lengwa za uafikishaji. |
| | Mwongozo wa uandishi. | - Tathmini mazoezi yake yanayozingatia kujaza nafasi katika sentensi, kuandika sentensi kutokana na picha au hadithi. Zingatia usahihi wa sentensi zake katika maandishi. |

## Kamusi ya Kiswahili

| Msamiati | Maana |
|---|---|
| **Adhuhuri** | muda kati ya saa sita na saa tisa mchana. |
| **Akaamua** | akakata kauli. |
| **Akamuuma** | akashika na kukata kwa meno. |
| **Akihesabu** | akitaja tarakimu moja hadi nyingine. |
| **Akijikaza** | akitia bidii. |
| **Alhamisi** | siku ya tano ya wiki kuanzia Jumapili. |
| **Alifaulu** | alipata aliyokusudia. |
| **Aligaagaa** | alijipindua pindua sakafuni au mahali alipolala. |
| **Alimkumbatia** | alimsogeza kifuani na kumzungushia mikono. |
| **Alioga** | alisafisha mwili kwa kutumia maji ili kuondoa uchafu. |
| **Alitaga** | alitoa mayai. |
| **Aliteguka** | fanya maungo ya mifupa ya mwili yafyatuke. |
| **Alizuru** | alitembelea. |
| **Ameangua** | ametoa vifaranga kutoka kwenye mayai. |
| **Ametoweka** | alikosa kuonekana. |
| **Anaoga** | anasafisha mwili kwa kutumia maji. |

| | |
|---|---|
| **Asali** | uki/kitu kitamu na cha rangi ya hudhurungi ambacho hutengenezwa na nyuki. |
| **Asante** | shukurani, tamko la kushukuru. |
| **Bega** | sehemu ya mwili iliyoko kati ya mkono na shingo. |
| **Bendera** | kitambaa chenye rangi au alama inayowakilisha nchi, shirika au chama fulani. |
| **Bidhaa** | vitu vinavyouzwa na kununuliwa katika biashara. |
| **Binamu** | mtoto wa mjomba au shangazi. |
| **Bisi** | punje za mahindi au mtama zilizokaangwa. |
| **Bokoboko** | chakula ambacho ni mchanganyiko wa ngano na nyama uliosongwa kwa mafuta (samli). |
| **Bonde** | sehemu ya nchi iliyo katikati ya milima. |
| **Dada** | ndugu wa kike wa kuzaliwa nawe. |
| **Dawati** | kiti kilichounganishwa na meza kinachokaliwa na mwanafunzi darasani; deski. |
| **Dhahabu** | madini ya rangi ya manjano yenye thamini kubwa sana. Hutumiwa kutengeneza mapambo. |
| **Dharau** | tabia ya mtu ya kupuuza mambo na kutofuata kanuni au taratibu zilizowekwa. |
| **Eropleni** | ndege/chombo cha usafiri cha hewani/angani. |
| **Fedha** | madini ya rangi ya bati au pesa. |
| **Fisi** | mnyama wa porini mkubwa kama beberu, ana rangi ya kijivu ni mwoga anayependa kula mizoga. |
| **Foronya** | mfuko wa kitambaa wa kuhifadhi mto wa kulalia. |
| **Futa kamasi** | kutoa uchafu puani kwa kutumia kitambaa. |
| **Goti** | sehemu ya mwili inayounganisha paja na muundi. |
| **Gredi** | kiwango au daraja ya kitu k.v gredi ya kwanza. |
| **Gumba** | kidole kikubwa cha mwisho cha mguu au cha mkono. |
| **Hamjambo** | neno la salamu linalotumiwa kuulizia hali ya mtu mwingine. |
| **Hamu** | hali ya kutaka kupata kitu fulani; kutaka sana. |
| **Hekaya** | hadithi. |
| **Hekima** | maarifa yaliyopatikana kutokana na uzoefu wa muda mrefu. |
| **Hoteli** | jengo maalumu mnamouzwa vyakula na vinywaji. |
| **Humeremeta** | hung'ara. |
| **Hutuokea** | hutupikia kwa kuweka chakula katika jiko au tanuri. Ni njia moja ya kupika mkate. |
| **Huzikata kucha** | hutumia kitu kilicho na makali kupunguza au kukata kucha. |
| **Ijumaa** | siku ya tano katika wiki. |
| **Ijumaa** | siku ya sita ya juma kuanzia Jumapili. |
| **Jikoni** | mahali pa kupikia. |
| **Jivu** | mabaki ya kitu kilichochomwa. |
| **Jumamosi** | siku ya saba ya wiki kuanzia Jumapili. |
| **Jumanne** | siku ya tatu ya wiki kuanzia Jumapili. |
| **Jumapili** | siku ya kwanza ya wiki. |
| **Jumatano** | siku ya nne ya wiki kuanzia Jumapili. |
| **Jumatatu** | siku ya pili ya juma kuanzia Jumapili. |
| **Kaa** | mnyama mdogo wa majini mwenye miguu sita au zaidi na gamba mwilini. |
| **Kahawa** | kinywaji kinachotengenezwa kwa unga wa buni na maji. |
| **Kaimati** | aina ya chakula kinachopikwa kwa sukari na unga wa ngano mfano wa andazi. |
| **Kalamu** | kifaa cha kuandikia juu ya karatasi chenye wino. |
| **Kalenda** | orodha ya siku, majuma na miezi ya mwaka. |
| **Kichwa** | sehemu ya juu ya mwili wa mnyama au mtu iliyoshikiliwa na shingo. |
| **Kidole** | sehemu ya mwili iliyo katika ncha ya mikono au miguu. |
| **Kifahari** | ya kujivunia, kinachopatia mtu heshima au utukufu. |
| **Kifua** | sehemu ya mbele iliyo baina ya shingo na tumbo. |
| **Kifutio** | kitu kilichotengenezwa kwa mpira kinachotumika kufutia maandishi ya penseli au kalamu ya wino. |
| **Kiganja** | sehemu ya mwisho ya mkono yenye vidole. |
| **Kima** | mnyama mdogo jamii ya nyani, mkubwa kuliko tumbiri na mwenye rangi ya kijivujivu mwili mzima. |
| **Kinanda** | ala ya muziki yenye kutoa sauti kwa kupulizwa au kubonyezwa vitufe. |
| **Kitabu** | mkusanyiko wa kurasa za karatasi zilizochapwa au kuandikwa kwa mkono. |
| **Kitinda mimba** | mtoto wa mwisho kuzaliwa katika familia. |
| **Kofia** | vazi linalovaliwa kichwani. |
| **Kuchana nywele** | hali ya kutumia kichana ili kuzifanya nywele ziwe laini. |
| **Kudumisha** | kuhakikisha, kutimiza. |



Hakiuzwi

| | |
|---|---|
| **Kufuta kamasi** | kutoa kamasi. |
| **Kugawana** | kukata kitu na kupatiana katika mafungu mbalimbali. |
| **Kukanda** | kusugua sehemu fulani ili kupata nafuu. |
| **Kumi** | idadi iliyo sawa na vidole vya mikono miwili ya binadamu; namba 10. |
| **Kunawa mikono** | kuosha mikono. |
| **Kunde** | aina ya maharagwe madogo yenye rangi ya kahawia,matawi hutumika kama mboga. |
| **Kunyoa nywele** | kukata nywele. |
| **Kusemezana** | kuongea na mtu mwingine. |
| **Kusugua meno** | kuosha meno kutumia mswaki (na dawa). |
| **Kutabasamu** | kuonyesha uso wa furaha unaoambatana na haja ya kucheka bila kutoa sauti wala kufungua kinywa. |
| **Kuwasiliana** | kutoa na pokea habari toka kwa mtu au watu juu ya jambo fulani. |
| **Likizo** | kipindi ambacho mtu hupewa ruhusa ya kupumzika baada ya kazi ama masomo. |
| **Limau** | aina ya tunda ambalo hufanana na chungwa lakini lina ladha kali sana. |
| **Mabuyu** | matunda ya mbuyu. |
| **Macho** | sehemu ya mwili unayotumia kuonea. |
| **Madawati** | viti vilichounganishwa na meza vinavyokaliwa na wanafunzi. |
| **Magimbi** | viazi vyeupe kama muhogo vinavyotokana na mimea yenye majani mapana, hufanana na nduma. |
| **Magoti** | viungo vya miguu vilivyo na umbo la duara ndani kinachounganisha paja na miguu. |
| **Maharagwe** | mbegu za jamii ya kunde ambazo ni kubwa na hupikwa kama kitoweo. |
| **Mahindi** | mbegu za mimea ya mihindi. |
| **Mali** | jumla ya vitu vyenye thamani kubwa alivyonavyo mtu; kitu cha thamani kubwa. |
| **Mapaipai** | tunda kubwa linaloliwa lenye uwazi katikati na mbegu nyeusi. |
| **Mapera** | matunda madogo yenye ngozi laini na mbegu ngumu ndogondogo zilizozungukwa na nyamanyama. |
| **Marafiki** | watu wanaoaminiana na kushirikiana katika mambo mengi. |
| **Masikio** | viungo vya mwili wa kiumbe vinavyotumika kwa kupokelea mawimbi ya sauti na kuyapeleka akilini/hutumiwa kusikilia. |
| **Matunda** | matunda madogo yenye ngozi laini na mbegu ngumu ndogondogo; mazao ya mimea yenye mbegu |
| **Maua** | sehemu ya mmea inayochanua, inapendeza kwa rangi mbalimbali. |
| **Mbili** | nambari/tarakimu iliyo kati ya moja na tatu; idadi ya pili ya pamoja |
| **Mboga** | majani yanayoliwa na binadamu, baada ya kupikwa. |
| **Mchicha** | mmea mdogo wenye majani mapana ambao hutumiwa kama mboga. |
| **Mdomo** | sehemu ya nje ya mwili inayomwezesha kiumbe kupitisha kitu, hasa chakula. |
| **Meli** | chombo cha usafiri cha majini. |
| **Mgongo** | sehemu ya nyuma ya mwili wa binadamu au mnyama kutoka kiungo cha shingo na mabega hadi kiunoni. |
| **Mguu** | sehemu ya mwili wa binadamu, mnyama au mdudu inayomwezesha kusimama au kutembea. |
| **Muhogo** | mmea ambao mzizi wake huliwa. |
| **Miaka** | vipindi vinavyofikia miezi kumi na miwili. |
| **Midomo** | sehemu ya nje ya kinywa ambayo hufunguliwa ili kuingiza kitu kinywani. |
| **Mikono** | sehemu ya mwili inayotokeza kwenye bega inayotumiwa kushika vitu. |
| **Mjomba** | ndugu wa kiume wa mama; kaka wa mama. |
| **Mkia** | sehemu inayotokeza baada ya kifupa cha mwisho cha uti wa mgongo wa mnyama au samaki. |
| **Moja** | neno la kuwakilisha tarakimu ya kwanza katika hesabu. |
| **Msichana** | mtoto wa kike; binti au mwanamke kijana ambaye hajaolewa wala kuzaa. |
| **Mtama** | mmea wa nafaka wenye bua refu kama mahindi hutoa masuke nchani yenye punje ndogondogo. |
| **Mtanashati** | mtu anayevutia au nadhifu. |
| **Muundi** | mfupa wa mbele unaotoka kwenye mguu mpaka kwenye goti. |
| **Mvulana** | mtoto/kijana wa kiume. |
| **Mwanya** | nafasi nyembamba kati ya vitu viwili. |
| **Mwewe** | aina ya ndege ambaye hula nyama. Anapenda kula vifaranga wa kuku na ndege. |
| **Mwili** | umbo zima la mtu au mnyama kutoka kichwa mpaka miguu. |
| **Nadhifu** | inayopendeza, safi. |

| | |
|---|---|
| **Nane** | nambari iliyo kati ya saba na tisa. |
| **Nazi** | tunda la mnazi lenye maji na nyama nyeupe ndani. |
| **Ng'ambo** | nje ya mipaka ya nchi, hasa baada ya kuvuka bahari. |
| **Nimekusamehe** | nimekuwia radhi. |
| **Nitaitunza** | nitailinda, nitaichunga. |
| **Njugu** | mmea wa jamii ya nafaka uzaao punje za duara au mviringo zinazoliwa au kutumiwa kutengeneza mafuta. |
| **Nne** | nambari iliyo kati ya tatu na tano. |
| **Nyikani** | katika uwanda ulioota nyasi na miti iliyotawanyika hapa na pale. |
| **Nywele** | malaika yanayoota mwilini kwa mfano kichwani. |
| **Paka** | mnyama mdogo anayefugwa nyumbani na anayependa kula panya. |
| **Parachichi** | tunda la mviringo la rangi ya kahawia au kijani lenye nyama laini ya mafuta yenye rangi ya kijani. |
| **Pasaka** | sikukuu ya kusherehekea kufufuka kwa Yesu Kristo. |
| **Pole** | neno la kumliwaza mtu aliyepata shida fulani *k.m. Mama alimwambia kaka pole.* |
| **Pua** | sehemu ya mwili inayotuwezesha kuvuta pumzi na kunusia. |
| **Pure** | chakula mchanganyiko wa mahindi na maharagwe. |
| **Pweza** | mnyama wa baharini mwenye umbo la duara lililozungukwa na mikono au minyiri minane. |
| **Rafiki** | mtu unayempenda na kumwamini. |
| **Raia** | mtu mwenye haki kisheria kwa sababu ya kuzaliwa au kujiandikisha katika taifa fulani. |
| **Rinda** | nguo ya kike iliyokatwa kiunoni. |
| **Saba** | tarakimu iliyo kati ya sita na nane. |
| **Safi** | isiyokuwa chafu. |
| **Safisha nguo** | kutoa uchafu kutoka kwa nguo kwa kutumia maji na sabuni. |
| **Samaki** | kiumbe anayeishi majini mwenye mapezi na mkia ambavyo humwezesha kuogelea; hutumika kama chakula. |
| **Shahada** | cheti apewacho mtu baada ya kuhitimu masomo ya chuo cha elimu ya juu |
| **Shangazi** | dada wa baba. |
| **Shati** | nguo yenye ukosi na mikoni inayovaliwa sehemu ya juu ya mwili. |
| **Shingo** | sehemu ya mwili inayounganisha kichwa na sehemu nyingine za mwili. |
| **Shuleni** | mahali pa kusomesha wanafunzi. |
| **Sikio** | kiungo cha mwili kinachomsaidia mtu kusikia. |
| **Sita** | nambari iliyo kati ya tano na saba. |
| **Sungura** | mnyama mdogo mwenye masikio marefu na mkia mfupi. |
| **Tai** | ndege mkubwa mwenye kucha ndefu na kali, ambaye chakula chake kikuu ni mizoga. |
| **Takataka** | uchafu. |
| **Tano** | nambari iliyo kati ya nne na sita. |
| **Tarakimu** | alama ya hesabu iliyoandikwa kuonyesha idadi. |
| **Tatu** | nambari iliyo kati ya mbili na nne. |
| **Tikiti** | aina ya tunda lenye ngozi ya rangi ya kijani na rangi nyekundu ndani. Tunda hili pia huitwa tikiti maji. |
| **Tisa** | nambari iliyo kati ya nane na kumi. |
| **Tufaha** | tunda tamu lenye mbegu chache na nyama nyingi nyeupe. |
| **Tulizibe** | tulifunike. |
| **Tumbili** | mnyama wa jamii ya nyani,mwenye rangi ya kijivu. |
| **Tumbo** | sehemu ya mbele ya mwili iliyo kati ya kifua na kiuno. |
| **Uchafu** | hali ya kukosa kuwa safi. |
| **Uki** | asali. |
| **Ukingoni** | mwishoni. |
| **Uma** | kifaa mfano wa kijiko chenye meno meno kinachotumiwa kwa kulia chakula. |
| **Umaarufu** | hali ya kuwa na sifa nyingi. |
| **Umri** | muda wa uhai wa mtu au kitu kwa hesabu ya miaka yake. |
| **Usafi** | hali ya kukosa uchafu. |
| **Uso** | sehemu ya mbele ya kichwa kuanzia kwenye paji hadi kidevuni. |
| **Uyoga** | mmea wenye umbo la mwavuli unaoota mara nyingi katika sehemu zenye udongo wa mimea iliyooza. |
| **Vesti** | vazi linalovaliwa ndani ya shati au kanzu |
| **Viazi tamu/vitamu** | mimea inayotambaa ambayo mizizi yake hutengeneza viazi vyenye ladha tamu. |
| **Vidole** | viungo vya mwili vilivyo katika sehemu ya mikono na miguu. |



Hakiuzwi

| | |
|---|---|
| **Vifaranga** | watoto wa ndege kama kuku. |
| **Vijito** | mito midogomidogo. |
| **Vilima** | sehemu ndogondogo za ardhi zilizoinuka juu kidogo. |
| **Vimepigwa rangi** | vimepakwa rangi. |
| **Virutubisho** | viini kwenye vyakula vinavyofanya mwili wa binadamu kuwa na nguvu, joto na kuweza kukua. |
| **Waliabiri** | walisafiri kwa chombo cha usafiri. |
| **Walimkanya** | walimwonya. |
| **Walimteka nyara** | walimchukua kwa nguvu na kumfungia mahali. |
| **Wazazi** | watu waliokuzaa. |
| **Wenzangu** | watu walio marafiki zangu/rika langu. |
| **Wimbi** | mmea aina ya nyasi ndefu unaopandwa, na kuzaa mashuke yenye nafaka. |
| **Yaya** | mwanamke anayeajiriwa ili kufanya kazi ya kulea mtoto. |
| **Zabibu** | tunda la mzabibu. |
| **Zeze** | ala ya mziki inayopigwa kwa kutumia nyuzi. |
| **Ziara** | tendo la kwenda mahali fulani kwa sababu maalumu k.v. kutembelea au kufanya mazungumzo fulani. |
| **Zimenyolewa** | zimekatwa au zimefupishwa. |

## Michoro ya Kuashiria

| | |
|---|---|
| Ufahamu wa fonimu | |
| Ufahamu wa herufi | |
| Kusoma silabi | |
| Kusoma maneno kwa kutumia silabi | |
| Kusoma maneno marefu | |
| Sarufi | |
| Kabla ya kusoma | |
| Kusoma hadithi | |
| Maswali | ? |
| Kuandika | |
| Kazi ya ziada | |
| Zoezi | |
| Jedwali la silabi | |
| Msamiati | |
| Hadithi ya mwalimu | |
| Kutazama na kujadili picha | |
| Kuimba wimbo | |
| Kuandika maneno | |

Kipindi cha 1 **Karibu darasani**

Tazama picha. Eleza unachokiona.




Igiza maamkuzi.

1 Hakiuzwi

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Karibu darasani. Leo tutajifunza kuhusu maamkuzi. Hebu tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachofanyika katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ninamwona mwalimu. Je, mwalimu anafanya nini?

**Unafanya:** *Waelekeze kujadili picha kuhusu maamkuzi pamoja nawe. Waulize maswali haya: Hawa ni akina nani? Wako wapi? Wanafanya nini? Wanafanya vipi? Wanafanya hivyo wakati gani? Kwa nini?*

### Zoezi

**Kuigiza maamkuzi**

**Ninafanya:** Sasa nitaigiza maamkuzi pamoja na mmoja wenu. Nitazame. *Igiza maamkuzi katika picha pamoja na mwanafunzi mmoja. Hakikisha wanafunzi wanatazama unachofanya.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Fanya nilivyofanya. *Waelekeze kuunda vikundi vya wanafunzi wawili wawili na kuigiza maamkuzi kama ilivyo katika picha. Chagua baadhi yao waigizie darasani.*

**Ninafanya:** Sasa nitaigiza maamkuzi mengine. Nitazame. Wamaasai husalimiana hivi. *Igiza wanavyosalimiana Wamaasai. Ita mwanafunzi mmoja na kumwekelea mkono wako utosini mwake. Hakikisha wanafunzi wanatazama unachofanya.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu kuigiza maamkuzi ya Kimaasai. *Waelekeze kuunda vikundi vya wanafunzi wawili wawili na kuigiza maamkuzi peke yao. Hakikisha wanachangia kwa kuigiza maamkuzi mengine. Chagua baadhi yao waigizie mbele ya darasa zima.*

**Ninafanya:** Je, maamkuzi yana umuhimu gani? Maamkuzi hutusaidia kujuliana hali.

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Eleza umuhimu wa maamkuzi. *Waelekeze kujadili kuhusu umuhimu wa maamkuzi wakiwa katika makundi ya wawili wawili. Chagua baadhi yao kutoa hoja zao mbele ya darasa zima.*


### Kazi ya ziada

Wawaigizie walezi wao maamkuzi waliyofunzwa katika kipindi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 2 **Karibu darasani**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

Jibu maswali.

Igiza maamkuzi.

Mali ya Serikali ya Kenya 2

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Karibu tena darasani. Leo tutaendelea kujifunza kuhusu maamkuzi. Hebu kwanza tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachofanyika katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ni zamu yenu sasa. Mnaona nini katika picha? Hawa ni akina nani? Wako wapi? Wanafanya nini? Wanafanya vipi? Wanafanya hivyo wakati gani? Kwa nini?

**Unafanya:** *Wanafunzi wajibu maswali.*

### Hadithi ya mwalimu

**Salamu**

Jana nilifika shuleni Furaha. Ilikuwa mara yangu ya kwanza kuingia shuleni. Nilijawa na furaha. Sare yangu ilikuwa mpya. Soksi zilikuwa mpya. Nilivaa viatu vipya. Nilikutana na wanafunzi wengi: wasichana kwa wavulana. Sare zao zilikuwa mpya pia. Kila mtoto alitumia lugha ya mama. Sikuweza kuzungumza na watoto wengi. Tulipoingia darasani mwalimu alisema, "Hamjambo watoto?" Wengi wetu hatukujibu. Mwalimu alisema, "Nikisema hamjambo watoto, mnanijibu, hatujambo mwalimu. " Mwalimu aliendelea kutufunza salamu zaidi.

**Ninafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni **hamjambo?** Nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **hamjambo.** *Waongoze wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **hamjambo.** Mwambie mwenzako sentensi uliyoitunga. *Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.*

*Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* ***hatujambo, salamu.*** *Andika maneno haya ubaoni:* ***hamjambo, hatujambo, salamu***. Tazama ubaoni. Tusome maneno haya pamoja.

**Tunafanya:** Hamjambo? Hatujambo.

**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni. Soma kichwa cha hadithi.*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome kichwa cha hadithi. **Salamu**

**Ninafanya:** Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hii hadithi inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu salamu?

**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2-4 kutoa majibu yao.*

**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Sikiliza kwa makini.

Mwambie mwenzako iwapo ulichosema kitatendeka katika hadithi kilitendeka au la. Inua mkono iwapo utabiri wako ulitimia. *Waeleze maana ya maneno* ***utabiri*** *na* ***kutimia***. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.


### Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka kwenye hadithi*. Swali la 1: Taja vitu vipya alivyovaa anayezungumziwa. Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu. Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo. Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. *Jibu swali la kwanza*. Jibu: sare, soksi, viatu.

**Tunafanya:** Swali la 2: Wanafunzi walipoingia darasani walifanya nini? Nitasoma sentensi iliyo na jibu au tufikirie jibu iwapo halipo kwenye hadithi.

*Jibu swali pamoja na wanafunzi.* Jibu: Walijifunza kuhusu salamu; walimsikiliza mwalimu. *Toa mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswali.*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Kipindi cha 2 | Karibu darasani

Tazama picha. Eleza unachokiona.

Sikiliza hadithi.

Jibu maswali.

Igiza maamkuzi.

Mali ya Serikali ya Kenya

2

**Unafanya:** Swali la 3: Siku yako ya kwanza shuleni ulifanya nini? *Mwanafunzi ajibu. Kubali jibu lolote sahihi.*

### Zoezi

**Kuigiza maamkuzi**

**Ninafanya:** Kabla ya kukamilisha kipindi, tutaigiza maamkuzi yaliyofunzwa katika hadithi. Nitazame kisha mjibu. Hamjambo?

**Unafanya:** *Waelekeze kuigiza maamkuzi hayo. Ita mmoja mmoja ili waje mbele ya darasa kuwaamkua wenzao. Waelekeze pia kutumia hujambo na sijambo.*

### Kazi ya ziada

Watumie maamkuzi waliyojifunza kuwaamkua walezi wao kwa njia inayofaa na kwa heshima.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Hakiuzwi


Kipindi cha 3 Karibu darasani

Tazama picha. Eleza unachokiona.

Igiza maagizo.

Imba wimbo.

**Simama kaa**

Simama, kaa, simama, kaa,
Ruka, ruka, ruka, ruka,
Simama kaa.

Tembea, tembea, tembea, tembea,
Kimbia, kimbia, kimbia, kimbia
Simama kaa.

3 Hakiuzwi

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu maagizo. Maagizo hutolewa ili mtu afanye alivyoambiwa. Kwa mfano: simama. Mtu huinuka juu. Keti. Mtu hurudi kukaa kitini ama chini. Hebu tutazame picha ya kwanza. *Eleza kinachotendeka katika picha ya kwanza. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.*

**Unafanya:** Ni zamu yako sasa. Eleza unachoona katika picha ya pili. Je, huyu ni nani? Yuko wapi? Anafanya nini? Anafanya vipi? Anafanya hivyo wakati gani? Kwa nini? *Mwanafunzi ajibu. Hakikisha wanatofautisha kukimbia na kutembea.*

### Zoezi

**Kuigiza maagizo**

**Ninafanya:** Tutaigiza maagizo katika picha ya kwanza. Nitazame.

**Unafanya:** Igiza kukimbia. *Ita mwanafunzi mmoja na kumwagiza akimbie. Hakikisha wanafunzi wanatazama unachofanya. Waelekeze kuigiza maagizo wanayoyaona katika picha zote mbili peke yao. Waelekeze pia kuigiza maagizo mengine wanayoyajua kama vile lia, cheka, lala, simama, keti.*

### Kuimba wimbo

**Ninafanya:** Sasa tutaimba wimbo kuhusu maagizo. Nitazame. *Imba wimbo huku ukifanya vitendo.*

**Simama kaa**

*Simama, kaa ×2*

*Ruka, ruka ×2*

*Simama, kaa.*

*Tembea, tembea ×2*

*Kimbia, kimbia ×2*

*Simama, kaa.*

**Tunafanya:** *Imba wimbo pamoja na wanafunzi huku mkifanya vitendo.*

**Unafanya:** *Waelekeze kuimba wimbo huu pekee yao. Hakikisha kila mwanafunzi anaimba na kufuata maagizo haya: simama, kaa, ruka, tembea, kimbia.*

### Kazi ya ziada

Wawaimbie/wawafunze walezi wao wimbo na kufanya vitendo.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 4 **Karibu darasani**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



anaandika



anafuta

Toa maagizo.

Fuata maagizo.

Mali ya Serikali ya Kenya 4

## Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu maagizo. Kwanza tutazame picha. *Eleza kinachofanyika katika picha ya kwanza. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yenu. Eleza unachokiona katika picha. Je, huyu ni nani? Yuko wapi? Anafanya nini? Anafanya vipi? Anafanya hivyo wakati gani? Kwa nini? *Mwanafunzi ajibu. Waelekeze kujadili picha wakiwa peke yao.*

**Ninafanya:** Sasa hebu tutoe maagizo. Nitazame. *Sema neno tembea. Fuata hayo maagizo. Hakikisha wanafunzi wanatazama unachokifanya.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. *Waongoze kuunda makundi ya wanafunzi wawili wawili. Waelekeze kutoa maagizo haya: andika, futa, lia, cheka, lala. Kila kundi litoe na kufuata maagizo yake. Hakikisha wanabadilishana zamu kutoa na kuigiza maagizo hayo. Hakikisha pia wanatoa na kuigiza maagizo mengine wayajuayo.*

## Hadithi ya mwalimu

**Kato darasani**
Kato ni mvulana. Anasoma gredi ya kwanza kule Minto. Mwalimu wao anaitwa Bi. Menza. Yeye hupenda kuandika ubaoni. Leo Bi. Menza alisema, "Kato, futa ubao. Nataka kuandika kazi yenu." Kato alichukua kifutio. Alipanda juu ya kiti afute ubao. Kiti kilivunjika. Kato alianguka chini. Mwalimu alisema, "Pole Kato. Umeumia? Hebu simama." Kato alijibu, "Sijaumia mwalimu." Mwalimu alisema, "Ukihisi maumivu niambie. Siku nyingine usipande juu ya kiti."

**Ninafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni: **ubao.** Nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **ubao.** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **ubao.** Mwambie mwenzako sentensi uliyoitunga. *Mwanafunzi ajibu. Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.*

*Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* **kifutio, pole.** *Andika* ***ubao, kifutio, pole*** *ubaoni.*

**Tunafanya:** *Sema:* Nataka tusome maneno haya pamoja. **ubao, kifutio, pole**

**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni. Soma kichwa cha hadithi.*

**Tunafanya:** Sasa tusome kichwa cha hadithi. **Kato darasani**


**Ninafanya:** Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu darasani?

**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2 - 4 kutoa majibu yao.*

**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Sikiliza kwa makini.

Mwambie mwenzako iwapo ulichosema kilitendeka au la. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia. *Waeleze maana ya utabiri na kutimia*. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Kipindi cha 4 **Karibu darasani**

Tazama picha. Eleza unachokiona.

anaandika

anafuta

Toa maagizo.

Fuata maagizo.

Mali ya Serikali ya Kenya 4

## Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka* kwenye *hadithi.*

Swali la 1: Mwalimu wa Kato anaitwaje? Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu. Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo. Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. *Jibu swali la kwanza.* Jibu: Bi Menza.

**Tunafanya:** Swali la 2: Nini kilifanyika baada ya kato kupanda juu ya kiti? Nitasoma sentensi iliyo na jibu au tufikirie jibu iwapo halipo kwenye hadithi.

*Jibu swali pamoja na wanafunzi.* Jibu: kiti kilivunjika; alianguka chini; aliumia; mwalimu alimkagua. *Toa mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswali.*

**Unafanya:** Swali la 3: Ni mambo gani unayoweza kumfanyia rafiki yako ikiwa ataumia?


*Mwanafunzi ajibu. Kubali jibu lolote sahihi kama vile kumtuliza; kumuitia mtu mkubwa amsaidie.*

## Kazi ya ziada

Watoe maagizo kwa walezi wao kwa njia faafu na kwa heshima.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 5: Karibu darasani



Kipindi cha 5 **Karibu darasani**

Tazama picha. Eleza unachokiona.

Ambatanisha picha na jina.

| | |
|---|---|
| | kifutio |
| | dawati |
| | meza |
| | kitabu |

Chora umbo la kitabu.

5 Hakiuzwi

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu vitu mbalimbali darasani kama vile dawati, kifutio, kitabu na meza. Hebu kwanza tutazame picha hizi. *Eleza unachoona katika picha ya kwanza. Hakikisha wanafunzi wanatazama picha kitabuni.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Je, hii ni nini? *dawati*; Hiki ni nini? *kitabu, kifutio*. Hii ni nini? *meza. Waongoze kuunda makundi manne kisha waeleze wanachokiona katika kila picha. Kila kundi litaje wanachokiona katika picha.*

### Zoezi

**Kuambatanisha jina na picha**

**Ninafanya:** Sasa tutafanya zoezi la kuambatanisha picha na jina. Nitazame. Picha hii ni ya dawati. Natafuta neno dawati. Hili hapa. *Waonyeshe jinsi ya kuambatanisha jina na picha.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa kuambatanisha picha na jina. *Wafanye zoezi. Unaweza kuwapa picha na kadi, ama watumie kitabu cha mwanafunzi kuambatanisha. Tumia mwelekeo huo kuonyesha kifutio, meza na kitabu.*


**Kuchora umbo la kitabu**

*Waonyeshe jinsi ya kuchora kisha uwape fursa wachore.*

### Kazi ya ziada

Wachore dawati na kitabu. Waeleze walezi wao umuhimu wa vitu hivyo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________



Kipindi cha 6 **Mimi na wenzangu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Igiza maelezo.

| | |
|---|---|
| Unaitwa nani? | Mimi ninaitwa ________. |
| Wewe ni msichana au mvulana? | Mimi ni ________. |
| Una umri wa miaka mingapi? | Nina umri wa miaka ________. |
| Unasoma katika gredi gani? | Ninasoma katika gredi ya ________ |

Mali ya Serikali ya Kenya 6

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu mimi na wenzangu. Hebu tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachofanyika katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako*. Naona msichana. Je, unafikiri msichana huyu yuko wapi? Anasema nini? *Wasomee maneno yaliyo katika kibofu. Hakikisha wanafuatilia unavyosoma. Hakikisha pia kuwa wanatambua maelezo ya kila picha kuhusu **jina, jinsia, umri** na **gredi**.*

**Unafanya:** *Waelekeze kujadili picha. Waulize maswali haya: Hawa ni akina nani? Wako wapi? Wanafanya nini? Wanafanya vipi? Wanafanya hivyo wakati gani? Kwa nini?* Hebu tuitazame picha hii na kusema kinachotendeka.

**Tunafanya:** *Jadili picha zote mbili na wanafunzi. Pitia nao maneno ya kila picha. Unaweza kuanza kusoma nao wakirudia nyuma yako.*

**Unafanya:** *Waelekeze kujadili picha kuhusu maelezo peke yao. Chagua baadhi yao waeleze kwa kifupi maelezo yanayotolewa katika kila picha. Hakikisha wanafululiza maelezo kama vile yalivyoendelezwa katika maelezo yaliyo* kwenye *picha.*

### Zoezi

**Kuigiza Maelezo**

**Ninafanya:** Hebu sasa tuigize maelezo hayo. Nitatumia chati kuigiza maelezo hayo. Nitazame: *Hakikisha wanafunzi wanatazama unavyofanya*. Ninajiuliza: Unaitwa nani? Ninajijibu: Mimi ninaitwa __________. Ninajiuliza tena: Wewe ni msichana au mvulana? Ninajijibu: Mimi ni _____________. Ninajiuliza: Una umri wa miaka mingapi? Ninajijibu: Nina umri wa miaka ____________. Ninajiuliza tena: Unasoma katika gredi ipi? Ninajijibu: Ninasoma katika gredi ya _______. *Hakikisha umetumia chati ya kufululiza maigizo hayo.*

**Tunafanya:** Hebu nifanye sasa na mmoja wenu. *Igiza maelezo katika picha pamoja na mwanafunzi mmoja. Hakikisha wanafunzi wanatazama mnachofanya. Uliza mwanafunzi: Unaitwaje? Akujibu: Mimi ninaitwa __________. Muulize tena: Wewe ni msichana au mvulana? Akujibu: Mimi ni _____________. Muulize: Una umri wa miaka mingapi? Akujibu: Nina umri wa miaka ____________. Muulize tena: Unasoma katika gredi ipi? Akujibu: Nasoma katika gredi ya _______. Hakikisha anafuata muundo kujitambulisha jina, jinsia, umri/miaka na darasa lake.*

**Unafanya:** *Waelekeze kuigiza maelezo wakiwa katika makundi ya wawili wawili. Hakikisha wanafuata mfululizo huu ambao utakuwa umeuandika katika chati au ubaoni. Hakikisha kuwa wanasikiliza kwa makini wenzao wanapotoa maelezo kuwahusu wao wenyewe. Unaweza kuwarekodi huku wakitoleana maelezo. Chagua baadhi ya makundi ya wanafunzi kuulizana na kujibizana wakiwa mbele ya darasa.*

### Kazi ya ziada


Mwanafunzi aulize mlezi wake nyumbani maswali haya:

1. Unaitwa nani?
2. Una umri wa miaka mingapi?

Tarehe: ________________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 7 **Mimi na wenzangu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.




Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. miaka
2. mvulana
3. msichana

7 Hakiuzwi

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Tutaendelea kujifunza kuhusu mimi na wenzangu. Hebu tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachotendeka katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ninaona mvulana. Je, mvulana huyu yuko wapi? Anafanya nini? Unafikiri anasema nini?

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. *Jadili picha pamoja na wanafunzi.* Waulize: Huyu ni nani? Yuko wapi? Unafikiri anasema nini? *Waelekeze kujibu ipasavyo.*

### Hadithi ya mwalimu

**Salim Mwanakombo**

Mimi ninaitwa Salim Mwanakombo. Wazazi wangu ni Bwana na Bi. Wanjala Mambo. Nina kaka na dada mmoja. Nina umri wa miaka sita. Ninaishi Mishomoroni. Ninasoma katika shule ya Msingi ya Mombasa. Ninasoma katika gredi ya kwanza. Mwalimu wangu anaitwa Rahab Maneno. Darasani tuna wanafunzi ishirini na watano. Wavulana ni kumi na watano na wasichana ni kumi. Rafiki yangu ni Maria Atieno. Mimi hupenda kula wali kwa kuku. Wakati wa kupumzika mimi hucheza na wenzangu uwanjani. Darasani ninasoma kwa bidii nifaulu maishani. Ndoto yangu ni kuwa mwalimu bora maishani.

**Ninafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni: **umri.** Nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno, ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **umri**. *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2 - 3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.* Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **umri.** Mwambie mwenzako sentensi uliyoitunga.

**Unafanya:** *Mwanafunzi ajibu. Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo. Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* **miaka, gredi.** *Andika maneno haya ubaoni:* ***umri, miaka, gredi****. Soma maneno.*

**Tunafanya:** Nataka tusome maneno haya pamoja. **umri, miaka, gredi**

**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni. Soma kichwa cha hadithi.*

**Tunafanya:** Sasa tusome kichwa cha hadithi. **Salim Mwanakombo**

Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu Salim Mwanakombo?

**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2 - 4 kutoa majibu yao.*

**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Sikiliza kwa makini.

**Tunafanya:** Mwambie mwenzako iwapo ulichosema kitatendeka kilitendeka au la. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia. *Waeleze maana ya utabiri na kutimia*. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.

### ? Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka* kwenye *hadithi.*

Swali la 1: Salim ana umri wa miaka mingapi? Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu. Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo. Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. *Jibu swali.* Jibu: Miaka tisa.

**Tunafanya:** Swali la 2: Rafiki yake Salim anaitwa nani? Nitasoma sentensi iliyo na jibu au tufikirie jibu iwapo halipo kwenye hadithi.


*Jibu swali pamoja na wanafunzi.* Jibu: Rafiki yake ni Maria Atieno. *Toa mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswali.*

**Unafanya:** Swali la 3: Ukiwa mkubwa ungependa kufanya kazi gani? *Mwanafunzi ajibu. Kubali jibu lolote sahihi.*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 7 **Mimi na wenzangu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. miaka
2. mvulana
3. msichana

7

Hakiuzwi

## Zoezi

**Kutunga sentensi**

**Ninafanya:** Hebu tutumie maneno haya kutunga sentensi: miaka, mvulana, msichana. Nitazame: Neno ni miaka. Sentensi ni: Nina umri wa miaka arobaini.

**Tunafanya:** Hebu tutunge sentensi zingine pamoja. Neno ni mvulana. *Waelekeze kutunga angalau sentensi nne.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Tunga sentensi ukitumia neno **msichana.** *Waelekeze kutunga angalau sentensi nne wakitumia neno msichana. Hakikisha pia wanatunga sentensi wakitumia:* ***gredi*** *na* ***rafiki****.*

## Kazi ya ziada

Wawahadithie walezi wao hadithi waliyosoma darasani.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 8 **Mimi na wenzangu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Mweleze mwenzako kuhusu rafiki yako.

1. Mimi ninaitwa __________.
2. Rafiki yangu anaitwa __________.
3. Sisi tunapenda ku __________.

Mali ya Serikali ya Kenya 8

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Tutaendelea kujifunza kuhusu mimi na wenzangu. Hebu tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachofanyika katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Naona mvulana. Anacheza mchezo wa kati. *Eleza maana ya kati*. Je, wasichana wanafanya nini?

**Tunafanya:** Ni zamu yetu kujadili. *Waelekeze kujadili picha. Waulize maswali haya: Huyu ni nani? Yuko wapi? Anafanya nini? Hakikisha mmejibu maswali hayo pamoja.*

**Unafanya:** *Waelekeze kujadili picha peke yao. Waulize maswali haya: Hawa ni akina nani? Wako wapi? Wanafanya nini? Wanafanya vipi? Wanafanya hivyo wakati gani? Kwa nini? Chagua baadhi yao waeleze kwa kifupi wanachofikiria kinatendeka katika picha.*

### Zoezi

**Kutoa maelezo**

**Ninafanya:** Ni wakati wa kutoa maelezo kutuhusu. Nitazame. Mimi ninaitwa __________. *Sema jina lako.* Rafiki yangu anaitwa __________. *Taja jina la rafiki yako.* Sisi hupenda ku __________. *Taja unachopenda kufanya kama vile kusoma, kuimba, kucheza. Hakikisha wanasikiliza kwa makini unapowatolea maelezo. Unaweza kunasa maelezo yako katika kifaa cha kidijitali kisha wanafunzi wasikilize tena maelezo hayo. Toa muhtasari wa yale uliyosema.*

**Tunafanya:** *Husisha mwanafunzi mmoja. Mwelekeze jinsi atatoa maelezo kuhusu rafiki yake pale shuleni au nyumbani. Baada ya kumaliza, toa muhtasari wa yale aliyosema.*

**Unafanya:** *Waelekeze kuunda makundi ya wawili wawili na kutoleana maelezo kuhusu rafiki zao pale shuleni au nyumbani. Hakikisha wanatoleana muhtasari kuhusu maelezo yao. Wafuate mpangilio huu:*

1. Mimi ninaitwa __________________.
2. Rafiki yangu anaitwa __________________.
3. Sisi tunapenda ku __________________.

### Kazi ya ziada

Watolee walezi wao maelezo kuhusu rafiki yao.

Tarehe: ____________________ Muda: _______________ Idadi: _______________




Hakiuzwi

# Kipindi cha 9: Mimi na wenzangu 1

Kipindi cha 9 **Mimi na wenzangu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

Toa muhtasari wa hadithi.

9

Hakiuzwi

### Kutazama na kujadili picha


**Ninafanya:** Tunaendelea kujifunza kuhusu mimi na wenzangu. Hebu tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachofanyika katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ninaona msichana. Je, msichana huyu anafanya nini?
**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. Huyu ni nani? Yuko wapi? Anafanya nini? *Waelekeze kujadili picha pamoja nawe.*
**Unafanya:** *Waelekeze kujadili picha pekee yao. Waulize maswali yale yale: Hawa ni akina nani? Wako wapi? Wanafanya nini? Chagua baadhi yao waeleze kwa kifupi wanachofikiria kinatendeka katika picha.*

### Hadithi ya mwalimu

**Lelei Matano**
Jina langu ni Lelei Matano. Mimi ni msichana. Nina umri wa miaka minane. Ninaishi kijijini Kinga. Mimi ni kitinda mimba. Nina kaka mmoja na dada wawili. Wazazi wangu ni Bwana na Bi. Wanjala Simeo. Rafiki yangu ni Salma Njeri. Ninasoma shule ya Msingi ya Maji Mazuri. Niko katika gredi ya kwanza. Mwalimu wangu wa darasa ni Bw. Kiplimo Yegon. Yeye ni mwalimu mzuri. Yeye hunihimiza nisome kwa bidii. Muhula uliopita niliposhindwa kufanya hesabu za kuongeza, Mwalimu Yegon alinisaidia. Alisema, "Lelei usife moyo. Fanya mazoezi ya hesabu ya kuongeza kila siku. Utafaulu." Sasa hivi mimi ni mwanafunzi bora darasani. Mimi huwasaidia wanafunzi wengine kukamilisha kazi. Nikiwa uwanjani mimi hucheza na Salma pamoja na wanafunzi wengine. Tufikapo nyumbani, mimi huwasaidia wazazi wangu kufanya kazi za nyumbani.

**Ninafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni: **kaka.** Nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **kaka.** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.*
**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **kaka.** Mweleze mwenzako sentensi uliyoitunga. *Mwanafunzi ajibu. Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.*
*Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* **dada, wazazi.** *Andika maneno haya ubaoni:* ***kaka, dada, wazazi***. *Soma maneno.*
**Tunafanya:** *Sema:* Nataka tusome maneno haya pamoja.
**kaka, dada, wazazi**
**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni.* Hebu sasa tusome kichwa cha hadithi.
**Tunafanya: Lelei Matano**
Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu Lelei Matano?
**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2 - 4 kutoa majibu yao.*

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________




**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Sikiliza kwa makini.
**Tunafanya:** Mwambie mwenzako iwapo ulichosema kingetendeka kilitendeka au la. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia. *Waeleze maana ya utabiri na kama ulitimia.* Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.

## ? Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka kwenye hadithi.* Swali la 1: Lelei Matano ana umri wa miaka mingapi? Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu. Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo. Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. *Jibu swali la kwanza.* Jibu: Lelei ana miaka minane.
**Tunafanya:** Swali la 2: Lelei yuko na dada wangapi? Nitasoma sentensi iliyo na jibu au tufikirie jibu iwapo halipo kwenye hadithi. *Jibu: Lelei ana dada wawili.*
*Toa mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswali.*
**Unafanya:** Swali la 3: Ukiwa shuleni wewe hucheza mchezo gani na wenzako?
*Wajibu. Kubali jibu lolote sahihi.*

## Zoezi

**Kutoleana muhtasari**

**Ninafanya:** Sasa ni wakati wa kutoleana muhtasari kuhusu maelezo ya Lelei. Lelei ni msichana wa miaka minane.
**Tunafanya:** Ni zamu yetu. Tunajua jambo lipi jingine kuhusu Lelei? *Waelekeze kutoa maelezo mengine kumhusu Lelei kama vile baadhi ya watu wa familia yake. Hakikisha wanajumuisha hoja 10 wakitumia mfululizo huu: 1. jina lake; 2. jinsia; 3. nafasi katika familia; 4. watu wa familia; 5. anakoishi; 6. shule anakosoma; 7. walimu wake; 8. masomo anayopenda; 9. michezo anayopenda na 10. jinsi anavyosaidia wazazi.*
**Unafanya:** *Waelekeze kuunda vikundi vya wanafunzi wawiliwawili na kutoleana muhtasari kuhusu Lelei. Wape mfululizo wa hoja hizo 10 watumie.*

## Kazi ya ziada

Watolee walezi wao muhtasari kuhusu hadithi ya Lelei.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 10: Mimi na wenzangu 1

Kipindi cha 10 **Mimi na wenzangu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. miaka
2. gredi
3. rafiki

Chagua jibu sahihi.

a. Mimi ni __________ (msichana, mvulana).

b. Nina umri wa miaka __________ (6, 7, 8, 9, 10).

c. Ninasoma katika gredi ya __________ (1, 2)

Finyanga umbo la msichana au mvulana.

Mali ya Serikali ya Kenya 10

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Tutaendelea kujifunza kuhusu mimi na wenzangu. Hebu tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachofanyika katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Naona msichana. Amekalia kiti. *Eleza maana ya kiti*. Je, msichana anafanya nini?

**Tunafanya:** Ni zamu yetu kujadili. *Waelekeze kujadili picha. Waulize maswali haya: Huyu ni nani? Yuko wapi? Anafanya nini? Hakikisha mmejibu maswali hayo pamoja.*
**Unafanya:** *Waelekeze kujadili picha pekee yao. Waulize maswali haya: Huyu ni nani? Yuko wapi? Anafanya nini? Anafanya vipi? Anafanya hivyo wakati gani? Kwa nini? Chagua baadhi yao waeleze kwa kifupi wanachofikiria kinatendeka katika picha.*

### Zoezi

**Kutunga sentensi**

**Ninafanya:** Tunaendelea kujifunza kuhusu mimi na wenzangu. Leo tutatunga sentensi huku tukitumia maneno haya: **msichana, mvulana, rafiki**. Nitazame: Neno ni **msichana**. Sentensi ni: **Msichana huyu ana viatu vizuri.**
**Tunafanya:** Ni zamu yetu. Neno ni: **mvulana**. Hebu tutunge sentensi kadhaa. *Watunge angalau sentensi nne kwa kutumia neno mvulana. Hakikisha sentensi zenyewe ni tofauti na zile walizotoa katika kipindi cha awali.*
**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Tunga sentensi mkitumia neno **rafiki**. *Watunge angalau sentensi nne enye neno rafiki.*

**Kujaza mapengo**
**Ninafanya:** Hebu sasa tujaze mapengo kwa kuchagua jibu sahihi. Sentensi ya kwanza. Mimi ni______. Ikiwa wewe ni msichana, utachagua neno msichana. Na ukiwa mvulana, chagua neno mvulana.
**Tunafanya:** *Waelekeze kujaza pengo.*
**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Jaza pengo katika sentensi ya pili na ya tatu: Nina miaka ________.
Ninasoma katika gredi ya ________.
*Waelekeze kutoa jibu sahihi.*

**Kuchora**
*Waelekeze kujichora. Kwanza watambue ikiwa ni msichana au mvulana kisha wajichore na kupaka mchoro wao rangi.*


### Kazi ya ziada

Wafinyange umbo la rafiki yao msichana au mvulana.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 11 **Tarakimu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Imba wimbo.

**Wimbo wa tarakimu**

| | | |
|---|---|---|
| moja, moja, moja,<br>kalamu ni moja,<br>moja, moja, moja<br>meza nayo moja | mbili, mbili, mbili,<br>madawati ni mawili,<br>mbili, mbili, mbili,<br>na viti viwili | tatu, tatu, tatu,<br>vitabu ni vitatu,<br>tatu, tatu, tatu,<br>vifutio vitatu |

Andika nambari na jina katika daftari lako.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| moja | mbili | tatu | nne | tano | sita | saba | nane | tisa | kumi |

11

Hakiuzwi

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu tarakimu. Tarakimu ni nambari. Huonyesha idadi ya vitu au vitu ni vingapi. Tazama picha. *Eleza kitu kimoja katika picha. Hakikisha wanafunzi wanatambua idadi ya vitu katika picha.* Naona kitabu. Je, kitabu kiko wapi? Vitabu ni vingapi?

**Tunafanya:** *Waelekeze kutambua vitu vya darasani katika picha na idadi yake.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tambua vitu vingine vinavyotokana na picha. *Waelekeze kujadili picha peke yao. Hakikisha wanang'amua idadi ya vitu katika picha na pia wanasikiliza kwa makini maelezo ya wenzao.*

### Kuimba wimbo

**Ninafanya:** Sasa nitawafunza wimbo kuhusu tarakimu au nambari. Nitazame. *Imba wimbo huu huku wanafunzi wakikusikiliza kwa makini. Fanya vitendo vinavyoambatana na idadi ya kitu utakachotaja. Tumia mdundo wa ule wimbo wa moja, mbili, tatu, nne, tano, sita...*

**Moja mbili tatu**

Moja, moja, moja,
kalamu ni moja,
moja, moja, moja,
meza nayo moja,
Mbili, mbili, mbili,
madawati ni mawili,
mbili, mbili, mbili,
na viti viwili,
Tatu, tatu, tatu,
vitabu vitatu,
tatu, tatu, tatu,
vifutio vitatu.

**Tunafanya:** Hebu sasa tuimbe pamoja. *Imba wimbo pamoja na wanafunzi. Hakikisha unaongeza vitu vingine na kuzidisha idadi hadi kumi.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Imba wimbo peke yenu. *Waelekeze kuimba peke yao. Hakikisha wanataja vitu na idadi hadi kumi.*

### Zoezi

**Kunakili tarakimu**

**Ninafanya:** Ni wakati wa kuandika tarakimu au nambari tulizokuwa tunaimba. Nitazame. *Andika nambari moja hadi kumi ubaoni.* Sasa nitasoma tarakimu au nambari hizi. Nitazame. *Soma nambari moja hadi kumi.*

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. Tutaandika tarakimu au nambari hizi hewani na kuzisoma. *Andika kila nambari hewani huku ukiisoma pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Andika tarakimu au nambari hizi katika daftari lako na kuzisoma. *Waelekeze kuandika tena kila tarakimu huku wakizisoma.*

### Kazi ya ziada

Wawahesabie na kuwafunza walezi wao nambari moja hadi kumi. Watumie vitu vya nyumbani kama vile nafaka, vijiko, viti na kadhalika kufanya hivyo. Wanaweza kujirekodi kwenye kifaa cha kidijitali.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 12 **Tarakimu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

Jibu maswali.

Toa muhtasari kuhusu kisa ulichosimuliwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 12

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu tarakimu au nambari. Hebu tutazame picha. *Eleza kitu kimoja unachokiona katika picha. Sema idadi yake. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ninaona madawati. Hebu niyahesabu. *Hesabu kisha sema.* Madawati haya ni kumi.

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. Hebu tuhesabu madawati haya pamoja. *Hesabu madawati pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Hesabu viti katika picha.

*Waelekeze kuvihesabu viti. Hakikisha wanabadilishana zamu kuhesabu viti na madawati.*

**Ninafanya:** Sasa ningependa tuhesabu wanafunzi. Ninataka wasichana watano na wavulana watano waje hapa. *Wakija wahesabu. Sema:* Wanafunzi hawa ni kumi. Wasichana watano. Wavulana watano. Hebu tuwahesabu pamoja.

**Tunafanya:** *Hesabu pamoja.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Hesabu peke yenu.

*Wahesabu pekee yao.*

### Hadithi ya mwalimu

**Darasa la Berea**

Berea husoma shule ya msingi ya Sifa, darasa la kwanza. Mwalimu Mkuu ni Bi. Mambo. Kila asubuhi Bi. Mambo husema, "Hamjambo wanafunzi?" Wao humjibu, "Hatujambo, Bi. Mambo." Kiranja wao ni Salome. Yeye hufuta ubao kwa kifutio. Kisha yeye huvikusanya vitabu na madaftari na kumpelekea mwalimu majilisini. Salome huhakikisha wanafunzi wametulia.

Darasa la Berea lina madawati kumi. Viti navyo ni kumi. Wasichana na wavulana ni kumi pia. Meza ya mwalimu ni moja. Ukutani kuna chati tano. Darasa hilo lina madirisha manne ya chuma na mlango mmoja. Kabatini kuna kompyuta tano. Wanafunzi wa shule ya Sifa hushirikiana na kusoma kwa bidii. Wao huhakikisha sare zao na darasa lao ni safi.

**Ninafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni: **kifutio.** Nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **kifutio.** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2 - 3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **kifutio**. Onyesha mwenzako sentensi uliyoitunga. *Mwanafunzi ajibu. Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.*

*Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* **madawati, chati.** *Andika maneno haya ubaoni:* **kifutio, madawati, chati**. *Soma maneno.*

**Tunafanya:** *Sema:* Nataka tusome maneno haya pamoja. **kifutio, madawati, chati**

**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni. Soma kichwa cha hadithi.*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome kichwa cha hadithi. **Darasa la Berea**

Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu Darasa la Berea?

**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2 - 4 kutoa majibu yao.*

**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Silikiliza kwa makini.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 12: Tarakimu 1

Kipindi cha 12 **Tarakimu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

Toa muhtasari kuhusu kisa ulichosimuliwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 12

**Ninafanya:** Mwambie mwenzako iwapo ulichosema kingetendeka kilitendeka au la. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia. *Waeleze maana ya utabiri na kutimia*. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.

## ? Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka* kwenye *hadithi.* Swali la 1: Berea anasomea shule gani? Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu. Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo. Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. *Jibu swali la kwanza.* Jibu: Shule ya msingi ya Sifa.

**Tunafanya:** Swali la 2: Darasa la Berea lina madawati mangapi? Nitasoma sentensi iliyo na jibu au tufikirie jibu iwapo halipo kwenye hadithi.

*Wanajibu swali.* Jibu: Darasa la Berea lina madawati kumi. *Toa mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswali.*

**Unafanya:** Swali la 3: Darasa lenu lina madawati ngapi?

*Wajibu. Kubali jibu lolote sahihi.*

## Zoezi

**Toa muhtasari kuhusu kisa ulichosimuliwa**

**Ninafanya:** Kabla ya kukamilisha somo tutatoa muhtasari kuhusu hadithi tuliyosoma. Tunapotoa muhtasari, tunajibu maswali haya: Hadithi ilihusu nani? Hadithi ilihusu nini? Hadithi ilifanyika wapi? Ni mambo yapi mengine yalizungumziwa?

**Tunafanya:** Hebu tuyajibu maswali haya pamoja. *Jibu pamoja na wanafunzi. Hakikisha wanafunzi wanazingatia wahusika yaani: Berea, Mwalimu Mambo, Kiranja na idadi ya wanafunzi darasani. Hakikisha wanatoa maelezo kuhusu kila mhusika. Vilevile, wazingatie idadi ya: madawati, viti, meza ya mwalimu, chati, madirisha na mlango.*

## Kazi ya ziada

Wahesabu watu wanaoshi nao na kuleta ripoti kwa mwalimu.


Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Hakiuzwi

Kipindi cha 13 **Tarakimu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.




Imba wimbo.

**Uko wapi?**
Dole gumba, dole gumba,
Uko wapi? Uko wapi?
Niko hapa, niko hapa,
Umeshindaje? Umeshindaje?

Hesabu vidole vyako.

Panga kadi za majina ya nambari hivi.

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| moja | mbili | tatu | nne | tano | sita | saba | nane | tisa | kumi |

13

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** *Eleza kuhusu picha. Hakikisha wanafunzi wanatambua kuwa mtu amenyoosha mkono.*
**Tunafanya:** *Jadili picha pamoja na wanafunzi. Waulize maswali yanayojenga uelewa wao wa matukio katika picha.*
**Unafanya:** *Waelekeze kujadili picha peke yao. Hakikisha wanang'amua kinachotendeka katika picha na pia wanasikiliza kwa makini maelezo ya wenzao.*
**Ninafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu tarakimu au nambari. Hebu tutazame mchoro. *Eleza kuhusu mchoro wa mkono. Wasomee jina la kila vidole. Sema:* Naona mchoro wa mkono. Kidole hiki kinaitwa gumba. Na hiki ni shahada, hiki cha kati, hiki cha pete na hiki cha mwisho.
**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. Hebu tutaje kila kidole katika mchoro. *Tajeni kila kidole.*
**Ninafanya:** Ni zamu yenu sasa. Taja kila kidole peke yenu.
**Unafanya:** *Wataje jina la kila kidole.*

### Kuimba wimbo

**Ninafanya:** Ningependa tuimbe wimbo kuhusu vidole. Nitazame. *Imba wimbo huu huku wanafunzi wakikusikiliza kwa makini. Nyoosha vidole vyako vya gumba na kufanya vitendo vinavyoambatana na wimbo. Tumia mdundo wa: Tom Thumb, Tom Thumb, where are you? Where are you? Here I am. Here I am. Run and hide.*

**Wimbo wa vidole**
Dole gumba, dole gumba,
Uko wapi? Uko wapi?
Niko hapa, niko hapa,
Umeshindaje? Umeshindaje?

Nitaendelea kuimba nikitaja vidole vingine. *Taja cha shahada; na cha kati; na cha pete; na cha mwisho.*

**Tunafanya:** Hebu tuimbe pamoja. *Imba wimbo wote pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Mtaimba wimbo peke yenu. *Waelekeze waimbe peke yao katika makundi matano. Kila kundi liimbe ubeti mmoja. Hakikisha wanataja vidole husika na kufanya vitendo.*

### Zoezi

**Kuhesabu vidole**
**Ninafanya:** Sasa nitahesabu vidole vyangu vyote. Nitazame. *Hesabu vidole vyote.*

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa kuhesabu. *Hesabu vidole pamoja na wanafunzi. Kila mtu ahesabu vidole vyake - kimoja hadi kumi.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Hesabu vidole vyako peke yako. *Waelekeze kuunda makundi ya wanafunzi wawili walili. Kila mwanafunzi ahesabu vidole vya mwenzake. Hakikisha wanahesabu hadi kumi.*

**Kupanga kadi za majina ya nambari**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| moja | mbili | tatu | nne | tano |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| sita | saba | nane | tisa | kumi |

**Ninafanya:** Sasa nitapanga kadi ya neno na jina. Nitazame. *Tumia kadi za tarakimu na neno na kupanga. Onyesha kila tarakimu na jina lake. Tumia chati iliyochorwa kama hapo juu.*

**Tunafanya:** Ni zamu yetu, hebu tupange. *Chagua wanafunzi kumi. Kila mmoja awe na nambari na jina. Wapange kama ilivyo pale juu huku ukiwakosoa.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa kupanga peke yenu.

*Waelekeze wanafunzi kupanga jina na tarakimu kama pale juu. Wakosoe ipasavyo.*

### Kazi ya ziada

Afunze wenzake nyumbani wimbo waliofunzwa shuleni.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________


Kipindi cha 14 Tarakimu 1

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

Jibu maswali.

Toa muhtasari kuhusu kisa ulichosimuliwa.

Mali ya Serikali ya Kenya

14

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu tarakimu au nambari. Hebu tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachotendeka katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ninaona mvulana katika bembea. Je, mvulana yuko wapi? Anafanya nini? Anafanya vipi? Anafanya hivyo wakati gani? Kwa nini? Unafikiri anahisi vipi?

**Tunafanya:** *Waelekeze kujadili picha ya mvulana. Waulize maswali yale moja baada ya jingine. Hakikisha wanachangia vilivyo. Waulize vilevile ikiwa wamewahi kuchezea bembea. Watoe maoni yao.*

### Hadithi ya mwalimu

**Mchezo wa siku**

Wiki ina siku saba. Kila siku, Juma hucheza mchezo mmoja. Siku ya Jumatatu aliruka kamba. Alihesabu: moja, mbili, tatu. Siku ya Jumanne alicheza kibe. Alihesabu: moja, mbili, tatu, nne. Siku ya Jumatano alicheza kati. Alihesabu: moja, mbili, tatu, nne, tano. Siku ya Jumatano alicheza kalongo. Alihesabu: moja, mbili, tatu, nne, tano, sita. Siku ya Alhamisi alicheza bano. Alihesabu: moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Siku ya Ijumaa alibembea. Alihesabu: moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane. Unafikiri atacheza michezo ipi Jumamosi na Jumapili? Atahesabu hadi namba ipi siku ya Jumapili?

**Ninafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni: **kibe.** Nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **kibe.** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.* Sasa ni zamu yako.

**Unafanya:** Tunga sentensi ukitumia neno **kibe.** Mwambie mwenzako sentensi uliyoitunga. *Wajibu. Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.*

*Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* **kalongo, kubembea.** *Andika maneno haya ubaoni:* **kibe, kalongo, kubembea.** *Soma maneno.*

**Tunafanya:** *Sema:* Nataka tusome maneno hayo pamoja. **kibe, kalongo, alibembea**

**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni. Soma kichwa cha hadithi.*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome kichwa cha hadithi. **Mchezo wa siku**


Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________



Hakiuzwi

Kipindi cha 14 Tarakimu 1

Tazama picha. Eleza unachokiona.




Sikiliza hadithi.

Jibu maswali.

Toa muhtasari kuhusu kisa ulichosimuliwa.

Mali ya Serikali ya Kenya 14

Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu mchezo wa siku?

**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2 - 4 kutoa majibu yao.*

**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Silikiliza kwa makini.

Mwambie mwenzako iwapo ulichosema kingetendeka kilitendeka au la. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia. *Waeleze maana ya utabiri na kutimia*. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.

## Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka* kwenye *hadithi.* Swali la 1: Wiki ina siku ngapi? Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu. Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo. Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. *Jibu swali la kwanza.* Jibu: Wiki ina siku saba.

**Tunafanya:** Swali la 2: Juma alihesabu vipi siku ya Jumatano? Nitasoma sentensi iliyo na jibu au tufikirie jibu iwapo halipo kwenye hadithi.

*Wanajibu swali.* Jibu: Juma alihesabu moja, mbili, tatu, nne, tano, sita. *Toa mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswali.*

**Unafanya:** Swali la 3: Je, wewe ni mtoto wa ngapi katika familia yenu?

*Wajibu. Kubali jibu lolote sahihi.*

## Zoezi

**Kusimulia kisa cha mchezo wa kuhesabu**

**Ninafanya:** Tutasimulia tena hadithi ya Juma ya kuhesabu. Tutapanga alichofanya kila siku. Siku ya Jumatatu Juma aliruka kamba na kuhesabu: moja, mbili tatu.

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa kusema alichofanya Juma siku ya Jumanne na Jumatano. *Waongoze kueleza alichofanya Juma Jumanne na Jumatano.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa kusema alichofanya Juma siku ya Alhamisi na Ijumaa.

*Waelekeze kueleza matukio katika siku ya Alhamisi na Ijumaa. Waelekeze kutoa muhtasari kuhusu masimulizi ya Juma.*


## Kazi ya ziada

Mwanafunzi afunze wenzake nyumbani kuruka kamba na kuhesabu kutoka moja hadi kumi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 15 **Tarakimu 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Ambatanisha jina na nambari.

| | |
|---|---|
| moja | 3 |
| mbili | 4 |
| tatu | 1 |
| nne | 2 |
| tano | 7 |
| sita | 5 |
| saba | 6 |
| nane | 10 |
| tisa | 8 |
| kumi | 9 |

Hesabu vidole vya mchoro na vyako.

Andika nambari hizi kwenye daftari lako.
1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, 8, 9, 10

15 Hakiuzwi

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu tarakimu au nambari. Hebu tutazame picha hii. *Eleza kitu kimoja kinachotendeka katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ninaona vidole. Je, vidole ni vingapi? Vinafanya nini? Vinafanya vipi? Vinafanya hivyo wakati gani? Kwa nini?

**Tunafanya:** *Waelekeze kujadili picha ya vidole. Waulize maswali yale moja baada ya jingine. Hakikisha wanachangia vilivyo. Waulize vilevile ikiwa wamewahi kuchezea vidole. Watoe maoni yao.*

### Zoezi

**Kuambatanisha nambari na maneno.**
**Ninafanya:** *Chora jedwali lilillo **ukurasa wa 15** kwenye ubao.* Leo tutaambatanisha neno na nambari. Nitazame. *Ambatanisha maneno haya na nambari zake: moja, mbili, tatu.*

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. Hebu tuambatanishe maneno haya na nambari: nne, tano, sita. *Ambatanisha maneno na nambari pamoja na wanafunzi.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Ambatanisha maneno haya na nambari: saba, nane, tisa, kumi.

**Majibu**

| | |
|---|---|
| moja | 3 |
| mbili | 4 |
| tatu | 1 |
| nne | 2 |
| tano | 7 |
| sita | 5 |
| saba | 6 |
| nane | 10 |
| tisa | 8 |
| kumi | 9 |

**Kuhesabu**

**Ninafanya:** Sasa tutarejelea kuhesabu vidole kwenye michoro kisha tuhesabu vidole vya mikono yetu. Nitazame. *Hesabu vidole* kwenye *michoro kisha uhesabu vidole vya mikono yako.*

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. Hebu tuhesabu vidole kwenye michoro kisha tuhesabu vidole vya mikono yetu. *Hesabu vidole vya michoro na vya mikono. Kila mwanafunzi atumie kitabu chake kisha atumie vidole vyake.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Hesabu vidole kwenye michoro kisha uhesabu vidole vya mikono yako.

*Waelekeze kuhesabu vidole vya michoro na vya mikono. Kila mwanafunzi atumie kitabu chake kisha atumie vidole vyake.*

**Kuandika nambari.**
**Ninafanya:** *Andika nambari 1 hadi 10 ubaoni.*
**Unafanya:** *Waelekeze wanafunzi kundika tarakimu kwenye madaftari yao.*

### Kazi ya ziada

Wahesabu vidole vya walezi wao nyumbani na kusema majina ya kila kidole.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________


Kipindi cha 16 Siku za wiki 1

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Imba wimbo wa siku za wiki.

**Siku za wiki**
Jumamosi na Jumapili,
Ni siku za wiki.
Jumatatu na Jumanne,
Ni siku za wiki,
Jumatano, Alhamisi, Ijumaa,
Ni siku za wiki.
Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa,
Ni siku za wiki.

Mali ya Serikali ya Kenya 16

## Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutajifunza kuhusu siku za wiki. Hebu kwanza tutazame picha. *Eleza kuhusu kalenda. Sema kuwa katika lugha ya Kiswahili wakati huelezwa kwa kutumia saa, siku, wiki, miezi na miaka. Unapoeleza, hakikisha wanafunzi wanatambua siku za wiki na nambari zinazoambatana na siku hizo kama ilivyo katika Kiswahili. Sema:* Jumamosi ni siku ya 1 ya wiki. Jumapili ni siku ya 2 ya wiki. Jumatatu ni siku ya 3 ya wiki. Jumanne ni siku ya 4 ya wiki. Jumatano ni siku ya 5 ya wiki. Alhamisi ni siku ya 6 ya wiki. Ijumaa ni siku ya 7 ya wiki. *Waeleze pia kuwa siku saba huwa ni wiki moja. Waeleze kuwa neno jingine la wiki ni juma. Waeleze pia kuwa wiki nne ni mwezi mmoja. Waeleze umuhimu wa kalenda na jinsi ya kuisoma. Sema:* Siku saba za wiki ni wiki moja. Jina lingine la wiki ni juma. Wiki nne huwa mwezi.

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. Hebu tusome siku za wiki. *Soma pamoja na wanafunzi siku za wiki. Waulize maswali yanayojenga uelewa wao kuhusu siku za wiki.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Soma siku za wiki. *Waelekeze kusoma siku za wiki peke yao. Hakikisha wanang'amua kinachotendeka katika picha na pia wanasikilza kwa makini maelezo ya wenzao.*

## Kuimba wimbo

**Siku za wiki**
Jumamosi na Jumapili
Ni siku za wiki
Jumatatu na Jumanne
Ni siku za wiki
Jumatano, Alhamisi, Ijumaa,
Ni siku za wiki.
Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa,
Ni siku za wiki.

**Ninafanya:** Sasa tutaimba wimbo kuhusu siku za wiki. Nitazame. *Imba wimbo huku ukifanya vitendo. Hakikisha wanakusikiliza kwa makini. Tumia mdundo wa 'Old MacDonald had a dog'. Ashiria kwa vidole wakati unapoimba.*

**Tunafanya***:* Ni zamu yetu sasa. Hebu tuimbe pamoja. *Imba wimbo pamoja na wanafunzi. Waongoze kuashiria kwa vidole huku wakiimba wimbo wa siku za wiki.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Imbeni peke yenu.

*Waelekeze jinsi watakavyoimba. Hakikisha wanaashiria kwa vidole huku wakiimba wimbo wa siku za wiki.*

## Kazi ya ziada

Wafunze walezi wao wimbo wa siku za wiki.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 17: Siku za wiki 1

Kipindi cha 17 **Siku za wiki 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

17 Hakiuzwi

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu siku za wiki. Hebu tutazame picha. *Eleza kitu kimoja kinachotendeka katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ninaona mtu mzima. Ninaona watoto pia. Ninafikiri huyu ni baba na hawa ni watoto wake. Je, baba na watoto wako wapi? Wanafanya nini? Wanafanya vipi? Wanafanya hivyo wakati gani? Kwa nini?

**Tunafanya:** *Waelekeze kujibu maswali pamoja nawe.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Eleza kinachotendeka katika picha.

*Tumia maswali kuwaelekeza kujadili picha.*

### Hadithi ya mwalimu

**Shughuli za siku za wiki**
Siku za wiki huwa na shughuli nyingi. Hivyo basi ifikapo Jumamosi, watu wengi hupumzika. Wengine huenda kanisani kusali. Wao husema Jumamosi ni siku ya Sabato. Ifikapo Jumapili, watu wengine huenda kanisani kuabudu Mungu. Kuna wanaokwenda msikitini kila Ijumaa kusali. Jumatatu ifikapo watu wengi hurudi kazini mwao. Wanafunzi nao hurudi shuleni. Watu wote huendelea kufanya shughuli mbalimbali siku ya Jumanne, Jumatano, Alhamisi na Ijumaa. Siku hizi saba za wiki huanza tena.

**Ninafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni: **shughuli.** Ni nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **shughuli.** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.* Sasa ni zamu yako.

Tunga sentensi ukitumia neno **shughuli.** Mweleze mwenzako sentensi uliyoitunga.

**Unafanya:** *Mwanafunzi ajibu. Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.*

**Ninafanya:** *Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* ***kusali, kuabudu.*** Andika maneno haya ubaoni: **shughuli, kusali, kuabudu**. *Soma maneno.*

**Tunafanya:** *Sema:* Nataka tusome maneno haya pamoja. *Soma maneno pamoja na wanafunzi.*

**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni. Soma kichwa cha hadithi.*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome kichwa cha hadithi. **Shughuli za siku za wiki.**

Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu shughuli za siku za wiki?

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 17 **Siku za wiki 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

17 Hakiluzwi

**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2 - 4 kutoa majibu yao.*

**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Silikiliza kwa makini.

**Ninafanya:** Mwambie mwenzako iwapo ulichosema kingetendeka kilitendeka au la. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia. *Waeleze maana ya utabiri na kutimia*. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.

## ? Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka* kwenye *hadithi.* Swali la 1: Watu wengi hufanya nini siku ya Jumamosi? Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu. Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo.

Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. *Jibu swali la kwanza. Jibu: Watu wengi hupumzika.*

**Tunafanya:** Swali la 2: Siku ya mwisho kwenda shuleni ni gani? Nitasoma sentensi iliyo na jibu au tufikirie jibu iwapo halipo kwenye hadithi. *Wanajibu swali.* Jibu: Siku ya mwisho kwenda shuleni huwa Ijumaa. *Peana mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswali.*

**Unafanya:** Swali la 3: Wewe hufanya nini siku ya Jumapili? *Wajibu. Kubali jibu lolote sahihi.*

## Kazi ya ziada

Wanafunzi wazuru eneo lao la kusali na kueleza walichokiona huko.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 18: Siku za wiki 1

Kipindi cha 18 **Siku za wiki 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Eleza unachofanya katika siku za wiki.

Siku ya Jumamosi mimi hu____________.
Siku ya Jumapili mimi hu____________.
Siku ya Jumatatu mimi hu____________.
Siku ya Jumanne mimi hu____________.
Siku ya Jumatano mimi hu____________.
Siku ya Alhamisi mimi hu____________.
Siku ya Ijumaa sisi hu____________.

Mali ya Serikali ya Kenya

18

## Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu siku za wiki. Kumbuka hadithi tuliyosoma ya siku za wiki. Siku hizi ni Jumamosi na Jumapili.

**Tunafanya:** Hebu tutaje siku mbili zinazofuata. Jumatatu na Jumanne.

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Taja siku za wiki ambazo hazijatajwa.

*Mwanafunzi ajibu. Hakikisha wametaja Jumatano, Alhamisi na Ijumaa.*

**Ninafanya:** Katika hadithi tuliyoisoma Juma alicheza mchezo tofauti kila siku. Alianza kwa kuruka kamba. Hebu tuangalie picha hii. Nani hawa? Wako wapi? Wanafanya nini? Wanafanya vipi? Wanafanya hivyo wakati gani? Kwa nini?

**Tunafanya:** *Wajibu pamoja nawe. Hakikisha wanataja mambo mengine ambayo yanatendeka.*

## Zoezi

**Eleza matukio ya siku za wiki**

**Ninafanya:** Sasa tutaeleza mambo tunayofanya sisi kila siku ya wiki. Nisikilize. Siku ya Jumamosi mimi hufua nguo. Siku ya Jumapili mimi huenda kanisani kusali. Je, nyinyi hufanya nini siku za wiki?

**Tunafanya:** *Waelekeze kutaja vitu wanavyofanya katika kila siku ya wiki. Watumie mpangilio uliotolewa hapa chini. Wanapotoa hoja zao, jaza nafasi katika ubao.*

Siku ya Jumamosi mimi hu _________

Siku ya Jumapili mimi hu _________

Siku ya Jumatatu mimi hu _________

Siku ya Jumanne mimi hu _________

Siku ya Jumatano mimi hu _________

Siku ya Alhamisi mimi hu _________

Siku ya Ijumaa sisi hu _________

**Ninafanya:** Tumeandika mambo mbalimbali ambayo sisi hufanya siku za wiki. Hebu tusome pamoja. Tufanye pia vitendo. Nitazame. Siku ya Jumamosi mimi hufua nguo hivi. *Onyesha kitendo cha kufua.*
**Tunafanya:** Someni sentensi huku mkifanya vitendo.

## Kazi ya ziada

Wanafunzi waruke kamba huku wakitaja siku za wiki. Wanaweza kuongeza pia kuhesabu moja hadi kumi.

Tarehe: __________________ Muda: ______________ Idadi: _____________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 19: Siku za wiki 1

Kipindi cha 19 **Siku za wiki 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

Jibu maswali.

Toa muhtasari wa masimulizi ya siku za wiki.

19

Hakiluzwi

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu siku za wiki. Hebu kwanza tutazame picha. *Eleza kitu kimoja kinachotendeka katika picha. Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.*

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa kueleza tunachokiona katika picha. *Waelekeze kujadili kuhusu picha.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Mnaona nini katika picha? Hawa ni akina nani? Wako wapi? Wanafanya nini? Wanafanya vipi? Wanafanya hivyo wakati gani? Kwa nini?

*Mwanafunzi ajibu.*

### Hadithi ya mwalimu

**Siku za wiki**

Wanakijiji wa Mbalamwezi hushirikiana kufanya kazi za ukulima na ufugaji wa mifugo. Kukiwa na tatizo, chifu wao, Mzee Muchalwa, huwaita mkutanoni. Juzi kulipokuwa na mafuriko, chifu huyo aliwaongoza kuzibua mitaro yote. Hakuna yeyote aliyekufa maji. Ushirikiano huu umepelekea Mbalamwezi kujulikana. Watoto wote wa Mbalamwezi huenda shuleni Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi na Ijumaa. Siku ya Jumamosi na Jumapili wao huwasaidia wazazi wao kufanya kazi za nyumbani. Kuna baadhi yao huenda kanisani Jumamosi au Jumapili. Wengine husali msikitini Ijumaa.

**Ninafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni: **hushirikiana.** Nani anayejua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **hushirikiana.** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili. Wanafunzi 2 - 3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.*

**Unafanya:** Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **hushirikiana.** Mwambie mwenzako sentensi uliyoitunga. *Mwanafunzi ajibu. Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.*

*Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* ***mafuriko, kuzibua.***

**Ninafanya:** *Andika maneno haya ubaoni:* **hushirikiana**, **mafuriko**, **kuzibua**. *Soma maneno.*

**Tunafanya:** *Sema:* Nataka tusome maneno hayo pamoja. *Soma maneno pamoja na wanafunzi.*

**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni. Soma kichwa cha hadithi.*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome kichwa cha hadithi. **Siku za wiki.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 19 **Siku za wiki 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.



Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

Toa muhtasari wa masimulizi ya siku za wiki.

19 Hakiuzwi

Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hadithi hii inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu siku za wiki?

**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2 - 4 kutoa majibu yao.*

**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Silikiliza kwa makini.

Waelekeze kudhibitisha utabiri wao baada ya kusomewa hadithi.

## ? Maswali

**Ninafanya:** *Waongoze wanafunzi jinsi ya kusoma swali na kulijibu kwa kutafuta jibu kutoka* kwenye *hadithi.*
Swali la 1: Wanakijiji wa Mbalamwezi hushirikiana kufanya nini? Kwanza ninaenda kwenye hadithi kutafuta jibu. Nikipata jibu, nitaisoma sentensi iliyo na jibu sahihi. Kama jibu halipo, nitafikiria jinsi ya kulijibu swali hilo. Nitasema jibu la sentensi kikamilifu. *Jibu swali la kwanza.* Jibu: Wanakijiji wa Mbalamwezi hushirikiana kufanya kazi za ukulima na ufugaji wa mifugo.

**Tunafanya:** Swali la 2: Taja siku ambazo watoto huenda shuleni. Nitasoma sentensi iliyo na jibu au tufikirie jibu iwapo halipo kwenye hadithi.

*Wanajibu swali.* Jibu: Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi na Ijumaa. *Peana mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu maswali. Kumbuka wale walio katika shule za mabweni huwa shuleni siku zote. Hivyo wao hukaa shuleni kwa muhula mzima.*

**Unafanya:** Swali la 3: Wewe hufanya nini kila jioni?

*Mwanafunzi ajibu. Kubali jibu lolote sahihi.*

**Ninafanya:** Sasa tutatoa muhtasari wa hadithi tuliyosoma. Hadithi inazungumzia nini? Hadithi inazungumzia nani? Hadithi inazungumzia wanakijiji. Wao hushirikiana kufanya kazi.

**Tunafanya:** Ni zamu yetu. Hebu tutoe muhtasari pamoja. *Waelekeze kutoa muhtasari. Hakikisha wamezingatia yanayozungumziwa kama vile: Chifu na watoto.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Hadithi imetaja nini? Kitu kimoja kilichotajwa ni ushirikiano wa wanakijiji. Ni nini kingine kimezungumziwa.


*Waelekeze kutoa muhtasari. Hakikisha wamezingatia kinachozungumziwa kama vile: siku za wiki, siku za kusali, kazi zinazofanyika Mbalamwezi.*

## Kazi ya ziada

Wanafunzi waorodheshe kazi zinazofanywa na watu wa kwao kila siku ya wiki.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 20: Siku za wiki 1



Kipindi cha 20 Siku za wiki 1

Tazama picha. Jaza mapengo.



Jaza mapengo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jumamosi | | Jumatatu | | Jumatano |
| Alhamisi | | | | |

Panga majina ya siku za wiki ipasavyo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jumamosi | Jumatano | Jumatatu | Ijumaa | Alhamisi |
| Jumanne | Jumapili | | | |

Andika maneno haya katika daftari lako.

1. Juma
2. Wiki
3. Jumatatu

Mali ya Serikali ya Kenya 20

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Leo tutarejelea tuliyoyasoma kuhusu siku za wiki kwa kujaza mapengo au nafasi. Je, Jumapili ni siku ya ngapi ya wiki? Jumapili ni siku ya kwanza. Najaza hii nafasi kwa kuandika moja.

**Tunafanya:** Hebu tujaze nafasi ya pili pamoja. *Waelekeze kujaza pengo la pili.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Jaza nafasi mbili za mwisho zilizosalia. *Waelekeze kujaza mapengo yaliyosalia.*

**Ninafanya:** Soma siku za wiki na mbari pamoja.

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome siku ya wiki na nambari pamoja.

**Unafanya:** *Waelekeze kusema siku ya wiki na nambari yake kama vile: Jumapili, moja. Jumatatu: mbili na kadhalika.*

### Zoezi

**Tazama jedwali. Jaza mapengo.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumamosi | | Jumatatu | |
| Jumatano | | Ijumaa | |

**Ninafanya:** Tutaendelea kujifunza kuhusu siku za wiki kwa kujaza mapengo au nafasi nyingine. Hapa tumeanza na Jumamosi. Siku inayofuata ni ipi? Ni Jumapili. Ninaandika jina Jumapili hapa.

**Tunafanya:** Hebu tujaze nafasi ya pili pamoja. *Waelekeze kujaza pengo la pili.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Jaza nafasi ya mwisho.

*Waelekeze kujaza pengo la mwisho.*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome siku za wiki pamoja.

*Waelekeze kusoma siku hizo za wiki.*

**Kupanga majina ya siku za wiki**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumamosi | Jumatano | Jumatatu | Ijumaa |
| Alhamisi | Jumanne | Jumapili | |

**Ninafanya:** Sasa tutapanga majina ya wiki kuanzia Jumamosi. Ni siku ipi inafuata Jumamosi? Ni Jumapili.

**Tunafanya:** Hebu tupange siku zingine. Ni siku gani inafuata Jumapili? *Waelekeze kupanga siku ya Jumatatu*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Panga siku za wiki zilizosalia. *Waelekeze kupanga Jumatano, Alhamisi na Ijumaa.*

**Tunafanya:** Hebu sasa tusome siku hizi za wiki pamoja.

*Waelekeze kusoma siku hizo za wiki.*

**Kunakili na kusoma maneno**

**Ninafanya:** Hebu sasa tunakili na kuyasoma maneno haya. Nitazame. *Nakili **juma** na **wiki** ubaoni huku unasoma kila neno.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Nakili maneno haya katika madaftari yenu. *Waelekeze kunakili maneno na kuyasoma.*

### Kazi ya ziada

Kuwasomea walezi walichonakili katika madaftari yao na kuwaeleza maana.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 21: Familia 1

Kipindi cha 21 **Familia 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.

Taja jina la herufi na utamke sauti.

m



Eleza uhusiano wa watu wa familia.

21 Hakiuzwi

### Ufahamu wa fonimu

Leo tutajifunza sauti **/m/**. Kwanza tutaitamka sauti hiyo. Baadaye nitataja maneno; neno moja baada ya jingine. Mtasema iwapo neno hilo linaanza kwa sauti hiyo.

**Ninafanya:** Sauti ni /m/. Neno la kwanza ni **mama**. Neno hili linaanza kwa sauti /m/. Kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno la pili ni **ama**. Neno **ama** halianzi kwa sauti /m/. Kwa hivyo nitaonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Sasa tutatamka sauti /m/ pamoja. Sauti ni? /m/. Sasa nitataja neno. Iwapo neno hilo linaanza kwa sauti /m/, tutaonyesha kidole juu. Iwapo halianzi kwa sauti /m/, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni **mama.** *Mwalimu na wanafunzi waonyeshe pamoja.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Sauti ni /m/. Onyesha kidole juu iwapo neno hilo linaanza kwa sauti /m/. Iwapo halianzi kwa sauti /m/, onyesha kidole chini. Neno la kwanza ni mama. *Wanafunzi waonyeshe kidole juu. Tumia hatua ya tatu kufunza maneno haya:* **makaa, kaka, matatu** na **uma**.

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi ndogo '**m**' ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo* kwenye *mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi hii kwa kidole. Sema:* Jina la herufi hii ni **'m'**. Sauti ni /m/. Sauti hii ni sawa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

**Tunafanya:** Sasa tutataja jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni **'m'**. Sauti yake ni /m/.

**Unafanya:** Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ni? **'m'**. Sauti yake ni? /m/.

Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 21**. Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

### Kutazama na kujadili picha

**Ninafanya:** Hebu sasa tujifunze kuhusu familia. Kwanza tutatazama picha. *Eleza kuhusu picha. Unapoeleza, hakikisha wanafunzi wanatambua watu tofauti tofauti katika picha. Sema:* Hii ni picha ya familia. Familia ni jamaa ya watu wanaoishi pamoja. Huwa na baba, mama na watoto. Pia hujumuisha nyanya na babu, wajomba, mashangazi na binamu.

**Tunafanya:** Ni zamu yetu sasa. Nani huyu? Yuko wapi? Anafanya nini? Anafanya vipi? Anafanya hivyo wakati gani? Kwa nini? *Waelekeze kuongea kuhusu kila mtu katika picha huku wakijibu maswali.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Eleza unachokiona katika picha. *Waelekeze kueleza kuhusu picha. Hakikisha wanang'amua uhusiano kati ya jamaa* kwenye *picha kama wazazi, mjomba, shangazi, binamu*.

### Zoezi

**Kusikiliza na kuongea**

**Ninafanya:** Sasa tutaeleza kuhusu uhusiano wa watu wa familia. *Waelekeze kuunda makundi ya watu 15. Wapange ifuatavyo: mama, baba, watoto wao, nyanya, babu, mjomba, shangazi na watoto wao.*

**Tunafanya:** *Waelekeze kujipanga kulingana na uhusiano kuanzia kwa nyanya na babu hadi wajukuu.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Eleza uhusiano wa familia peke yenu. *Waeleze uhusiano huo wa familia peke yao, nawe uwakosoe ipasavyo.*

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waulize walezi wao wawatajie watu wa familia yao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 22 **Familia 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.

**Majukumu ya watu wa familia**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

M



Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

Mali ya Serikali ya Kenya 22

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya:** *Andika herufi kubwa* ***'M'*** *ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo* kwenye *mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi hii kwa kidole. Sema:* Jina la herufi hii ni **'m'**. Sauti ni **/m/**. Sauti hii ni sawa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

**Tunafanya:** Sasa tutataja jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni **'m'**. Sauti yake ni /m/.

**Unafanya:** Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ni? **'m'** Sauti yake ni? /m/.

Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 22**. Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

### Hadithi ya mwalimu

**Vitendawili vya babu**

Nyanya na babu walitutembelea. Baada ya chakula babu alisema, "Kitendawili?" Tulitabasamu. Nyanya alisema, "Sema tega!" Babu aliuliza tena, "Kitendawili?" Tulijibu, "Tega!" Babu alisema, "Tik! Tak! Tik! Tak!" Tulitabasamu. Nyanya aliileta saa. Aliiweka karibu na masikio yetu. "Ni saa! Inafanya Tik! Tak!" Tulisema kwa furaha. Babu alitega kitendawili kingine. "Nyumba yangu kubwa mlango mdogo." Tulitabasamu. Nyanya aliileta chupa. Alisema, "Chupa ni kubwa upande huu wa chini. Mdomo wake mdogo. Jibu ni chupa." Babu alitega, "Mama nieleke." Tulitabasamu. Babu alisema, "Nipe mji." Nyanya alisema, "Ukishindwa kutegua kitendawili, unampa aliyetega mji." "Tunakupa Mayanja." Tulimjibu. Babu alisema, "Shukrani. Nimefika Mayanja. Wanamayanja wamewasalimu. Jibu ni kitanda." Babu alitega, "Nikimpiga mwanangu watu hucheza." Tulifurahia vitendawili vya babu. Tulijifunza mengi.

**Tunafanya:** Leo tutaendelea kujifunza kuhusu familia. Hebu tutazame picha. Eleza kitu kimoja kinachotendeka katika picha. *Hakikisha wanafunzi wanafuata maelezo yako.* Ninaona msichana. Amesimama. Je, msichana yuko wapi? Anafanya nini? Anafanya vipi? Anafanya hivyo wakati gani? Kwa nini? *Waelekeze kujibu maswali pamoja nawe.*

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Eleza kinachotendeka katika picha. *Tumia maswali kuwaelekeza kujadili picha.*

**Tunafanya:** Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, hebu tujifunze maneno mapya. Neno la kwanza ni **nyanya.** Nani anajua maana ya neno hili? *Waelekeze wanafunzi ipasavyo. Eleza maana ya neno hili ikiwa hakuna mwanafunzi yeyote anayejua maana. Tunga sentensi inayoonyesha maana ya neno* **nyanya.** *Waulize wanafunzi wajadiliane na wenzao huku wakitumia maneno yao wenyewe kueleza maana ya neno hili.*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 22: Familia 1

Kipindi cha 22 **Familia 1**

Tazama picha. Eleza unachokiona.

**Majukumu ya watu wa familia**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

M



Sikiliza hadithi.

? Jibu maswali.

Mali ya Serikali ya Kenya

22

*Wanafunzi 2-3 wapewe nafasi kueleza maana ya neno hili.* Sasa ni zamu yako. Tunga sentensi ukitumia neno **nyanya.** Mwambie mwenzako sentensi uliyoitunga. *Chagua wanafunzi wachache watunge sentensi huku ukiwakosoa ipasavyo.*

*Tumia hatua hii kufunza maneno yafuatayo:* **babu, nieleke**.

**Ninafanya:** *Andika* **nyanya, babu, nieleke** *ubaoni. Soma maneno.*

**Tunafanya:** Nataka tusome maneno hayo pamoja. **nyanya, babu, nieleke.**

**Ninafanya:** *Andika kichwa cha hadithi ubaoni. Soma kichwa cha hadithi.* Hebu sasa tusome kichwa cha hadithi.

**Tunafanya: Vitendawili vya babu.**

Kumbuka yale tuliyozungumzia tulipojadili picha hapo mwanzoni mwa somo. Unafikiri hii hadithi inazungumzia nini? Unajua nini kuhusu vitendawili vya babu?

**Unafanya:** Mgeukie mwenzako na umweleze jambo moja ambalo unafikiri litatendeka kwenye hadithi. *Waulize wanafunzi 2 - 4 kutoa majibu yao.*

**Ninafanya:** Sasa nitawasomea hadithi. Silikiliza kwa makini huku ukitazama picha kwenye **ukurasa wa 22.**

**Tunafanya:** Mwambie mwenzako iwapo ulichosema kitatendeka kilitendeka au la. Inua mkono juu iwapo utabiri wako ulitimia. *Waeleze maana ya utabiri na kutimia*. Sasa tutazingatia sehemu ya ufahamu ili tuelewe hadithi hii zaidi.

## ? Maswali

**Ninafanya:** Swali la 1: Ni akina nani walitutembelea? Nitafikiri jinsi ya kujibu swali hili kwa kukumbuka yale niliyosoma. Nitasema jibu na sentensi kikamilifu. Jibu la swali hili ni nyanya na babu walitutembelea.

**Tunafanya:** Swali la 2: Nani alitega vitendawili? Hebu tufikirie yale tuliyosoma kwenye hadithi. *Wanajibu swali.* Jibu: babu ndiye aliyetega witendwili. *Peana mwelekeo unaopaswa kwa wanafunzi wanapojibu swali.*

**Unafanya:** Swali la 3: Nani hukufunza mambo mengi nyumbani kwenu? Fikiria kuhusu swali na utoe jibu sahihi. *Wajibu. Kubali jibu lolote sahihi.*

## Zoezi

Katika vikundi vya watu wawili wanafunzi waeleze maana ya majina ya watu wa familia.

## Kazi ya ziada

Waulize walezi wao wawategee vitendawili huku wakitegua.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________



Hakiuzwi

Kipindi cha 23 na 24 **Familia 1**

**Kipindi 23**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **a** **m**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  m a → **ma** a → **a**

- Soma silabi na maneno.

  ma ma → **mama** a ma → **ama**

**Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi.

1. Mimi ninasoma.
2. Mimi ninaketi.
3. Mimi ninaandika.

**Kusoma hadithi**

**Asante**

Mama anasema, "Asante."
Mama anasema asante ama pole?



23 Hakiuzwi

Kipindi cha 23 na 24 **Familia 1**

**Kipindi 24**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **A** **a**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  m a → **ma** a → **a**

- Soma silabi na maneno.

  ma ma → **mama** a ma → **ama**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Jukumu la watu wa familia**



Mali ya Serikali ya Kenya 24

## Ufahamu wa fonimu

Tutajifunza sauti **/a/**. Kwanza tutaitamka sauti hiyo. Baadaye nitataja maneno; neno moja baada ya jingine. Mtasema iwapo neno hilo linaanza kwa sauti hiyo.
**Ninafanya:** Sauti ni? **/a/**. Neno la kwanza ni **ama**. Neno hili linaanza kwa sauti **/a/**. Kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno la pili ni mama. Neno mama halianzi kwa sauti **/a/** kwa hivyo nitaonyesha kidole chini.
**Tunafanya:** Sasa tutatamka sauti pamoja **/a/**. Sauti ya hii ni? **/a/**. Sasa nitataja neno. Iwapo neno hilo linaanza kwa sauti **/a/**, tutaonyesha kidole juu. Iwapo halianzi kwa sauti **/a/**, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni ama. *Mwalimu na wanafunzi waonyeshe pamoja.*
*Endelea na neno* ***mama***.
**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Sauti ni **/a/**. Onyesha kidole juu iwapo neno linaanza kwa sauti **/a/**. Iwapo halianzi kwa sauti onyesha kidole chini. Neno la kwanza ni ama. *Wanafunzi waonyeshe kidole juu.*
*Tumia hatua ya tatu kufunza maneno haya:* **acha**, **angu**, **letu**, **apa**.

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya**: *Andika herufi ndogo* **'a'** *ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo kwenye mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi hii kwa kidole.*
Jina la herufi hii ni **'a'**. Sauti ni **/a/**.
**Tunafanya:** Sasa, tutataja jina la herufi pamoja. Je, jina la herufi hii ni? **'a'**. Sauti yake ni? **/a/**.
**Unafanya**: Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ni **'a'**. Sauti yake ni **/a/**.
Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 23.** Soma kila herufi na sauti husika.

## Kusoma silabi

Andika silabi **ma** ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi.
**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitatamka sauti kisha nisome silabi. Sauti hizi ni **/m//a/**. Nikiunganisha sauti zote mbili **/m//a/** silabi ni **ma**.
**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Sauti ni **/m/**, **/a/**. Silabi ni **ma.**
**Unafanya:** Sasa mtafanya peke yenu. Sauti ni **/m/**, **/a/**. Silabi ni gani? **ma**
*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi* **a**. *Soma silabi* kwenye **ukurasa wa 23.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

**Ubao/mfuko wa kadi za herufi**: Soma kila silabi kwa kila neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** ma ma - mama
**U:** mama, ama
**Kitabu cha mwanafunzi**: Katika vikundi vya wawili wawili wape wanafunzi nafasi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 23.**

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 23 na 24 **Familia 1**

**Kipindi 23**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **a** **m**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  m a → **ma** a → **a**

- Soma silabi na maneno.

  ma ma → **mama** a ma → **ama**

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi.

1. Mimi ninasoma.
2. Mimi ninaketi.
3. Mimi ninaandika.

**Kusoma hadithi**

**Asante**

Mama anasema, "Asante."
Mama anasema asante ama pole?



23 Hakiuzwi

Kipindi cha 23 na 24 **Familia 1**

**Kipindi 24**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **A** **a**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  m a → **ma** a → **a**

- Soma silabi na maneno.

  ma ma → **mama** a ma → **ama**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Jukumu la watu wa familia**



Mali ya Serikali ya Kenya 24

## Msamiati

*Andika neno ubaoni. Soma neno hilo. Waulize wanafunzi kuelezea maana ya neno. Iwapo wanafunzi hawajui maana ya neno hilo, waeleze. Tunga sentensi. Wanafunzi watumie neno hilo kutunga sentensi zitakazoonyesha maana ya neno.*

Maneno: **asante, pole, anasema**

## Kabla ya kusoma

**Tunafanya**: Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 23.** Tusome kichwa cha hadithi kwa pamoja. Hadithi hii inahusu **Asante.** Je, umewahi kusikia neno asante? *Jadili picha. Wanafunzi wawaeleze wanafunzi wenzao kile wanafikiri kitatokea* kwenye *hadithi. Chagua wanafunzi wawili au watatu wachangie utabiri.*

## Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** Mwalimu anasoma.

**Tunafanya:** Mwalimu anasoma hadithi pamoja na wanafunzi.

**Unafanya:** Wanafunzi wanasoma peke yao.

**Tunafanya:** Ulimweleza mwenzako kile kitatokea kwenye hadithi. Je, utabiri wako ulitimia?

## Maswali

**Ninafanya:** Mama alisema nini? (Mama alisema asante.)
**Tunafanya:** Wewe husemaje ukipewa zawadi? (Majibu ni kama vile asante na shukrani)

## Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na 'mimi' au 'ni'. Wakati uliopo huonyesha kitendo kinafanyika sasa hivi. Kwa mfano: Mimi ninasoma.

## Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi kwenye **ukurasa wa 23.**

## Kazi ya ziada

*Andika herufi* ***a*** *ndogo ubaoni kwa hati nadhifu kama ilivyoonyeshwa hapa. Waagize wanafunzi waandike* kwenye *madaftari yao.*

a a a a a a a a a a a

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 24: Familia 1

Kipindi cha 23 na 24 **Familia 1**

**Kipindi 23**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **a** **m**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  m a **ma** a **a**

- Soma silabi na maneno.

  ma ma **mama** a ma **ama**

**Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi.

1. Mimi ninasoma.
2. Mimi ninaketi.
3. Mimi ninaandika.

**Kusoma hadithi**

**Asante**

Mama anasema, "Asante."
Mama anasema asante ama pole?



23 Hakiluzwi

Kipindi cha 23 na 24 **Familia 1**

**Kipindi 24**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **A** **a**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  m a **ma** a **a**

- Soma silabi na maneno.

  ma ma **mama** a ma **ama**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Jukumu la watu wa familia**



Mali ya Serikali ya Kenya 24

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya**: *Andika herufi kubwa* **'A'** *ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo kwenye mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi hii kwa kidole.* Jina la herufi hii ni **'a'**. Sauti ni **/a/**.
**Tunafanya:** Sasa, tutamka jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni **a**. Sauti yake ni **/a/**.
**Unafanya**: Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ni **'a'**. Sauti yake ni **/a/**.
*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi* ***m***.
Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 24**. Soma kila herufi na sauti husika.

### Kusoma silabi

*Andika silabi* **ma** *ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi.*
**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitatamka sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni **/m//a/**. Naunganisha sauti zote mbili **/m//a/**. Silabi ni **ma**.
**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Nitatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni **/m/**, **/a/**. Silabi ni **ma**.
**Unafanya:** Sasa mtafanya peke yenu. Sauti ni **/m/**, **/a/**. Silabi ni gani? **ma**
*(Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi* **ma, a.***)* Waelekeze wasome silabi kwenye **ukurasa wa 24**.

### Kusoma maneno kutumia silabi

**Ubao/mfuko wa kadi za herufi:** Soma kila silabi kwa kila neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** ma ma - mama,
**U:** mama, ama
**Kitabu cha mwanafunzi:** *Katika vikundi vya wawili wawili wape wanafunzi nafasi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao* kwenye ***ukurasa wa 23***.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi.

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya**: Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 24**. Tusome kichwa cha hadithi kwa pamoja. Hadithi hii inahusu Jukumu la watu wa familia. Je, umewahi kusikia kuhusu watu wa familia? *Jadili picha. Wanafunzi wawaeleze wanafunzi wenzao kile wanafikiri kitatokea* kwenye *hadithi. Chagua wanafunzi wawili au watatu wachangie utabiri.*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 23 na 24 **Familia 1**

**Kipindi 23**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

a m

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

m a → ma a → a

- Soma silabi na maneno.

ma ma → mama a ma → ama

**Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi.

1. Mimi ninasoma.
2. Mimi ninaketi.
3. Mimi ninaandika.

**Kusoma hadithi**

**Asante**

Mama anasema, "Asante."
Mama anasema asante ama pole?



23 Hakiuzwi

Kipindi cha 23 na 24 **Familia 1**

**Kipindi 24**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

A a

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

m a → ma a → a

- Soma silabi na maneno.

ma ma → mama a ma → ama

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Jukumu la watu wa familia**



Mali ya Serikali ya Kenya 24

## Hadithi ya mwalimu

**Jukumu la watu wa familia**

Katika familia baba na mama ndio wasimamizi wa familia. Yeye huhakikisha familia yake inapata mahitaji muhimu. Mama na baba husaidiana kuhakikisha kuwa familia ina chakula. Pia wanashirikiana kuhakikisha usafi nyumbani.

Lakini mambo hubadilika maishani. Kama Mzee Mamboleo hivi majuzi alipata ajali. Majukumu aliyokuwa akitekeleza yakawa hayafanyiki. Ilimbidi mke wake kuyatekeleza majukumu hayo. Mkewe Mzee mamboleo aliomba usaidizi kutoka kwa kaka, dada na halati na jamaa zake wengine.

Kaka ni ndugu wa kiume. Dada naye ni ndugu wa kike. Dada na kaka husaidiana kwa kazi zote za nyumbani. Mjomba ni kaka wa mama. Halati ni dada wa mama. Wao hushirikiana katika familia.

*Mwalimu anasoma. Wanafunzi wanasikiliza hadithi huku wakiitazama picha husika. Waulize wanafunzi iwapo utabiri wao ulitimia.*

## Maswali

**N:** Zainabu ana kaka wangapi? (Zainabu ana kaka wawili).
**T:** Baba alienda kwa nani kutafuta ushauri? (Alienda kwa shangazi kutafuta ushauri.)
**U:** Je, familia yenu ina watu wangapi?

## Zoezi

Wanafunzi watambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi katika vikundi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atambue herufi inayowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi katika vikundi.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 25: Familia 1

Kipindi cha 25 **Familia 1**

**Kipindi 25**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

mM aA

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

m a → ma    a → a

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: a ma – ama**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma | a | ma | a |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Igiza vitendo katika sentensi hizi.

1. **Mimi** ni**na**andika.
2. **Mimi** ni**na**futa.
3. **Mimi** ni**na**keti.
4. **Mimi** ni**na**tembea.
5. **Mimi** ni**na**soma.
6. **Mimi** ni**na**pika.
7. **Mimi** ni**na**fua.
8. **Mimi** ni**na**nawa.

**Zoezi: Kuandika**

Andika herufi hii katika daftari lako.

m m m m m m m m m m m

25

Hakiluzwi

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya**: *Andika herufi* **mM** *(ndogo na kubwa), ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo* kwenye *mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi kwa kidole.*

Hii ni **m** ndogo na **M** kubwa. Sauti ni **/m/** kwa **m** ndogo na **M** kubwa.

**Tunafanya:** Sasa, tutataja jina la herufi pamoja. *Onyesha m.* Je, jina la herufi hii ni? **m** ndogo. *Onyesha* **M**. Je, jina la herufi hii ni? **M** kubwa.

**Unafanya**: Sasa jaribu peke yako. *Onyesha m.* Jina la herufi hii ni? **m** ndogo *Onyesha* **M**. Jina la herufi hii ni? **M** kubwa. Sauti yake ni **/m/**.

*Rudia hatua ya 1-3 kufunza herufi **a** na **A**.*

Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 25**. Soma kila herufi na kutamka sauti husika.

## Jedwali

**Ninafanya:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **a** na **ma** kuandika neno **ama**.

**Tunafanya:** Soma neno pamoja na wanafunzi.

**Unafanya:** *Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi* kwenye **ukurasa wa 25**.

## Kusoma maneno kutumia silabi

**Tunafanya:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **a** na **ma** kuandika neno **ama.**

Soma neno pamoja na wanafunzi.

**Unafanya:** *Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi* kwenye **ukurasa wa 25**.

## Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo.**

Rejelea matumizi ya nafsi ya kwanza.

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na 'mimi' au 'ni'.

Wakati uliopo huonyesha kitendo kinafanyika sasa hivi.

**Ninafanya:** Mwalimu aigize sentensi ya kwanza *(Mimi ninaandika.)*

**Tunafanya:** Mwalimu na wanafunzi waigize *(Mimi ninaandika.)*

## Zoezi

Wanafunzi waigize sentensi kwenye **ukurasa wa 25.**

## Kuandika

**Ninafanya**: Andika herufi **'m'** ubaoni.

**Tunafanya:** Andika herufi **'m'** ubaoni huku wanafunzi wakiandika kwenye madaftari yao.

**Unafanya:** Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 25.**

## Kazi ya ziada

Andika herufi **'m'** mara tano kwenye daftari lako kisha umsomee mlezi au mzazi wako sauti ya herufi hiyo.

## Kazi ya nyongeza

Ukienda nyumbani, muulize mzazi wako au mlezi wako akupeleke katika makao yawasiojiweza.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 26: Familia 1

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 26**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**u** **a** **m**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| m u | a | m a |
|---|---|---|
| **mu** | **a** | **ma** |

● Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | u ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **uma** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi hizi katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Mimi** ni**na**soma. | **Sisi** tu**na**soma. |
| 2. **Mimi** ni**na**keti. | **Sisi** tu**na**keti. |
| 3. **Mimi** ni**na**andika. | **Sisi** tu**na**andika. |

**Kusoma hadithi**

**Paka na maua**

Mama anaona uma na maua. Paka anaona maua. Paka ana uma maua.



Mali ya Serikali ya Kenya

26

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 27**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**U** **u**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| u u | m u | a a | m a |
|---|---|---|---|
| **uu** | **mu** | **aa** | **ma** |

● Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | a ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **ama** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sultan Suleiman**



27

Hakiuzwi

## Ufahamu wa fonimu

Tutajifunza sauti **/u/**. Kwanza tutaitamka sauti hiyo. Baadaye nitataja maneno; neno moja baada ya jingine. Mtasema iwapo neno hilo linaanza kwa sauti **/u/**.

**Ninafanya:** Sauti ni? **/u/**. Neno la kwanza ni **ukuta**. Neno hili linaanza kwa sauti **/u/** Kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno la pili ni **tatu**. Neno hili halianzi kwa sauti **/u/**. Kwa hivyo nitaonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Sasa tutamke sauti **/u/** pamoja

Sauti ni? **/u/**. Sasa nitataja neno. Iwapo neno hilo linaanza kwa sauti **/u/**, tutaonyesha kidole juu. Iwapo halianzi kwa sauti **/u/**, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni **ukuta**. *Mwalimu na mwanafunzi waonyeshe pamoja. Endelea na neno* **tatu**.

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Sauti ni **/u/**. Onyesha kidole juu iwapo neno linaanza kwa sauti **/u/**. Iwapo halianzi onyesha kidole chini. Neno la kwanza ni **ukuta**. *Wanafunzi waonyeshe kidole juu.*

*Tumia hatua ya tatu kufunza maneno haya:* **uma, kuku, ua, uki**.

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya**: *Andika herufi ndogo '**u**' ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo* kwenye *mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi hii kwa kidole.*

Jina la herufi hii ni 'u'. Sauti ni **/u/**.

**Tunafanya**: Sasa, tutataja jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni? **u**. Sauti yake ni? **/u/**.

**Unafanya**: Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ni? **u**. Sauti yake ni? **/u/**.

*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi **a**, **m**.*

Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 26**. Soma kila herufi na kutamka sauti husika.

## Kusoma silabi

*Andika silabi* **ma** *ubaoni au utumie mfuko wa kadi za silabi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitatamka sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni **/m//u/**. Naunganisha sauti zote mbili **/m//u/**. Silabi ni **mu**.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Nitatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni **/m/**, **/u/**. Silabi ni **mu**.

**Unafanya:** Sasa mtafanya peke yenu. Mtatamka sauti kisha mtamke silabi. Sauti ni **/m/**, **/u/**. Silabi ni gani? (**mu**).

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi* **ma**. *Waelekeze kusoma silabi* kwenye ***ukurasa wa 26***.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 26**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**u** **a** **m**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| m u | a | m a |
|---|---|---|
| **mu** | **a** | **ma** |

● Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | u ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **uma** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi hizi katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Mimi** ni**na**soma. | **Sisi** tu**na**soma. |
| 2. **Mimi** ni**na**keti. | **Sisi** tu**na**keti. |
| 3. **Mimi** ni**na**andika. | **Sisi** tu**na**andika. |

**Kusoma hadithi**

**Paka na maua**

Mama anaona uma na maua. Paka anaona maua. Paka ana uma maua.



Mali ya Serikali ya Kenya

26

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 27**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**U** **u**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| u u | m u | a a | m a |
|---|---|---|---|
| **uu** | **mu** | **aa** | **ma** |

● Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | a ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **ama** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sultan Suleiman**



27

Hakiuzwi

### Kusoma maneno kutumia silabi

**Ubao/mfuko wa kadi za herufi**: Soma kila silabi kwa kila neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**Ninafanya/Tunafanya/Unafanya:** ma ma - mama
**Unafanya:** mama, ama, uma
**Kitabu cha mwanafunzi**: Katika vikundi vya wawili wawili wape wanafunzi nafasi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 26.**

### Msamiati

*Andika neno ubaoni:* ***uma***
**Tunafanya:** *Soma neno hilo. Waelekeze wanafunzi waeleze maana ya neno. Iwapo wanafunzi hawataweza kuelezea maana ya neno hilo, waeleze maana ya neno. Tunga sentensi. Wanafunzi watumie neno hilo kutunga sentensi zitakazoonyesha maana ya neno.*
*Rudia na neno* **maua.**
*Waongoze wanafunzi kusoma maneno katika kitabu cha wanafunzi* kwenye **ukurasa wa 26.**

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya**: Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 26.** Tusome kichwa cha hadithi kwa pamoja. Hadithi hii inahusu paka na maua. Je, umewahi sikia kuhusu paka au ua? Je ulifanya nini? *Jadili picha. Wanafunzi wawaeleze wenzao kile wanafikiri kitatokea* kwenye *hadithi. Chagua wanafunzi wawili au watatu wachangie utabiri.*

### Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** *Mwalimu anasoma hadithi peke yake.*
**Tunafanya:** *Mwalimu anasoma na wanafunzi.*
**Unafanya:** *Wanafunzi wanasoma peke yao.*

### Baada ya kusoma

Je, utabiri wako ulitimia?

### Maswali

**Ninafanya**: Taja kitu ambacho mama anakiona. *Uma*
**Tunafanya**: Taja kitu kingine ambacho mama anakiona. maua
**Unafanya**: Je, paka anaona nini? *maua*

### Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**
Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na 'mimi' au 'ni'. Wakati uliopo huonyesha kitendo kinafanyika sasa hivi. Kwa mfano: Mimi ninaimba.

### Zoezi

*Wanafunzi wasome vifungu vya maneno* kwenye **ukurasa wa 26.**

### Kazi ya ziada

Andika herufi 'u' mara tano kwenye daftari lako kisha umsomee mlezi au mzazi wako sauti ya herufi hiyo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 27: Familia 1

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 26**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

u a m

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| m u | a | m a |
|---|---|---|
| **mu** | **a** | **ma** |

● Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | u ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **uma** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi hizi katika umoja na wingi.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | **Mimi** nina**soma**. | **Sisi** tuna**soma**. |
| 2. | **Mimi** nina**keti**. | **Sisi** tuna**keti**. |
| 3. | **Mimi** nina**andika**. | **Sisi** tuna**andika**. |

**Kusoma hadithi**

**Paka na maua**

Mama anaona uma na maua. Paka anaona maua. Paka ana uma maua.



Mali ya Serikali ya Kenya

26

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 27**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

U u

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| u u | m u | a a | m a |
|---|---|---|---|
| **uu** | **mu** | **aa** | **ma** |

● Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | a ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **ama** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sultan Suleiman**



27

Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

**Ninafanya**: *Andika herufi kubwa* **'U'** *ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo* kwenye *mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi kwa kidole.*

**Ninafanya:** Jina la herufi hii ni **'U'** kubwa. Sauti ni **/u/**.

**Tunafanya**: Sasa, tutamke jina la herufi pamoja. Jina la herufi hii ni **'U'** kubwa. Sauti yake ni **/u/**.

**Unafanya**: Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ni? **'U'** kubwa. Sauti yake ni **/u/**.

*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi* **a**.

Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 27.** Soma kila herufi na sauti husika.

## ● Kusoma silabi

*Andika silabi* **uu** *ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitataja sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni **/u/ /u/**. Naunganisha sauti zote mbili **/u//u/**. Silabi ni uu.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Tutatamka sauti kisha tutamke silabi pamoja. Sauti ni **/u/**, **/u/**. Silabi ni uu.

**Unafanya:** Sasa mtafanya peke yenu. Mtatamka sauti kisha mtamke silabi. Sauti ni? **/u/**, **/u/**. Silabi ni gani? uu

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi* **mu, a, ma**.

Soma silabi kwenye **ukurasa wa 27.**

## ★ Kusoma maneno kutumia silabi

**Ubao/mfuko wa kadi za herufi**: Soma kila silabi kwa kila neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**Ninafanya/Tunafanya/Unafanya:** ma ma - mama, ma u a - maua

**Unafanya:** maua, ua, uma.

**Kitabu cha mwanafunzi**: Katika vikundi vya wawili wawili wape wanafunzi nafasi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 27.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**Unafanya:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 26.**

## Msamiati

**Ninafanya :** *Andika neno ubaoni:* ***mapacha***

**Tunafanya:** *Soma neno hilo. Waelekeze wanafunzi waeleze maana ya neno. Iwapo wanafunzi hawataweza kuelezea maana ya neno hilo, waeleze maana ya neno. Tunga sentensi. Wanafunzi watumie neno hilo kutunga sentensi zitakazoonyesha maana ya neno.*

*Rudia na neno* **binamu, mke wake, mapacha.**

## Kabla ya kusoma

**Tunafanya**: Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 27.** Tusome kichwa cha hadithi kwa pamoja. Hadithi hii inahusu Sultan Suleiman. Je, unajua sultan ni nani? *Jadili picha. Wanafunzi wawaeleze wanafunzi wenzao kile wanafikiri kitatokea* kwenye *hadithi. Chagua wanafunzi wawili au watatu wachangie utabiri.*

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 26**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

u a m

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

m u → **mu**  a → **a**  m a → **ma**

- Soma silabi na maneno.

ma ma → **mama**  ma u a → **maua**  u a → **ua**  u ma → **uma**

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi hizi katika umoja na wingi.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | **Mimi** ni**na**soma. | **Sisi** tu**na**soma. |
| 2. | **Mimi** ni**na**keti. | **Sisi** tu**na**keti. |
| 3. | **Mimi** ni**na**andika. | **Sisi** tu**na**andika. |

**Kusoma hadithi**

**Paka na maua**

Mama anaona uma na maua. Paka anaona maua. Paka ana uma maua.



Mali ya Serikali ya Kenya

26

Kipindi cha 26 na 27 **Familia 1**

**Kipindi 27**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

U u

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

u u → **uu**  m u → **mu**  a a → **aa**  m a → **ma**

- Soma silabi na maneno.

ma ma → **mama**  ma u a → **maua**  u a → **ua**  a ma → **ama**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sultan Suleiman**



27

Hakiluzwi

### Hadithi ya mwalimu

**Sultani Suleiman**

Katika makazi yake Sultani, waliishi Sultani Suleiman, mke wake na binti wao wa pekee Neema. Neema alikuwa mwenye heshima. Sultani Suleiman na mke wake walikawia miaka kumi kabla ya kupata mtoto mwingine. Walimuomba Mungu awajalie na watoto wengine. Hawakukosa msikitini kila Ijumaa. Kweli maombi yao yalijibiwa. Mke wake Sultani alijifungua pacha, mvulana na msichana.

Sultani Suleiman na mkewe walifurahi na kusema, "Kweli kazi ya Mungu haina makosa. Maombi yetu yamejibiwa."

Mwalimu anasoma. Wanafunzi wanasikiliza hadithi huku wakiitazama picha husika. Waulize wanafunzi iwapo utabiri wao ulitimia.

Waulize wanafunzi iwapo utabiri wao ulitimia.

### Maswali

**Ninafanya:** Nani waliishi katika makazi ya Sultani Suleiman?

(Makazi ya Sultani Suleiman waliishi Sultan Suleiman, mke wake na binti wao Neema.)

**Tunafanya:** Kwa nini familia ya Sultan Suleiman walifurahi?

(Walijaliwa kupata pacha – mvulana na msichana.)

**Unafanya:** Unafikiri maombi ni muhimu? (Toa sababu, wanafunzi waeleze majibu yao.)

### Zoezi

*Mwanafunzi ahusishwe katika mjadala kuhusu umuhimu wa kutumia maneno ya heshima.*

### Kazi ya ziada

*Mwanafunzi afinyange maumbo ya herufi alizosoma darasani hadi sasa: m, a, u. Hakikisha maumbo ni ya herufi kubwa na ndogo.*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 28: Familia 1

Kipindi cha 28 na 29 **Familia 1**

**Kipindi 28**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**k** **m** **a** **u**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| k a | k u | a | u |
|---|---|---|---|
| **ka** | **ku** | **a** | **u** |

- Soma silabi na maneno.

| ku ku | u ku ta | ka a | ku u |
|---|---|---|---|
| **kuku** | **ukuta** | **kaa** | **kuu** |

♦ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma katika umoja na wingi.

1. **Nina**cheza. **Tuna**cheza.
2. **Nina**futa. **Tuna**futa.
3. **Nina**pika. **Tuna**pika.

**Kusoma hadithi**

**Kaka ajikwaa**

Rafiki Paka akaamua kukaa. Mama akaamua kukaa. Kaka akaamua kukaa.

Kaka akajikwaa. Mama akasema, "Pole." Kaka akasema, "Asante mama."



Mali ya Serikali ya Kenya

28

Kipindi cha 28 na 29 **Familia 1**

**Kipindi 29**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**K** **k**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| k a | k u | m u | m a |
|---|---|---|---|
| **ka** | **ku** | **mu** | **ma** |

- Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | a ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **ama** |

- Soma sehemu ya neno na neno zima.

| a ka amua | a ka ji kwaa | ku kaa |
|---|---|---|
| **akaamua** | **akajikwaa** | **kukaa** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Babu Limika**



29 Hakiuzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tutajifunza sauti **/k/**. Kwanza tutaitamka sauti hiyo. Baadaye nitatamka maneno; neno moja baada ya jingine. Mtasema iwapo neno hilo linaanza kwa sauti hiyo.

**Ninafanya:** Sauti ni? **/k/**. Neno la kwanza ni **kaka**. Neno hili linaanza kwa sauti **/k/,** kwa hivyo nitaonyesha kidole juu. Neno la pili ni **mama**. Neno hili halianzi kwa sauti **/k/,** kwa hivyo nitaonyesha kidole chini.

**Tunafanya:** Sasa tutatamka sauti **/k/** pamoja. Sauti hii ni? **/k/**. Sasa nitataja neno. Iwapo neno hilo linaanza kwa sauti **/k/**, tutaonyesha kidole juu. Iwapo halianzi kwa sauti **/k/**, tutaonyesha kidole chini. Neno la kwanza ni **kaka**. *Mwalimu na wanafunzi waonyeshe pamoja.*

*Endelea na neno* **mama.**

**Unafanya:** Ni zamu yenu sasa. Sauti ni **/k/**. Onyesha kidole juu iwapo neno linaanza kwa sauti **/k/**. Iwapo halianzi onyesha kidole chini. Neno la kwanza ni **kaka**. *Wanafunzi waonyeshe kidole juu.*

*Tumia hatua ya tatu kufunza maneno haya:* **kuku, tatu, kama, ukuta**.

### Ufahamu wa herufi

**Ninafanya**: *Andika herufi 'k' ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo* kwenye *mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi hii na kusema sauti lengwa.*

Jina la herufi hii ni **'k'**. Sauti ni **/k/**.

**Tunafanya**: Sasa, tutatamka jina la herufi pamoja. Je, jina la herufi hii ni? **'k'**. Sauti yake ni **/k/**.

**Unafanya**: Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ni **'k'**. Sauti yake ni **/k/**.

*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi* **m, a, u**.

Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 28**. Soma kila herufi na kutamka sauti husika.

### Kusoma silabi

*Andika silabi ka ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitatamka sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni **/k//a/**. Naunganisha sauti zote mbili **/k//a/**. Silabi ni **ka**.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Nitatamka sauti kisha tutataja silabi pamoja. Sauti ni **/k/**, **/a/**. Silabi ni **ka**.

**Unafanya:** Sasa mtafanya peke yenu. Mtatamka sauti kisha mtatamka silabi. Sauti ni? **/k/**, **/a/**. Silabi ni gani? **ka**.

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi* ***ku, a, u***.

Soma silabi kwenye **ukurasa wa 28.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

**Ubao/mfuko wa kadi za herufi**: *Soma kila silabi kwa kila neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.*

**Ninafanya/Tunafanya/Unafanya:** ku ku - kuku

**Unafanya:** ukuta, kaka, kaa, mkuu

**Kitabu cha mwanafunzi**: Katika vikundi vya wawili wawili wape wanafunzi nafasi wasomeane maneno waliyojifunza

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 28 na 29 **Familia 1**

**Kipindi 28**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**k** **m** **a** **u**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

k a — **ka**; k u — **ku**; a — **a**; u — **u**

- Soma silabi na maneno.

ku ku — **kuku**; u ku ta — **ukuta**; ka a — **kaa**; ku u — **kuu**

- **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma katika umoja na wingi.

1. **Nina**cheza. **Tuna**cheza.
2. **Nina**futa. **Tuna**futa.
3. **Nina**pika. **Tuna**pika.

**Kusoma hadithi**

**Kaka ajikwaa**

Rafiki Paka akaamua kukaa. Mama akaamua kukaa. Kaka akaamua kukaa.

Kaka akajikwaa. Mama akasema, "Pole." Kaka akasema, "Asante mama."



Mali ya Serikali ya Kenya

28

Kipindi cha 28 na 29 **Familia 1**

**Kipindi 29**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**K** **k**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

k a — **ka**; k u — **ku**; m u — **mu**; m a — **ma**

- Soma silabi na maneno.

ma ma — **mama**; ma u a — **maua**; u a — **ua**; a ma — **ama**

- Soma sehemu ya neno na neno zima.

a ka amua — **akaamua**; a ka ji kwaa — **akajikwaa**; ku kaa — **kukaa**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Babu Limika**



29

Hakiuzwi

vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 28.**

### Msamiati

**Ninafanya:** *Andika neno ubaoni:* **akaamua**

**Tunafanya:** *Soma neno hilo. Waelekeze wanafunzi waeleze maana ya neno. Iwapo wanafunzi hawataweza kuelezea maana ya neno hilo, waeleze maana ya neno. Tunga sentensi. Wanafunzi watumie neno hilo kutunga sentensi zitakazoonyesha maana ya neno.*

*Rudia na maneno* **akajikwaa, kukaa.**

*Waongoze wanafunzi kusoma maneno katika kitabu cha wanafunzi* kwenye **ukurasa wa 28.**

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya**: Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 28.** Tusome kichwa cha hadithi kwa pamoja. Sema: Hadithi hii inamhusu **Kaka ajikwaa.** Je, umewahi kusikia kuhusu kaka? Jadili picha. Mwanafunzi awaeleze mwanafunzi mwenzake kile anafikiri kitatokea kwenye hadithi. Chagua wanafunzi wawili au watatu wachangie utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**Ninafanya:** Mwalimu anasoma.

**Tunafanya:** Mwalimu anasoma hadithi pamoja na wanafunzi.

**Unafanya:** Wanafunzi wanasoma peke yao.

Ulimweleza mwenzako kile kitatokea kwenye hadithi. Je, utabiri wako ulitimia?

### Maswali

**Ninafanya:** Taja watu wawili walioamua kukaa. (rafiki, paka, kaka na mama)

**Tunafanya**: Nani alijikwaa? (kaka)

**Unafanya:** Je, nani alisema, "Pole?" (mama)

### Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na 'mimi' au 'ni'. Wakati uliopo huonyesha kitendo kinafanyika sasa hivi. Kwa mfano: Mimi ninaandika.

### Zoezi

*Wanafunzi wasome maneno* kwenye **ukurasa wa 28.**

### Kazi ya ziada

*Mwanafunzi anakili maneno haya na asomee mlezi wake.*

1. Ninacheza
2. Ninafuta
3. Ninapika

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 28 na 29 — **Familia 1**

**Kipindi 28**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**k** **m** **a** **u**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| k a | k u | a | u |
|---|---|---|---|
| **ka** | **ku** | **a** | **u** |

● Soma silabi na maneno.

| ku ku | u ku ta | ka a | ku u |
|---|---|---|---|
| **kuku** | **ukuta** | **kaa** | **kuu** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma katika umoja na wingi.

1. **Nina**cheza. **Tuna**cheza.
2. **Nina**futa. **Tuna**futa.
3. **Nina**pika. **Tuna**pika.

**Kusoma hadithi**

**Kaka ajikwaa**

Rafiki Paka akaamua kukaa. Mama akaamua kukaa. Kaka akaamua kukaa.

Kaka akajikwaa. Mama akasema, "Pole." Kaka akasema, "Asante mama."



Mali ya Serikali ya Kenya

28

Kipindi cha 28 na 29 — **Familia 1**

**Kipindi 29**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**K** **k**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| k a | k u | m u | m a |
|---|---|---|---|
| **ka** | **ku** | **mu** | **ma** |

● Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | a ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **ama** |

▬ Soma sehemu ya neno na neno zima.

| a ka amua | a ka ji kwaa | ku kaa |
|---|---|---|
| **akaamua** | **akajikwaa** | **kukaa** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Babu Limika**



29

Hakiuzwi

### ■ Ufahamu wa herufi

**Ninafanya**: *Andika herufi kubwa **'K'** ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo* kwenye *mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi hii kwa kidole.*

Jina la herufi hii ni **'K'**. Sauti ni **/k/**.

**Tunafanya:** Sasa, tutataja jina la herufi pamoja. Je, jina la herufi hii ni **'K'**. Sauti yake ni **/k/**.

**Unafanya**: Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ni **'K'**. Sauti yake ni **/k/**.

*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi* **m, a, u**.

Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 29.** Soma kila herufi na sauti husika.

### ● Kusoma silabi

*Andika silabi **ka** ubaoni au utumie mfuko wa kadi za herufi.*

**Ninafanya:** Leo tutaunda silabi kwa kuunganisha sauti. Nitataja sauti kisha nitamke silabi. Sauti hizi ni **/k//a/**. Naunganisha sauti zote mbili **/k//a/**. Silabi ni **ka**.

**Tunafanya:** Tufanye pamoja. Nitatamka sauti kisha tutatamka silabi pamoja. Sauti ni **/k/**, **/a/**. Silabi ni **ka**.

**Unafanya:** Sasa mtafanya peke yenu. Mtatamka sauti kisha mtatamka silabi. Sauti ni? **/k/**, **/a/**. Silabi ni gani? **ka**

*Rudia hatua 1-3 kwa kutumia silabi* **ku, ma, mu**. Soma silabi kwenye **ukurasa wa 29**.

### ★ Kusoma maneno kutumia silabi

**Ubao/mfuko wa kadi za herufi**: *Tamka kila silabi kwa kila neno. Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.*

**Ninafanya/Tunafanya/Unafanya:** ma ma - mama

**Unafanya:** maua, ua, ama

**Kitabu cha mwanafunzi**: Kwa vikundi vya wawili wawili wape wanafunzi nafasi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 29.**

### ▬ Kusoma maneno marefu

Soma kila sehemu ya neno. Soma neno lote upesi.

**N/T/U:** a ka amua - akaamua

**U:** akajikwaa, kukaa

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 29.**

### Wakati wa kusoma

**Unafanya:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 28.**

### Msamiati

**Ninafanya:** *Andika neno ubaoni:* ***shangazi***

**Tunafanya:** *Soma neno hilo. Waelekeze wanafunzi waeleze maana ya neno hilo. Iwapo wanafunzi hawataweza kuelezea maana ya neno hilo, waeleze maana ya neno. Tunga sentensi. Wanafunzi watumie neno hilo kutunga sentensi zitakazoonyesha maana ya neno.*

*Rudia na neno* **babu.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 28 na 29 **Familia 1**

**Kipindi 28**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**k** **m** **a** **u**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| k a | k u | a | u |
|---|---|---|---|
| **ka** | **ku** | **a** | **u** |

- Soma silabi na maneno.

| ku ku | u ku ta | ka a | ku u |
|---|---|---|---|
| **kuku** | **ukuta** | **kaa** | **kuu** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma katika umoja na wingi.

1. **Nina**cheza. **Tuna**cheza.
2. **Nina**futa. **Tuna**futa.
3. **Nina**pika. **Tuna**pika.

**Kusoma hadithi**

**Kaka ajikwaa**

Rafiki Paka akaamua kukaa. Mama akaamua kukaa. Kaka akaamua kukaa.

Kaka akajikwaa. Mama akasema, "Pole." Kaka akasema, "Asante mama."



Mali ya Serikali ya Kenya 28

Kipindi cha 28 na 29 **Familia 1**

**Kipindi 29**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**K** **k**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| k a | k u | m u | m a |
|---|---|---|---|
| **ka** | **ku** | **mu** | **ma** |

- Soma silabi na maneno.

| ma ma | ma u a | u a | a ma |
|---|---|---|---|
| **mama** | **maua** | **ua** | **ama** |

- Soma sehemu ya neno na neno zima.

| a ka amua | a ka ji kwaa | ku kaa |
|---|---|---|
| **akaamua** | **akajikwaa** | **kukaa** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Babu Limika**



29 Hakiuzwi

### Kabla ya kusoma

**Tunafanya**: Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 29.** Tusome kichwa cha hadithi kwa pamoja. Hadithi hii inahusu Babu Limika. Je, babu yako anaitwaje? *Jadili picha. Wanafunzi wawaeleze wanafunzi wenzao kile wanafikiri kitatokea* kwenye *hadithi. Chagua wanafunzi wawili au watatu wachangie utabiri.*

### Hadithi ya mwalimu

**Hadithi ya Babu Limika**

Mimi na dada zangu tulimtembelea Babu Limika wakati wa likizo ya Desemba. Alitusimulia hadithi baada ya chakula cha jioni. Babu alisema, "Palikuwa na kijana moja aliyeitwa Abunuasi. Alikuwa na tabia ya kutoka nyumbani bila kujulisha wazazi wake. Siku moja, Abunuasi alimtembelea shangazi wake. Safari ilikuwa ndefu. Alipofika kwenye msitu, alijawa na hofu. Punde, jitu lilitokezea. Jitu lilitabasamu likiimba, 'Kitoweo, kitoweo, nimepata!' Abunuasi alifanikiwa kutoroka. Alikutana na mchungaji mmoja aliyempeleka kwa shangazi yake" Babu alimaliza kwa kusema, "Ni vyema kuomba ruhusa au kuwaarifu walezi wetu kabla ya kwenda popote."

Mwalimu anasoma. Wanafunzi wanasikiliza hadithi huku wakiitazama picha husika.

Waulize wanafunzi iwapo utabiri wao ulitimia.

### Maswali

**Ninafanya/Tunafanya/Unafanya:** Hadithi ya babu ilisimuliwa wakati gani?

(Hadithi ya babu ilisimuliwa baada ya kula chakula cha jioni.)

**Tunafanya:** Abunuasi alifunga safari bila kuaga akaelekea wapi?

(Abunuasi alienda kumtembelea shangazi.)

**Unafanya:** Hadithi ya Babu Limika inakufunza nini?

(Majibu ni kama: kuwa mtiifu, kuomba ruhusa unapotaka kutoka nyumbani, kutembea na watu wazima.)

### Zoezi


*Mwanafunzi ahusishwe katika mjadala kuhusu umuhimu wa kutumia maneno ya heshima: asante, pole, tafadhali, samahani, n.k.*

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi anakili maneno yafuatayo ya heshima, kisha amsomee mlezi wake: *asante, pole, tafadhali, samahani, nashukuru.*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 30: Familia 1



Kipindi cha 30 **Familia 1**

**Kipindi 30**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

uU kK

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ma ka a - makaa**

| | | |
|---|---|---|
| ma | ka | u |
| mu | ku | a |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Igiza vitendo katika vikundi.

1. **Mimi** nin**a**andika.
   **Sisi** tun**a**andika.
2. **Mimi** nin**a**tembea.
   **Sisi** tun**a**tembea.
3. **Mimi** nin**a**soma.
   **Sisi** tun**a**soma.
4. **Mimi** nin**a**fua.
   **Sisi** tun**a**fua.
5. **Mimi** nin**a**lala.
   **Sisi** tun**a**lala.

**Zoezi: Kuandika**

Andika herufi hii kwenye daftari lako.

a a a a a a a a a a

Mali ya Serikali ya Kenya 30

## Ufahamu wa herufi

**Ninafanya**: *Andika herufi* **u** *ubaoni au weka kadi ya herufi hiyo* kwenye *mfuko wa kadi za herufi. Ionyeshe herufi hii kwa kidole*.

Jina la herufi hii ni **u** ndogo na **U** kubwa. Sauti ni **/u/**.

**Tunafanya:** Sasa, tutatamka jina la herufi pamoja. Je, jina la herufi hii ni? **u**. Sauti yake ni **/u/**.

**Unafanya**: Sasa jaribu peke yako. Jina la herufi hii ndogo ni? **u** Sauti yake ni **/u/**.

*Rudia hatua ya 1-3 kwa kutumia herufi **U, K, k.***

Fungueni vitabu vyenu kwenye **ukurasa wa 30**. Soma kila herufi na kutamka sauti husika.

## Jedwali la silabi

**Ninafanya:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ma ka a** kuandika neno **makaa**.

**Tunafanya:** Soma neno pamoja na wanafunzi.

**Unafanya:** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 30.**

## Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Rejelea matumizi ya nafsi ya kwanza.

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na 'mimi' au 'ni'.

Wakati uliopo huonyesha kitendo kinafanyika sasa hivi.

**Ninafanya:** Igiza kitendo 'tunaandika'.

**Tunafanya:** Igiza kitendo 'tunaandika' pamoja na wanafunzi.

**Unafanya:** Wanafunzi waigize vitendo kwenye **ukurasa wa 30** katika vikundi.

## Zoezi

Mwanafunzi atambue herufi inayowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi: u, U , k, K

## Kuandika

**Ninafanya:** Andika herufi 'a' ubaoni.

**Tunafanya:** Andika herufi 'a' ubaoni huku wanafunzi wakiandika kwenye madaftari yao.

**Unafanya:** Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 30.**

## Kazi ya ziada

Tumia maneno haya kutunga sentensi.

1. binamu
2. shangazi

## Kazi ya nyongeza

Mweleze mwenzako umuhimu wa watu wa familia yako: baba, mama, kaka, dada n. k.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________



Hakiuzwi

Kipindi cha 31 na 32 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 31**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

t k u

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

t a → ta   k a → ka   t u → tu   k u → ku

- Soma silabi na maneno.

ta ka ta ka → **takataka**   a ta ka → **ataka**

a ka ta ka → **akataka**   a mu → **amu**

**Sarufi: Umoja na wingi**

Soma vifungu hivi kuhusu sehemu za mwili katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mguu wangu. | 1. Miguu yetu. |
| 2. Mkono wangu. | 2. Mikono yetu. |
| 3. Kichwa changu. | 3. Vichwa vyetu. |

**Kusoma hadithi**

**Paka na kaa**

Kaka anasema, "Naona paka na takataka."
Mama anasema, "Naona paka, takataka na makaa."



31 Hakiuzwi

Kipindi cha 31 na 32 **Mwili wangu 1**

Amu anasema, "Naona paka, takataka, makaa na kaa." Paka anaona kaka, mama na amu. Anaona takataka, makaa na kaa. Kaa anataka kumuuma amu. Paka anaamua kumuua kaa.

**Kipindi 32**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

T t

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

t u → tu   t a → ta   m u → mu   k u → ku

- Soma sehemu za neno na neno lote.

ku mu ua → **kumuua**   a na taka → **anataka**

ku mu uma → **kumuuma**   a na amua → **anaamua**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Tuchunge miili yetu**



Mali ya Serikali ya Kenya 32

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/t/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.
**N/T/U:** taka, mama
**U:** taa, takataka, amu, tamu

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **t** na utamke sauti yake.
**U:** Endelea na herufi **k** na **u**.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 31.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti ili kusoma silabi.
**N/T/U:** /t/ /a/ ta
**U:** Endelea na tu, ka, ku
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 31.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** ta ka ta ka - takataka
**U:** ataka, akataka
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 31.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **takataka, amu, kaa**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Taja watu walio kwenye hadithi hii. (Kaka na amu, mama)
**T**: Taja vitu vitatu ambavyo amu anaona. (Paka, takataka, makaa)
**U:** Nani aliamua kumuua kaa? (Paka)

### Sarufi

**Umoja na Wingi**
Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika, kwa mfano: **M**guu - **Mi**guu
Soma sentensi kuhusu sehemu za mwili kwenye **ukurasa wa 31.**

### Kazi ya ziada

Tunga sentensi katika umoja na wingi ukitumia sehemu za mwili.

1. kichwa   2. kidole   3. mkono

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 32: Mwili wangu 1

Kipindi cha 31 na 32 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 31**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**t** **k** **u**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| t a | k a | t u | k u |
|---|---|---|---|
| **ta** | **ka** | **tu** | **ku** |

● Soma silabi na maneno.

ta ka ta ka
**takataka**

a ta ka
**ataka**

a ka ta ka
**akataka**

a mu
**amu**

◆ **Sarufi: Umoja na wingi**

Soma vifungu hivi kuhusu sehemu za mwili katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mguu wangu. | 1. Miguu yetu. |
| 2. Mkono wangu. | 2. Mikono yetu. |
| 3. Kichwa changu. | 3. Vichwa vyetu. |

**Kusoma hadithi**

**Paka na kaa**

Kaka anasema, "Naona paka na takataka."
Mama anasema, "Naona paka, takataka na makaa."



31 Hakiuzwi

Kipindi cha 31 na 32 **Mwili wangu 1**

Amu anasema, "Naona paka, takataka, makaa na kaa." Paka anaona kaka, mama na amu. Anaona takataka, makaa na kaa. Kaa anataka kumuuma amu. Paka anaamua kumuua kaa.

**Kipindi 32**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**T** **t**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| t u | t a | m u | k u |
|---|---|---|---|
| **tu** | **ta** | **mu** | **ku** |

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

ku mu ua
**kumuua**

a na taka
**anataka**

ku mu uma
**kumuuma**

a na amua
**anaamua**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Tuchunge miili yetu**



Mali ya Serikali ya Kenya 32

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi T na utamke sauti yake.
**N/T/U:** T
**U:** Endelea na herufi t
Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti yake kwenye **ukurasa wa 32.**

### ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na kusoma silabi.
**N/T/U:** /t/ /u/ silabi ni tu
**U:** Endelea na ta, mu, ku
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 32.**

### ▬ Kusoma maneno marefu

Soma kila sehemu ya neno. Soma neno lote upesi.
**N/T/U:** ku mu ua - kumuua
**U:** anataka, kumuuma, anaamua
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 32.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 31.**

### Hadithi ya mwalimu

**Tuchunge miili yetu**
Mwalimu wangu anaitwa Hana. Ninampenda kwa sababu yeye huzingatia usafi. Kila siku ya Jumatatu tukiwa gwaride yeye hutukagua ili kuhakikisha kila mwanafunzi ni safi.
Wiki iliyopita, Mwalimu Hana alitukagua vichwa, kucha na miguu. Wanafunzi wengi walikuwa na kucha chafu. Mwalimu Hana alitushauri tukate kucha. Alisema kucha ndefu na chafu huleta maradhi. Alisisitiza pia tuchane nywele vizuri. Alitushauri tuoge kila siku na kusugua meno baada ya kula. Hii inazuia mdomo kunuka na meno kuoza.

Funza maana ya maneno mapya: **kucha, meno.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi wanafunzi wasikize huku wakitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Kwa nini mwanafunzi alimpenda Mwalimu Hana?
*(Yeye huzingatia usafi /Wanafunzi walimpenda mwalimu wao kwa sababu aliwakumbusha kuwa safi.)*
**T:** Ni kwa nini tusugue meno baada ya kula?
*(Kuzuia mdomo kunuka na meno kuoza)*
**U:** Unatunza vipi mwili wako? *(Mwalimu azingatie kwa makini maelezo ya wanafunzi na kukubali majibu sahihi.)*

### Zoezi

Wanafunzi wafafanue maana ya msamiati wa sehemu za mwili.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi wachore baadhi ya sehemu za mwili za nje.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 33: Mwili wangu 1

Kipindi cha 33 na 34 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 33**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**i** **t** **k**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

t i → **ti** m i → **mi** k i → **ki** i → **i**

● Soma silabi na maneno.

ti ki ti → **tikiti** ki ma → **kima** m ku u → **mkuu** ma ka a → **makaa**

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **J**icho linaona. | 1. **Ma**cho yanaona. |
| 2. **Ki**fua kinauma. | 2. **Vi**fua vinauma. |
| 3. **U**kucha unakatwa. | 3. **Ku**cha zinakatwa. |

**Kusoma hadithi**

**Mama na Kima Mkuu**

**Mama:** Nina, naona Kima Mkuu, tikiti na uki.
**Kima Mkuu:** Rafiki.
**Mama:** Kima Mkuu, uma tikiti.



33 Hakiuzwi

Kipindi cha 33 na 34 **Mwili wangu 1**

**Kima Mkuu:** Sitaki!
**Nina:** Unakataa tikiti tamu?
**Kima Mkuu:** Uki!
**Mama:** Uki mtamu. Tikiti tamu.
**Kima Mkuu:** (Anauma tikiti) Tamu!

**Kipindi 34**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**I** **i**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

t i → **ti** k i → **ki** m i → **mi** i → **i**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

u na kataa → **unakataa** a na uma → **anauma**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Majivuno ya kichwa**



Mali ya Serikali ya Kenya 34

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/i/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ita, kiti

**U:** inuka, kima, tikiti, itika

## Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **i** na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi t na k.

**U:** Mwanafunzi ataje majina ya herufi na kutamka sauti zake kwenye **ukurasa wa 33.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na kusoma silabi.

**N/T/U:** /t/ /i/ silabi ni ti

**U:** Endelea na silabi mi, ki, i

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 33.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila sehemu ya neno. Soma neno lote upesi.

**N/T/U:** ti ki ti - tikiti

**U:** Endelea na kima, mkuu, makaa

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 33.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kima, mkuu, tikiti, uki**

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Wakati wa kusoma

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Mama alisema nini? *(Anamwambia Kima Mkuu aume tikiti.)*

**T:** Kima Mkuu aliita nani rafiki? *(Mama)*

**U:** Rafiki yako anaitwa nani? *(Wanafunzi wataje marafiki wao.)*

## Sarufi

**Umoja na Wingi**

Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika, kwa mfano: **Mkono - Mikono**

## Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi kwenye **ukurasa wa 33.**

## Kazi ya ziada

Andika wingi au umoja wa sentensi hizi.

1. Mguu umeumia. ____________________.
2. ____________________. Mikono ni safi.
3. Mkono umechafuka. ____________________.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 34: Mwili wangu 1

Kipindi cha 33 na 34 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 33**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**i** **t** **k**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

t i → **ti** m i → **mi** k i → **ki** i → **i**

● Soma silabi na maneno.

ti ki ti → **tikiti** ki ma → **kima** m ku u → **mkuu** ma ka a → **makaa**

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **J**icho linaona. | 1. **M**acho yanaona. |
| 2. **Ki**fua kinauma. | 2. **Vi**fua vinauma. |
| 3. **U**kucha unakatwa. | 3. **K**ucha zinakatwa. |

**Kusoma hadithi**

**Mama na Kima Mkuu**



**Mama:** Nina, naona Kima Mkuu, tikiti na uki.
**Kima Mkuu:** Rafiki.
**Mama:** Kima Mkuu, uma tikiti.

33 Hakiuzwi

Kipindi cha 33 na 34 **Mwili wangu 1**

**Kima Mkuu:** Sitaki!
**Nina:** Unakataa tikiti tamu?
**Kima Mkuu:** Uki!
**Mama:** Uki mtamu. Tikiti tamu.
**Kima Mkuu:** (Anauma tikiti) Tamu!

**Kipindi 34**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**I** **i**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

t i → **ti** k i → **ki** m i → **mi** i → **i**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

u na kataa → **unakataa** a na uma → **anauma**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Majivuno ya kichwa**



Mali ya Serikali ya Kenya 34

### ▲ Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **I** na utamke sauti yake.
**U:** Endelea na herufi i.
**U:** Mwanafunzi ataje jina la herufi na kutamka sauti yake kwenye **ukurasa wa 34**.

### ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.
**N/T/U:** /t/ /i/ silabi ni ti
**U:** Endelea na silabi ki, mi, li
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 34**.

### ▬ Kusoma maneno marefu

Soma kila sehemu ya neno. Soma neno lote upesi.
**N/T/U:** u na ka taa - unakataa
**U:** unauma, unataka
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 34**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa 33**.

### Hadithi ya mwalimu

**Majivuno ya kichwa**
Siku moja kichwa alijivuna kuhusu umuhimu wake. "Bila mimi nyinyi nyote hamuwezi kufanya lolote. Mimi hushikilia pua, masikio na macho." Kichwa akajidai. Shingo naye akasema, "Bila mimi huwezi kusimama imara."
Mabega nayo yakasema, "Sisi husaidia mikono kufanya kazi." Mikono wakasema wao hutia chakula mdomoni. Miguu walijidai kuwa bora zaidi kwa sababu wanashikilia mwili wote.
Mwishowe kichwa alisema, "Kila kiungo kina manufaa mwilini. Kiungo kimoja kikikosekana mwili hautafanya kazi ipasavyo. Kwa hivyo ni vyema kushirikiana."

Funza maana ya maneno mapya: **pua, shingo, mdomoni.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Kichwa kina kazi gani? *(Kichwa hufanya kazi ya hushikilia pua, masikio na macho.)*
**T:** Taja manufaa ya miguu. *(Miguu hushikilia mwili wote.)*
**U:** Unajifunza nini kutokana na hadithi hii? *(Wanafunzi watoe maelezo ya majibu yao.)*

### Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi zinazorejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Kichwa changu kinauma. | 1. Vichwa vyetu vinauma |
| 2. Mguu wake ni mrefu. | 2. Miguu yake/yao ni mirefu. |
| 3. Mkono huu ni safi. | 3. Mikono hii ni safi. |
| 4. Jino hili ni chafu. | 4. Meno haya ni machafu. |

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno yaliyo na sauti zilizofunzwa.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

Kipindi cha 35 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 35**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**t T** **i l**

Jedwali la silabi.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ta tu - tatu**

| | | | |
|---|---|---|---|
| mi | ka | mu | ki |
| ma | ku | ta | tu |

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Andika umoja au wingi wa sentensi hizi katika daftari lako.

1. **Ki**dole kinauma.
2. **Pu**a inauma.
3. **M**gongo umechoka.
4. **Ji**no linauma.
5. **Mi**guu inauma.
6. **Vi**chwa vinauma.
7. **Si**kio linauma
8. **Mi**domo inauma.
9. **Ki**uno kinauma.
10. **Ki**sigino kinauma.

**Zoezi: Kuandika**

Chora mkono na kichwa katika daftari lako.

35 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja majina ya herufi na utamke sauti.

**N/T/U:** tT, il

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 35.**

## Jedwali

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'ta' na 'ka' kuandika neno taka.

**T:** Unda neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 35.**

## Sarufi

**Umoja na Wingi**

Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika.

Waelekeze wanafunzi kuandika vifungu vya maneno kwenye **ukurasa wa 35.**

**Umoja**

1. Kidole kinauma.
2. Pua inauma.
3. Migongo imechoka.

## Kuandika

**Alama ya hisi**

**N:** *Andika sentensi zenye alama za hisi. Soma sentensi na usisitize matumizi ya alama ya hisi inayoonyesha kufurahi.* Wakati mwingine tunapoandika huwa tunataka kuonyesha kwamba jambo fulani la kufurahisha au la ghafla limetokea. Tunapotaka kuonyesha aina hizi za hisia kimaandishi, tunamalizia sentensi zetu kwa alama ya hisi.

**T:** *Waongoze wanafunzi kuandika sentensi za kuvutia kuhusu hadithi.* Hakikisha kuwa umeweka alama ya hisi mwishoni mwa sentensi.

**U:** *Wanafunzi waandike na wenzao sentensi za kuvutia kuhusu hadithi.*

## Kazi ya ziada

Wanafunzi wachore sehemu nne za mwili za nje.

## Kazi ya nyongeza

Wanafunzi wachore sehemu nne za mwili.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 36 na 37 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 36**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**n** **i** **t**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| n a | n u | n i | t u |
|---|---|---|---|
| **na** | **nu** | **ni** | **tu** |

Soma silabi na maneno.

| m ti ni | ki ti ni | a na ka a | a na o na |
|---|---|---|---|
| **mtini** | **kitini** | **anakaa** | **anaona** |

**Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **ki**chwa | 1. **vi**chwa |
| 2. **pa**ja | 2. **ma**paja |
| 3. **go**ti | 3. **ma**goti |

**Kusoma hadithi**

**Tai na paka**



Tai anakaa mtini.
Paka anakaa na kuku kitini.
Tai anaona paka na kuku.
Tai anataka kumuuma kuku.
Paka anasema, "Tai paa mtini."
Kuku anasema, "Asante rafiki paka."

Mali ya Serikali ya Kenya 36

Kipindi cha 36 na 37 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 37**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**N** **t**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| n a | k a | m a | t a |
|---|---|---|---|
| **na** | **ka** | **ma** | **ta** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na kaa | a na o na |
|---|---|
| **anakaa** | **anaona** |
| u ki mu uma | |
| **ukimuuma** | |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Daktari**



37 Hakiuzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/n/**. Taja neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno. Wanafunzi waonyeshe kidole chini iwapo neno hilo halina sauti hiyo.
**N/T/U:** nini, mama
**U:** nani, kana, ita, nena

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** n
**U:** Endelea na herufi i, t.
Mwanafunzi ataje jina la herufi na kutamka sauti yake kwa usahihi kwenye **ukurasa wa 36.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti ili kusoma silabi.
**N/T/U:** /n/ /a/ silabi ni na
**U:** Endelea na nu, ni, tu
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa36.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** m ti ni- mtini
**U:** kitini, anakaa, anaona
Katika vikundi vya wawili wawili wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 36.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **mtini, utaona.**
Soma maneno kwenye **ukurasa wa 36.**

### Kabla ya kusoma

**N/T**: Soma kichwa cha hadithi. Wanafunzi wajadili picha na kutoa utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N:** Soma peke yako.
**T:** Soma pamoja na wanafunzi.
**U:** Wanafunzi wasome peke yao.
Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Nani anakaa mtini? *(Tai)*
**T**: Nani anakaa kitini? *(Paka na kuku)*
**U:** Nani hukaa karibu nanyi kule nyumbani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**
Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika.

### Zoezi

Mwanafunzi asome maneno yanayorejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi kwenye **ukurasa wa 36.**

### Kazi ya ziada

Andika herufi n (kubwa na ndogo) ubaoni kwa hati hadhifu. Waagize wanafunzi waandike kwenye madaftari yao.
n n n n n n n n n n n          N N N N N N N N N N N

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 36 na 37 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 36**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**n** **i** **t**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| n a | n u | n i | t u |
| **na** | **nu** | **ni** | **tu** |

● Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| m ti ni | ki ti ni | a na ka a | a na o na |
| **mtini** | **kitini** | **anakaa** | **anaona** |

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **ki**chwa | 1. **vi**chwa |
| 2. paja | 2. **ma**paja |
| 3. goti | 3. **ma**goti |

**Kusoma hadithi**

**Tai na paka**



Tai anakaa mtini.
Paka anakaa na kuku kitini.
Tai anaona paka na kuku.
Tai anataka kumuuma kuku.
Paka anasema, "Tai paa mtini."
Kuku anasema, "Asante rafiki paka."

Mali ya Serikali ya Kenya 36

Kipindi cha 36 na 37 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 37**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**N** **t**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| n a | k a | m a | t a |
| **na** | **ka** | **ma** | **ta** |

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a na kaa | a na o na |
| **anakaa** | **anaona** |
| u ki mu uma | |
| **ukimuuma** | |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Daktari**



37 Hakiuzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** N

**U:** Endelea na herufi t.

**U:** Mwanafunzi ataje jina la herufi na kutamka sauti yake kwa usahihi kwenye **ukurasa wa 37.**

### ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti ili kusoma silabi.

**N/T/U:** /n/ /a/ silabi ni **na**.

**U:** Endelea na silabi ka, ma, ta

**U:** Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 37.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Soma kila sehemu ya neno. Soma neno lote upesi.

**N/T/U:** a na kaa - anakaa

**U:** anaona, ukimmuma

**U:** Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza kwenye **ukurasa wa 37.**

### Msamiati

Funza maneno mapya: **kichwa, viungo**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 36.**

### Hadithi ya mwalimu

**Daktari**

Hapo zamani za kale kulikuwepo na madaktari wa kienyeji. Madaktari hao walikuwa na ujuzi wa kutibu magonjwa mbalimbali. Kichwa kilichouma kilichanjwa na kutiwa dawa, kikapona. Damu chafu ilitolewa kutumia pembe. Viungo vilivyovunjika viliunganishwa kwa kufunga kamba. Kwa jumla madaktari hawa walikuwa wajuzi.

Madaktari wa kiasili au wa kisasa wana jukumu kubwa. Wao hututibu na kutushauri juu ya malezi mema ya miili yetu. Ni muhimu kushirikiana nao ili afya zetu ziwe bora.

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi.

Wanafunzi wajadili picha na kutoa utabiri.

Mwalimu asome. Wanafunzi wasikilize hadithi huku wakiitazama picha husika.

Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao umetimia.

### ? Maswali

**N:** Pembe ilitumika kufanya nini?

*(Pembe ilitumika kutoa damu chafu.)*

**T:** Viungo vilivyovunjika viliunganishwa kutumia nini?

*(Viungo viliunganishwa kwa kufunga kamba.)*

**U:** Je, unafikiri madaktari wa kienyeji ni muhimu sasa?

*(Mwalimu azingatie kwa makini maelezo ya wanafunzi na kukubali majibu sahihi.)*

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 37: Mwili wangu 1

Kipindi cha 36 na 37 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 36**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **n** **i** **t**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  n a → **na** n u → **nu** n i → **ni** t u → **tu**

- Soma silabi na maneno.

  m ti ni → **mtini** ki ti ni → **kitini** a na ka a → **anakaa** a na o na → **anaona**

**Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **ki**chwa | 1. **vi**chwa |
| 2. **pa**ja | 2. **ma**paja |
| 3. **go**ti | 3. **ma**goti |

**Kusoma hadithi**

**Tai na paka**



Tai anakaa mtini.
Paka anakaa na kuku kitini.
Tai anaona paka na kuku.
Tai anataka kumuuma kuku.
Paka anasema, "Tai paa mtini."
Kuku anasema, "Asante rafiki paka."

Mali ya Serikali ya Kenya 36

Kipindi cha 36 na 37 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 37**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **N** **t**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  n a → **na** k a → **ka** m a → **ma** t a → **ta**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  a na kaa → **anakaa** a na o na → **anaona**

  u ki mu uma → **ukimuuma**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Daktari**



37 Hakiuzwi

### Zoezi

Mwanafunzi aandike maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa kwa kunakili aliyoandika mwalimu kama vile: kiuno, nenepa, mikono, uso, natazama.

### Kazi ya ziada

Jaza pengo kwa kuzingatia wingi wa neno ulilopewa:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Kichwa | ____________ |
| 2. Paja | ____________ |
| 3. Goti | ____________ |
| 4. Kiungo | ____________ |
| 5. Mguu | ____________ |

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 38: Mwili wangu 1

Kipindi cha | 38 na 39 | **Mwili wangu 1**

**Kipindi 38**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**o** **n** **i**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

n o → **no**  k o → **ko**  m o → **mo**  t o → **to**

● Soma silabi na maneno.

no no → **nono**  mo to → **moto**  mo to ni → **motoni**

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma sentensi katika vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **A**nanyoa nywele. | 1. **Wa**nanyoa nywele. |
| 2. **Ki**ungo **ki**navunjika. | 2. **Vi**ungo **vi**navunjika. |
| 3. **Ki**devu **ki**nachafuka. | 3. **Vi**devu **vi**nachafuka. |

**Kusoma hadithi**

**Kanini na Katana**



Kanini anakaa na kaka Katana.

Kanini anataka kuota moto. Katana anakata kuni. Anatia kuni motoni.

Kanini anaota moto. Katana anatia ini nono motoni.

Anamkatia Kanini ini. Kanini anasema, "Asante, kaka. Ini ni tamu."

Mali ya Serikali ya Kenya 38

Kipindi cha | 38 na 39 | **Mwili wangu 1**

**Kipindi 39**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**O** **o**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

n o → **no**  k oo → **koo**  n i → **ni**  t ii → **tii**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

a na kaa → **anakaa**  a na m katia → **anamkatia**

a na taka → **anataka**  a na tia → **anatia**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Dubu mpenda kula**




39 Hakiuzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/o/**. Taja neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini iwapo neno hilo halina sauti hiyo.

**N/T:** ona, nono

**U:** ota, toto, okoa, tamaa

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** o

**U:** Endelea na n, i

**U:** Mwanafunzi ataje jina la herufi na kutamka sauti yake kwa usahihi kwenye **ukurasa wa 38.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti ili kusoma silabi.

**N/T/U:** /n/ /o/ silabi ni no

**U:** /n//o/ -silabi ni no

Soma silabi kwenye **ukurasa wa 38.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** no no - nono

**U:** moto, motoni

Kwa vikundi vya wawili wawili wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 38.**

### Msamiati

Funza maneno haya: **moto, nono, motoni**

### Kabla ya kusoma

**N/T**: Soma kichwa cha hadithi. Wanafunzi wajadili picha na kutoa utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N:** Soma hadithi peke yako.

**T:** Soma hadithi pamoja na wanafunzi.

**U:** Wanafunzi wasome peke yao.

Waeleze ikiwa utabiri wao ulitimia au la.

### Maswali

**N:** Kanini anakaa na nani? *(Kaka Katana.)*

**T**: Kuni ilikuwa ya kufanyia nini? *(Kuwasha moto.)*

**U:** Nyinyi hutumia nini kupikia chakula?

*(Wanafunzi watoe maelezo ya majibu yao.)*

### Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**

Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika.

### Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi kwa vikundi kwa kuzingatia umoja na wingi kwenye **ukurasa wa 38.**

### Kazi ya ziada

**Kuandika:** Andika herufi **o** (kubwa na ndogo) ubaoni kwa hati nadhifu. Waagize wanafunzi waandike kwenye madaftari yao.

o o o o o o o o o o o    O O O O O O O O O O O

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 39: Mwili wangu 1

Kipindi cha 38 na 39 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 38**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

o n i

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| n o | k o | m o | t o |
|---|---|---|---|
| no | ko | mo | to |

● Soma silabi na maneno.

| no no | mo to | mo to ni |
|---|---|---|
| nono | moto | motoni |

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma sentensi katika vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **A**nanyoa nywele. | 1. **Wa**nanyoa nywele. |
| 2. **Ki**ungo kinavunjika. | 2. **Vi**ungo vinavunjika. |
| 3. **Ki**devu kinachafuka. | 3. **Vi**devu vinachafuka. |

**Kusoma hadithi**

**Kanini na Katana**



Kanini anakaa na kaka Katana.
Kanini anataka kuota moto.
Katana anakata kuni. Anatia kuni motoni.
Kanini anaota moto. Katana anatia ini nono motoni.
Anamkatia Kanini ini. Kanini anasema, "Asante, kaka. Ini ni tamu."

Mali ya Serikali ya Kenya 38

Kipindi cha 38 na 39 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 39**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

O o

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| n o | k oo | n i | t ii |
|---|---|---|---|
| no | koo | ni | tii |

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na kaa | a na m katia |
|---|---|
| anakaa | anamkatia |
| a na taka | a na tia |
| anataka | anatia |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Dubu mpenda kula**




39 Hakiuzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** O

**U:** Endelea na herufi o.

**U:** Mwanafunzi ataje jina la herufi na kutamka sauti yake kwa usahihi kwenye **ukurasa wa 39.**

### ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti ili kusoma silabi.

**N/T/U:** /n/ /o/ - no

**U:** ko, mo

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 39.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** a na kaa - anakaa

**U:** anamkatia, anataka, anatia

Katika vikundi vya wawili wawili wape wanafunzi nafasi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 39.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 38.**

### Msamiati

Funza maana ya neno **kitambi, kiafya.**

### Kabla ya kusoma

**N/T:** Soma kichwa. Wanafunzi wajadili picha na kutoa utabiri.

### Hadithi ya mwalimu

**Dubu Mpenda Kula**

Dubu alikuwa kijana aliyependa kula sana. Mwili wake ulinenepa zaidi ya miaka yake.
Tumbo la Dubu lilikuwa kubwa, akawa na kitambi.
Alipata matatizo ya kiafya. Hakuweza kutembea mwendo mrefu. Alipojaribu alihema au kupumua kwa shida pia. Alichoka miguu. Wazazi wake walimpeleka hospitalini. Daktari alimchunguza na kumshauri ale vizuri na kufanya mazoezi.
Dubu aliepuka vyakula vyenye sukari na mafuta.
Alifanya mazoezi ya kutembea asubuhi na jioni. Pia alikunywa maji mengi.

Soma peke yako. Wanafunzi wasikilize hadithi huku wakiitazama picha husika.
Wanafunzi waseme iwapo utabiri wao ulitimia au la.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 38 na 39 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 38**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **o** **n** **i**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| n o | k o | m o | t o |
|---|---|---|---|
| **no** | **ko** | **mo** | **to** |

- Soma silabi na maneno.

| no no | mo to | mo to ni |
|---|---|---|
| **nono** | **moto** | **motoni** |

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma sentensi katika vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **A**nanyoa nywele. | 1. **Wa**nanyoa nywele. |
| 2. **Ki**ungo kinavunjika. | 2. **Vi**ungo vinavunjika. |
| 3. **Ki**devu kinachafuka. | 3. **Vi**devu vinachafuka. |

**Kusoma hadithi**

**Kanini na Katana**



Kanini anakaa na kaka Katana.

Kanini anataka kuota moto. Katana anakata kuni. Anatia kuni motoni.

Kanini anaota moto. Katana anatia ini nono motoni.

Anamkatia Kanini ini. Kanini anasema, "Asante, kaka. Ini ni tamu."

Mali ya Serikali ya Kenya 38

Kipindi cha 38 na 39 **Mwili wangu 1**

**Kipindi 39**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **O** **o**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| n o | k oo | n i | t ii |
|---|---|---|---|
| **no** | **koo** | **ni** | **tii** |

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na kaa | a na m katia |
|---|---|
| **anakaa** | **anamkatia** |
| a na taka | a na tia |
| **anataka** | **anatia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Dubu mpenda kula**




39 Hakiuzwi

## ? Maswali

**N:** Taja tabia mbaya ya Dubu.

*(Dubu alipenda kula sana.)*

**T.** Kupenda kula sana kunasababisha nini?

*(Kula sana kunasababisha matatizo ya kiafya.)*

**U:** Taja njia zingine za kuboresha mwili kiafya.

*(Wanafunzi waeleze majibu yao.)*

## Zoezi

Mwanafunzi aambanitishe kadi za maneno na sehemu za mwili za nje. k. m. tumbo, uso, macho, kisugudi, kichwa, mabega, mguu, magoti


## Kazi ya ziada

Aaandike wingi wa maneno haya.

1. Kichwa
2. Jicho
3. Bega
4. Mguu
5. Goti

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 40: Mwili wangu 1


Kipindi cha 40 Mwili wangu 1

Kipindi 40

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

n N o O i i t T

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: m to – mto**

| | | |
|---|---|---|
| m | ko | ma |
| mo | na | to |

♦ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma sentensi hizi katika vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Pa**ja ni safi. | 1. **Ma**paja ni safi. |
| 2. **Go**ti linavunjika. | 2. **Ma**goti yanavunjika. |
| 3. **Ki**sigino kinauma. | 3. **Vi**sigino vinauma. |
| 4. **Me**za inapakwa rangi. | 4. **Me**za zinapakwa rangi. |
| 5. **Ngu**o inaanikwa. | 5. **Ngu**o zinaanikwa. |
| 6. **Ki**tabu kinanunuliwa. | 6. **Vi**tabu vinanunuliwa. |
| 7. **Ji**no linang'olewa. | 7. **Me**no yanang'olewa. |

**Zoezi: Kuandika**

Chora mguu na macho katika daftari lako.

Mali ya Serikali ya Kenya 40

## Ufahamu wa herufi

Taja majina ya herufi na utamke sauti.

**N/T/U:** n N

**U:** Endelea na herufi o, O, i, I, t, T

**U:** Wanafunzi wasome jina la herufi na kutamka sauti yake kwa usahihi kwenye **ukurasa wa 40.**

## Jedwali la silabi

**N:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **m** na **to** kuandika neno **mto.**

**T:** Soma neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Wanafunzi waunde maneno halisi wakitumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 40.**

## Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**

Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika.

Wanafunzi wasome sentensi hizi kwa vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Paja ni safi. | mapaja ni safi. |
| 2. Goti limevunjika. | magoti yamevunjika. |
| 3. Kisigino kinauma. | visigino vinauma. |

## Kuandika

**Alama ya hisi**

**N**: *Andika sentensi zenye alama ya hisi. Soma sentensi na usisitize matumizi ya alama ya hisi inayoonyesha kufurahi*. Wakati mwingine tunapoandika huwa tunataka kuonyesha kwamba jambo fulani la kufurahisha au la ghafla limetokea. Tunapotaka kuonyesha aina hizi za hisia kimaandishi, tunamalizia sentensi zetu kwa alama ya hisi.

**T**: Waongoze wanafunzi kuandika sentensi za kuvutia kuhusu hadithi. Hakikisha kuwa umeweka alama ya hisi mwishoni mwa sentensi.

**U**: Waulize wanafunzi waandike na wenzao sentensi za kuvutia kuhusu hadithi.

## Kazi ya ziada

Wanafunzi wasomee walezi wao sentensi zifuatazo.

1. Mwili wangu ni safi.
2. Ni muhumu kukata kucha.
3. Nawa mikono unapotoka msalani.
4. Tumia mswaki na dawa unaposugua meno.

## Kazi ya nyongeza

Watajie wazazi au walezi wao sehemu za mwili za nje.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 41: Usafi wa mwili 1

Kipindi cha 41 na 42 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 41**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**w** **o** **n**

- Tamke sauti ya herufi na usome silabi.

w a → **wa**   w i → **wi**   w u → **wu**   w o → **wo**

- Soma silabi na maneno.

wa tu → **watu**   wa to to → **watoto**   wa na → **wana**   wa ta no → **watano**

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu** ni kima. | 1. **Hawa** ni kima. |
| 2. **Huyu** ni mtoto. | 2. **Hawa** ni watoto. |
| 3. **Huyu** ni mwalimu. | 3. **Hawa** ni walimu. |

**Kusoma hadithi**

**Watoto wa kima**

Kima ana watoto watano. Watoto wa kima wana mikia mirefu. Watoto wanataka mtama mtamu wa mama. Mama anawaona watoto wa kima mtamani. Mama anawaita watu. Watu wanawatoa watoto wa kima mtamani.



Hakiuzwi



Kipindi cha 41 na 42 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 42**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**W** **w**

- Tamke sauti ya herufi na usome silabi.

w a → **wa**   k o → **ko**   n a → **na**   t o → **to**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

wa na taka → **wanataka**   wa na wa toa → **wanawatoa**

a na wa ona → **anawaona**   a na wa ita → **anawaita**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mkutano kijijini Lelan**



Mali ya Serikali ya Kenya



### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/w/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** watu, awamu

**U:** watoto, kote, wana, watano

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** w

**U:** Endelea na herufi o, n.

**U:** Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 41.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti ili kusoma silabi.

**N/T/U:** /w/ /a/ wa

**U:** Endelea na wi, wu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 41.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** wa tu - watu

**U:** watoto, wana

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 41.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **mikia, mtamani**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kima ana watoto wangapi? *(Watano)*

**T:** Mtama mtamu ulikuwa wa nani? *(Mama)*

**U:** Ukihisi njaa, unafaa kufanya nini? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

Eleza matumizi ya **huyu** na **hawa**. Huyu hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. Hawa hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi. Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 41.**

### Kazi ya ziada

Wanafunzi wafinyange na kuandika maumbo ya herufi walizosoma. w na o

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 41 na 42 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 41**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

w o n

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

w a → **wa** w i → **wi** w u → **wu** w o → **wo**

● Soma silabi na maneno.

wa tu → **watu** wa to to → **watoto** wa na → **wana** wa ta no → **watano**

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu** ni kima. | 1. **Hawa** ni kima. |
| 2. **Huyu** ni mtoto. | 2. **Hawa** ni watoto. |
| 3. **Huyu** ni mwalimu. | 3. **Hawa** ni walimu. |

**Kusoma hadithi**

**Watoto wa kima**

Kima ana watoto watano. Watoto wa kima wana mikia mirefu. Watoto wanataka mtama mtamu wa mama. Mama anawaona watoto wa kima mtamani. Mama anawaita watu. Watu wanawatoa watoto wa kima mtamani.



41 Hakiuzwi

Kipindi cha 41 na 42 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 42**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

W w

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

w a → **wa** k o → **ko** n a → **na** t o → **to**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

wa na taka → **wanataka** wa na wa toa → **wanawatoa**

a na wa ona → **anawaona** a na wa ita → **anawaita**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mkutano kijijini Lelan**



Mali ya Serikali ya Kenya 42

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** W

**U:** Endelea na herufi w.

Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti yake kwenye **ukurasa wa 42.**

### ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti na kusoma silabi.

**N/T/U:** /k/ /o/ silabi ni ko

**U:** Endelea na wa, ta

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 42.**

### Kusoma maneno marefu

Soma kila sehemu ya neno. Soma neno lote upesi.

**N/T/U:** wa na taka - wanataka

**U:** wanawatoa, anawaona

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 42.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 41.**

### Hadithi ya mwalimu

**Mkutano kijijini Lelan**

Magonjwa yaliongezeka katika kijiji cha Lelan. Wengi walienda hospitalini kutibiwa. Madaktari wakawa na shaka. Afisa wa afya Bwana Silom aliandaa mkutano wa kuwaelimisha wanakijiji jinsi ya kudumisha usafi ili kuepukana na magonjwa.

Wanakijiji waliwasili katika uwanja wa mkutano. Bwana Silom aliwaelezea chanzo cha magonjwa waliyougua. Aliwafundisha kunawa mikono kwa kutumia maji safi na sabuni. Aliwaambia pia watumie maji safi katika kupika na kunywa. Walitahadharishwa dhidi ya kutema mate ovyo ovyo na kufuta kamasi kwa kutumia mikono. Walisisitiziwa kuoga miili yao na kuvaa nguo safi. Wanakijiji walifurahi na kumshukuru afisa wa afya kwa mafunzo.

Funza maana ya maneno mapya: **kunawa mikono, kufuta kamasi.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi wanafunzi wasikize huku wakitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Kwa nini mkutano uliandaliwa Kijijini Lelan? *(Mkutano uliandaliwa kwa sababu magonjwa yalikuwa yameongezeka.)*

**T:** Bwana Silom aliwaelimisha wanakijiji kuhusu nini? *(Kunawa mkono na kutumia maji safi kupikia na kunywa.)*

**U:** Unafikiri kwa nini ni vibaya kutema mate ovyo ovyo? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Wanafunzi kushirikikishwa katika mjadala kuhusu usafi wa mwili.

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike sentensi tatu kueleza jinsi anavyohifadhi usafi wa mwili kila siku.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 43 na 44 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 43**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

e w o

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| n e | t e | w e | n a |
|---|---|---|---|
| **ne** | **te** | **we** | **na** |

- Soma silabi na maneno.

| te na | ne e ma | m ke ka ni | mwe we |
|---|---|---|---|
| **tena** | **neema** | **mkekani** | **mwewe** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Jaza mapengo ukitumia **'huyu'**, **'hawa'**.

1. ________ anaosha nywele.
2. ________ wanakata nywele.
3. ________ anakata kucha.

**Kusoma hadithi**

**Neema na mwewe**

Amina aliketi mkekani akiota moto.
Alimuona mwewe akimkamata kuku.
Aliita, "Neema, Neema!"
Neema aliitika, "Naam, Amina."
Amina aliita tena, "Neema! Ona mwewe!"
Neema aliokota mawe na kumtimua mwewe.



43

Hakiuzwi

Kipindi cha 43 na 44 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 44**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

E e

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| w e | k e | w i | w o |
|---|---|---|---|
| **we** | **ke** | **wi** | **wo** |

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a ka mu ona | a ki m kamata |
|---|---|
| **akamuona** | **akimkamata** |
| a ka mu ita | a ka m timua |
| **akamuita** | **akamtimua** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sega mchafu**



Mali ya Serikali ya Kenya

44

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/e/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.
**N/T/U:** eka, maua
**U:** ewe, keki, enda, keti

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** e
**U:** Endelea na herufi w, o
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na kutamka sauti zake kwenye **ukurasa wa 43.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na kusoma silabi.
**N/T/U:** /n/ /e/ silabi ni ne
**U:** Endelea na silabi te, we
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 43.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila sehemu ya neno. Soma neno lote upesi.
**N/T/U:** te na - tena
**U:** Endelea na Neema, mkekani
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 43.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **akiota**, **kumtimua**

### Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Amina aliketi mkekani akifanya nini? *(Akiota jua)*
**T**: Nani alimfukuza mwewe? *(Neema)*
**U:** Eleza sifa za mwewe. *(Kubali jibu sahihi)*

### Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**
Eleza matumizi ya **huyu** na **hawa.** Huyu hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. Hawa hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

### Zoezi

Jaza mapengo kutumia huyu au hawa kwenye **ukurasa wa 43.**

### Kazi ya ziada

Andika sentensi ukitumia maneno haya: makasi, kunawa mikono, kuoga.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 44: Usafi wa mwili 1

Kipindi cha 43 na 44 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 43**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**e** **w** **o**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| n e | t e | w e | n a |
|---|---|---|---|
| **ne** | **te** | **we** | **na** |

● Soma silabi na maneno.

| te na | ne e ma | m ke ka ni | mwe we |
|---|---|---|---|
| **tena** | **neema** | **mkekani** | **mwewe** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Jaza mapengo ukitumia **'huyu'**, **'hawa'**.

1. ________ anaosha nywele.
2. ________ wanakata nywele.
3. ________ anakata kucha.

**Kusoma hadithi**

**Neema na mwewe**

Amina aliketi mkekani akiota moto.

Alimuona mwewe akimkamata kuku.

Aliita, "Neema, Neema!"

Neema aliitika, "Naam, Amina."

Amina aliita tena, "Neema! Ona mwewe!"

Neema aliokota mawe na kumtimua mwewe.



43 Hakiuzwi

Kipindi cha 43 na 44 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 44**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**E** **e**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| w e | k e | w i | w o |
|---|---|---|---|
| **we** | **ke** | **wi** | **wo** |

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a ka mu ona | a ki m kamata |
|---|---|
| **akamuona** | **akimkamata** |
| a ka mu ita | a ka m timua |
| **akamuita** | **akamtimua** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sega mchafu**



Mali ya Serikali ya Kenya 44

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** E

**U:** Endelea na herufi e

Mwanafunzi ataje jina la herufi na kutamka sauti yake kwenye **ukurasa wa 44**.

### ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /w/ /e/ silabi ni we

**U:** Endelea na ke, wi

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 44**.

### ▬ Kusoma maneno marefu

Soma kila sehemu ya neno. Soma neno lote upesi.

**N/T/U:** a ka mu ona - akamuona

**U:** akimkamata, akamtimua

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 44**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 43**.

### Hadithi ya mwalimu

**Sega mchafu**

Katika kituo cha matatu cha Zuruwata, kulitokea kijana mmoja aliyeitwa Sega. Kijana huyo alikuwa mchafu. Nywele, kucha na nguo zake zilikuwa chafu. Hakuwa akiyasugua meno yake. Hakupenda kuoga, alikuwa ananuka. Makamasi yalimtoka puani kila wakati. Utingo wenzake hawakupenda tabia zake. Siku moja, utingo wenzake waliandaa mchango wakanunua sabuni, wembe, nguo mpya, maji na mswaki.

Sega alipoingia kituoni alikamatwa, akaingizwa katika bafu la umma. Kazi ya kumuosha ikaanza. Nywele zake zikakatwa. Alipakwa mafuta na kuvalishwa nguo mpya. Sega akapendeza. Kuanzia siku hiyo, Sega aliacha tabia za uchafu. Kila mara alipoenda kituoni, alioga na kuchana nywele zake. Utingo wengine walimpenda sana, walifurahia kufanya kazi pamoja.

Funza maana ya maneno mapya: **kuoga, kuchana nywele.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Ni vifaa gani vya usafi vilivyonunuliwa na utingo? *(Utingo walinunua kichana, wembe na sabuni.)*

**T:** Sega alipoingia kituoni kulitokea nini? *(Alikamatwa, akaingizwa katika bafu la umma na kuoshwa.)*

**U:** Eleza manufaa ya usafi wa mwili. *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike maneno akitumia herufi alizofunzwa.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore sehemu hizi: mikono, miguu.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 45: Usafi wa mwili 1

Kipindi cha 45 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 45**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

e E w W

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: a mu - amu**

| | | |
|---|---|---|
| wa | mu | tu |
| e | a | ne |

**Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Andika sentensi zifuatazo kwenye daftari lako.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu a**nachana nywele. | 1. **Hawa wa**nachana nywele. |
| 2. **Huyu a**na kidole kinene. | 2. **Hawa wa**na vidole vinene. |
| 3. **Huyu a**na kifua kipana. | 3. **Hawa wa**na vifua vipana. |
| 4. Kijana **huyu a**napaka meza rangi. | 4. Vijana **hawa wa**napaka meza rangi. |
| 5. Mvulana **huyu a**nafua nguo. | 5. Wavulana **hawa wa**nafua nguo. |

**Zoezi: Kuandika**

Chora mswaki.

45

Hakluzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja majina ya herufi na utamke sauti.

**N/T/U:** w

**U:** Endelea na herufi W, e, E

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 45.**

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi a na **mu** kuandika neno **amu.**

**T:** Unda neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 45.**

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

Eleza matumizi ya **huyu** na **hawa.** Huyu hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. Hawa hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

## Kuandika

**T**: Rejelea usafi wa mwili.

**U**: Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 45.**

Mwanafunzi achore mswaki katika daftari lake.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore mswaki wa kusugua meno.

## Kazi ya nyongeza

Sisitiza kuhusu utunzaji wa mwili. Mwanafunzi ajadili na walezi wake kuhusu usafi wa mwili wake.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 46: Usafi wa mwili 1

Kipindi cha 46 na 47 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 46**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  l e w

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  | l e | l i | l u | l o |
  |---|---|---|---|
  | le | li | lu | lo |

- Soma silabi na maneno.

  | Lo la ni | li ma u | Ne li ma | a ka la |
  |---|---|---|---|
  | Lolani | limau | Nelima | akala |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mnyama **huyu** anapendeza. | 1. Wanyama **hawa** wanapendeza. |
| 2. Paka **huyu** ana kucha. | 2. Paka **hawa** wana kucha. |
| 3. Mtoto **huyu** anasoma. | 3. Watoto **hawa** wanasoma. |

**Kusoma hadithi**

**Lolani na Nelima**



Lolani alilala kitini. Nelima alimletea limau. Lolani akala. Lo! Limau lilikuwa kali. Lolani alilitema limau. Nelima alimletea Lolani muwa. Lolani aliukataa muwa. Nelima alimletea uki. Lolani alikula uki.

Mali ya Serikali ya Kenya

46

Kipindi cha 46 na 47 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 47**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  L l

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  | l a | w e | n e | k e |
  |---|---|---|---|
  | la | we | ne | ke |

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  | a li m letea | a li li tema |
  |---|---|
  | alimletea | alilitema |
  | a li u kataa | li li kuwa |
  | aliukataa | lilikuwa |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sungura mpenda usafi**



47 Hakiuzwi

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/l/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni wa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** limau, ala

**U:** lala, Nelima, lakini, Lolani

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** l

**U:** Endelea na herufi e na **w.**

Mwanafunzi ataje jina la herufi naatamke sauti kwenye **ukurasa wa 46.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti usome silabi.

**N/T/U:** /l/ /e/ silabi ni le

**U:** Endelea na li, lu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 46.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** Lo la ni - Lolani

**U:** limau, Nelima

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 46.**

## Msamiati

Funza maneno haya: **limau, alilitema, muwa**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi asome hadithi.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

## Maswali

**N:** Lolani alilala wapi? *(Kitini)*

**T**: Nani alileta limau? *(Nelima)*

**U:** Mtu anafaa kufanyiwa nini anapokuwa mgonjwa? *(Kupelekwa hospitali, kupewa dawa.)*

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

Eleza matumizi ya **huyu** na **hawa.** Huyu hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. Hawa hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi. Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 46.**

## Kazi ya ziada

Andika herufi **l** (kubwa na ndogo) ubaoni kwa hati nadhifu. Waelekeze wanafunzi wanakili kwenye madaftari yao.

1. l l l l l l l l l l     2. L L L L L L L L L L

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 47: Usafi wa mwili 1

Kipindi cha 46 na 47 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 46**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  l e w

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  l e → **le**  l i → **li**  l u → **lu**  l o → **lo**

- Soma silabi na maneno.

  Lo la ni → **Lolani**  li ma u → **limau**  Ne li ma → **Nelima**  a ka la → **akala**

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mnyama **huyu** anapendeza. | 1. Wanyama **hawa** wanapendeza. |
| 2. Paka **huyu** ana kucha. | 2. Paka **hawa** wana kucha. |
| 3. Mtoto **huyu** anasoma. | 3. Watoto **hawa** wanasoma. |

**Kusoma hadithi**

**Lolani na Nelima**



Lolani alilala kitini. Nelima alimletea limau. Lolani akala. Lo! Limau lilikuwa kali. Lolani alilitema limau. Nelima alimletea Lolani muwa. Lolani aliukataa muwa. Nelima alimletea uki. Lolani alikula uki.

Mali ya Serikali ya Kenya

46

Kipindi cha 46 na 47 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 47**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  L l

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  l a → **la**  w e → **we**  n e → **ne**  k e → **ke**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  a li m letea → **alimletea**  a li li tema → **alilitema**

  a li u kataa → **aliukataa**  li li kuwa → **lilikuwa**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sungura mpenda usafi**



47 Hakiuzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** L
**U:** Endelea na herufi l
Mwanafunzi ataje jina la herufi na atamke sauti yake kwenye **ukurasa wa 47**.

### ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti kusoma silabi.
**N/T/U:** /l/ /a/ silabi ni la
**U:** Endelea na silabi na, we
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 47**.

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo kisha usome neno kwa upesi.
**N/T/U:** a li m letea - alimletea
**U:** Endelea na maneno: aliukata, lilikuwa
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 47**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 46**.

### Hadithi ya mwalimu

**Sungura mpenda usafi**
Sungura na simba walikuwa marafiki. Walipendana sana. Sungura alikuwa na meno ya kupendeza. Simba alitamani meno yake. Simba alimuuliza, "Sungura siri ya kuwa na meno ya kupendeza ni nini?" Sungura alicheka, "Ha! Ha! Siri ni usafi!"
Sungura alisema ni vyema kusugua meno kila siku baada ya kula. Simba akaanza kusugua meno lakini bado mdomo ulinuka.
Simba akamuuliza "Kwa nini ulinidanganya? Nimesugua meno lakini mdomo bado unanuka." Sungura alimuuliza, "Je, ulitumia dawa ya meno?" "La!" Simba alijibu. Sungura alimweleza umuhimu wa kutumia dawa anaposugua meno. Simba akasugua meno kwa mswaki na dawa. Kinywa chake kikawa safi.

Funza maana ya maneno mapya: **usafi, akasugua meno.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi. Wanafunzi wasikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**T:** Simba alitamani kuwa na nini? *(Meno kama ya sungura)*
**T:** Sungura alisema yeye husugua meno wakati gani? *(Asubuhi akiamka)*
**U:** Wewe hufanya nini kuweka mwili safi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Soma maneno. Mwanafunzi aandike kwenye daftari lake:
1. msichana 2. kila 3. siku 4. kamasi 5. usafi

### Kazi ya ziada

Andika maneno haya ubaoni: kukata kucha, kusugua meno, kufuta kamasi, kuoga, kunawa mikono. Mwanafunzi ayaandike kwenye daftari lake na baadaye awasomee wazazi au walezi wake.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 48 na 49 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 48**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**h** **l** **e**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

h a → **ha** | h o → **ho** | h u → **hu** | h e → **he**

● Soma silabi na maneno.

ha mu → **hamu** | ka ha wa → **kahawa** | ho te li ni → **hotelini** | He le na → **Helena**

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Jaza mapengo kwa jibu sahihi.

1. Watoto ________ wanasugua meno. (hawa, huyu)
2. Kijana ________ anafua nguo. (hawa, huyu)
3. Msichana ________ ana nywele ndefu. (hawa, huyu)

**Kusoma hadithi**

**Hotelini**

Helena alinawa mikono hotelini ikawa safi. Alinunua kaimati na kahawa tamu. Alikuwa na hamu ya kahawa tamu. Mama alinawa na kuketi kitini. Aliletewa wali kwa maini. Hakutaka kahawa tamu na kaimati kama Helena.



Mali ya Serikali ya Kenya

48

Kipindi cha 48 na 49 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 49**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**H** **h**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

h i → **hi** | w i → **wi** | l i → **li** | k i → **ki**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

a li nawa → **alinawa** | a li nunua → **alinunua**

a li letewa → **aliletewa** | ha ku taka → **hakutaka**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Makomo na Chifu**



49

Hakiuzwi

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/h/**. Soma maneno. mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** hamu, kahawa

**U:** hema, wahi, hotelini

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi **h** na utamke sauti yake.

**N/T/U:** h

**U:** Endelea na **l** na **e**. Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 48.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti kusoma silabi.

**N/T/U:** /h/ /a/ silabi ni ha

**U:** Endelea na silabi ho, hu. Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 48.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ha mu- hamu

**U:** kahawa, helena

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 48.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **hotelini, kaimati, hamu**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi watoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Helena alinawa mikono akiwa wapi? *(Hotelini)*

**T**: Helena alinunua nini? *(Kaimati na kahawa tamu)*

**U:** Wewe hufanya nini kabla ya kula chakula? *(Nawa mikono, kusali, kupika, kupakua, kuandaa meza)*

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

Eleza matumizi ya **huyu** na **hawa.** Huyu hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. Hawa hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

## Zoezi

Mwanafunzi ajaze mapengo kwa jibu sahihi kwenye **ukurasa wa 48.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi akamilishe sentensi zifuatazo kwa kuzingatia matumizi ya **huyu** na **hawa.**

1. Huyu anakata kucha. (Hawa wanakata kucha.)
2. Huyu anachana nywele. (Hawa wanachana nywele.)
3. Hawa wanaoga. (Huyu anaoga.)

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 49: Usafi wa mwili 1

Kipindi cha 48 na 49 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 48**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **h** **l** **e**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  h a **ha** h o **ho** h u **hu** h e **he**

- Soma silabi na maneno.

  ha mu **hamu** ka ha wa **kahawa** ho te li ni **hotelini** He le na **Helena**

**Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Jaza mapengo kwa jibu sahihi.

1. Watoto ________ wanasugua meno. (hawa, huyu)
2. Kijana ________ anafua nguo. (hawa, huyu)
3. Msichana ________ ana nywele ndefu. (hawa, huyu)

**Kusoma hadithi**

**Hotelini**

Helena alinawa mikono hotelini ikawa safi. Alinunua kaimati na kahawa tamu. Alikuwa na hamu ya kahawa tamu. Mama alinawa na kuketi kitini. Aliletewa wali kwa maini. Hakutaka kahawa tamu na kaimati kama Helena.



Mali ya Serikali ya Kenya 48

Kipindi cha 48 na 49 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 49**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **H** **h**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  h i **hi** w i **wi** l i **li** k i **ki**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  a li nawa **alinawa** a li nunua **alinunua**

  a li letewa **aliletewa** ha ku taka **hakutaka**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Makomo na Chifu**



49 Hakiluzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** H

**U:** Endelea na herufi h

Mwanafunzi ataje jina la herufi na kutamka sauti yake kwenye **ukurasa wa 49.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti kusoma silabi.

**N/T/U:** /h/ /i/ silabi ni hi

**U:** Endelea na wi, li, ki

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 49.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno. Unganisha sehemu hizo na usome neno upesi.

**N/T/U:** a li nawa - alinawa

**U:** Endelea na maneno alinunua, aliletewa

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 49.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 48.**

### Hadithi ya mwalimu

**Makomo na Chifu**

Makomo alikuwa mtoto aliyependa kuranda randa. Tabia zake hazikupendeza. Kila wakati alipatikana na makosa. Alikuwa mchafu pia. Wazazi wake walihuzunika. "Huyu mtoto anatusumbua sana, " mama yake alisema.

Kila siku afya ya Makomo ilidhoofika. Alivaa nguo chafu. Kucha zilikuwa ndefu na chafu. Hakuchana nywele zake. Siku moja Makomo alishikwa na kupelekwa kwa chifu. Chifu alimhurumia. Alisema, "Nataka kukurudisha shuleni. Uwaheshimu wazazi wako." Makomo aliomba msamaha. Alikubali kurudi shuleni. Alikata kucha na kusafisha nguo zake. Alinyoa nywele na kuoga akawa safi. Walimu na wanafunzi walimkaribisha kwa shangwe na nderemo. Aliendelea na masomo bila tatizo.

Funza maana ya maneno haya: **chafu, kucha**. Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiku utabiri.

### Maswali

**T:** Kila wakati Makomo alipatikana na nini? *(Makosa)*

**T:** Chifu alimwambia nini Makomo? *(Kuwa alitaka kumrudisha shuleni.)*

**U:** Mwanafunzi safi hufanya nini? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi apewe kadi za maneno asome kwa sauti katika vikundi.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno matano yaliyo na herufi alizofunzwa.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 50: Usafi wa mwili 1

Kipindi cha 50 **Usafi wa mwili 1**

**Kipindi 50**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

h H　　i I　　w W　　e E

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: li wa - liwa**

| | | |
|---|---|---|
| ho | wa | li |
| mu | te | ha |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi hizi katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu** anacheka. | 1. **Hawa** wanacheka. |
| 2. Mtoto **huyu** anatembea. | 2. Watoto **hawa** wanatembea. |
| 3. Nguo ya **huyu** ni safi. | 3. Nguo za **hawa** ni safi. |
| 4. **Huyu** anapendeza. | 4. **Hawa** wanapendeza. |

**Zoezi: Kuandika**

Andika maneno haya kwenye daftari lako.

1. Kucha
2. Maji
3. Sabuni

Mali ya Serikali ya Kenya　　50

## Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**U:** Mwanafunzi ataje jina la herufi na kutamka sauti yakee kwenye **ukurasa wa 50.**

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi **li** na **wa** kuandika neno **liwa.**

**T:** Unda neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Mpe mwanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 50.**

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

Eleza matumizi ya **huyu** na **hawa.** Huyu hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. Hawa hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi. Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 50.**

## Kuandika maneno

**T**: Rejelea usafi wa mwili.

**U**: Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 50.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi kuhusu sehemu za mwili za nje. kwa mfano kukata kucha, kunyoa nywele, kusafisha nguo, kuoga, kunawa mikono, msafi

## Kazi ya nyongeza

Onyesha mlezi wako jinsi ya kukata kucha.

Tarehe: ____________________　Muda: ______________　Idadi: ______________



Hakiuzwi

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 1**

**Kipindi 51**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**a** **k** **l** **t**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| l a | k i | t u | k o |
|---|---|---|---|
| **la** | **ki** | **tu** | **ko** |

● Soma silabi na maneno.

| ta la ka | a li ke ti | te le ke za |
|---|---|---|
| **talaka** | **aliketi** | **telekeza** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Mimi** ni**na**osha sikio. | 1. **Sisi** tu**na**osha masikio. |
| 2. **Mimi** ni**na**kata ukucha. | 2. **Sisi** tu**na**kata kucha. |
| 3. **Mimi** ni**na**fumba jicho. | 3. **Sisi** tu**na**fumba macho. |

**Kusoma hadithi**

**Ayoo**



Ayoo ni mtoto. Baba yake ni Otieno. Mama yake anaitwa Kanini. Ayoo hukaa na babu yake katika kaunti ya Kiambu. Ayoo huletewa mayai na shangazi yake Zainabu. Bibi humpa mabuyu. Ayoo hutamani chakula kitamu zaidi ya mabuyu. Yeye huomba ili babu yake apate mali.

51

Hakiuzwi

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 1**

**Kipindi 52**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**A a** **K k** **L l** **T t**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| k e | l i | t a | a |
|---|---|---|---|
| **ke** | **li** | **ta** | **a** |

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu kaa | hu letewa |
|---|---|
| **hukaa** | **huletewa** |
| hu tamani | hu omba |
| **hutamani** | **huomba** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Safari ya Kimtai**



Mali ya Serikali ya Kenya

52

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/a/**. Taja neno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** amka, embe

**U:** alika, omba, ahadi, uki, akiba

**U:** Endelea na sauti **/k/**: kaka, kata, tafuta, kichwa, kuoga, taka, kitu, kesha

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **t** na utamke sauti yake.

**U**: Endelea na **k, l, a.** Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 51.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti katika silabi. Unganisha sauti kusoma silabi.

**N/T/U:** /l/ /a/ silabi ni la

**U:** Endelea na ki, tu.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 51.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ta la ka - talaka, a li ke ti - aliketi

**U:** telekeza

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 51.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kaunti, mabuyu, mali**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ayoo na babu yake wanaishi wapi? *(Kaunti ya Kiambu)*

**T:** Je, Ayoo husali kila siku kwa nini? *(Kumuombea babu yake awe na mali.)*

**U:** Unafikiri kama Ayoo na babu yake wangepata mali wangefanya nini? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Umoja na wingi**

Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika, kwa mfano: **M**walimu - **Wa**limu

### Zoezi

Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 51.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike herufi mara tano katika kitabu chake: A, a, K, k

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 1**

**Kipindi 51**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

a  k  l  t

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

l a → **la**  k i → **ki**  t u → **tu**  k o → **ko**

● Soma silabi na maneno.

ta la ka → **talaka**  a li ke ti → **aliketi**  te le ke za → **telekeza**

◆ **Sarufi: Matumizi ya nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Mimi** ni**na**osha sikio. | 1. **Sisi** tu**na**osha masikio. |
| 2. **Mimi** ni**na**kata ukucha. | 2. **Sisi** tu**na**kata kucha. |
| 3. **Mimi** ni**na**fumba jicho. | 3. **Sisi** tu**na**fumba macho. |

**Kusoma hadithi**

**Ayoo**



Ayoo ni mtoto. Baba yake ni Otieno. Mama yake anaitwa Kanini. Ayoo hukaa na babu yake katika kaunti ya Kiambu. Ayoo huletewa mayai na shangazi yake Zainabu. Bibi humpa mabuyu. Ayoo hutamani chakula kitamu zaidi ya mabuyu. Yeye huomba ili babu yake apate mali.

51 Hakiuzwi

Kipindi cha 51 na 52 **Marejeleo 1**

**Kipindi 52**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

A a  K k  L l  T t

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

k e → **ke**  l i → **li**  t a → **ta**  a → **a**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

hu kaa → **hukaa**  hu letewa → **huletewa**

hu tamani → **hutamani**  hu omba → **huomba**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Safari ya Kimtai**



Mali ya Serikali ya Kenya  52

## ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** A

**U:** Endelea na herufi a, K, k, L, l, T, t

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 52.**

## ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti unganisha sauti na kusoma silabi.

**N/T/U:** /k/ /e/ ke

**U:** Endelea na le ta a

Soma silabi kwenye **ukurasa wa 52.**

## Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'hu kaa' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'hukaa' kwa upesi.

**U:** Endelea na maneno: huletewa, hutamani, huomba. Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 52.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 51.**

## Hadithi ya mwalimu

**Safari ya Kimtai**

Mwezi wa Aprili umefika. Huu ni mwezi wa likizo. Kimtai na Korir ni pacha. Wana umri wa miaka saba. "Baba ulisema tutasafiri nyumbani Baringo shule zikifungwa. Je, tutaenda lini?" aliuliza Kimtai. "Kesho asubuhi," alijibu baba.

Alhamisi asubuhi walianza safari. Waliabiri gari la moshi. Gari hilo lilipitia mbuga ya wanyama ya Tsavo. Huko Kimtai aliwaona ndovu, nyani na twiga. Walipofika Nairobi waliabiri basi hadi Baringo - mjini walikoishi mama na dada yao Kerubo.

"Tumefika nyumbani," alisema Korir. Kimtai alikimbia na kumkumbatia dada yao huku akicheka kwa furaha. Dada na mama yao walifurahi kuwaona. Kimtai na Korir walioga, wakala na kulala.

Funza maana ya maneno: **umri, alhamisi.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikilize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## ? Maswali

1. Taja majina ya pacha wahusika. *(Kimtai na Korir)*
2. Nyumbani kwa akina Korir ni wapi? *(Baringo)*
3. Zaidi ya wazazi taja watu wengine unaofaa kuwatembelea katika familia. *(Kubali majibu sahihi.)*

## Zoezi

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno ya msamiati aliousoma.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike herufi **l** na **t** kubwa na ndogo mara tano tano katika vitabu vyao.

Tarehe: ____________________  Muda: ______________  Idadi: ______________

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 1**

**Kipindi 53**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**m** **n** **o** **u**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

m a — **ma** n i — **ni** o — **o** u — **u**

● Soma silabi na maneno.

a ma ni — **amani** no mi no — **nomino** mi mi na — **mimina** hu ko — **huko**

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza**

Soma sentensi zifuatazo katika vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Mimi** nina kitabu. | 1. **Sisi** tuna vitabu. |
| 2. **Mimi** nina kalamu. | 2. **Sisi** tuna kalamu. |
| 3. **Mimi** nina kifutio. | 3. **Sisi** tuna vifutio. |

**Kusoma hadithi**

**Wasia wa babu**

**Babu:** Karibia. Sikilizeni wasia huu. Nawasihi msome. Masomo huleta hekima. Hekima huleta mali.

**Watoto:** Naam, Babu. Sisi sote tutasoma. Usiwe na wasiwasi.



Hakluzwi

53

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 1**

**Babu:** Msisahau kuwasiliana na walimu wenu na kukaa kwa amani.

**Watoto:** Naam, babu. Hatutasahau. Asante kwa wasia wako.

**Kipindi 54**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**M m** **N n** **O o** **U u**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

m e — **me** n i — **ni** o — **o** u — **u**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

na wa sihi — **nawasihi** m ta wa somea — **mtawasomea**

ha tu ta sahau — **hatutasahau**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kibibi mtiifu**



Mali ya Serikali ya Kenya

54

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/m/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** mama, kiti

**U:** mkono, dawati, mtini, laki, mafunzo, futa

**U:** Endelea na sauti **/u/**: ubao, hukumu, umri, nyuso

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi **m** na utamke sauti yake.

**U:** m

**N/T/U:** Endelea na herufi n, o, u

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 53**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na kusoma silabi.

**N/T/U:** /m/ /a/ silabi ni ma

**U:** Endelea na silabi ni, o, u

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 53**.

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma silabi katika kila neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** a ma ni - amani

**U:** Endelea na mimina, huko, nomino

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza kwenye **ukurasa wa 53.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno: **wasia**, **kuwasiliana**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U**: Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Babu aliwasihi watoto wafanye nini? *(Aliwasihi watoto wasome.)*

**T:** Babu alisema masomo huleta nini? *(Alisema masomo huleta hekima.)*

**U:** Je, ungependa kufanya kazi gani ukiwa mkubwa? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Umoja na wingi**

Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika, kwa mfano: **K**iti - **V**iti.

### Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi kwenye **ukurasa wa 53.**

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike herufi kubwa na ndogo zifuatazo mara tano tano katika vitabu vyao.

M ________________ m ________________

U ________________ u ________________

Tarehe: ____________________________ Muda: ___________________ Idadi: __________________

# Kipindi cha 54: Marejeleo

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 1**

**Kipindi 53**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **m**    **n**    **o**    **u**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  m a → **ma**    n i → **ni**    o → **o**    u → **u**

- Soma silabi na maneno.

  a ma ni → **amani**    no mi no → **nomino**    mi mi na → **mimina**    hu ko → **huko**

**Sarufi: Nafsi ya kwanza**

Soma sentensi zifuatazo katika vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Mimi** nina kitabu. | 1. **Sisi** tuna vitabu. |
| 2. **Mimi** nina kalamu. | 2. **Sisi** tuna kalamu. |
| 3. **Mimi** nina kifutio. | 3. **Sisi** tuna vifutio. |

**Kusoma hadithi**

**Wasia wa babu**

**Babu:** Karibia. Sikilizeni wasia huu. Nawasihi msome. Masomo huleta hekima. Hekima huleta mali.

**Watoto:** Naam, Babu. Sisi sote tutasoma. Usiwe na wasiwasi.



53

Hakiuzwi

Kipindi cha 53 na 54 **Marejeleo 1**

**Babu:** Msisahau kuwasiliana na walimu wenu na kukaa kwa amani.

**Watoto:** Naam, babu. Hatutasahau. Asante kwa wasia wako.

**Kipindi 54**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **M m**    **N n**    **O o**    **U u**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  m e → **me**    n i → **ni**    o → **o**    u → **u**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  na wa sihi → **nawasihi**    m ta wa somea → **mtawasomea**

  ha tu ta sahau → **hatutasahau**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kibibi mtiifu**



Mali ya Serikali ya Kenya

54

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** M
**U:** Endelea na herufi m, N, n, O, o, U, u
Mwanafunzi asome jina la herufi na kutamka sauti yake kwenye **ukurasa wa 54**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti unganisha sauti na kusoma silabi.
**N/T/U:** /m/ /e/ silabi ni me
**U:** Endelea na silabi ni, o, u
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 54.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'na wa sihi' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'nawasihi' upesi.
**U:** Endelea na maneno: tutasoma, hatutasahau
Mwanafunzi asomeane maneno aliyojifunza vitabuni mwake kwenye **ukurasa wa 54.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 53.**

### Hadithi ya mwalimu

**Kibibi mtiifu**

Kengele ilipolia, wanafunzi walitoka darasani. Walielekea nyumbani kwa chakula cha mchana. Kibibi alikuwa wa mwisho kutoka darasani. Alimuaga mwalimu na kukimbia haraka hadi nyumbani. Chakula kilipoiva, Kibibi alikula haraka na kurudi shuleni. Aliwapita wanafunzi wengine waliojikokota kurudi shuleni. Mwalimu alimpongeza kwa kuzingatia wakati. Jioni ya siku hiyo,wazazi wake Kibibi walimfuata shuleni. Walimchukua Kibibi na kumnunulia nguo mbili za kupendeza. Tabia nzuri ya Kibibi ilimfanya kupendwa na walimu wake shuleni na wazazi wake nyumbani. Ni muhimu watoto kuwa na tabia njema. Watoto wenye tabia njema hupata zawadi kutoka kwa walimu na wazazi wao.

Funza maana ya neno mapya: **mbili, zawadi.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi. Mwanafunzi asikilize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kibibi alikuwa wa ngapi kutoka darasani? *(Wa mwisho.)*
**T:** Kibibi alifanya nini alipofika nyumbani? *(Kibibi alikila chakula chake haraka na kurudi shuleni.)*
**U:** Je, ukiwa na tabia njema mzazi wako hukufanyia nini? *(Kubali jibu lolote sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi asome maneno haya: amani, nomino, hatutawasahau, nawasili, mimina

### Kazi ya ziada

Wanafunzi watunge sentensi kwa kurejelea msamiati waliousoma.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 55: Marejeleo

Kipindi cha 55 **Marejeleo 1**

**Kipindi 55**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

aA kK lL mM nN oO tT uU

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: m ke ka – mkeka**

| | | | |
|---|---|---|---|
| tu | ka | m | na |
| ne | ku | o | ke |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Nakili sentensi zifuatazo.

1. Hili ni tunda **langu**.
2. Chakula **chetu** kimeletwa.
3. Maziwa **yangu** yamemwagika.
4. Huyu ni mtoto **wangu**.
5. Viti **vyetu** vimevunjika.
6. Mwalimu **wangu** ni mzuri.
7. Basi **letu** limeharibika.
8. Nguo **yangu** ni fupi.
9. Barabara **yetu** haipitiki.
10. Kalamu **yangu** imepotea.

**Zoezi: Kuandika**

Andika herufi kubwa

a m u k w e o t n h

55

Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** a

**U:** Endelea na herufi: A, k, K, l, L, m, M, n, N, o, O, t, T, u, U.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 55.**

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi zote. Tumia silabi **ku ku** kuandika neno **kuku.**

**T:** Unda neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mpe mwanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 55.**

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: kitabu changu - vitabu vyetu.

Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 55.**

## Kuandika

**T:** Rejelea uakifishaji - matumizi ya herufi kubwa.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 55.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno yaliyo na sauti walizosoma.

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi ajadiliane na mlezi kuhusu sehemu za mwili zinazopaswa kuangaziwa zaidi katika usafi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

# Kipindi cha 56: Vyakula vya kiasili 1

Kipindi cha 56 na 57 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 56**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

b o u

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| b o | b u | b a | b e |
|---|---|---|---|
| **bo** | **bu** | **ba** | **be** |

- Soma silabi na maneno.

| bo ga | mbo ga | a na li la | a na se ma |
|---|---|---|---|
| **boga** | **mboga** | **analila** | **anasema** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo katika vikundi.

| -angu | -etu |
|---|---|
| 1. Tunda **langu** limeiva. | 1. Matunda **yetu** yameiva. |
| 2. Chakula **changu** kimeiva. | 2. Vyakula **vyetu** vimeiva. |
| 3. Muhogo **wangu** umekomaa. | 3. Mihogo **yetu** imekomaa. |

**Kusoma hadithi**

**Boga tamu**

Baba ana boga. Tunu anataka kulila boga hilo. Tunu anaomba baba boga. Analila boga. "Asante, baba. Boga hili ni tamu," Tunu anasema. "Hebu tule wali kwa mboga sasa," Baba anasema.



Mali ya Serikali ya Kenya

56

Kipindi cha 56 na 57 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 57**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

B b

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na omba | a na sema | a li babaika |
|---|---|---|
| **anaomba** | **anasema** | **alibabaika** |
| a li burudika | a li bobea | |
| **aliburudika** | **alibobea** | |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Muhogo wa nazi**



57

Hakiuzwi

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/b/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** boga, mboga

**U:** boga, embe, buchari, cheche

## Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **b** na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi **o** na **u.**

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 56.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti ili kusoma silabi.

**N/T/U:** /b/ /o/ bo

**U:** Endelea na bu, ba, be

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 56.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** bo ga - boga

**U:** analila, anasema , mboga

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 56.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **boga, mboga**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N**: Nani alikuwa na boga? *(Baba alikuwa na boga.)*

**T:** Nani alitaka kula boga? *(Tunu alitaka kula boga.)*

**U:** Unapenda chakula gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na –etu.**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: kitabu **changu** - vitabu **vyetu.**

Wanafunzi wasome sentensi kwenye **ukurasa wa 56.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike herufi hizi: **b, B, o** mara tano tano katika daftari lake.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 57: Vyakula vya kiasili 1

Kipindi cha 56 na 57 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 56**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**b** **o** **u**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| b o | b u | b a | b e |
|---|---|---|---|
| **bo** | **bu** | **ba** | **be** |

● Soma silabi na maneno.

| bo ga | mbo ga | a na li la | a na se ma |
|---|---|---|---|
| **boga** | **mboga** | **analila** | **anasema** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo katika vikundi.

| -angu | -etu |
|---|---|
| 1. Tunda **langu** limeiva. | 1. Matunda **yetu** yameiva. |
| 2. Chakula **changu** kimeiva. | 2. Vyakula **vyetu** vimeiva. |
| 3. Muhogo **wangu** umekomaa. | 3. Mihogo **yetu** imekomaa. |

**Kusoma hadithi**

**Boga tamu**



Baba ana boga. Tunu anataka kulila boga hilo. Tunu anaomba baba boga. Analila boga. "Asante, baba. Boga hili ni tamu," Tunu anasema. "Hebu tule wali kwa mboga sasa," Baba anasema.

Mali ya Serikali ya Kenya 56

Kipindi cha 56 na 57 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 57**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**B** **b**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na omba | a na sema | a li babaika |
|---|---|---|
| **anaomba** | **anasema** | **alibabaika** |
| a li burudika | a li bobea | |
| **aliburudika** | **alibobea** | |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Muhogo wa nazi**



57 Hakiluzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** B

**U:** Endelea na herufi b.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 57**.

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo na kusoma neno lote upesi.

**N/T/U:** a na se ma - anasema

**U:** Endelea na maneno: alibabaika, aliburudika, alibobea

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 57**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 56**.

### Hadithi ya mwalimu

**Muhogo wa nazi**

Saumu alipofika nyumbani kutoka shuleni, alielekea jikoni alikokuwa mama yake. "Shikamoo mama!" "Marahaba mwanangu," Mama alijibu. "Mmmhh! Ni nini chanukia hivyo?" Saumu aliuliza. Mama alisema wamepika muhogo wa nazi kwa samaki.

Mama alimwambia amsubiri kaka yake wale pamoja. "Hodi! nimefika," baba yake Saumu alibisha. Saumu alifungua mlango. Baba pamoja na kaka yake waliingia ndani. "Shikamoo baba! Kaka hujambo?" Saumu aliwasalimia. Mama aliwakaribisha na kuwapakulia mihogo, nusura mate yamdondoke Saumu! Alikimbia harakaharaka kunawa mikono. Walikula muhogo kwa samaki wakashiba. "Asante mama kwa chakula kitamu," Saumu alisema.

Funza maana ya maneno mapya: **muhogo, nazi, samaki.** Soma kichwa cha hadithi. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi na mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Saumu alikuwa amefika nyumbani kutoka wapi? *(Shuleni)*

**T:** Mama alikuwa amepika nini? *(Muhogo wa nazi kwa samaki)*

**U:** Ni kwa nini ni muhimu watu kula pamoja? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi atambue sauti /b/ katika maneno: boga, baba, bakuli, anabatiza.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno matano yaliyo na herufi lengwa.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 58: Vyakula vya kiasili 1

Kipindi cha 58 na 59 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 58**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  s   b   o

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  s e → **se**   s i → **si**   s o → **so**   s u → **su**

- Soma silabi na maneno.

  bo ko bo ko → **bokoboko**   bi si → **bisi**   ku ta ba sa mu → **kutabasamu**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Haya ni matunda **yetu**.
2. Kitunguu **changu** kimeoza.
3. Boga **langu** limeiva.

**Kusoma hadithi**

**Biskuti**

Asubuhi Sara, Saumu na Salim waliamka. Walitaka kula biskuti. Mkebe wa biskuti ulikuwa kabatini. Salim alitoa bakuli la bokoboko na la bisi. Aliinua mkebe wa biskuti. Wakala biskuti na kutabasamu.



Mali ya Serikali ya Kenya

58

Kipindi cha 58 na 59 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 59**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  S   s

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  wa li amka → **waliamka**   wa li taka → **walitaka**   ku tabasamu → **kutabasamu**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Orinda na mbwa**



59

Hakiuzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/s/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.
**N/T/U:** supu, chai
**U:** sare, bisi, sungura, zima, sehemu

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi s na utamke sauti yake.
**U:** Endelea na herufi **b** na **o**.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 58.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:** /s/ /e/ se
**U:** Endelea na si, so, su
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 58.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** bo ko bo ko - bokoboko
**U:** kutabasamu, samaki, bisi
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 58.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **bokoboko, bisi, kutabasamu**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

N: Ni akina nani waliamka asubuhi? *(Sara, Saumu na Salim waliamka asubuhi.)*
T: Walitaka kula nini? *(Walitaka kula biskuti.)*
U: Wewe hula nini asubuhi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu.**
**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: kiti **changu** - viti **vyetu.**

### Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi kwenye **ukurasa wa 58.**

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike herufi **S** mara tano katika vitabu vyao.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 59: Vyakula vya kiasili 1

Kipindi cha 58 na 59 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 58**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **s** **b** **o**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  s e **se** s i **si** s o **so** s u **su**

- Soma silabi na maneno.

  bo ko bo ko **bokoboko** bi si **bisi** ku ta ba sa mu **kutabasamu**

**Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Haya ni matunda **yetu**.
2. Kitunguu **changu** kimeoza.
3. Boga **langu** limeiva.

**Kusoma hadithi**

**Biskuti**

Asubuhi Sara, Saumu na Salim waliamka. Walitaka kula biskuti. Mkebe wa biskuti ulikuwa kabatini. Salim alitoa bakuli la bokoboko na la bisi. Aliinua mkebe wa biskuti. Wakala biskuti na kutabasamu.



Mali ya Serikali ya Kenya

58

Kipindi cha 58 na 59 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 59**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **S** **s**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  wa li amka **waliamka** wa li taka **walitaka** ku tabasamu **kutabasamu**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Orinda na mbwa**



59 Hakiluzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** S
**U:** Endelea na herufi s.
Wanafunzi wataje majina ya herufi na watamke sauti kwenye **ukurasa wa 58.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'wa li taka' kisha uunganishe sehemu hizo usome neno 'walitaka' upesi.
**U:** Endelea na maneno: waliamka, kutabasamu
Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 58.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 58.**

### Hadithi ya mwalimu

**Orinda na mbwa**

Orinda alipenda kufanya kazi mbalimbali. Alifuga sungura na kulinda shamba lao kwa kutumia mbwa. Mbwa wake alijulikana kama Pulo. Ungemsikia Orinda akimwita mbwa wake, "Pulo! Pulo! Sususuu!, njoo!" Naye Pulo angesogea karibu. Angetoa sauti ya kuitikia huku akitikisa mkia kwa furaha.
Orinda alipenda kulinda mimea mwitu isiharibiwe na sungura. Pulo alifukuzana na sungura hao siku nzima ili wasiharibu mimea. Nyumbani, Orinda alikuwa amejenga kibanda kidogo cha kufugia sungura.
Orinda aliwashangaza watu waliomtembelea. Alikuwa akiwapatia sungura hata mboga. Aina ya mboga waliyopewa sungura ni kama karoti na kabeji. Sungura hao wa kufuga walipenda sana mboga. Watu wengi walikuwa wakifika kwa Orinda kununua sungura. Pulo aliwalinda sungura wale. Nyama ya sungura ni tamu kama ya kuku.

Funza maana ya maneno mapya: **sungura, mboga.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Orinda alipenda kuwinda kwa kutumia nini? *(Mbwa)*

**T:** Sungura walipewa aina gani ya vyakula? *(Kabeji na karoti.)*

**U:** Unafikiri ni kwa nini watu walinunua sungura kwa Orinda? *(Kubali majibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi atambue vyakula mbalimbali vya kiasili kwa kutumia vyakula halisi, picha na michoro

### Kazi ya ziada

Wanafunzi watunge sentensi kwa kurejelea msamiati wa vyakula vya kiasili.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 60 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 60**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**b B** **s S**

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Mfano: bo ga - boga**

| | | |
|---|---|---|
| ki | ma | ho |
| m | go | ti |
| bo | sa | ga |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Somea mwenzako sentensi zifuatazo.

1. Tunda **langu** ni hili.
2. Chakula **chetu** kimeletwa.
3. Maziwa **yangu** yamemwagika.
4. Hawa ni watoto **wetu**.
5. Kiti **changu** kimevunjika.
6. Walimu **wetu** ni wazuri.
7. Mabasi **yetu** yameharibika.

**Zoezi: Kuandika**

Chora matunda haya.

1. chungwa
2. ndizi
3. embe

Mali ya Serikali ya Kenya 60

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** b

**U:** Endelea na herufi B, S na s.

Wanafunzi wataje majina ya herufi na watamke sauti zao kwenye **ukurasa wa 60.**

## Jedwali la silabi

**N/T/U:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi 'ki ma' kuandika neno 'kima'. Soma neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 60.**

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na –etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Simu **yangu** - Simu **zetu**

Wanafunzi wasome sentensi zote kwenye **ukurasa wa 60** wakisisitiza sarufi husika. Kisha wanakili sentensi hizo kwenye madaftari yao.

## Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika: **sungura, supu**

## Kuandika

**T:** Rejelea vyakula vya kiasili.

**U:** Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 60.**

## Kazi ya ziada

Wanafunzi wafinyange maumbo ya herufi walizosoma: **b, B; s, S**

## Kazi ya nyongeza

Katika makundi mawili wanafunzi wawe na mjadala kuhusu umuhimu wa vyakula vya kiasili.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 61: Vyakula vya kiasili 1

Kipindi cha 61 na 62 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 61**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**y** **s** **b**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| y a | y i | y o | y u | s e |
|---|---|---|---|---|
| **ya** | **yi** | **yo** | **yu** | **se** |

● Soma silabi na maneno.

| ya ya | he ka ya | ma ya i | ya nge ya nge |
|---|---|---|---|
| **yaya** | **hekaya** | **mayai** | **yangeyange** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Maziwa **yangu** yamemwagika. | 1. Maziwa **yetu** yamemwagika. |
| 2. Chakula **changu** kimepikwa. | 2. Vyakula **vyetu** vimepikwa. |
| 3. Muhogo **wangu** umekomaa. | 3. Mihogo **yetu** imekomaa. |

**Kusoma hadithi**

**Yaya Yerusa**



Yaya wetu anaitwa Yerusa. Kila asubuhi yeye hutuokea keki. Keki huwa ya bokoboko, mabuyu na mayai. Kabla ya kulala Yerusa hutusomea hekaya tamutamu. Leo atatusomea kuhusu yangeyange na yai lake.

61 Hakluzwi

Kipindi cha 61 na 62 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 62**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Y** **y**


■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na itwa | hu tu okea |
|---|---|
| **anaitwa** | **hutuokea** |
| hu tu somea | a ta tu somea |
| **hutusomea** | **atatusomea** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vyakula mbalimbali**



Mali ya Serikali ya Kenya 62

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/y/**. Soma maneno. Wanafunzi waonyeshe kidole juu wakisikia sauti mwanzoni mwa neno au waonyeshe kidole chini wasiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** yetu, kibuyu

**U:** yaliyomo, hiyo, yaya, saa

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **y** na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi s na **b.**

Wanafunzi wataje majina ya herufi na watamke sauti zao kwenye **ukurasa wa 61.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /y/ /e/ - ye

**U**: Endelea na ni ,ye, yi, yo, yu, se

Wanafunzi wasome silabi kwenye **ukurasa wa 61.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** he ka ya - hekaya

**U:** yaya, mayai, yangeyange

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 61.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **yaya, hutuokea, hekaya.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N**: Taja jina la yaya. *(Jina la yaya ni Yerusa.)*

**T**: Yaya huoka nini kila asubuhi? *(Huoka keki.)*

**U:** Nani huwapikia chakula kwenu? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na –etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Embe **langu** - Maembe **yetu**

### Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi kwenye **ukurasa wa 61.**

Wanafunzi watumie teknolojia (papaya) kutamkia sauti **/y/**.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 61: Vyakula vya kiasili 1

Kipindi cha 61 na 62 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 61**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**y** **s** **b**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| y a | y i | y o | y u | s e |
|---|---|---|---|---|
| **ya** | **yi** | **yo** | **yu** | **se** |

- Soma silabi na maneno.

| ya ya | he ka ya | ma ya i | ya nge ya nge |
|---|---|---|---|
| **yaya** | **hekaya** | **mayai** | **yangeyange** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Maziwa **yangu** yamemwagika. | 1. Maziwa **yetu** yamemwagika. |
| 2. Chakula **changu** kimepikwa. | 2. Vyakula **vyetu** vimepikwa. |
| 3. Muhogo **wangu** umekomaa. | 3. Mihogo **yetu** imekomaa. |

**Kusoma hadithi**

**Yaya Yerusa**



Yaya wetu anaitwa Yerusa. Kila asubuhi yeye hutuokea keki. Keki huwa ya bokoboko, mabuyu na mayai. Kabla ya kulala Yerusa hutusomea hekaya tamutamu. Leo atatusomea kuhusu yangeyange na yai lake.

61 Hakiuzwi

Kipindi cha 61 na 62 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 62**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Y** **y**


- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na itwa | hu tu okea |
|---|---|
| **anaitwa** | **hutuokea** |
| hu tu somea | a ta tu somea |
| **hutusomea** | **atatusomea** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vyakula mbalimbali**



Mali ya Serikali ya Kenya 62

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi zenye kuhusisha **-angu** na **-etu**. Kisha asomee mzazi au mlezi wake nyumbani

1. Maziwa yangu yamemwagika.

   Maziwa yetu yamemwagika

2. Chakula changu kimepikwa

   Chakula chetu kimepikwa

3. Muhogo wangu umekomaa.

   Muhogo wetu umekomaa

4. Viazi vyangu vimechongwa.

   Viazi vyetu vimechongwa.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 62: Vyakula vya kiasili 1

**Kipindi cha 61 na 62** Vyakula vya kiasili 1

**Kipindi 61**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**y** **s** **b**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| y a | y i | y o | y u | s e |
|---|---|---|---|---|
| **ya** | **yi** | **yo** | **yu** | **se** |

● Soma silabi na maneno.

| ya ya | he ka ya | ma ya i | ya nge ya nge |
|---|---|---|---|
| **yaya** | **hekaya** | **mayai** | **yangeyange** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Maziwa **yangu** yamemwagika. | 1. Maziwa **yetu** yamemwagika. |
| 2. Chakula **changu** kimepikwa. | 2. Vyakula **vyetu** vimepikwa. |
| 3. Muhogo **wangu** umekomaa. | 3. Mihogo **yetu** imekomaa. |

**Kusoma hadithi**

**Yaya Yerusa**



Yaya wetu anaitwa Yerusa. Kila asubuhi yeye hutuokea keki. Keki huwa ya bokoboko, mabuyu na mayai. Kabla ya kulala Yerusa hutusomea hekaya tamutamu. Leo atatusomea kuhusu yangeyange na yai lake.

61

Hakluzwi

**Kipindi cha 61 na 62** Vyakula vya kiasili 1

**Kipindi 62**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Y** **y**


■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na itwa | hu tu okea |
|---|---|
| **anaitwa** | **hutuokea** |
| hu tu somea | a ta tu somea |
| **hutusomea** | **atatusomea** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vyakula mbalimbali**



Mali ya Serikali ya Kenya

62

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** Y

**U:** Endelea na herufi y.

Wanafunzi wataje majina ya herufi na watamke sauti zao kwenye **ukurasa wa 62.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Soma sehemu za neno 'a na itwa' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'anaitwa' upesi.

**U:** Endelea na maneno: hutuokea, hutusomea, atatusomea

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 62.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 61.**

### Hadithi ya mwalimu

**Vyakula mbalimbali**

Chakula ni muhimu mwilini. Mtu asipokula vizuri hatakuwa na afya nzuri. Hatakuwa na nguvu za kufanya kazi. Atashikwa na magonjwa na hatapona haraka. Chakula pia hutusaidia kukua.

Kuna vyakula vya aina mbalimbali. Kuna vyakula vya kujenga mwili. Vyakula hivi ni kama vile nyama, mayai, maziwa, maharagwe na samaki.

Pia kuna vyakula vya kulinda mwili. Vyakula hivi huzuia watu kupatwa na magonjwa mbalimbali. Vyakula hivi ni mboga kama kabeji, sukumawiki, mchicha na karoti.

Matunda ni kama maembe, machungwa, ndizi na ndimu. Vilevile kuna vyakula kama mahindi, mchele na viazi. Vyakula hivi huupa mwili nguvu.

Funza maana ya maneno mapya: **mchicha, maharagwe, matunda.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri. Soma hadithi, wanafunzi wasikize huku wakitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Mtu asiyekula vizuri atapata shida gani? *(Mtu asipokula vizuri hatakuwa na afya nzuri.)*

**T:** Ni vyakula gani vya kujenga mwili? *(Nyama, mayai, maziwa, maharagwe na samaki.)*

**U:** Taja vyakula vingine unavyovijua. *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Wanafunzi waweza kupewa kadi za majina ya vyakula vya kiasili wasome kwa sauti. k. m: viazi, mihogo, mahindi, maharagwe, mboga, matunda.

### Kazi ya ziada

Andika maneno yafuatayo ubaoni:

**Viazi vitamu, maziwa, maharagwe, mchicha, matunda.**

Wanafunzi wayaandike kwenye madaftari yao. Baadaye wawasomee wazazi au walezi wao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 63: Vyakula vya kiasili 1

Kipindi cha 63 na 64 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 63**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

z y s

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| z o | z u | z e | z i | y e |
|---|---|---|---|---|
| **zo** | **zu** | **ze** | **zi** | **ye** |

● Soma silabi na maneno.

| li ki zo | ze ze | za wa di | ma zi wa |
|---|---|---|---|
| **likizo** | **zeze** | **zawadi** | **maziwa** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi hizi kwa sauti, kwenye vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Tunda **langu** ni hili. | 1. Matunda **yetu** ni haya. |
| 2. Chumba **changu** kimefungwa. | 2. Vyumba **vyetu** vimefungwa. |
| 3. Darasa **langu** limeoshwa. | 3. Madarasa **yetu** yameoshwa. |

**Kusoma hadithi**

**Eliza na Lazizi**



Wakati wa likizo Eliza na Lazizi walielekea ziwani. Waliona minazi na mizabibu. Wakala zabibu. Waliwabebea wazazi wao zabibu na nazi. Wazazi waliwanunulia zawadi. Lazizi alizawadiwa zeze. Eliza alinunuliwa miwani.

63 Hakiuzwi

Kipindi cha 63 na 64 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 64**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

Z z

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li tazama | wa li ona |
|---|---|
| **walitazama** | **waliona** |
| wa li wa bebea | wa li wa nunulia |
| **waliwabebea** | **waliwanunulia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kacheche na nyuki**



Mali ya Serikali ya Kenya 64

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/z/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** zabibu, riziki

**U:** zake, walicheza, kazi, zuru, siafu, ziara

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **z** na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi **y** na **s**.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 63.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na kusoma silabi.

**N/T/U:** /z/ /o/ silabi ni zo

**U:** Endelea na silabi zu, ze, zi, ye

Wanafunzi wasome silabi kwenye **ukurasa wa 63.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** li ki zo - likizo

**U:** Endelea na zawadi, maziwa, zeze

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 63.**

### Msamiati

Funza maneno haya: **likizo, zabibu, zeze**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Wanafunzi watoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

### Maswali

**N:** Taja watu wawili walio katika hadithi. *(Eliza, Lazizi na wazazi.)*

**T:** Taja walikokwenda kabla ya kuelekea ziwani? *(Eliza na Lazizi walienda kwenye zizi/zizini.)*

**U:** Taja aina nyingine za matunda unayoyajua? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kiazi kitamu ni **changu.** - Viazi vitamu ni **vyetu.**

### Zoezi

Wanafunzi wafanye zoezi kwenye **ukurasa wa 63.**

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike herufi kubwa na ndogo y na z.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 63 na 64 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 63**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

z y s

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

z o — **zo** | z u — **zu** | z e — **ze** | z i — **zi** | y e — **ye**

- Soma silabi na maneno.

li ki zo — **likizo** | ze ze — **zeze** | za wa di — **zawadi** | ma zi wa — **maziwa**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi hizi kwa sauti, kwenye vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Tunda **langu** ni hili. | 1. Matunda **yetu** ni haya. |
| 2. Chumba **changu** kimefungwa. | 2. Vyumba **vyetu** vimefungwa. |
| 3. Darasa **langu** limeoshwa. | 3. Madarasa **yetu** yameoshwa. |

**Kusoma hadithi**

**Eliza na Lazizi**



Wakati wa likizo Eliza na Lazizi walielekea ziwani. Waliona minazi na mizabibu. Wakala zabibu. Waliwabebea wazazi wao zabibu na nazi. Wazazi waliwanunulia zawadi. Lazizi alizawadiwa zeze. Eliza alinunuliwa miwani.

63 Hakluzwi

Kipindi cha 63 na 64 **Vyakula vya kiasili 1**

**Kipindi 64**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

Z z

- Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li tazama — **walitazama** | wa li ona — **waliona**

wa li wa bebea — **waliwabebea** | wa li wa nunulia — **waliwanunulia**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kacheche na nyuki**



Mali ya Serikali ya Kenya 64

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi Z na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi z Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 63.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Soma sehemu za neno 'wa li tazama' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'walitazama' upesi.

**U:** Endelea na maneno: waliona, waliwabebea, waliwanunulia. Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 64** kwenye kitabu chake.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 63.**

### Hadithi ya mwalimu

**Kacheche na nyuki**

Kacheche na ndugu zake walifanya kazi ya kuwachunga wanyama. Vilevile, walitafuta asali ya nyuki. Kila walipoenda kulisha, walibeba vyakula kama viazi vitamu, ndizi na maziwa.

Siku moja, Kacheche alisikia nyuki wakivuma ndani ya mzinga uliokuwa juu ya mti. Kacheche alidhani kuwa mzinga huo ulikuwa na asali.

Ndugu mkubwa alisema, "Hawa nyuki bado wanavuma. Tuendelee kuwachunga wanyama." Kacheche hakufurahishwa na jambo hilo. Alirudi na kuwachokoza wale nyuki.

Nyuki walimshambulia. Kacheche alipiga mayowe, "Mwili wangu! Mwili wangu!"Lakini hapakuwa na wa kumsaidia. Alianguka chini na kuzirai.

Ndugu yake alikuja na kumsaidia asishambuliwe zaidi. Kacheche alipewa huduma ya kwanza. Siku hizi Kacheche hawezi kuwachezea nyuki. Hata hivyo anaipenda asali ya nyuki.

Funza maana ya maneno mapya: **asali, viazi vitamu.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kacheche na ndugu zake walifanya kazi gani? *(Kacheche na ndugu zake walifanya kazi ya kuwachunga wanyama.)*

**T:** Nyuki walikuwa wakivuma wapi? *(Ndani ya mzinga.)*

**U:** Uzuri wa nyuki ni upi? *(Mwanafunzi aelezee jibu lake.)*

### Zoezi

Mwanafunzi ajaze pengo kwa kutumia **-angu** na **-etu** kwenye sentensi zifuatazo.


1. Matunda _____ yameiva.
2. Kikapu _____ kimepotea.
3. Mihogo _____ imepikwa.

### Kazi ya ziada

Andika majina nane ya vyakula unavyovijua.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

# Kipindi cha 65: Vyakula vya kiasili 1


Kipindi cha 65 Vyakula vya kiasili 1

Kipindi 65

Taja jina la herufi na utamke sauti.

y Y z Z s S b B

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno. **Kwa mfano: ma zi wa - maziwa**

| | | |
|---|---|---|
| sa | ya | ki |
| li | ho | wa |
| zi | zo | ma |

**Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi hizi kwa sauti.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Huu ni ukwaju **wangu.** | Hizi ni kwaju **zetu**. |
| 2. Chakula **changu** kimemwagika. | Vyakula **vyetu** vimemwagika. |
| 3. Gari **langu** limeletwa. | Magari **yetu** yameletwa. |
| 4. Mzinga huu ni **wangu**. | Mizinga hii ni **yetu**. |
| 5. Asali **yangu** ni tamu. | Asali **yetu** ni tamu. |

**Zoezi: Kuandika**

Andika majina haya.

1. muhogo
2. viazi vitamu
3. matunda

65 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** Y

**U:** Endelea na herufi y, Z, s, S, b na B.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 65.**

## Jedwali la silabi

**N:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi 'ma zi wa' kuandika neno 'maziwa'. Soma neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno halisi akitumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 65**.

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kalamu **yangu** - Kalamu **zetu.**

Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 65.**

## Kuandika maneno

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika: **mihogo, zambarau**

## Kuandika

**T:** Rejela vyakula vya kiasili.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 65**.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze pengo kwa kutumia **-angu** na **-etu**

| **-angu** | **-etu** |
|---|---|
| 1. Ukwaju ____ huu. (wangu) | Kwaju ____ hizi. (zetu) |
| 2. Chakula ____ kimeletwa. (changu) | Vyakula ____ vimeletwa. (vyetu) |
| 3. Zambarau ____ imeletwa. (yangu) | Zambarau ____ zimeletwa. (zetu) |

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi ajadiliane na mlezi kuhusu vyakula vya kiasili vinavyopatikana katika jamii. Kisha aandike majina ya vyakula hivyo.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________



Hakiuzwi

# Kipindi cha 66: Mimi na wenzangu 2

Kipindi cha 66 na 67 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 66**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **d** **z** **y**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| d o | d u | d i | d e | z e |
|---|---|---|---|---|
| **do** | **du** | **di** | **de** | **ze** |

- Soma silabi na maneno.

| gre di | a ka u mi a | a li ga a ga a | a li m sa i di a |
|---|---|---|---|
| **gredi** | **akaumia** | **aligaagaa** | **alimsaidia** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Huyu ni rafiki **yangu**. | 1. Hawa ni marafiki **zetu**. |
| 2. Huyu ni mzazi **wangu**. | 2. Hawa ni wazazi **wetu**. |
| 3. Huyu ni msichana **wangu**. | 3. Hawa ni wasichana **wetu**. |

**Kusoma hadithi**

**Donadi aumia**



Bidu ni mvulana. Yuko katika gredi ya kwanza. Bidu ana marafiki wawili. Marafiki hawa ni Donadi na Daudi. Jana Donadi aliteguka akaumia. Aligaagaa na kusema, "Bidu! Daudi! Nimeumia." Bidu alimsaidia kukaa na kumtuliza. Daudi alikimbia kumwita mama.

Mali ya Serikali ya Kenya

66

Kipindi cha 66 na 67 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 67**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **D** **d**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li teguka | a li m saidia |
|---|---|
| **aliteguka** | **alimsaidia** |
| ni me umia | ku m tuliza |
| **nimeumia** | **kumtuliza** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Rafiki yangu**



67

Hakiuzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/d/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** dada, kaka

**U:** dau, dawati,tamu, damu

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **d** na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi **z** na **y**.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 66**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /d/ /o/ do

**U:** Endelea na do, du, di, de, ze

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 66.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** gre di - gredi

**U:** aligaagaa, alimsaidia

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 66.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **gredi, aliteguka, aligaagaa.**

### Kabla ya kusoma

**N/T:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

### Maswali

**N:** Bidu yuko katika gredi gani? *(Bidu yuko katika gredi ya kwanza.)*

**T**: Taja marafiki wa Bidu. *(Donadi na Daudi)*

**U:** Je wewe una marafiki wangapi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kitabu **changu** - Vitabu **vyetu**

### Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi kwenye **ukurasa wa 66.** Kila mwanafunzi amweleze mwenzake kumhusu, akitumia mwongozo ufuatao: jina lake; anakoishi, familia yake na rafiki yake.

### Kazi ya ziada

Watunge sentensi nne wakitumia maneno haya: gredi; mvulana; umri; miaka.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 67: Mimi na wenzangu 2

Kipindi cha 66 na 67 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 66**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**d** **z** **y**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| d o | d u | d i | d e | z e |
|---|---|---|---|---|
| **do** | **du** | **di** | **de** | **ze** |

● Soma silabi na maneno.

| gre di | a ka u mi a | a li ga a ga a | a li m sa i di a |
|---|---|---|---|
| **gredi** | **akaumia** | **aligaagaa** | **alimsaidia** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Huyu ni rafiki **yangu**. | 1. Hawa ni marafiki **zetu**. |
| 2. Huyu ni mzazi **wangu**. | 2. Hawa ni wazazi **wetu**. |
| 3. Huyu ni msichana **wangu**. | 3. Hawa ni wasichana **wetu**. |

**Kusoma hadithi**

**Donadi aumia**



Bidu ni mvulana. Yuko katika gredi ya kwanza. Bidu ana marafiki wawili. Marafiki hawa ni Donadi na Daudi. Jana Donadi aliteguka akaumia. Aligaagaa na kusema, "Bidu! Daudi! Nimeumia." Bidu alimsaidia kukaa na kumtuliza. Daudi alikimbia kumwita mama.

Mali ya Serikali ya Kenya

66

Kipindi cha 66 na 67 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 67**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**D** **d**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li teguka | a li m saidia |
|---|---|
| **aliteguka** | **alimsaidia** |
| ni me umia | ku m tuliza |
| **nimeumia** | **kumtuliza** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Rafiki yangu**



67 Hakiuzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** D

**U:** Endelea na herufi d.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 66.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Soma sehemu za neno 'a li teguka' kisha uunganishe sehemu hizo na kusoma neno 'aliteguka' upesi.

**U:** Endelea na maneno: alimsaidia, nimeumia, kumtuliza

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 66.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 66.**

### Hadithi ya mwalimu

**Rafiki yangu**

Rafiki yangu anaitwa Malenya Limo. Malenya ni mvulana. Anasoma katika shule ya msingi ya Birongo. Malenya ana umri wa miaka saba. Sisi hucheza kandanda pamoja wakati mwingine. Malenya hunisaidia kuosha vyombo nami humsaidia kuwalisha kuku wake.

Malenya ni mwanafunzi mwenye bidii. Shuleni yeye hufanya kazi ya walimu vizuri. Mara nyingi yeye hupewa zawadi kwa bidii yake. Hii imewafanya walimu na wanafunzi wote kumpenda. Mimi nampenda rafiki yangu Malenya. Kazi yangu ya shule imeanza kuwa nzuri kwa sababu yeye hunisaidia. Sisi hufanya mazoezi pamoja.

Funza maana ya maneno mapya: **mvulana, umri, miaka.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Malenya humsaidia rafiki yake kufanya nini? *(Humsaidia rafiki yake kuosha vyombo.)*

**T:** Rafiki hawa hucheza mchezo upi? *(Kandanda)*

**U:** Je, wewe hufanya nini na rafiki yako? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Katika vikundi vya wanafunzi wawili. Shiriki mchezo wa maswali na majibu: Unaitwa nani? Una miaka mingapi? Unapenda nini? Je, ungetaka kuwa rafiki yangu?

### Kazi ya ziada

Mchore rafiki yako na uandike jina lake.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 68 na 69 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 68**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  g d z

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  g o **go** g u **gu** g a **ga** d e **de**

- Soma silabi na maneno.

  ma gu ni a **magunia** mi ho go **mihogo** mi zi go **mizigo** ku ga wa na **kugawana**

- **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

  Tunga sentensi nne ukitumia **-angu** au **-etu**.

**Kusoma hadithi**

**Kogo na Ragoli**



Kogo na Ragoli walikuwa marafiki. Walikuwa wakibeba mizigo huko Migori. Kila asubuhi walibeba magunia mazito ya mboga na mihogo. Kila usiku walioga na kukanda mabega na miguu yao ili kupunguza maumivu. Walikula ugali kwa uyoga na kugawana hela za kazi.

Mali ya Serikali ya Kenya 68

Kipindi cha 68 na 69 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 69**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  G g

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  wa li kuwa **walikuwa** wa li beba **walibeba**

  ku gawana **kugawana** wa li gogota **waligogota**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Safari ya kambini**



69 Hakiluzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/g/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.
**N/T/U:** gari, ghali
**U:** godoro, domo, giza, ghorofa

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **g** na utamke sauti yake.
**U:** Endelea na herufi **d** na **z**.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 68.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:** /g/ /o/ silabi ni go
**U:** Endelea na silabi gu, ga, de
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 68.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** ma gu ni a - magunia, mi ho go - mihogo
**U:** Endelea na mizigo, kugawana
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 68.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kukanda**, **uyoga**, **kugawana.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N**: Ni akina nani walikuwa marafiki? *(Kogo na Ragoli walikuwa marafiki.)*
**T:** Kazi ya Kogo na Ragoli ni gani? *(Kazi yao ni kubeba mizigo)*
**U:** Walezi wako hufanya kazi gani? *(Kubali jibu sahihi)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na –etu.**
**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Mwalimu **wangu** - Walimu **wetu.**

### Zoezi

Mwanafunzi atunge sentensi nne wakitumia **-angu** au **-etu.**

### Kazi ya ziada

Tunga sentensi ukitumia maneno haya:
1. Maskauti 2. Rafiki 3. Msichana 4. Shule

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

Kipindi cha 68 na 69 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 68**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**g** **d** **z**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| g o | g u | g a | d e |
|---|---|---|---|
| **go** | **gu** | **ga** | **de** |

- Soma silabi na maneno.

| ma gu ni a | mi ho go | mi zi go | ku ga wa na |
|---|---|---|---|
| **magunia** | **mihogo** | **mizigo** | **kugawana** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Tunga sentensi nne ukitumia **-angu** au **-etu**.

**Kusoma hadithi**

**Kogo na Ragoli**



Kogo na Ragoli walikuwa marafiki. Walikuwa wakibeba mizigo huko Migori. Kila asubuhi walibeba magunia mazito ya mboga na mihogo. Kila usiku walioga na kukanda mabega na miguu yao ili kupunguza maumivu. Walikula ugali kwa uyoga na kugawana hela za kazi.

Mali ya Serikali ya Kenya



Kipindi cha 68 na 69 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 69**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**G** **g**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li kuwa | wa li beba |
|---|---|
| **walikuwa** | **walibeba** |
| ku gawana | wa li gogota |
| **kugawana** | **waligogota** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Safari ya kambini**





Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** G

**U:** Endelea na herufi g.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 69.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Soma sehemu za neno 'wa li kuwa' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'walikuwa' upesi.

**U:** Endelea na maneno: walibeba, kugawana, waligogota

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 69.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 68.**

### Hadithi ya mwalimu

**Safari ya kambini**

Mimi na marafiki zangu tulijiandikisha kwa chama cha maskauti. Tulipenda kazi ya kupandisha bendera na nidhamu ya uanaskauti. Wakati wa kuenda kambini ulifika. Tulibeba mifuko ya kulalia na vyakula. Bwana Menza alituletea hema. Tuligawiwa kazi ya kupika, kukusanya kuni na kufyeka nyasi.

Siku moja tulipokuwa tukilala, upepo mkali uling'oa hema. Tulijikumbusha wito wetu, "Kuwa tayari kila mara." Tulishirikiana na kukita hema. Tulipomaliza kila mmoja wetu alitunukiwa. Tulirudi shuleni na kusimulia yote kuhusu ziara yetu. Wanafunzi walitamani kuingia chama cha maskauti.

Funza maneno mapya: **maskauti, kambini, hema.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Wanafunzi hawa walijiunga na kikundi gani shuleni? *(Chama cha maskauti.)*

**T:** Mwalimu wa maskauti alikuwa nani? *(Bw. Menza)*

**U:** Shuleni mwako ungependa kujiunga na kikundi gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Eleza mwenzako kazi wanazofanya maskauti shuleni kwenu.

### Kazi ya ziada

Tumia **–angu** au **–etu** kutunga sentensi nne.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________



Hakiuzwi

Kipindi cha 70 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 70**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

d D   y Y   g G   z Z

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Mfano: u yo ga - uyoga**

| | | |
|---|---|---|
| go | yo | zi |
| ta | u | wa |
| mi | ga | na |

**Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Somea mwenzako sentensi zifuatazo.

1. Hii ni shule **yetu**.
2. Huyu ni mbuzi **wangu**.
3. Hawa ni watoto **wetu**.
4. Mipira hii ni **yetu**.
5. Baiskeli **yangu** imepotea.
6. Hawa ni mbwa **wetu**.
7. Firimbi **yangu** imepulizwa.

**Zoezi: Kuandika**

Jaza mapengo haya.

1. Jina lako ni ___________.
2. Unasoma katika gredi ya ___________.
3. Una umri wa miaka ___________.

Mali ya Serikali ya Kenya   70

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** D
**U:** Endelea na herufi d, Y, y, G, g, Z na z.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 70**.

## Jedwali la silabi

**N/T/U:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi 'u yo ga' kuandika neno 'uyoga'. Soma neno pamoja na wanafunzi.
**U:** Mwanafunzi aunde maneno kutokana na jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 70**.

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**
**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Vikombe **vyangu** - Vikombe **vyetu**
Mwanafunzi aandike sentensi kwenye **ukurasa wa 70** na kusomea mwenzake.

## Kuandika maneno

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika: **gredi, dawati.**

## Kuandika

**T:** Rejelea mimi na mwenzangu.
**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 70** kwenye daftari lake.

## Kazi ya ziada

Andika sentensi zifuatazo ukitumia **-etu**
1. Shule yangu ni nzuri.
2. Mbwa wangu ni mkubwa.
3. Kitabu changu kimepotea.
4. Baba yangu ni mwalimu.

Tarehe: ___________________________ Muda: __________________ Idadi: __________________

# Kipindi cha 71: Mimi na wenzangu 2

**Kipindi cha** 71 na 72 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 71**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**j** **g** **d**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

j e — **je** | j i — **ji** | j o — **jo** | j u — **ju** | d e — **de**

● Soma silabi na maneno.

ji vu — **jivu** | a ki ji ka za — **akijikaza** | ji ko ni — **jikoni** | Ju ma mo si — **Jumamosi**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Jaza mapengo kwa jibu sahihi.

1. Huyu ni rafiki ___________. (yangu, zetu)
2. Hizi ni meza ___________. (zetu, changu)
3. Hiki ni kitabu ___________. (vyangu, changu)

**Kusoma hadithi**

**Jino la Jakoyo**



Jumamosi asubuhi Jakoyo alilala kitini. Jino lake lilikuwa likimuuma. Alilala huku akilisugua jino hilo kwa kidole. Aliinuka, akajikaza na kuelekea jikoni. Huko alichota jivu na kuliweka kwenye jino. Mama yake alimsikia akilia. "Jakoyo, unaumwa wapi?" Mama alimuuliza. "Jinoooo!" Jakoyo alisema. Mama alielekea dukani. Alinunua dawa na kumletea. Jakoyo alimeza dawa. Baadaye jino lilitulia. Mama alimuonya kutoweka jivu kwenye jino siku nyingine.



**Kipindi cha** 71 na 72 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 72**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**J** **j**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

li na mu uma — **linamuuma** | a ka jikaza — **akajikaza**

a ki li sugua — **akilisugua** | li li tulia — **lilitulia**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mchezo tuupendao**





### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/j/** Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** jivu, akajikaza

**U:** jikoni, Jumamosi, rafiki

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **j** na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi **d** na **g**.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 71.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /j/ /e/ - je

**U:** Endelea na ji jo ju de

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 71.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ji vu - jivu, a ki ji ka za - akijikaza

**U:** jikoni, Jumamosi

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 71.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **jivu, akijikaza, jikoni.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

### Maswali

N: Taja jina la mtoto aliyelala kitini. *(Jina lake ni Zakayo.)*

**T:** Zakayo alilala kitini siku gani? *(Siku ya Jumamosi.)*

**U:** Kwa nini Zakayo alilia? *(Kwa sababu jino lake lilikuwa linauma)*

Eleza ulivyohisi wakati ulikuwa mgonjwa. *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Jino **langu** - Meno **yetu**

### Zoezi

Mwanafunzi ajaze pengo kwa jibu sahihi kwenye **ukurasa wa 71.**

Kwa vikundi vya watu wawili wanafunzi waulize na kujibu maswali yafuatayo: Unaitwa nani? Uko katika gredi ya ngapi? Unaishi katika kijiji kipi? Unaishi na nani?

### Kazi ya ziada

Andika sentensi ukitumia maneno haya: wasichana, wavulana, gredi.

Tarehe: ____________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

Kipindi cha 71 na 72 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 71**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **j** **g** **d**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  j e → **je**; j i → **ji**; j o → **jo**; j u → **ju**; d e → **de**

- Soma silabi na maneno.

  ji vu → **jivu**; a ki ji ka za → **akijikaza**; ji ko ni → **jikoni**; Ju ma mo si → **Jumamosi**

**Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Jaza mapengo kwa jibu sahihi.

1. Huyu ni rafiki ___________. (yangu, zetu)
2. Hizi ni meza ___________. (zetu, changu)
3. Hiki ni kitabu ___________. (vyangu, changu)

**Kusoma hadithi**

**Jino la Jakoyo**



Jumamosi asubuhi Jakoyo alilala kitini. Jino lake lilikuwa likimuuma. Alilala huku akilisugua jino hilo kwa kidole. Aliinuka, akajikaza na kuelekea jikoni. Huko alichota jivu na kuliweka kwenye jino. Mama yake alimsikia akilia. "Jakoyo, unaumwa wapi?" Mama alimuuliza. "Jinoooo!" Jakoyo alisema. Mama alielekea dukani. Alinunua dawa na kumletea. Jakoyo alimeza dawa. Baadaye jino lilitulia. Mama alimuonya kutoweka jivu kwenye jino siku nyingine.

71 Hakiuzwi

Kipindi cha 71 na 72 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 72**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **J** **j**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  li na mu uma → **linamuuma**; a ka jikaza → **akajikaza**

  a ki li sugua → **akilisugua**; li li tulia → **lilitulia**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mchezo tuupendao**



Mali ya Serikali ya Kenya 72

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** J

**U:** Endelea na herufi j.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 72**.

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'a ki li sugua' kisha uunganishe sehemu hizo na kusoma neno 'akilisugua' upesi.

**U:** Endelea na maneno: lilitulia, linamuuma, akajikaza

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 72**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 71**.

### Hadithi ya mwalimu

**Mchezo tuupendao**

Mimi na rafiki zangu wa gredi ya kwanza tunapenda kucheza. Mchezo tunaoupenda ni wa kandanda. Sisi hutumia mpira kuucheza. Ni mchezo tulioanza kucheza tukiwa na umri mdogo. Sisi huchezea uwanjani. Sisi huwa na timu mbili. Moja ya wasichana na nyingine ya wavulana. Kila timu huwa na wachezaji kumi na moja. Mwalimu wetu huwa ni refa. Jana rafiki yangu alianguka akicheza. Mguu wake ukateguka. Mwalimu akampeleka hospitalini kutibiwa.Mwalimu mkuu akatuita. Tukaambiwa tuwe waangalifu tunapocheza tusije tukaanguka. Baada ya kucheza sisi hurudi darasani na kuendelea na masomo.

Funza maana ya maneno mapya: **mvulana, umri, rafiki.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Ni mchezo gani unaozungumziwa kwenye hadithi? *(Kandanda)*

**T:** Ni nani refa wa mchezo huu? *(Mwalimu)*

**U:** Je, unastahili kufany anini mwenzako akiteguka mguu? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Toa maelezo mbele ya darasa ukizingatia jina lako, umri wako na gredi yako

### Kazi ya ziada

Chora vifaa vinne vinavyopatikana darasani.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 73: Mimi na wenzangu 2

Kipindi cha 73 na 74 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 73**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**r** **g** **d**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| r e | r i | r o | r u | g e |
|---|---|---|---|---|
| **re** | **ri** | **ro** | **ru** | **ge** |

● Soma silabi na maneno.

| a li zu ru | ra i a | ji n si a | zi a ra |
|---|---|---|---|
| **alizuru** | **raia** | **jinsia** | **ziara** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Andika vifungu hivi katika wingi.

1. Kitabu **changu**.
2. Kalamu **yangu**.
3. Kikombe **chetu**.

**Kusoma hadithi**

**Rais azuru Rodi**



Rais alizuru mji wetu wa Rodi. Gari lake lilisimama barabarani. Rais alishuka. Alikutana nasi raia. Tulisimama kulingana na miaka na jinsia. Rais alisema, "Hamjambo wananchi wa Rodi? Nawasihi mkae kwa amani." Habari ya ziara ya rais iliwekwa kwenye jarida la Rodi na Redio Rodi.

73

Hakiuzwi

Kipindi cha 73 na 74 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 74**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**R** **r**


▬ Soma sehemu za neno na neno zima.

| li li simama | a li zuru |
|---|---|
| **lilisimama** | **alizuru** |
| na wa sihi | i li wekwa |
| **nawasihi** | **iliwekwa** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kuogelea mtoni**



Mali ya Serikali ya Kenya

74

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/j/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.
**N/T/U:** jinsia, cheza
**U:** jeraha, raha, jarida, majani

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **r** na utamke sauti yake.
**U:** Endelea na herufi **g** na **d**.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 73.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:** /r/ /e/ silabi ni re
**U:** Endelea na silabi ri ro ru
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 73.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** a li zu ru - alizuru
**U:** jinsia, ziara, raia
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 73.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **alizuru, raia, ziara**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Rais alizuru mji gani? *(Alizuru mji wa Rodi)*
**T**: Rais alikutana na akina nani? *(Alikutana na raia)*
**U:** Unafikiri ni kwa nini rais aliwasihi raia wakae kwa amani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu.**
**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kiti **changu** - Viti **vyetu**

### Zoezi

Wanafunzi waandike sentensi kwenye **ukurasa wa 73** kwa wingi.

### Kazi ya ziada

Jadiliana na mlezi wako kuhusu maagizo yafaayo na yasiyofaa kufuatwa ukiwa shuleni.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

Kipindi cha 73 na 74 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 73**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **r** **g** **d**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  r e → **re** r i → **ri** r o → **ro** r u → **ru** g e → **ge**

- Soma silabi na maneno.

  a li zu ru → **alizuru** ra i a → **raia** ji n si a → **jinsia** zi a ra → **ziara**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Andika vifungu hivi katika wingi.

1. Kitabu **changu**.
2. Kalamu **yangu**.
3. Kikombe **chetu**.

**Kusoma hadithi**

**Rais azuru Rodi**



Rais alizuru mji wetu wa Rodi. Gari lake lilisimama barabarani. Rais alishuka. Alikutana nasi raia. Tulisimama kulingana na miaka na jinsia. Rais alisema,"Hamjambo wananchi wa Rodi? Nawasihi mkae kwa amani." Habari ya ziara ya rais iliwekwa kwenye jarida la Rodi na Redio Rodi.

73 Hakiluzwi

Kipindi cha 73 na 74 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 74**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **R** **r**

- Soma sehemu za neno na neno zima.


  li li simama → **lilisimama** a li zuru → **alizuru**

  na wa sihi → **nawasihi** i li wekwa → **iliwekwa**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kuogelea mtoni**



Mali ya Serikali ya Kenya 74

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** R

**U:** Endelea na herufi r.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 74.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'li li simama' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'lilisimama' upesi.

**U:** Endelea na maneno: iliwekwa, alizuru, nawasihi

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 74.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 73.**

### Hadithi ya mwalimu

**Kuoga mtoni**

Jumamosi iliyopita tulienda na rafiki Musa mtoni. Tulipofika mtoni tulivua nguo zetu na kuanza kuoga mtoni. Maji yalikuwa baridi sana. Tulipokuwa tukiogelea mvulana mmoja wa umri mkubwa alikuja na kuchukua nguo zetu. Tukashindwa ni nini tutafanya. Musa akaniuliza "Je,tutaendaje nyumbani bila nguo?". Nikamjibu, "Tumwite huyo mvulana tumwombe aturudishie nguo zetu." Musa akaita, "Weee! Eee! Wee tafadhali turudishie nguo zetu. Hatuna cha kuvaa." Huyo mvulana akasikia. Akarudi nyuma na kuja karibu na mto. Akasema, "Hii iwe mara ya mwisho kuoga hapa, ni hatari kuoga kwenye mto. Mto huu una nyoka na mamba wakali" Tukachukua nguo zetu na kwenda nyumbani mbio.

Funza maana ya maneno mapya: **wenzangu, nimekusamehe.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Musa na rafiki yake walienda wapi siku ya Jumamosi? *(Walienda mtoni.)*

**T:** Je, ni kwa nini kijana huyo alichukua nguo za akina Musa na rafiki yake? *(Kwa sababu ni hatari kuoga kwenye mto.)*

**U:** Je, unafikiri Musa na rafiki yake wangefanyaje kama hawangerudishiwa nguo zao? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Katika vikundi, toleana maagizo haya na mwenzako

1. Simama 2. Keti 3. Andika 4. Chora

### Kazi ya ziada

Mueleze mlezi wako kuhusu:

1. jina lako 2. jina la rafiki yako
3. gredi yako

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 75: Mimi na Wenzangu 2

Kipindi cha 75 **Mimi na wenzangu 2**

**Kipindi 75**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

r R g G j J d D

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ri ka – rika**

| | | |
|---|---|---|
| vu | cha | m |
| ri | u | la |
| si | na | ka |

**Sarufi: Matumizi ya '-angu'**

Andika sentensi tatu ukitumia **-angu**.

**Kwa mfano: Hii ni chaki yangu.**

**Zoezi: Kuandika**

Andika sentensi hizi kwenye daftari lako.

1. Mimi hucheza na rafiki **yangu**.
2. Rafiki **yangu** amenipa kalamu.
3. Gari **langu** si safi.
4. Rais alizuru mji **wetu.**
5. Kiatu **changu** kimepotea.
6. Mabegi **yetu** yana vitabu.
7. Shule **yangu** imefungwa.
8. Tutaenda nyumbani **kwetu**.
9. Gari **langu** liko barabarani.
10. Mchezo **wetu** ulipendeza.

75 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** R

**U:** Endelea na herufi r, g, G, j, J, d na D.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 75.**

## Jedwali la silabi

**N/T/U:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi 'ri ka' kuandika neno 'rika'. Soma neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi wakirejelea jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 75**.

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Mti **wangu** - Miti **yetu**.

Wanafunzi waandike sentensi tatu wakitumia **-angu.**

## Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika: **jarida, rafiki.**

## Kuandika

**T:** Rejelea mada ya mimi na wenzangu pamoja na wanafunzi.

**U:** Wanafunzi wafanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 75** katika madaftari yao.

## Kazi ya ziada

Wanafunzi watunge sentensi nne wakitumia **-angu** na **-etu.**

## Kazi ya nyongeza

Waeleze wanafunzi wanaporudi nyumbani wawatambue majirani kwa majina.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 76 na 77 | **Siku za wiki 2**

**Kipindi 76**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **p** **r** **g**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  p e → **pe**  p i → **pi**  p o → **po**  p u → **pu**  r e → **re**

- Soma silabi na maneno.

  pa sa ka → **pasaka**  pwe za → **pweza**  a li pe wa → **alipewa**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Jaza mapengo kwa jibu sahihi.

1. Rais alikuja katika kijiji ________. (chetu, vyetu)
2. Chifu ________ alimkaribisha. (letu, wetu)
3. Rais alimtuza mtoto ________. (wangu, changu)

**Kusoma hadithi**

**Pweza Paulo**




Siku ya pasaka Petero alisema, "Jana niliona pweza pale majini." Hatukumuamini. Tulimuuliza mwalimu, "Je, pweza hupatikana wapi?" Mwalimu alituletea tarakilishi.
Tulisoma kuhusu pweza aliyeitwa Paulo. Pweza huyo alizaliwa Jumatatu. Alipewa jina la Paulo Jumanne. Alibatizwa Jumatano. Aliajiriwa Alhamisi. Alilipwa mshahara Ijumaa. Alioa Jumamosi. Alipata mtoto Jumapili. Baadaye alihamia Pemba anakoishi.

Mali ya Serikali ya Kenya 76

Kipindi cha 76 na 77 | **Siku za wiki 2**

**Kipindi 77**

- Tamka sauti

  **P** **p**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  hu patikana → **hupatikana**  tu li mu uliza → **tulimuuliza**

  ha tu ku mu amini → **hatukumuamini**  a li ye itwa → **aliyeitwa**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Ziara ya rais**



77 Hakiuzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/p/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** pacha, furaha

**U:** pasaka, mapaja, paka, pemba

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **p** na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi r na g.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 76.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /p/ /e/ pe

**U:** Endelea na pi, po, pu, re

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 76.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** pa ka - paka

**U:** pweza, alipewa, pasaka

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 76.**

### Msamiati

Funza maneno haya: **pasaka, pweza**

### Kabla ya kusoma

**N/T:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

### Maswali

N: Petero aliona nini majini? *(Aliona pweza.)*

T: Pweza alipewa jina gani? *(Alipewa jina la Paulo.)*

U: Pweza ana miguu mingapi? *(Nane)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Nguo **yangu** - Nguo **zetu**

### Zoezi

Wanafunzi wajaze mapengo kwenye **ukurasa wa 76.**

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike majina ya siku za wiki kwa mfuatano.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

Kipindi cha 76 na 77 **Siku za wiki 2**

**Kipindi 76**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**p** **r** **g**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| p e | p i | p o | p u | r e |
|---|---|---|---|---|
| **pe** | **pi** | **po** | **pu** | **re** |

● Soma silabi na maneno.

| pa sa ka | pwe za | a li pe wa |
|---|---|---|
| **pasaka** | **pweza** | **alipewa** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Jaza mapengo kwa jibu sahihi.

1. Rais alikuja katika kijiji ________. (chetu, vyetu)
2. Chifu ________ alimkaribisha. (letu, wetu)
3. Rais alimtuza mtoto ________. (wangu, changu)

**Kusoma hadithi**

**Pweza Paulo**




Siku ya pasaka Petero alisema,
"Jana niliona pweza pale majini."
Hatukumuamini. Tulimuuliza mwalimu,
"Je, pweza hupatikana wapi?"
Mwalimu alituletea tarakilishi.
Tulisoma kuhusu pweza aliyeitwa Paulo. Pweza huyo alizaliwa Jumatatu. Alipewa jina la Paulo Jumanne. Alibatizwa Jumatano. Aliajiriwa Alhamisi. Alilipwa mshahara Ijumaa. Alioa Jumamosi. Alipata mtoto Jumapili. Baadaye alihamia Pemba anakoishi.

Mali ya Serikali ya Kenya 76

Kipindi cha 76 na 77 **Siku za wiki 2**

**Kipindi 77**

■ Tamka sauti

**P** **p**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu patikana | tu li mu uliza |
|---|---|
| **hupatikana** | **tulimuuliza** |
| ha tu ku mu amini | a li ye itwa |
| **hatukumuamini** | **aliyeitwa** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Ziara ya rais**



77 Hakiuzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** P

**U:** Endelea na herufi p.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 77.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'hu patikana' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'hupatikana' upesi.

**U:** Endelea na maneno: tulimuuliza, hatukumuamini, aliyeitwa

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 77.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 76.**

### Hadithi ya mwalimu

**Ziara ya Rais**

Chifu Kidiya alikutana na wanakijiji. Aliwaeleza kuwa siku ya Ijumaa, Rais alikuwa amepanga kutembelea kijiji chetu cha Doro. Alikuwa anakuja kufungua rasmi shule ya Msingi ya Doro.
Chifu Kidiya aliwaambia wanakijiji wajiunge katika makundi ili wajitayarishe kumpokea Rais. Aliwaambia kuwe na kundi la kina mama, la wazee na la watoto. Alisema makundi tofauti yakutane siku ya Jumanne na Jumatano. Waliambiwa wajitayarishe. Wanafunzi wa shule zote walitakiwa kudumisha usafi na kuvipanga viti vya wageni siku ya Alhamisi. Siku ilipofika Rais alipokelewa kwa shangwe na nderemo. Baada ya kutumbuizwa aliwahutubia wananchi. Watu walifurahi sana.

Funza maana ya maneno haya: **Ijumaa, Jumatano, Alhamisi.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikizehuku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Rais alikuwa anakuja kufanya nini? *(Kutembelea kijiji cha Doro na kufungua rasmi shule ya Msingi ya Doro.)*

**T:** Wanafunzi wa shule zote walitakiwa kufanya nini siku ya Alhamisi? *(Kudumisha usafi na kupanga viti vya wageni.)*

**U:** Ni siku gani hazijatajwa kwenye hadithi? *(Jumatatu, Jumamosi na Jumapili.)*

### Zoezi

Katika vikundi vya wawili wawili wanafunzi waeleze shughuli zao za siku za wiki.

### Kazi ya ziada

Jifunze shairi ya siku za wiki.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 78: Siku za wiki 2

Kipindi cha 78 na 79 **Siku za wiki 2**

**Kipindi 78**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**f** **p** **r**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| f e | f i | f o | f u | p e |
|---|---|---|---|---|
| **fe** | **fi** | **fo** | **fu** | **pe** |

● Soma silabi na maneno.

| a li fa u lu | wa li fu ra hi | i li po fi ka | fa ra si |
|---|---|---|---|
| **alifaulu** | **walifurahi** | **ilipofika** | **farasi** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Andika wingi wa vifungu vifuatavyo.

1. Kanisa **langu**.
2. Kijiji **changu**.
3. Mwalimu **wangu**.

**Kusoma hadithi**

**Filomena**




Ijumaa iliyopita, Filomena alikuwa na furaha. Alifaulu mtihani wake. Alifurahi sana. Wazazi wake walifurahi pia. Mama yake alimkumbatia. Jumatatu ilipofika, familia ya Filomena ilisafiri hadi Kilifi kwa farasi. Siku ya Jumanne walipiga foleni katika uwanja wa ndege. Waliabiri ndege. Walifika Ufaransa Jumatano.

Mali ya Serikali ya Kenya

78

Kipindi cha 78 na 79 **Siku za wiki 2**

**Kipindi 79**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**F** **f**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| i li yo pita | a li faulu |
|---|---|
| **iliyopita** | **alifaulu** |
| a li m kumbatia | wa li abiri |
| **alimkumbatia** | **waliabiri** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mwalimu wetu**




79 Hakluzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/f/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** farasi, valia

**U:** Filomena, foleni, poleni, vaa

### Ufahamu wa herufi

**N/T/U:** Taja jina la herufi **f** na utamke sauti yake.

**U:** Endelea na herufi **p** na **r**.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 78.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /f/ /e/ - fe

**U:** Endelea na silabi fi, fo, fu, pe

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 78.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** a li fa u lu - alifaulu

**U:** ilipofika, farasi, walifurahi

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 78.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **alifaulu, alimkumbatia, waliabiri**

### Kabla ya kusoma

**N/T:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Nani alifaulu mtihani wake? *(Filomena alifaulu mtihani wake.)*

**T:** Familia ilisafiri kwenda Kilifi siku gani? *(Ilisafiri siku ya Jumatatu.)*

**U:** Wewe huenda shule siku gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Mpira **wangu** - Mipira **yetu**

### Zoezi

Mwanafunzi aandike wingi wa maneno kwenye **ukurasa wa 78.**

### Kazi ya ziada

Tumia **-angu** au **-etu** kujaza mapengo yaliyoachwa.

| **-angu** | **-etu** |
|---|---|
| 1. Mtoto____________ | Mtoto wetu |
| 2. Kiti changu | Viti ________ |

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 79: Siku za wiki 2

Kipindi cha 78 na 79 **Siku za wiki 2**

**Kipindi 78**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**f** **p** **r**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| f e | f i | f o | f u | p e |
|---|---|---|---|---|
| **fe** | **fi** | **fo** | **fu** | **pe** |

● Soma silabi na maneno.

| a li fa u lu | wa li fu ra hi | i li po fi ka | fa ra si |
|---|---|---|---|
| **alifaulu** | **walifurahi** | **ilipofika** | **farasi** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Andika wingi wa vifungu vifuatavyo.

1. Kanisa **langu**.
2. Kijiji **changu**.
3. Mwalimu **wangu**.

**Kusoma hadithi**

**Filomena**




Ijumaa iliyopita, Filomena alikuwa na furaha. Alifaulu mtihani wake. Alifurahi sana. Wazazi wake walifurahi pia. Mama yake alimkumbatia. Jumatatu ilipofika, familia ya Filomena ilisafiri hadi Kilifi kwa farasi. Siku ya Jumanne walipiga foleni katika uwanja wa ndege. Waliabiri ndege. Walifika Ufaransa Jumatano.

Mali ya Serikali ya Kenya

78

Kipindi cha 78 na 79 **Siku za wiki 2**

**Kipindi 79**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**F** **f**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| i li yo pita | a li faulu |
|---|---|
| **iliyopita** | **alifaulu** |
| a li m kumbatia | wa li abiri |
| **alimkumbatia** | **waliabiri** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mwalimu wetu**



79 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** F

**U:** Endelea na herufi f.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 79.**

### Kusoma maneno marefu

**N/T/U:** Tamka sehemu za neno 'i li yo pita' kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno 'iliyopita' upesi.

**U:** Endelea na maneno: alifaulu, alimkumbatia, waliabiri.

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 79.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 78.**

### Hadithi ya mwalimu

**Mwalimu wetu**

Muhula wa tatu ulikaribia kuisha. Tulikuwa tumejifunza mambo mengi sana. Wanafunzi wengi walikumbuka aliyokuwa ametufunza mwalimu. Wengine walisahau waliyosoma.

Bi. Amani alikubali kurejelea kazi ambayo tulikuwa tumefunzwa.

Alisema kuwa wiki huwa na siku saba. Ilipofika Jumatatu, mwalimu alitufunza kuhusu familia.

Siku iliyofuata tulikumbushwa kuhusu tarakimu.

Jumatano na Alhamisi tulisoma kuhusu usafi wa miili yetu. Ijumaa tulirejelea somo la vyakula vya kiasili.

Tulipokuwa nyumbani siku ya Jumamosi, tulifanya kazi ya ziada kuhusu yote aliyotufunza mwalimu.

Jumapili nikaenda kanisani na kumuomba Mungu.

Funza maana ya maneno mapya: **Jumamosi, Jumapili, Jumatatu.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kwa nini mwalimu alirejelea kazi ambayo alikuwa amefunza? *(Wanafunzi wengine walikuwa wamesahau waliyoyasoma.)*

**T:** Wiki huwa na siku ngapi? *(Saba)*

**U:** Ni siku gani ya wiki uipendayo? Kwa nini? *(Wanafunzi wajibu na kuelezea ni kwa nini wanaipenda.)*

### Zoezi

Sikiliza masimulizi ya matukio ya siku za wiki kupitia vifaa vya kiteknolojia kama kipakatalishi.

### Kazi ya ziada

Andika kazi unazofanya katika siku zifuatazo.

1. Jumamosi
2. Jumapili
3. Jumatatu
4. Ijumaa

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 80: Siku za wiki 2

Kipindi cha 80 **Siku za wiki 2**

**Kipindi 80**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**p P** **j J** **f F** **r R**

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Mfano: Ju ma ta tu – Jumatatu**

| | | |
|---|---|---|
| ta | le | fo |
| Ju | ma | i |
| ni | a | tu |

**Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Mama **yangu** atakuja Jumatatu.
2. Watoto **wetu** watakuja Ijumaa.
3. Magari **yetu** yataletwa Jumamosi.
4. Nimefaulu mtihani **wangu**.
5. Farasi **wetu** walitufikisha Kilifi.
6. Pweza Paulo ni rafiki **yangu**.

**Zoezi: Kuandika**

Andika siku hizi za wiki.

1. Jumatatu
2. Jumanne
3. Jumatano
4. Alhamisi
5. Ijumaa
6. Jumamosi
7. Jumapili

Mali ya Serikali ya Kenya

80

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** P

**U:** Endelea na herufi **p, j, J, f, F, r na R.**

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 80.**

## Jedwali la silabi

**N/T/U:** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi 'ju ma ta tu' kuandika neno 'jumatatu'. Soma neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 80.**

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kidole **changu** - Vidole **vyetu.**

Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 80.**

## Kuandika maneno

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika:

**Jumatatu, Jumanne**

## Kuandika

**T:** Rejelea siku mbalimbali za wiki pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 80** katika daftari lake.

## Kazi ya ziada

Tunga sentensi ukitumia siku hizi za wiki:

1. Jumatatu
2. Jumanne
3. Ijumaa
4. Jumamosi
5. Jumapili

## Kazi ya nyongeza

Wazazi wawaelezee watoto wao kuhusu jamii yao wanapo rudi nyumbani.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 81: Tarakimu 2

**Kipindi cha** 81 na 82 **Tarakimu 2**

**Kipindi 81**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**v** **p**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| v e | v i | v o | v u | f e |
|---|---|---|---|---|
| **ve** | **vi** | **vo** | **vu** | **fe** |

● Soma silabi na maneno.

| vi a tu | ve li | vi lima | vi jito |
|---|---|---|---|
| **viatu** | **veli** | **vilima** | **vijito** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Tunga sentensi tatu ukitumia **–angu**.

**Kusoma hadithi**

**Kisiwa cha Vanuatu**



Veronika na familia yake walisafiri hadi Vanuatu. Walitumia motaboti mbili. Walivaa vesti za usalama. Walipofika kule, waliona visiwa vinne, vilima vitano na vijito sita. Walikutana na wavuvi saba. Walikula viazi vinane kwa samaki tisa. Walivilalia vitanda kumi hadi likizo ilipomalizika.

81

Hakiuzwi

**Kipindi cha** 81 na 82 **Tarakimu 2**

**Kipindi 82**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**V** **v**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li safiri | wa li vaa |
|---|---|
| **walisafiri** | **walivaa** |
| wa li po fika | wa li vi lalia |
| **walipofika** | **walivilalia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Ndugu za Halima**



Mali ya Serikali ya Kenya

82

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/v/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** vesti, pasi

**U:** vilima, tikiti, vijito, jitu

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U: v**

**U:** Endelea na herufi **p.**

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 81.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /v/ /e/ - ve

**U:** Endelea na vi vo vu fe

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 81.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** va zi - vazi

**U:** vilima, vijito, vesti

Wanafunzi wasomeane maneno waliojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 81.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **vesti, vilima, vijito**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Veronika na familia walisafiri hadi wapi? *(Veronika na familia yake walisafiri hadi Vanuatu.)*

**T:** Familia ya Veronika waliona vilima vingapi? *(Waliona vilima vitano.)*

**U:** Je, kwenu mna vingapi? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Matumizi ya –angu na –etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kalamu **yangu** - Kalamu **zetu.**

## Zoezi

Wanafunzi watunge sentensi tatu wakitumia -angu na -etu.

## Kazi ya ziada

Wanafunzi wawahesabie walezi wao moja hadi kumi.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 82: Tarakimu 2

Kipindi cha 81 na 82 | **Tarakimu 2**

**Kipindi 81**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

v p

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| v e | v i | v o | v u | f e |
|---|---|---|---|---|
| **ve** | **vi** | **vo** | **vu** | **fe** |

● Soma silabi na maneno.

| vi a tu | ve li | vi lima | vi jito |
|---|---|---|---|
| **viatu** | **veli** | **vilima** | **vijito** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Tunga sentensi tatu ukitumia **–angu**.

**Kusoma hadithi**

**Kisiwa cha Vanuatu**



Veronika na familia yake walisafiri hadi Vanuatu. Walitumia motaboti mbili. Walivaa vesti za usalama. Walipofika kule, waliona visiwa vinne, vilima vitano na vijito sita. Walikutana na wavuvi saba. Walikula viazi vinane kwa samaki tisa. Walivilalia vitanda kumi hadi likizo ilipomalizika.

81 Hakiuzwi

Kipindi cha 81 na 82 | **Tarakimu 2**

**Kipindi 82**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

V v

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li safiri | wa li vaa |
|---|---|
| **walisafiri** | **walivaa** |
| wa li po fika | wa li vi lalia |
| **walipofika** | **walivilalia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Ndugu za Halima**



Mali ya Serikali ya Kenya 82

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** V

**U:** Endelea na v

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 82.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** wa li safiri walisafiri

**U:** Endelea na maneno: walivaa, walipofika, walivilalia

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 82.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 81.**

### Hadithi ya mwalimu

**Ndugu za Halima**

Halima alikuwa katika gredi ya kwanza. Alikuwa mtoto wa pekee. Hakuwa na raha. Siku moja akipumzika chumbani mwake, Halima aliwaona watoto wengi. Alihesabu mmoja, wawili, watatu hadi kumi. Aliwaweka kwenye makundi ya wawili wawili. Kisha alihesabu tena: wawili, wanne... hadi kumi. Huzuni ya kukosa ndugu ikamuishia. Halima alisema, "Hawa wote ni ndugu zangu."

Nitawapa doli watano na mipira mitano wacheze. Mchezo ulipoanza Halima alijipata kitandani peke yake. Lahaula! Kumbe ilikuwa ndoto tu!

Funza maana ya maneno mapya: **wawili, alihesabu.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi. Mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Halima alihesabu watoto wangapi? *(Halima alihesabu watoto kumi.)*

**T:** Halima aliwaweka watoto katika makundi ya watoto wangapi? *(Watoto waliwekwa katika makundi ya watoto wawili wawili.)*

**U:** Je, ndoto huwa kweli? *(Wanafunzi waeleze majibu yao.)*

### Zoezi

Katika vikundi vya watu wawili ambatanisha nambari na maneno kwa kuonyesha nambari na kutaja jina la nambari husika.

### Kazi ya ziada

Andika tarakimu hizi kwa maneno.

1 2 4 6 8

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

Kipindi cha 83 na 84 **Tarakimu 2**

**Kipindi 83**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **sh** **v** **f**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  sh e → **she**; sh i → **shi**; sh o → **sho**; sh u → **shu**; v e → **ve**

- Soma silabi na maneno.

  shu ka → **shuka**; shu le → **shule**; u sha u ri → **ushauri**; sha u ku → **shauku**

- **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

  Tunga sentensi nne ukitumia **-etu**.

**Kusoma hadithi**

**Usafiri**



Watu hutumia vyombo mbalimbali kusafiri. Kuna wengine wanaotumia vyombo vya kifahari. Vyombo hivi ni eropleni, meli na farasi. Mimi hupenda kusafiri kwa miguu. Usafiri huu huniwezesha kunyoosha viungo. Pia mimi huhesabu hatua zote ninazopiga hivi: moja, mbili, hadi kumi. Kisha huanza tena. Nikisafiri hivi situmii hata senti moja.

83 Hakiuzwi

Kipindi cha 83 na 84 **Tarakimu 2**

**Kipindi 84**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **SH** **sh**

- Soma sehemu za neno na neno lote.


  hu ni wezesha → **huniwezesha**; hu hesabu → **huhesabu**

  ku nyoosha → **kunyoosha**; ni na zo piga → **ninazopiga**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Shamba la Mzee Kishombo**



Mali ya Serikali ya Kenya 84

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/sh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** shuka, choka

**U:** shule, ushauri, chakura, toka

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** sh

Endelea na herufi **v** na **f**.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 83.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /sh/ /e/ silabi ni she

**U:** Endelea na shi, sho, shu, ve

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 83.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** shu ka - shuka

**U:** ushauri, shauku, shule

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 83.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kifahari, eropleni, meli**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Watu wengi hutamani kusafiri vipi? *(Watu wengi hutamani kusafiri kifahari.)*

**T:** Taja njia za usafiri zilizotajwa kwenye hadithi. *(Eropleni, meli, farasi, kusafiri kwa miguu)*

**U:** Je, wewe ungependa kusafiri kwa njia gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Ng'ombe huyu ni **wangu**. - Ng'ombe hawa ni **wetu**. Wanafunzi watunge sentensi zilizo na **-angu** na **-etu**.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 83.**

## Kazi ya ziada

Andika tarakimu za nambari hizi.

1. Moja 2. Mbili 3. Tatu 4. Saba 5. Nane

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 83 na 84 **Tarakimu 2**

**Kipindi 83**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh** **v** **f**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| sh e | sh i | sh o | sh u | v e |
|---|---|---|---|---|
| **she** | **shi** | **sho** | **shu** | **ve** |

- Soma silabi na maneno.

| shu ka | shu le | u sha u ri | sha u ku |
|---|---|---|---|
| **shuka** | **shule** | **ushauri** | **shauku** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**
Tunga sentensi nne ukitumia **-etu**.

**Kusoma hadithi**

**Usafiri**



Watu hutumia vyombo mbalimbali kusafiri. Kuna wengine wanaotumia vyombo vya kifahari. Vyombo hivi ni eropleni, meli na farasi. Mimi hupenda kusafiri kwa miguu. Usafiri huu huniwezesha kunyoosha viungo. Pia mimi huhesabu hatua zote ninazopiga hivi: moja, mbili, hadi kumi. Kisha huanza tena. Nikisafiri hivi situmii hata senti moja.

83 Hakiuzwi

Kipindi cha 83 na 84 **Tarakimu 2**

**Kipindi 84**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH** **sh**


- Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu ni wezesha | hu hesabu |
|---|---|
| **huniwezesha** | **huhesabu** |
| ku nyoosha | ni na zo piga |
| **kunyoosha** | **ninazopiga** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Shamba la Mzee Kishombo**



Mali ya Serikali ya Kenya 84

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** SH
**U:** Endelea na herufi sh.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 84.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo na kusoma neno.
**N/T/U:** hu ni wezesha - huniwezesha
**U:** Endelea na maneno: huhesabu, kunyoosha
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 84.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 83.**

## Hadithi ya mwalimu

**Shamba la Mzee Kishombo**
Mzee Kishombo alikuwa na shamba kubwa. Alifuga ngamia tisa, ng'ombe sita, kuku saba na mbuzi kumi. Mzee Kishombo alikuwa na watoto sita. Wavulana wanne na wasichana wawili.
Watoto wake hawakuwa wenye bidii. Mali yake ikaanza kupungua. Wanyama walipungua shambani. Siku moja aliita watoto wake wote mkutanoni. Aliwashauri kuwa wakati wao ulikuwa umefika wa kuendeleza kazi zake. Kuanzia siku hiyo watoto wake waliamua kufanya bidii. Waligawana kazi. Punde si punde wanyama waliongezeka. Maisha yalikuwa mazuri.

Funza maana ya maneno: **tisa**, **saba**, **kumi.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mewanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Mzee Kishombo alikuwa na watoto wangapi? *(Mzee Kishombo alikuwa na watoto sita.)*
**T:** Mzee Kishombo alikuwa na wanyama wangapi? *(Mzee Kishombo alikuwa na ngamia tisa, ng'ombe sita, kuku saba na mbuzi kumi. Wanyama 32.)*
**U:** Je, ukiwa mkubwa utatumia njia gani uwe na shamba kama la mzee Kishombo? *(Wanafunzi waelezee majibu yao.)*

## Zoezi

Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili panga kadi za majina ya nambari hadi kumi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya:

| | | |
|---|---|---|
| 1. Moja | 2. Mbili | 3. Tatu |
| 4. Tano | 5. Saba | |

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 85: Tarakimu 2

Kipindi cha 85 **Tarakimu 2**

**Kipindi 85**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

V v    P p    SH sh    F f

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ta no – tano**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| pe | ta | na | vu | si |
| sha | sa | no | ati | ne |

♦ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Tunga sentensi ukitumia nambari zifuatazo pamoja na **-angu** au **-etu**.

1. saba
2. sita
3. tisa

**Zoezi: Kuandika**

Andika majina ya nambari hizi kwa maneno.

**Kwa mfano:**

| | |
|---|---|
| 1. moja | 2. mbili |
| 3. | 4. |
| 5. | 6. |
| 7. | 8. |
| 9. | 10. |

85    Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** V v

**U:** Endelea na herufi p, P, sh, SH, f na F.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 86**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'ta no' kuandika neno 'tano'. Soma neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno halisi akitumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 85**.

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kisu **changu** - Visu **vyetu**

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 85**.

## Kuandika maneno

Soma maneno haya huku mwanafunzi akiyaandika: **viatu, vizuri**

## Kuandika

**T:** Rejelea majina ya tarakimu moja hadi kumi pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 85** katika daftari lake.

## Kazi ya ziada

Chora

1. kalamu tatu
2. watoto wawili
3. ng'ombe mmoja
4. vifutio tano

## Kazi ya nyongeza

Wanafunzi wakifika nyumbani wahesabu idadi ya vitu mbalimbali vinavyopatikana nyumbani. Kwa **mfano**: miti sita.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 86: Familia 2

Kipindi cha 86 na 87 — Familia 2

**Kipindi 86**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**dh** **sh** **v**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| dh e | dh i | dh o | dh u | v e |
|---|---|---|---|---|
| **dhe** | **dhi** | **dho** | **dhu** | **ve** |

- Soma silabi na maneno.

| a dhu hu ri | bi dha a | fe dha | dha ha bu |
|---|---|---|---|
| **adhuhuri** | **bidhaa** | **fedha** | **dhahabu** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi zifuatazo.

1. **Mimi** ni**na**pika chakula.
2. **Mimi** ni**na**sukuma mkokoteni.
3. **Mimi** ni**na**ruka kamba.

**Kusoma hadithi**

**Dhodi apata dhahabu**

Dhodi alifika sokoni adhuhuri. Alitaka kununua bidhaa kadhaa. Lakini hakuwa na fedha za kutosha. Aliamua kumnunua samaki mdogo na kitunguu. Alipofika kwake, alimweka samaki mezani. Alipoanza kumkatakata, alikipata kijiwe kidogo. Alikiosha na kuona kinametameta. Alijua mara moja ni dhahabu. Siku iliyofuata aliiuza dhahabu hiyo.



Mali ya Serikali ya Kenya

86

Kipindi cha 86 na 87 — Familia 2

**Kipindi 87**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**DH** **dh**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku m nunua | a li ki osha |
|---|---|
| **kumnunua** | **alikiosha** |
| wa li fedhehesha | ku dhihirisha |
| **walifedhehesha** | **kudhihirisha** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Jamii ya siafu**



87

Hakiuzwi

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/dh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** dhahabu, debe

**U:** madhumuni, dhuluma, dhehebu, mada

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U: dh**

**U:** Endelea na herufi **sh** na **v**.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 86.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /dh/ /e/ dhe

**U:** Endelea na dhi dho ve

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 86.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.

**N/T/U:** a dhu hu ri

**U:** Endelera na maneno: fedha, dhahabu

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 86.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **adhuhuri, bidhaa, fedha, dhahabu**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Taja vitu alivyonunua Dhodi. *(Alinunua samaki mdogo na hoho.)*

**T:** Dhodi aliona nini alipoanza kumkatakata samaki? *(Aliona kijiwe kidogo.)*

**U:** Je, unafikiria familia ya Dhodi ilihisi vipi alipokuwa tajiri? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na **'mimi'** au **'ni'**.

## Zoezi

Wanafunzi wasome sentensi kwenye **ukurasa wa 86.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno manne ya heshima ambayo anatumia.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

**Kipindi cha 86 na 87** — **Familia 2**

**Kipindi 86**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **dh** **sh** **v**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| dh e | dh i | dh o | dh u | v e |
|---|---|---|---|---|
| **dhe** | **dhi** | **dho** | **dhu** | **ve** |

- Soma silabi na maneno.

| a dhu hu ri | bi dha a | fe dha | dha ha bu |
|---|---|---|---|
| **adhuhuri** | **bidhaa** | **fedha** | **dhahabu** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi zifuatazo.

1. **Mimi** ni**na**pika chakula.
2. **Mimi** ni**na**sukuma mkokoteni.
3. **Mimi** ni**na**ruka kamba.

**Kusoma hadithi**

**Dhodi apata dhahabu**

Dhodi alifika sokoni adhuhuri. Alitaka kununua bidhaa kadhaa. Lakini hakuwa na fedha za kutosha. Aliamua kumnunua samaki mdogo na kitunguu. Alipofika kwake, alimweka samaki mezani. Alipoanza kumkatakata, alikipata kijiwe kidogo. Alikiosha na kuona kinametameta. Alijua mara moja ni dhahabu. Siku iliyofuata aliiuza dhahabu hiyo.



Mali ya Serikali ya Kenya

86

**Kipindi cha 86 na 87** — **Familia 2**

**Kipindi 87**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **DH** **dh**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku m nunua | a li ki osha |
|---|---|
| **kumnunua** | **alikiosha** |
| wa li fedhehesha | ku dhihirisha |
| **walifedhehesha** | **kudhihirisha** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Jamii ya siafu**



87

Hakiuzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** DH

**U:** Endelea na herufi dh.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 87.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno upesi.

**N/T/U:** ku m nunua - kumnunua

**U:** Endelea na maneno: alikiosha, walifedhehesha

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 87.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 86.**

### Hadithi ya mwalimu

**Jamii ya siafu**

Siafu ni wadudu wadogo. Huishi kwa amani na umoja katika makundi. Hufanya kazi kwa bidii usiku na mchana. Siafu hugawana kazi. Jamii yao ina wafanyikazi wengi, kunao walinzi, vibarua na wawindaji.

Katika jamii hii kila mmoja ni mfanyikazi. Malkia wao ambaye ni kiongozi hutaga mayai. Adui akiwashambulia, wote humshambulia na kumuuma kwa ukali.

Wanapokuwa safarini huwa hawatawanyiki. Wote husafiri pamoja. Ndio maana kundi lao siku zote huwa kubwa sana. Siafu wanajua kuwa umoja ni nguvu.

Funza maana ya maneno mapya: **siafu, vibarua, malkia.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Siafu hufanya kazi za aina gani? *(Ulinzi, vibarua na uwindaji.)*

**T:** Malkia hufanya kazi gani? *(Malkia hufanya kazi ya kutaga mayai.)*

**U:** Je, unafikiria kundi la siafu linaweza kuwa na siafu wangapi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Andika sentensi nne ukitumia maneno haya:

1. hekima 2. wasia 3. mali 4. dhahabu

### Kazi ya ziada

Andika maneno manne yaliyo na herufi **dh**.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 88 na 89 **Familia 2**

**Kipindi 88**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ny** **dh** **sh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ny e | ny i | ny o | ny u | dh e |
|---|---|---|---|---|
| **nye** | **nyi** | **nyo** | **nyu** | **dhe** |

● Soma silabi na maneno.

| u ma a ru fu | wi vu | wa li m te ka | nyi ka ni |
|---|---|---|---|
| **umaarufu** | **wivu** | **walimteka** | **nyikani** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Tunga sentensi tatu ukitumia **mimi** na wakati uliopo.

**Kusoma hadithi**

**Nyamari na nyuki**



Nyamari aliishi Nyabisabo. Alipata umaarufu kwa kukariri mashairi ya wanyama na nyuki. Wengine walimwonea wivu. Walimteka nyara. Walimfunga mikono na miguu kwa nyororo. Walisafiri hadi nyikani. Nyamari alikariri shairi la nyuki. Nyuki walikuja na kuwauma wale watu wabaya. Walitoroka huku wakilia. Wanakijiji walimtafuta Nyamari kila mahali. Mwishowe walimpata nyikani.

Mali ya Serikali ya Kenya 88

Kipindi cha 88 na 89 **Familia 2**

**Kipindi 89**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NY** **ny**


■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li mwonea | wa li m teka |
|---|---|
| **walimwonea** | **walimteka** |
| wa li m funga | ku nyonya |
| **walimfunga** | **kunyonya** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Yusufu arithi mali**



89 Hakiuzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/ny/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** nyama, nyeupe

**U:** kamba, kunywa

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ny

**U:** Endelea na herufi dh na sh.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 88.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T:** /ny/ /e/ nye

**U:** Endelea na nyi, nyo, dhe

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 88.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** u ma a ru fu - umaarufu

**U:** walimteka, nyara, nyikani, wivu

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 88.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **umaarufu**, **walimteka**, **nyara**, **nyikani.**

### Kabla ya kusoma

**N/T:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Nyamari aliishi wapi? *(Nyamari aliishi Nyabisabo.)*

**T:** Nyamari alipata umarufu kwa kufanya nini? *(Alipata umaarufu kwa kukariri mashairi ya wanyama na nyuki.)*

**U:** Ikiwa mtu wenu atapotea, unafaa kufanya nini? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na **'mimi'** au **'ni'**.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 88.**

### Kazi ya ziada

Tumia jibu sahihi kwenye mabano kujaza pengo.
(**Nisamehe, asante, pole, tafadhali**)

1. Ukipewa zawadi utasema nini? __________ (asante)
2. Unatumia neno gani kuomba kitu? ________ (tafadhali)
3. Ukimkosea mtu utasema nini? __________ (nisamehe)

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 88 na 89 **Familia 2**

**Kipindi 88**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ny** **dh** **sh**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ny e | ny i | ny o | ny u | dh e |
|---|---|---|---|---|
| **nye** | **nyi** | **nyo** | **nyu** | **dhe** |

Soma silabi na maneno.

| u ma a ru fu | wi vu | wa li m te ka | nyi ka ni |
|---|---|---|---|
| **umaarufu** | **wivu** | **walimteka** | **nyikani** |

**Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Tunga sentensi tatu ukitumia **mimi** na wakati uliopo.

**Kusoma hadithi**

**Nyamari na nyuki**



Nyamari aliishi Nyabisabo. Alipata umaarufu kwa kukariri mashairi ya wanyama na nyuki. Wengine walimwonea wivu. Walimteka nyara. Walimfunga mikono na miguu kwa nyororo. Walisafiri hadi nyikani. Nyamari alikariri shairi la nyuki. Nyuki walikuja na kuwauma wale watu wabaya. Walitoroka huku wakilia. Wanakijiji walimtafuta Nyamari kila mahali. Mwishowe walimpata nyikani.

Mali ya Serikali ya Kenya

88

Kipindi cha 88 na 89 **Familia 2**

**Kipindi 89**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NY** **ny**

Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li mwonea | wa li m teka |
|---|---|
| **walimwonea** | **walimteka** |
| wa li m funga | ku nyonya |
| **walimfunga** | **kunyonya** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Yusufu arithi mali**



89

Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** NY

**U:** Endelea na herufi ny.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 89.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno upesi.

**N/T/U:** wa li mwonea - walimwonea

**U:** Endelea na maneno: walimteka, kunyonya

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 89.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 88.**

### Hadithi ya mwalimu

**Yusufu arithi mali**

Yusufu aliishi na jamii ya Mzee Tembo ijapokuwa hakuwa mwanawe. Mzee Tembo alikuwa na watoto wanne wa kike. Binti hao walimpenda Yusufu kama kaka yao. Mzee Tembo alitaka wote warithi mali yake. Aliwaita wazee wa kijiji kuwajulisha. Mila ya jamii ya Mitomiwili haikumruhusu Yusufu arithi mali. Mzee Tembo alisema, "Mbona hambadiliki?" Mzee Makuu akasema, "Mbona hutambui mila zetu?"

Mzee Tembo alijibu, "Yusufu ameishi hapa na sisi, jina lake ni Yusufu Tembo. Nimemlea na kumsomesha. Niungeni kufanya uamuzi huu."

Chifu Mwala alisema, "Mzee Tembo ameongea vizuri. Hebu tubadili baadhi ya mila zetu. Mimi ninamuunga mkono." Wazee wengine walikubaliana naye. Yusufu akarithi mali.

Funza maana ya maneno mpya: **warithi, uamuzi, mila.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Mzee Tembo alikuwa na watoto wangapi? *(Wanne wa kike. Kubali ikiwa watataja Yusufu pia.)*

**T:** Kwa nini wazee walipinga Yusufu kurithi mali? *(Kwa sababu mila zao hazikuruhusu mtoto ambaye hakuzaliwa na mzazi kurithi.)*

**U:** Je, ni haki ya Yufusu kurithi mali ya Mzee Tembo? *(Kubali jibu mwafaka.)*

### Zoezi

Katika vikundi vya wawili wawili, wanafunzi wawaeleze wenzao umuhimu wa heshima.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno manne yenye sauti **ny.**

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 90: Familia 2

Kipindi cha 90 **Familia 2**

**Kipindi 90**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

DH dh SH sh NY ny Vv

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Mfano: bi sha – bisha**

| | | | |
|---|---|---|---|
| nya | bu | bi | na |
| mu | ba | sha | a |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Soma sentensi zifuatazo huku ukiigiza vitendo.

1. **Mimi** nin**a**pika.
2. **Mimi** nin**a**chora.
3. **Mimi** nin**a**kula.
4. **Mimi** nin**a**imba.
5. **Mimi** nin**a**cheka.
6. **Mimi** nin**a**tembea.
7. **Mimi** nin**a**inama.
8. **Mimi** nin**a**simama.
9. **Mimi** nin**a**ruka.
10. **Mimi** nin**a**nawa.

**Zoezi: Kuandika**

Andika majina ya watu watatu mnaoishi nao nyumbani.

Mali ya Serikali ya Kenya

90

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** DH
**U:** Endelea na herufi dh, SH, sh, NY, ny, V na v.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 90.**

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.
**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'wa si a' kuandika neno 'wasia'. Soma neno pamoja na wanafunzi.
**U:** Wanafunzi waunde maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 90.**

## Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**
Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na **'mimi'** au **'ni'.**
Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 90.**

## Kuandika maneno

Soma maneno huku wanafunzi wakiyanakili: **nywele, dhuluma**

## Kuandika

Mwanafunzi aandike majina ya watu anaoishi nao nyumbani.
**T:** Rejelea majina ya watu wa familia pamoja na wanafunzi.
**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 90** katika daftari lake.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore familia yake na kuandika majina yao (mfano: baba, mama n. k).

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi awatembelee watoto mayatima katika jamii yao na kucheza nao.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 91: Familia 2

Kipindi cha 91 na 92 **Familia 2**

**Kipindi 91**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **th** **ny** **dh**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  th e — **the**; th i — **thi**; th o — **tho**; th u — **thu**; ny a — **nya**; dh e — **dhe**

- Soma silabi na maneno.

  the la thi ni — **thelathini**; the mo me ta — **themometa**; dhi ki — **dhiki**

**Sarufi: Nafsi ya kwanza na wakati uliopo**

Andika sentensi hizi katika wingi.

1. **Mimi** ni**na**angalia.
2. **Mimi** ni**na**lala.
3. **Mimi** ni**na**tembea.

**Kusoma hadithi**

**Jamaa ya Kathambi na kazi zao**



Baba ya Kathambi ni daktari. Yeye hupima joto kutumia themometa. Dada yake ni muuguzi. Baba na dada ya Kathambi hutibu wanaougua. Wao huwalipisha shilingi thelathini tu! Wanaohudumiwa huwashukuru kwa kusema asante.

91 Hakiuzwi

Kipindi cha 91 na 92 **Familia 2**

**Kipindi 92**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **TH** **th**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  wa na o ugua — **wanaougua**; hu wa lipisha — **huwalipisha**

  wa na o hudumiwa — **wanaohudumiwa**; hu wa shukuru — **huwashukuru**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Otonglo**



Mali ya Serikali ya Kenya 92

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/th/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** themometa, dhana

**U:** thelathini, dawati, themanini, tatu

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** th

**U:** Endelea na herufi ny na dh.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 91.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /th/ /e/ the

**U:** Endelea na thi, tho, nya, dhe

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 91.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** Ka tha mbi - Kathambi

**U:** thamani, themometa

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 91.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **asante, dada, thelathini**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Baba ya Kathambi anafanya kazi gani? *(Baba ya Kathambi anafanya kazi ya udaktari.)*

**T:** Dada ya Kathambi anafanya kazi gani? *(Dada ya Kathambi anafanya kazi ya uuguzi.)*

**U:** Je, mlezi wako hufanya kazi gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na 'mimi' au 'ni'.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 91.**

## Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno matano yaliyo na herufi 'th'.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 92: Familia 2

**Kipindi cha 91 na 92** **Familia 2**

**Kipindi 91**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**th** **ny** **dh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| th e | th i | th o | th u | ny a | dh e |
|---|---|---|---|---|---|
| **the** | **thi** | **tho** | **thu** | **nya** | **dhe** |

● Soma silabi na maneno.

| the la thi ni | the mo me ta | dhi ki |
|---|---|---|
| **thelathini** | **themometa** | **dhiki** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza na wakati uliopo**

Andika sentensi hizi katika wingi.

1. **Mimi** ni**na**angalia.
2. **Mimi** ni**na**lala.
3. **Mimi** ni**na**tembea.

**Kusoma hadithi**

**Jamaa ya Kathambi na kazi zao**



Baba ya Kathambi ni daktari. Yeye hupima joto kutumia themometa. Dada yake ni muuguzi. Baba na dada ya Kathambi hutibu wanaougua. Wao huwalipisha shilingi thelathini tu! Wanaohudumiwa huwashukuru kwa kusema asante.



Hakiuzwi

**Kipindi cha 91 na 92** **Familia 2**

**Kipindi 92**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**TH** **th**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa na o ugua | hu wa lipisha |
|---|---|
| **wanaougua** | **huwalipisha** |
| wa na o hudumiwa | hu wa shukuru |
| **wanaohudumiwa** | **huwashukuru** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Otonglo**



Mali ya Serikali ya Kenya



### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** TH

**U:** Endelea na herufi th.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 92**.

### Kusoma maneno marefu

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** wa na o ugua - wanaougua

**U:** Endelea na maneno wanaouhudumiwa, huwalipisha

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 92**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 91**.

### Hadithi ya mwalimu

**Otonglo**

Mzee Otonglo aliishi katika kijiji cha Mitimbili. Aliishi na watoto wake saba na wajukuu wake kumi. Alikuwa tajiri sana. Alikuwa maarufu wa kufuga mifugo na ukulima pale kijijini.

Wanakijiji walishangazwa na utajiri wake, wengine wakaanza kumchukia. Mara nyingi mifugo wake walipotelea malishoni. Otonglo aliamua kupiga ripoti kwa chifu. Chifu aliitisha mkutano wa wanakijiji kuzungumzia usalama wa mifugo.

Aliwahimiza wawe waangalifu na kukomesha wizi. Alisema pia wafanye kazi kwa bidii kwani ndiyo siri ya kufanikiwa. Wote walikubaliana kudumisha usalama kijijini na kutia bidii kazini.

Funza maana ya maneno: **wajukuu, mifugo.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanfunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Mzee Otonglo alikuwa na wajukuu wangapi? *(Kumi)*

**T:** Mzee Otongolo alikuwa na umaarufu gani? *(Umaarufu wa kufuga mifugo.)*

**U:** Je, unafikiri wizi uliisha kijijini Mitimbili? *(Majibu ni kama ndio, hapana n.k.)*

### Zoezi

Tunga sentensi ukitumia maneno haya:

1. Asante 2. Pole 3. Tafadhali 4. Samahani

### Kazi ya ziada

Tunga sentensi nne ukitumia nafsi ya kwanza wakati uliopo. Kwa mfano mimi ninacheka.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 93 na 94 **Familia 2**

**Kipindi 93**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  Ch th dh

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ch e | ch i | ch o | ch u | dh i | th i |
|---|---|---|---|---|---|
| **che** | **chi** | **cho** | **chu** | **dhi** | **thi** |

- Soma silabi na maneno.

| cha mbo | chu ra | cha tu | m che zo |
|---|---|---|---|
| **chambo** | **chura** | **chatu** | **mchezo** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Jaza mapengo kwa kutumia **nina** au **tuna**.

1. **Mimi** ________ cheza.
2. **Sisi** ________ lima.
3. **Sisi** ________ pika.

**Kusoma hadithi**

**Uvuvi wa samaki**



Jina langu ni Chacha. Mimi huishi Machakos. Ninapenda kumsaidia mjomba na kaka yangu Cheloti kuvua samaki. Sisi hutumia chambo na fimbo kuvua. Kelele za chura huwa hazitutishi. Mjomba na kaka Cheloti huuza samaki sokoni. Mimi huuza kachumbari. Sote huchoka baada ya kazi. "Pole," Shangazi Chelela husema.

93 Hakiuzwi

Kipindi cha 93 na 94 **Familia 2**

**Kipindi 94**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  CH ch

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku m saidia<br>**kumsaidia** | hu tumia<br>**hutumia** |
| ha zi tu tishi<br>**hazitutishi** | hu choka<br>**huchoka** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Panya nyumbani**



Mali ya Serikali ya Kenya 94

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/ch/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** chura, tupa

**U:** chacha, pipa, jambo, chambo

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ch

**U:** Endelea na herufi th na dh.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 93.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T:** /ch/ /e/ - che

**U:** Endelea na chi, cho, dhi, thi

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 93.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T:** cha mbo - chambo

**U:** chatu, mchezo

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 93.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **mjomba, pole**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Mjomba hufanya kazi gani? *(Mjomba hufanya kazi ya uvuvi.)*

**T:** Nani humsaidia mjomba kuuza samaki? *(Cheloti humsaidia mjomba kuuza samaki.)*

**U:** Je, ni vitu gani huuzwa kwa bei ghali sokoni? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na **'mimi'** au **'ni'**.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 93.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze mapengo akitumia maneno haya **pole, asante, tafadhali, samahani**

1. ____________ niruhusu niende msalani.
2. ____________ kwa kikombe cha chai.
3. Mwanangu ____________ kwa safari.

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 94: Familia 2

Kipindi cha 93 na 94 — **Familia 2**

**Kipindi 93**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Ch** **th** **dh**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ch e | ch i | ch o | ch u | dh i | th i |
|---|---|---|---|---|---|
| **che** | **chi** | **cho** | **chu** | **dhi** | **thi** |

● Soma silabi na maneno.

| cha mbo | chu ra | cha tu | m che zo |
|---|---|---|---|
| **chambo** | **chura** | **chatu** | **mchezo** |

◆ **Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Jaza mapengo kwa kutumia **nina** au **tuna**.

1. **Mimi** ________ cheza.
2. **Sisi** ________ lima.
3. **Sisi** ________ pika.

**Kusoma hadithi**

**Uvuvi wa samaki**



Jina langu ni Chacha. Mimi huishi Machakos. Ninapenda kumsaidia mjomba na kaka yangu Cheloti kuvua samaki. Sisi hutumia chambo na fimbo kuvua. Kelele za chura huwa hazitutishi.

Mjomba na kaka Cheloti huuza samaki sokoni. Mimi huuza kachumbari. Sote huchoka baada ya kazi. "Pole," Shangazi Chelela husema.

93 Hakiuzwi

Kipindi cha 93 na 94 — **Familia 2**

**Kipindi 94**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**CH** **ch**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| ku m saidia | hu tumia |
|---|---|
| **kumsaidia** | **hutumia** |
| ha zi tu tishi | hu choka |
| **hazitutishi** | **huchoka** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Panya nyumbani**



Mali ya Serikali ya Kenya 94

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** CH

**U:** Endelea na herufi ch.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 94.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** ku m saidia - kumsaidia

**U:** Endelea na maneno: hutumia, hazitutishi. Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 94.**

### Hadithi ya mwanafuzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 93.**

### Hadithi ya mwalimu

**Panya nyumbani**

Baada ya kutoka safarini, Karimi na mama yake walikuta godoro, mto na foronya vimeliwa na panya. Walishangaa na kujiuliza, "Huyu ni panya wa aina gani anayekula hata godoro?"

Walianza kumtafuta panya huyo. Karimi alichukua mwiko na mamake upanga. Karimi alisema, "Hebu tutafute mwanya alioingilia panya huyo." Mara waliona shimo kubwa. "Lo, shimo hili ni kubwa mno," Karimi akashangaa.

Mama yake Karimi akasema, "Ili kumzuia panya na wanyama wengine kuingia, tulizibe shimo hili kwa mchanga." Basi walisaidiana kulifunika shimo hilo. Panya hakuwasumbua tena.

Funza maana ya maneno mapya: **foronya**, **mwanya**, **tulizibe.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Taja vitu ambavyo vililiwa na panya. *(Godoro,mto na foronya.)*

**T:** Mama alichukua nini kumtafuta panya? *(Upanga)*

**U:** Je, unafikiri Karimi na mamake walimuua panya? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aeleze umuhimu wa matumizi ya maneno yafuatayo katika vikundi: pole, tafadhali, asante, samahani


### Kazi ya ziada

Kamilisha vifungu vifuatavyo kwa kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo.

| | |
|---|---|
| 1. Mimi _____ soma kitabu. | Sisi _____ soma kitabu. |
| 2. Mimi _____ enda shuleni. | Sisi _____ enda sokoni. |

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 95: Familia 2



Kipindi cha 95 Familia 2

Kipindi 95

Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch th sh ny

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: nya nya - nyanya**

| | | | |
|---|---|---|---|
| cha | che | chi | ma |
| ni | nya | dha | ni |

**Sarufi: Nafsi ya kwanza na wakati uliopo**

Igiza vitendo kwenye sentensi hizi katika vikundi.

1. **Sisi** tu**na**pika.
2. **Sisi** tu**na**chora.
3. **Sisi** tu**na**kula.
4. **Sisi** tu**na**imba.
5. **Sisi** tu**na**cheka.
6. **Sisi** tu**na**tembea.
7. **Sisi** tu**na**inama.
8. **Sisi** tu**na**simama.
9. **Sisi** tu**na**ruka.
10. **Sisi** tu**na**nawa.

**Zoezi: Kuandika**

Jaza mapengo haya kwa kutumia maneno yafuatayo. (pole, tafadhali, kwaheri)

1. Ukimkosea mtu utamwambia _______.
2. _________ nisaidie kalamu yako.
3. Ukimuaga mtu unasema _________ ya kuonana.

95 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ch

**U:** Endelea na herufi th, sh, na ny.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 95.**

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi ‘nya nya’ kuandika neno ‘nyanya’.

Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno halisi akitumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 95.**

## Sarufi

**Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Nafsi ya kwanza ni hali ya kuzungumzia kuhusu wewe mwenyewe. Nafsi hii huwakilishwa na **‘mimi’** au **‘ni’**. Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 95.**

## Kuandika maneno

Soma maneno haya huku mwanafunzi akiyaandika: **themometa, athari**

## Kuandika

**T:** Rejelea maneno ya heshima pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 95** katika daftari lake.

## Kazi ya ziada

Chagua jibu sahihi kwenye mabano (dada, wajukuu, binamu, nyanya, mjomba).

1. Ndugu wa kiume wa mama anaitwa nani?
2. Watoto wa mjomba wanaitwa nani?
3. Ndugu wa kike anaitwa nani?
4. Babu anawaita vipi watoto wa watoto wake?
5. Mzazi wa kike wa mama anaitwa nani?

## Kazi ya nyongeza

Wanafunzi wawaelimishe wenzao katika jamii umuhimu wa familia.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 96 na 97 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 96**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**gh** **th** **ch**

● Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| gha li | gha ri ka | ghu la mu |
| **ghali** | **gharika** | **ghulamu** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi hizi kwa usahihi na kwa sauti.

1. Mnyama **huyu** anakunywa maji.
2. Watoto **hawa** wananawa mikono.
3. Mama **huyu** anasugua meno.

**Kusoma hadithi**

**Usafi**



Wakati wa kiangazi, maji yalipungua. Iliwagharimu watu kununua maji. Wanafunzi wengi wa shule ya Ghulalu hawakuoga. Mwalimu mkuu alighadhabika. Ghafla aliwaambia wanafunzi wapange foleni. Aliangalia usafi wao. Aliwahimiza kukata kucha, kunyoa nywele na kunawa mikono. Wanafunzi safi walipewa zawadi za bei ghali.

Mali ya Serikali ya Kenya 96

Kipindi cha 96 na 97 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 97**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**GH** **gh**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ya li pungua | i li wa gharimu |
| **yalipungua** | **iliwagharimu** |
| a li ghadhabika | a li wa himiza |
| **alighadhabika** | **aliwahimiza** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Raha mtoto safi**



97 Hakiluzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/gh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ghafla, gari

**U:** ghali, gharika, pasaka, ghulamu

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** gh

**U:** Endelea na herufi th na ch.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 96.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** gha ri ka- gharika

**U:** ghulamu

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 96.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kunyoa nywele, kukata kucha, kunawa mikono**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kwa nini mwalimu mkuu alighadhabika? *(Wanafunzi wengi hawakuoga.)*

**T:** Mwalimu mkuu aliangalia nini? *(Usafi)*

**U:** Kwa nini ni muhimu kuzingatia usafi wa mwili? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 96.**

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike maneno manne yenye herufi 'gh'.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 96 na 97 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 96**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

gh th ch

- Soma silabi na maneno.

gha li → **ghali** | gha ri ka → **gharika** | ghu la mu → **ghulamu**

♦ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi hizi kwa usahihi na kwa sauti.

1. Mnyama **huyu** anakunywa maji.
2. Watoto **hawa** wananawa mikono.
3. Mama **huyu** anasugua meno.

**Kusoma hadithi**

**Usafi**



Wakati wa kiangazi, maji yalipungua. Iliwagharimu watu kununua maji. Wanafunzi wengi wa shule ya Ghulalu hawakuoga. Mwalimu mkuu alighadhabika. Ghafla aliwaambia wanafunzi wapange foleni. Aliangalia usafi wao. Aliwahimiza kukata kucha, kunyoa nywele na kunawa mikono. Wanafunzi safi walipewa zawadi za bei ghali.

Mali ya Serikali ya Kenya 96

Kipindi cha 96 na 97 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 97**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

GH gh

- Soma sehemu za neno na neno lote.

ya li pungua → **yalipungua** | i li wa gharimu → **iliwagharimu**

a li ghadhabika → **alighadhabika** | a li wa himiza → **aliwahimiza**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Raha mtoto safi**



97 Hakiuzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** GH

**U:** Endelea na herufi gh.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 97.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** ya li pungua - yalipungua

**U:** Endelea na maneno: **iliwagharimu, alighadhabika**

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 97.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 96.**

### Hadithi ya mwalimu

**Raha mtoto safi**

Raha alikuwa mwanafunzi katika shule ya msingi ya Bahati. Mtoto huyo alipenda usafi. Alijua usafi humfanya mtu asiwe mgonjwa. Kila asubuhi alikimbilia bafuni. Aliunawa uso na kusugua meno yake. Baadaye, alioga na kuvaa nguo safi.

Raha alikata kucha zake. Alipenda kucha fupi na safi. Alinyoa nywele zake. Alizoea kunawa mikono. Hakutaka kupata magonjwa ya tumbo.

Siku moja, Raha alisahau kunawa mikono. Rafiki yake alimpa embe. Raha alilikula embe hilo haraka haraka. Tumbo lake lilianza kumuuma. Alienda kwa mwalimu Auma. Mwalimu alimtuma kwa nesi akapewa dawa. Nesi alimkumbusha kunawa mikono kila mara kabla ya kula.

Funza maana ya maneno mapya: **kusugua meno, alioga.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Raha alipenda nini? *(Usafi)*

**T:** Raha alikuwa anafanya nini ili kuwa safi? *(Alisugua meno, osha uso, nawa mikono, oga)*

**U:** Kwa nini ni muhimu kunawa mikono? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Tunga sentensi nne ukitumia maneno yafuatayo:

1. kunyoa nywele
2. kukata kucha
3. kunawa mikono

### Kazi ya ziada

Andika sentensi nne katika hali ya umoja.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 98 na 99 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 98**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **gh** **dh**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ng' a | ng' i | ng' o | ng' u | gh i |
|---|---|---|---|---|
| **ng'a** | **ng'i** | **ng'o** | **ng'u** | **ghi** |

- Soma silabi na maneno.

Wa ng'o mbe — **Wang'ombe**
ya li ng'o ka — **yaling'oka**
ha vi ku ng'a ra — **havikung'ara**
nya ng'a u — **nyang'au**

- **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu** anashona nguo. | 1. **Hawa** wanashona nguo. |
| 2. **Huyu** anaosha vyombo. | 2. **Hawa** wanaosha vyombo. |
| 3. **Huyu** anakata kucha. | 3. **Hawa** wanakata kucha. |

**Kusoma hadithi**

**Wang'ombe**



Wang'ombe alikuwa mchafu. Viatu vyake havikung'ara. Wazazi walipong'amua kuwa Wang'ombe haogi, walighadhabika. Mama alisema, "Oga mwanangu. La sivyo utakuwa mgonjwa." Wang'ombe aliogopa kuwa mgonjwa. Alifuta kamasi. Alinawa mikono. Alisafisha nguo zake. Akadumisha usafi.

Mali ya Serikali ya Kenya 98

Kipindi cha 98 na 99 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 99**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

ya li ng'oka — **yaling'oka**
ha vi ku ng'ara — **havikung'ara**
wa li po ng'amua — **walipong'amua**
wa li ghadhabika — **walighadhabika**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mwanafunzi mchafu**



99 Hakiluzwi

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/ng'/** Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.
**N/T/U:** Wang'ombe, nguruwe
**U:** yaling'oka, ngarawa, mbolea

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** ng'
**U:** Endelea na herufi gh na dh.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 98.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:** /ng'/ /a/ ng'a
**U:** Endelea na ng'i, ng'o, ghi
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 98.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T:** Wa ng'o mbe - Wang'ombe
**U:** Endelea na maneno yaling'oka, nyang'au
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 98.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **futa kamasi, safisha nguo**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Wang'ombe alikuwa vipi? *(Mchafu)*

**T:** Mama alimuamrisha wang'ombe kufanya nini? *(Kuoga)*

**U:** Kwa nini wazazi hawakufurahia wang'ombe kuwa mchafu? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa.**
**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 98.**

## Kazi ya ziada

Tunga sentensi kuhusu matumizi ya sehemu za mwili zifuatazo:

1. pua 2. nyayo 3. tumbo 4. mdomo

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 98 na 99 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 98**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **gh** **dh**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ng' a — **ng'a** | ng' i — **ng'i** | ng' o — **ng'o** | ng' u — **ng'u** | gh i — **ghi**

- Soma silabi na maneno.

Wa ng'o mbe — **Wang'ombe**
ya li ng'o ka — **yaling'oka**
ha vi ku ng'a ra — **havikung'ara**
nya ng'a u — **nyang'au**

♦ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu** anashona nguo. | 1. **Hawa** wanashona nguo. |
| 2. **Huyu** anaosha vyombo. | 2. **Hawa** wanaosha vyombo. |
| 3. **Huyu** anakata kucha. | 3. **Hawa** wanakata kucha. |

**Kusoma hadithi**



**Wang'ombe**

Wang'ombe alikuwa mchafu. Viatu vyake havikung'ara. Wazazi walipong'amua kuwa Wang'ombe haogi, walighadhabika. Mama alisema, "Oga mwanangu. La sivyo utakuwa mgonjwa." Wang'ombe aliogopa kuwa mgonjwa. Alifuta kamasi. Alinawa mikono. Alisafisha nguo zake. Akadumisha usafi.

Mali ya Serikali ya Kenya

98

Kipindi cha 98 na 99 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 99**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG'** **ng'**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

ya li ng'oka — **yaling'oka**
ha vi ku ng'ara — **havikung'ara**
wa li po ng'amua — **walipong'amua**
wa li ghadhabika — **walighadhabika**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mwanafunzi mchafu**



99

Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** NG'

**U:** Endelea na herufi ng'.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 99.**

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo na usome neno upesi.

**N/T/U:** ya li ng'oka - yaling'oka

**U:** Endelea na maneno: havikung'ara, walipong'amua, walighadhabika

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 99.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 98.**

## Hadithi ya mwalimu

**Mwanafunzi mchafu**

"Njooni wajukuu wangu," babu aliita. Watoto wote walikimbia na kuenda kwa babu. "Leo nitawasimulia hadithi kuhusu mtoto mchafu," babu aliwaambia. Ogopa aliishi katika kijiji cha Vituko. Alikuwa mchafu sana. Kinywa chake kilinuka. Hakusugua meno yake. Sare yake ya shule ilikuwa chafu. Hakujali kufua nguo zake wala kuoga. Wanafunzi shuleni hawakupenda kucheza naye. Wanafunzi hawa walipenda usafi. Mwalimu alimwelezea Ogopa umuhimu wa kuwa safi. Ogopa aliamua kuoga na kuwa safi. Wenzake walianza kumpenda. Babu alimalizia kwa kuwahimiza watoto wasiwe wakiwabagua wengine.

Eleza wanafunzi maana ya maneno: **kuoga**, **kuosha nguo**. Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Babu alisimulia hadithi kuhusu nini? *(Ogopa – mtoto mchafu)*

**T:** Kwa nini kinywa cha Ogopa kilinuka? *(Hakusugua meno.)*

**U:** Utafanya nini ukiwa na rafiki mchafu? *(Mwambie adumishe usafi.)*

## Zoezi

Kwa vikundi vya watu wanne, imba wimbo unaoujua kuhusu sehemu za mwili.

## Kazi ya ziada

Chora mkono wako na vidole vyake.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 100 **Usafi wa mwili 2**

**Kipindi 100**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

gh GH ng' NG'

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: dhi ha ki - dhihaki**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| cha | ng'a | da | dha | na |
| ki | dhi | wa | thi | ha |

**Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Jaza mapengo yafuatayo kwa kutumia **huyu** au **hawa**.

1. Mwanafunzi ________ anaoga.
2. Watoto ________ wanacheza kwenye uchafu.
3. Mnyama ________ anaoshwa.
4. Wavulana _________wanacheza mpira.
5. Samaki _________ ni mkubwa.
6. _______mwanafunzi anafuta kamasi.
7. Wezi ndio _________.
8. Ng'ombe _________ ana maziwa mengi.

**Zoezi: Kuandika**

Tunga sentensi tatu ukitumia vifungu hivi vya maneno.

1. kukata kucha
2. kunyoa nywele
3. kusugua meno

Mali ya Serikali ya Kenya 100

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** NG'

**U:** Endelea na herufi ng' na gh.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 100**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'dhi ha ki' kuandika neno 'dhihaki'. Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mpe mwanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 100.**

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 100.**

## Kuandika maneno

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika katika madaftari: **mkono, ng'ara**

## Kuandika

**T:** Rejelea kuhusu jinsi ya kutunza usafi wa mwili pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 100** katika daftari lake.

## Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike wingi wa sehemu hizi za mwili.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. Mkono | |
| 2. Mguu | |
| 3. Pua | |
| 4. Kidole | |
| 5. Sikio | |

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi ajifunze wimbo juu ya kulinda usafi wa mwili wake.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo 2**

**Kipindi 101**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**w** **h** **s**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

y e — **ye**; w i — **wi**; w o — **wo**; y u — **yu**

● Soma silabi na maneno.

wa nya ma — **wanyama**; u we zo — **uwezo**; wa tu — **watu**; we ngi — **wengi**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Andika wingi wa vifungu hivi.

1. Mguu **wangu**
2. Mswaki **wangu**
3. Familia **yangu**

**Kusoma hadithi**

**Mchezo wa wanyama**



Chatu, chura na chui ni wanyama. Waliishi kwenye kichochoro. Walipenda mchezo wa kuhesabu nyota. Chatu alihesabu nyota tano. Chui naye alihesabu saba. Chura alihesabu kumi. Chura alishinda mchezo. Chui alikasirika. Akamweka Chura kwenye chupa.

101 Hakiuzwi

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo 2**

**Kipindi 102**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**W w** **H h** **S s**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.


a li kasirika — **alikasirika**; a li hesabu — **alihesabu**

wa li ishi — **waliishi**; a ka m weka — **akamweka**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Fisi na Tumbili**



Mali ya Serikali ya Kenya 102

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/w/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** wanyama, uwezo

**U:** wengi, tatu, watu, wengi

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 101**.

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** w

**U:** Endelea na herufi **h** na s.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 101**.

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /w/ /e/ we

**U:** Endelea na wi, wo, yu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 101.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.

**N/T/U:** wa nya ma - wanyama

**U:** uwezo, watu, wengi

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 101**.

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kuhesabu, kumi.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

## Maswali

**N:** Chura na chui waliishi wapi? *(Kichochoro)*

**T:** Wanyama walipenda mchezo gani? *(Kuhesabu nyota)*

**U:** Je, unafikiri wanyama walicheza mchezo wao saa ngapi? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kikombe **changu.** - Vikombe **vyetu.**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 101.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore aina nne ya matunda ya kiasilia ayapendayo na kuandika majina yake.

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo 2**

**Kipindi 101**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

w h s

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

y e → **ye**, w i → **wi**, w o → **wo**, y u → **yu**

- Soma silabi na maneno.

wa nya ma → **wanyama**, u we zo → **uwezo**, wa tu → **watu**, we ngi → **wengi**

- **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Andika wingi wa vifungu hivi.

1. Mguu **wangu**
2. Mswaki **wangu**
3. Familia **yangu**

**Kusoma hadithi**

**Mchezo wa wanyama**



Chatu, chura na chui ni wanyama. Waliishi kwenye kichochoro. Walipenda mchezo wa kuhesabu nyota. Chatu alihesabu nyota tano. Chui naye alihesabu saba. Chura alihesabu kumi. Chura alishinda mchezo. Chui alikasirika. Akamweka Chura kwenye chupa.

101 Hakiuzwi

Kipindi cha 101 na 102 **Marejeleo 2**

**Kipindi 102**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

W w H h S s


- Soma sehemu za neno na neno lote.

a li kasirika → **alikasirika**, a li hesabu → **alihesabu**
wa li ishi → **waliishi**, a ka m weka → **akamweka**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Fisi na Tumbili**



Mali ya Serikali ya Kenya 102

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** W
**U:** Endelea na herufi w, H, h, S, s.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 102.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo upesi na useme neno.
**N/T/U:** a li kasirika - alikasirika
**U:** Endelea na: alihesabu, waliishi
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 102.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 101.**

### Hadithi ya mwalimu

**Fisi na tumbili**

Fisi aliishi porini. Siku moja alienda kutafuta chakula. Alikutana na kondoo. Alimuuliza, "Wewe ni nani?" Kondoo alijibu kwa woga, "Mimi ni kondoo." Fisi alisema, "Nahisi njaa. Nitakula." Kondoo alijibu, "Usinile. Ngoja nimuite rafiki yangu. Ni mtamu zaidi." Kondoo alimuita sungura. Alipokuja fisi alimuuliza, "Wewe ni nani?" Sungura alijibu kwa woga, "Mimi ni sungura." Fisi alisema, "Nahisi njaa. Nitakula." Sungura alijibu, "Usinile. Ngoja nimuite rafiki yangu. Ni mtamu zaidi." Sungura alimuita tumbili. Alipokuja fisi alimuuliza, "Wewe ni nani?" Tumbili alijibu kwa woga, "Mimi ni tumbili." Fisi alisema, "Nahisi njaa. Nitakula." Tumbili alijibu, "Ningependa kuwa kitoweo chako. Lakini kabla ya kunila, nipeleke hadi pale mtini. Niliuacha moyo wangu mtini. Nao ndio mtamu zaidi." Fisi alimbeba tumbili hadi mtini. Tumbili aliruka haraka hadi kwenye tawi la juu zaidi la mti. Aliangua kicheko na kusema, "He! He! He! Nimeponea chupuchupu. Wajinga ndio waliwao."

Funza maana ya maneno mapya: **porini, kondoo, fisi.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Fisi alikutana na wanyama wangapi? *(Watatu)*
**T:** Taja wanyama ambao fisi alikutana nao. *(Sungura, tumbili, kondoo)*
**U:** Unafikiri fisi alikula nini? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Wanafunzi waandike tarakimu kwa maneno 1 - 10 katika vikundi vya watu wawili, kisha wacheze mchezo wa kuhesabu wanaoujua.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike aina nne ya vyakula vya kiasili anavyokula nyumbani.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 103: Marejeleo

**Kipindi cha** 103 na 104 **Marejeleo 2**

**Kipindi 103**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**nd** **y**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| nd e | nd i | nd o | y o |
|---|---|---|---|
| **nde** | **ndi** | **ndo** | **yo** |

- Soma silabi na maneno.

| ya ngu | nye u pe | ya ke | nya nya |
|---|---|---|---|
| **yangu** | **nyeupe** | **yake** | **nyanya** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Wazee **hawa** wanaugua.
2. Mtoto **huyu** ni mdogo.
3. Mwalimu **huyu** ni mrefu.

**Kusoma hadithi**

**Kaka Banda**



Mimi ni Ndunge. Nina ndugu mmoja anayeitwa Banda. Banda anaishi Suswa. Nyumba yake iko karibu na Bonde. Banda hutengeneza sabuni. Mke wake hupika maharagwe na mahindi. Juzi nilipomtembelea, Banda alininunulia kitanda, kinanda na kalenda kutoka kwa rafiki yake Janda. Banda alinishauri nisome kwa bidii ili niishi maisha mazuri baadaye.

103 Hakiuzwi

**Kipindi cha** 103 na 104 **Marejeleo 2**

**Kipindi 104**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ND** **nd**


- Soma sehemu za neno na neno lote.

| ni li po m tembelea | a li ni shauri |
|---|---|
| **nilipomtembelea** | **alinishauri** |
| a na ye itwa | a li ni nunulia |
| **anayeitwa** | **alininunulia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sehemu za mwili**



Mali ya Serikali ya Kenya

104

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/y/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** yangu, nyanya

**U:** yangu, nyeupe, yake, nyanya

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** nd

**U:** Endelea na herufi **y**.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 103**.

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /nd/ /e/ silabi ni nde

**U:** Endelea na ndi, ndo

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 103.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ya ngu - yangu

**U:** Endelea na maneno nyeupe, yake

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 103.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **bonde, kinanda, kalenda.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Banda anaishi wapi? *(Suswa)*

**T:** Mke wake Banda hufanya kazi gani? *(Hupika maharagwe na mahindi)*

**U:** Wewe una kaka wangapi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya hawa na huyu**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 103.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike watu wanne anaowapenda katika familia yake. Atumie majina ya familia kwa mfano: nyanya.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 103 na 104 **Marejeleo 2**

**Kipindi 103**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**nd** **y**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| nd e | nd i | nd o | y o |
|---|---|---|---|
| **nde** | **ndi** | **ndo** | **yo** |

- Soma silabi na maneno.

| ya ngu | nye u pe | ya ke | nya nya |
|---|---|---|---|
| **yangu** | **nyeupe** | **yake** | **nyanya** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi zifuatazo.

1. Wazee **hawa** wanaugua.
2. Mtoto **huyu** ni mdogo.
3. Mwalimu **huyu** ni mrefu.

**Kusoma hadithi**

**Kaka Banda**



Mimi ni Ndunge. Nina ndugu mmoja anayeitwa Banda. Banda anaishi Suswa. Nyumba yake iko karibu na Bonde. Banda hutengeneza sabuni. Mke wake hupika maharagwe na mahindi. Juzi nilipomtembelea, Banda alininunulia kitanda, kinanda na kalenda kutoka kwa rafiki yake Janda. Banda alinishauri nisome kwa bidii ili niishi maisha mazuri baadaye.

103 Hakiuzwi

Kipindi cha 103 na 104 **Marejeleo 2**

**Kipindi 104**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ND** **nd**


- Soma sehemu za neno na neno lote.

| ni li po m tembelea | a li ni shauri |
|---|---|
| **nilipomtembelea** | **alinishauri** |
| a na ye itwa | a li ni nunulia |
| **anayeitwa** | **alininunulia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Sehemu za mwili**



Mali ya Serikali ya Kenya 104

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ND

**U:** Endelea na herufi nd.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 104**.

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** ni li po m tembelea - nilipomtembelea

**U:** alinishauri, alininunulia, anayeitwa.

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 104**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 103**.

### Hadithi ya mwalimu

**Sehemu za mwili**

Kichwa, mabega, magoti, vidole,
Magoti vidole, magoti, vidole,
Kichwa, mabega, magoti, vidole,
Masikio, macho, pua na mdomo.

Nitazitunza sehemu za mwili,
sehemu za mwili, sehemu za mwili,
Nitazitunza sehemu za mwili,
Masikio, macho, pua na mdomo.

Kichwa, mabega, magoti vidole,
Magoti vidole, magoti vidole,
Kichwa, mabega, magoti, vidole,
Masikio, macho, pua na mdomo.

Tukiwa nyumbani, tutunze miguu,
Tutunze mgongo, tutunze tumbo,
Tukiwa nyumbani, tutunze shingo,
Sehemu zote, za mwili tutunze.

Tukiwa shuleni, tutunze nywele,
Tutunze pua, tutunze kucha,
Tukiwa shuleni, tutunze macho,
Sehemu zote, za mwili tutunze.

Funza maana ya maneno haya: **nitazitunza, magoti.** Soma kichwa cha shairi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Taja sehemu za mwili zilizotajwa kwenye shairi. *(Kichwa, vidole, magoti n.k)*

**T:** Taja sehemu za mwili unazojua. *(Kubali jibu sahihi.)*

**U:** Eleza umuhimu wa kutunza sehemu zetu za mwili. *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Eleza wanafunzi wajadiliane wakiwa katika vikundi vya wawili wawili kisha waandike siku wanazoenda shuleni.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno manne katika umoja na wingi. Kwa mfano: mtu – watu.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 105: Marejeleo

Kipindi cha 105 **Marejeleo 2**

**Kipindi 105**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Y y** **W w**

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: we za - weza**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| va | za | ye | we | wu |
| zi | vo | sa | za | i |

**Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo**

Kamilisha sentensi zifuatazo ukitumia nafsi ya kwanza na wakati uliopo. **Kwa mfano:**

| **Mimi ninaenda shuleni** | **Sisi tunaenda shuleni** |
|---|---|
| 1. **Mimi** ___ nunua kalamu. | **Sisi** ___ nunua kalamu. |
| 2. **Mimi** ___ cheza mpira. | **Sisi** ___ cheza mpira. |
| 3. **Mimi** ___ chota maji. | **Sisi** ___ chota maji. |
| 4. **Mimi** ___ kunywa uji. | **Sisi** ___ kunywa uji. |
| 5. **Mimi** ___ fyeka nyasi. | **Sisi** ___ fyeka nyasi. |
| 6. **Mimi** ___ pika sima. | **Sisi** ___ pika sima. |
| 7. **Mimi** ___ tazama runinga. | **Sisi** ___ tazama runinga. |

**Zoezi: Kuandika**

Andika maneno haya katika daftari lako.

1. Maharagwe
2. Gredi
3. Jumanne

105

Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** Y

**U:** Endelea na herufi y, W, w.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 105**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi 'we' na 'za' kuandika neno 'weza'. Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 105**.

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 105.**

## Kuandika maneno

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: yangu, zizi

## Kuandika

**T:** Rejelea aina mbalimbali za chakula pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 105** katika daftari lake.

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi ahamasishe mwenzake nyumbani kuhusu umuhimu wa vyakula vya kiasili.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 106: Mwili wangu 2

**Kipindi cha 106 na 107 — Mwili wangu 2**

**Kipindi 106**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ch** **w** **h**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ch e | ch i | ch o | dh o | b o |
|---|---|---|---|---|
| **che** | **chi** | **cho** | **dho** | **bo** |

● Soma silabi na maneno.

| m si cha na | ku cha na | cha ke | ku cha |
|---|---|---|---|
| **msichana** | **kuchana** | **chake** | **kucha** |

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma sentensi hizi kwa sauti.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Ki**dole kinauma. | 1. **Vi**dole vinauma. |
| 2. **M**guu umeoshwa. | 2. **Mi**guu imeoshwa. |
| 3. **Ki**fua kimepona. | 4. **Vi**fua vimepona. |

**Kusoma hadithi**

**Gacheri ajifunza usafi**



Chema alikuwa msichana safi. Alipenda kuoga, kusugua meno na kuchana nywele zake. Kila mtu alimpenda na kumsifu. Gacheri alitaka kuwa kama Chema. Chema alimfunza jinsi ya kudumisha usafi. Walimu walifurahi. Chema aliahidi kufundisha wasichana wengine usafi wa mwili.

Mali ya Serikali ya Kenya

106

**Kipindi cha 106 na 107 — Mwili wangu 2**

**Kipindi 107**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**V** **v**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li m penda | ku m sifu |
|---|---|
| **alimpenda** | **kumsifu** |
| a li m funza | wa li m zawadia |
| **alimfunza** | **walimzawadia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mwili wangu**



107

Hakiluzwi

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/ch/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T:** chafu, shavu

**U:** chake, chatu

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ch

**U:** Endelea na herufi h na w.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 106.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /ch/ /e/ silabi ni che

**U:** Endelea na silabi chi, cho, dho, bo

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 106.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** m si cha na - msichana

**U:** - Endelea na maneno kuchana, chake, kucha

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 106.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kusugua meno, kuchana nywele, kudumisha.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Nani alikuwa msichana safi? *(Chema)*

**T:** Taja vitu alivyofanya msichana safi. *(Kuoga, kusugua meno na kuchana nywele zake)*

**U:** Ungefanya nini kama ungekuwa na rafiki mchafu? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**

Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: **M**kono - **Mi**kono

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurusa wa 106.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike majina manne yanayohusu kutunza na kuheshimu mwili wake.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

Kipindi cha 106 na 107 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 106**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch w h

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ch e | ch i | ch o | dh o | b o |
|---|---|---|---|---|
| che | chi | cho | dho | bo |

- Soma silabi na maneno.

| m si cha na | ku cha na | cha ke | ku cha |
|---|---|---|---|
| msichana | kuchana | chake | kucha |

**Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Soma sentensi hizi kwa sauti.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Ki**dole kinauma. | 1. **Vi**dole vinauma. |
| 2. **M**guu umeoshwa. | 2. **Mi**guu imeoshwa. |
| 3. **Ki**fua kimepona. | 4. **Vi**fua vimepona. |

**Kusoma hadithi**

**Gacheri ajifunza usafi**



Chema alikuwa msichana safi. Alipenda kuoga, kusugua meno na kuchana nywele zake. Kila mtu alimpenda na kumsifu. Gacheri alitaka kuwa kama Chema. Chema alimfunza jinsi ya kudumisha usafi. Walimu walifurahi. Chema aliahidi kufundisha wasichana wengine usafi wa mwili.

Mali ya Serikali ya Kenya

106

Kipindi cha 106 na 107 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 107**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

V v

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li m penda | ku m sifu |
|---|---|
| alimpenda | kumsifu |
| a li m funza | wa li m zawadia |
| alimfunza | walimzawadia |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mwili wangu**



107

Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** V

**U:** Endelea na herufi v.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 107.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo useme neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li m penda - alimpenda

**U:** Endelea na maneno kumsifu, alimfunza, walimzawadia

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 107.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 106.**

### Hadithi ya mwalimu

**Mwili wangu**

Jana mchana mama yangu alimwosha dada yangu Maria. Nilimwomba mama aniruhusu nimwoshe Maria. Mama aliamua kunifunza kwanza. Kesho yake, nilimwosha Maria. Nilianza kwa kumwosha kichwa. Niliizisafisha nywele zake na masikio. kwenye uso, nikamwosha macho, pua na mdomo.
Kisha nikamwosha mikono, kifua, tumbo na magoti. Nilimaliza kwa kuiosha miguu yote miwili na kukata kucha. “Mama, kwa nini Maria huoshwa mara mbili kwa siku?” Nilimwuliza mama. “Kila mtu anatakiwa kuoga kila mara,” alijibu mama. Alisema kuwa wasichana kama mimi sawa na wavulana wanatakiwa kuoga baada ya kucheza.

Funza maana ya maneno haya: **uso, kifua, tumbo**. Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Maria huoshwa mara ngapi kwa siku? *(Mbili)*

**T:** Taja sehemu alizooshwa Maria kwenye uso. *(Kichwa, nywele, masikio, uso, macho, pua na mdomo)*

**U:** Kwa nini ni muhimu kuoga? *(Ili tuwe safi)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike sehemu tano za mwili.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike njia nne za kutunza na kuheshimu mwili wake.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 108 na 109 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 108**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**dh** **ch**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| dh e | dh i | dh o | dh u | ch i |
|---|---|---|---|---|
| **dhe** | **dhi** | **dho** | **dhu** | **chi** |

● Soma silabi na maneno.

| na dhi fu | dha ha bu | dha rau |
|---|---|---|
| **nadhifu** | **dhahabu** | **dharau** |

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Tumia maneno haya kutunga sentensi katika **umoja**.

1. kiuno
2. kichwa
3. mkono

**Kusoma hadithi**

**Chitai na Bukachi**



Chitai na Bukachi ni watoto nadhifu. Kila asubuhi wao huoga na kupiga meno mswaki. Kisha huvaa viatu na soksi za rangi ya dhahabu. Wao hufanya kazi za nyumbani bila dharau. Wao hunawa kabla ya kula na baada ya kutumia msala na kucheza. Wao hupata lishe bora. Wamefunzwa kuwa uchafu hudhuru afya.

Mali ya Serikali ya Kenya 108

Kipindi cha 108 na 109 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 109**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**DH** **dh**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu nawa | hu oga |
|---|---|
| **hunawa** | **huoga** |
| wa me funzwa | hu dhuru |
| **wamefunzwa** | **hudhuru** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Familia ya vidole**



109 Hakiluzwi

### Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/dh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.
**N/T/U:** dhahabu, thamani
**U:** dhahabu, thamani, nadhifu, dhati

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** dh
**U:** Endelea na herufi ch.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 108.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:** silabi ni /dh/ /e/ dhe
**U:** Endelea na silabi dhi, dho, dho, chi
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 108.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** na dhi fu - nadhifu
**U:** Endelea na maneno dhahabu na dharau
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 108.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya:**nadhifu, dhahabu, dharau.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Chitai na Bukachi hupenda nini? *(Kuoga na kupiga meno mswaki)*
**T:** Kila mara wakitoka msalani hufanya nini? *(Hunawa mikono)*
**U:** Eleza uhuhimu wa lishe bora. *(Kubali jibu sahihi)*

### Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**
Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: Jicho - **Macho**

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 108.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne akitumia sehemu za mwili zifuatazo: mkono, miguu, pua, mdomo.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 109: Mwili wangu 2

**Kipindi cha** 108 na 109 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 108**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **dh** **ch**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| dh e | dh i | dh o | dh u | ch i |
|---|---|---|---|---|
| **dhe** | **dhi** | **dho** | **dhu** | **chi** |

- Soma silabi na maneno.

| na dhi fu | dha ha bu | dha rau |
|---|---|---|
| **nadhifu** | **dhahabu** | **dharau** |

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Tumia maneno haya kutunga sentensi katika **umoja**.

1. kiuno
2. kichwa
3. mkono

**Kusoma hadithi**

**Chitai na Bukachi**



Chitai na Bukachi ni watoto nadhifu. Kila asubuhi wao huoga na kupiga meno mswaki. Kisha huvaa viatu na soksi za rangi ya dhahabu. Wao hufanya kazi za nyumbani bila dharau. Wao hunawa kabla ya kula na baada ya kutumia msala na kucheza. Wao hupata lishe bora. Wamefunzwa kuwa uchafu hudhuru afya.

Mali ya Serikali ya Kenya 108

**Kipindi cha** 108 na 109 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 109**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **DH** **dh**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu nawa | hu oga |
|---|---|
| **hunawa** | **huoga** |
| wa me funzwa | hu dhuru |
| **wamefunzwa** | **hudhuru** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Familia ya vidole**



109 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** DH

**U:** Endelea na dh.

Wanafunzi wasome jina la herufi na sauti kwenye **ukurasa wa 109.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha unganishe sehemu hizo useme neno lote kwa upesi.

**N/T/U:** hu nawa - hunawa

**U:** Endelea na huoga, wamefunzwa

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 109.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 108.**

### Hadithi ya mwalimu

**Familia ya vidole**

Familia ya vidole iliishi katika kijiji cha Mwili. Kulikuwa na vidole mbalimbali: kidole cha gumba, kidole cha shahada, kidole cha kati, kidole cha pete na kidole kidogo. Siku moja, vidole vilijadili kuhusu ni nani alikuwa muhimu zaidi kati yao.
Kidole cha gumba kikasema, "Bila mimi, nyinyi ni dhaifu kabisa." Kidole cha kati kikajibu kwa maringo, "Wee, mfupi! Huoni mimi ndimi mrefu zaidi?" Kidole cha pete kikasema, "Binadamu ananiheshimu sana. Ndio maana yeye hunivisha pete." Kidole cha shahada kikawaza na kusema, "Hamjui mimi ndimi alama ya nguvu?" Mwishowe kidole cha mwisho kikajibu, "Wacheni kusemezana. Kila mmoja wetu ana manufaa. Tukifanya kazi pamoja na kwa amani, tutaendelea kujenga familia yetu. Tunastahili kuishi pamoja na kushirikiana ili tufaulu maishani. Umoja ni nguvu."

Funza maana ya maneno haya: **gumba, shahada, kusemezana.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Siku moja vidole viliongea kuhusu nini? *(Ninani alikuwa muhimu zaidi kati yao)*

**T:** Kidole cha gumba kilisemaje? *(Bila mimi, nyinyi ni dhaifu sana)*

**U:** Je, kwa kujadiliana na mwenzako, unafikiri vidole hushirikiana vipi? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike majina ya vidole vya mkono.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aeleze umuhimu wa sehemu za mwili zifuatazo.

1. Macho
2. Mdomo
3. Nyayo
4. Mikono

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 110: Mwili wangu 2

Kipindi cha 110 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 110**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

DH dh CH ch

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: fe dhe ha - fedheha**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| dha | ha | cho | u | dhe |
| ho | ra | fe | che | da |

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Tumia maneno haya kutunga sentensi katika wingi.

1. masikio
2. vidole
3. mapaja
4. macho
5. midomo
6. pua

**Zoezi: Kuandika**

Andika wingi wa sehemu hizi za mwili.

1. mkono
2. mguu
3. kidole
4. tumbo
5. kiuno
6. kifua

Mali ya Serikali ya Kenya 110

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** DH
**U:** Endelea na herufi CH, ch na dh.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 110**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.
**N/T/U:** Soma silabi zote. Tumia silabi 'fe dhe ha' kuandika neno 'fedheha'. Soma neno pamoja na mwanafunzi.
**U:** Mpe mwanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 110.**

## Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**

Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: **M**gongo - **Mi**gongo
Mwanafunzi wafanye zoezi kwenye **ukurasa wa 110.**

## Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **chafu, shavu.**
Hakikisha wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

## Kuandika

**T:** Rejelea sarufi ya umoja na wingi pamoja na wanafunzi.
**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 110** katika daftari lake.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aimbie mlezi wake nyimbo anazozijua.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 111: Mwili wangu 2

Kipindi cha 111 na 112 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 111**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng** **dh** **d**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ng e — **nge**  ng i — **ngi**  ng o — **ngo**  ng u — **ngu**  dh e — **dhe**

- Soma silabi na maneno.

we nza ngu — **wenzangu**  tu zu ngu m ze — **tuzungumze**  nyi ngi — **nyingi**

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Andika wingi wa sehemu hizi za mwili.

**1.** ukucha **2.** goti **3.** kisigino

**Kusoma Shairi**

**Mwili**



Sikilizeni wenzangu, pamoja tuzungumze,
Shairi tulikariri, kuhusu mwili,
Mwili ni muhimu, amenipa Mungu,
Sehemu za mwili, tuzitunze vizuri.

Sehemu hizi ni nyingi, kama tunavyofahamu,
Tunayo macho, pua na mdomo,
Macho huona, pua hunusa,
Midomo huongea, tuitunze vizuri.

Zote sijazitaja, nawe uzitaje,
Mikono hushika, miguu hutembea,
Sikio husikia, yale anayosema mwalimu,
Sehemu unazozijua, unazitunzaje?

111 Hakiuzwi

Kipindi cha 111 na 112 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 112**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**NG** **ng**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

tu zungumze — **tuzungumze**  tu li kariri — **tulikariri**

tu zi tunzeni — **tuzitunzeni**  u ta zi taja — **utazitaja**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Safari yetu**



Mali ya Serikali ya Kenya 112

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/ng/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ngao, shingoni

**U:** ngapi, shanga, ngazi, mguu

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ng

**U:** Endelea na herufi dh na d.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 111**.

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /ng/ /e/ silabi ni nge

**U:** Endelea na ngi, ngo, dhe

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 111.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** we nza ngu - wenzangu

**U:** Endelea na neno tuzungumze

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 111**.

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **midomo, pua, sikio.**

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

## Maswali

**N:** Shairi hili linahusu nini? *(Mwili wangu)*

**T:** Pua hufanya kazi gani? *(Kunusa)*

**U:** Kwa nini ni muhimu kuutunza mwili wako? *(Kubali jibu sahihi)*

## Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**

Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: **Kifua - Vifua**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 111.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi akamilishe vifungu vifuatavyo akitumia **huyu** au **hawa.**

1. Walimu __________
2. Mbuzi ____________
3. Msichana __________
4. Madaktari __________

Tarehe: ____________________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Kipindi cha 111 na 112 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 111**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

ng  dh  d

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ng e → **nge**  ng i → **ngi**  ng o → **ngo**  ng u → **ngu**  dh e → **dhe**

- Soma silabi na maneno.

we nza ngu → **wenzangu**  tu zu ngu m ze → **tuzungumze**  nyi ngi → **nyingi**

- **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Andika wingi wa sehemu hizi za mwili.

**1.** ukucha **2.** goti **3.** kisigino

**Kusoma Shairi**

**Mwili**



Sikilizeni wenzangu, pamoja tuzungumze,
Shairi tulikariri, kuhusu mwili,
Mwili ni muhimu, amenipa Mungu,
Sehemu za mwili, tuzitunze vizuri.

Sehemu hizi ni nyingi, kama tunavyofahamu,
Tunayo macho, pua na mdomo,
Macho huona, pua hunusa,
Midomo huongea, tuitunze vizuri.

Zote sijazitaja, nawe uzitaje,
Mikono hushika, miguu hutembea,
Sikio husikia, yale anayosema mwalimu,
Sehemu unazozijua, unazitunzaje?

111 Hakluzwi

Kipindi cha 111 na 112 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 112**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

NG  ng

- Soma sehemu za neno na neno lote.

tu zungumze → **tuzungumze**  tu li kariri → **tulikariri**
tu zi tunzeni → **tuzitunzeni**  u ta zi taja → **utazitaja**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Safari yetu**



Mali ya Serikali ya Kenya  112

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** NG
**U:** Endelea na herufi ng.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 112**.

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo useme neno kwa upesi.
**N/T/U:** tu zungumze - tuzungumze
**U:** Endelea na maneno tulikariri, tuzitunzeni, utazitaja
Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 112**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 111**.

### Hadithi ya mwalimu

**Safari yetu**
Jumamosi tulienda kumtembelea nyanya. Nilivaa nguo mpya na viatu maridadi. Kaka yangu alijikwaa tukicheza, alivaa champali. Mama alinipa kikapu nibebe mgongoni. Mama alibeba gunia la viazi kichwani. Tulipoanza safari, mama alituambia tuchunge tusianguke. Tulipofika mtoni mimi na kaka yangu tulishindwa kuvuka. Mama alivuka upande wa pili na kutua gunia la viazi. Alirudi upande wetu. Alimbeba kaka yangu begani na kuvishika vidole vyangu vya mkono. Tulivuka mto na kuendelea na safari yetu hadi kwa nyanya. Nyanya alifurahi kutuona.

Funza maana ya maneno haya: **mgongoni, begani, champali**. Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Mama alibebea wapi gunia la viazi? *(Kwenye kichwa)*
**T:** Tunashika vitu kwa kutumia nini? *(Mikono)*
**U:** Kwa nini watu huvaa viatu? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike sentensi zifuatazo kwa wingi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Huu ni mkono. | ________________ |
| 2. Huu ni mpira. | ________________ |
| 3. Huu ni mkoba. | ________________ |

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi zifuatazo na awasomee walezi wake nyumbani.

1. Kuku huyu ni wetu.
2. Ng'ombe hawa wamekula nyasi.
3. Vifaranga hawa ni wengi.
4. Magari haya ni ya babu.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 113 na 114 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 113**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**gh** **ng** **ch**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

gh e **ghe** gh i **ghi** gh o **gho** gh u **ghu** ng a **nga** ch u **chu**

- Soma silabi na maneno.

gho ro fa ni **ghorofani** m cha nga ni **mchangani**

fo ro dha ni **forodhani** ki chwa **kichwa**

◆ **Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

**1.** sikio **2.** kiganja **3.** kiuno

**Kusoma hadithi**

**Marafiki watatu**



Mjini Mwili paliishi marafiki watatu. Wa kwanza aliitwa Kichwa. Aliishi ghorofani pamoja na ndugu zake Macho, Pua, Mdomo na Masikio. Wa pili alikuwa Mkono. Aliishi forodhani na ndugu zake Vidole na Kucha. Wa tatu alikuwa Mguu. Aliishi mchangani na ndugu zake, Nyayo na Visigino. Marafiki hao watatu walifaana kwa hali na mali. Waliishi raha mustarehe.

113 Hakiuzwi

Kipindi cha 113 na 114 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 114**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**GH** **gh**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

pa li ishi **paliishi** a li itwa **aliitwa**

a li ishi **aliishi** a li kuwa **alikuwa**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Nywele zetu**



Mali ya Serikali ya Kenya 114

## Ufahamu wa fonimu

Tamka sauti **/gh/**. Soma maneno. Mwanafunzi aonyeshe kidole juu akisikia sauti mwanzoni mwa neno au aonyeshe kidole chini asiposikia sauti mwanzoni mwa neno.

**N/T/U:** ghasia, kifua, gharama

**U:** gari, gharama, ghorofa

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** gh

**U:** Endelea na ng na ch.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 113**.

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /gh/ /e/ silabi ghe

**U:** Endelea na ghi, gho, ghu, chu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 113.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** gho ro fa ni - ghorofani

**U:** mchangani, forodhani, kichwa

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 113.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kichwa, macho, vidole.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Taja marafiki wanaozungumziwa katika hadithi? *(Kichwa, mkono, mguu)*

**T:** Taja ndugu wa kichwa. *(Macho, pua, mdomo na masikio)*

**U:** Sehemu zilizotajwa zina umuhimu gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**

Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: Goti - **Magoti**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 113.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentenzi akitumia maneno haya:

1. Kuoga 2. Rafiki 3. Safi

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 113 na 114 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 113**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**gh** **ng** **ch**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| gh e | gh i | gh o | gh u | ng a | ch u |
|---|---|---|---|---|---|
| **ghe** | **ghi** | **gho** | **ghu** | **nga** | **chu** |

Soma silabi na maneno.

gho ro fa ni
**ghorofani**

m cha nga ni
**mchangani**

fo ro dha ni
**forodhani**

ki chwa
**kichwa**

**Sarufi: Umoja na wingi wa majina**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

1. sikio 2. kiganja 3. kiuno

**Kusoma hadithi**

**Marafiki watatu**



Mjini Mwili paliishi marafiki watatu. Wa kwanza aliitwa Kichwa. Aliishi ghorofani pamoja na ndugu zake Macho, Pua, Mdomo na Masikio. Wa pili alikuwa Mkono. Aliishi forodhani na ndugu zake Vidole na Kucha. Wa tatu alikuwa Mguu. Aliishi mchangani na ndugu zake, Nyayo na Visigino. Marafiki hao watatu walifaana kwa hali na mali. Waliishi raha mustarehe.

113 Hakluzwi

Kipindi cha 113 na 114 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 114**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**GH** **gh**

Soma sehemu za neno na neno lote.

pa li ishi
**paliishi**

a li itwa
**aliitwa**

a li ishi
**aliishi**

a li kuwa
**alikuwa**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Nywele zetu**



Mali ya Serikali ya Kenya 114

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** GH

**U:** Endelea na herufi gh.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 114**.

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo useme neno lote kwa upesi.

**N/T/U:** Endelea na maneno pa li ishi - paliishi

**U:** aliitwa, aliishi, alikuwa

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 114**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 113**.

### Hadithi ya mwalimu

**Nywele zetu**

Nywele hupatikana sehemu ya juu ya kichwa. Watu wengi hupenda kufuga nywele. Wasichana hufuga nywele ndefu. Wavulana nao huwa na nywele fupi. Nywele za kupendeza ni muhimu kuwekwa safi kila wakati. Nywele chafu huingiwa na chawa. Nywele chafu zinaweza kuleta magonjwa. Nywele safi hupendeza na kumeremeta. Ukitaka kuwa na nywele za kupendeza ni sharti uzitunze vilivyo. Nywele lazima zioshwe vizuri na maji vuguvugu pamoja na sabuni. Baada ya kuoshwa sharti zipakwe mafuta na kuchanwa kwa kichana safi. Wale wapendao nywele fupi huzipeleka kwa kinyozi.

Funza maana ya maneno haya: **nywele, kumeremeta, kichwa.**

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Nywele hupatikana wapi? *(Hupatikana sehemu ya juu ya kichwa)*

**T:** Nywele chafu huleta nini? *(Huleta chawa, magonjwa ya ngozi)*

**U:** Wewe hutunza vipi nywele zako? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mwanafunzi atazame picha kisha aandike sentensi nne kuhusu picha hiyo.

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi nne kuhusu usafi wa mwili.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 115: Mwili wangu 2

Kipindi cha 115 **Mwili wangu 2**

**Kipindi 115**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

GH gh NG ng

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: chu nga - chunga**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| nga | li | chu | ge | gha |
| ngu | fa | ga | m | ni |

**Sarufi: Umoja na wingi**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Si**kio linauma. | **Ma**sikio yanauma. |
| 2. **M**kono umechafuka. | **Mi**kono imechafuka. |
| 3. **M**guu wake ni mfupi. | **Mi**guu yao ni mifupi. |
| 4. **Ji**cho langu linatoa machozi. | **Ma**cho yetu yanatoa machozi. |
| 5. **U**kucha wangu unapakwa rangi. | **Ku**cha zetu zinapakwa rangi. |

**Zoezi: Kuandika**

Chora umbo la kichwa na utaje sehemu hizi.

1. jicho
2. sikio
3. pua

115 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** GH
**U:** Endelea na herufi gh, NG, ng.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 115**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.
**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'chu' na 'nga' kuandika neno chunga. Soma neno pamoja na mwanafunzi.
**U:** Mpe mwanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 115**.

## Sarufi

**Umoja na wingi wa majina**
Eleza umoja na wingi wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: Sikio - **Ma**sikio
Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 115.**

## Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **kusugua, meno**
Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

## Kuandika

**T:** Rejelea sehemu mbalimbali za mwili pamoja na wanafunzi.
**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 115** katika daftari lake.

## Kazi ya nyongeza

Waongoze wanafunzi washiriki mchezo wa kuigiza kuhusu usafi wa mwili wakiwa katika vikundi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 116: Usafi wa mwili 3

Kipindi cha 116 na 117 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 116**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  k j l m

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  j o → jo  m a → ma  i → i  k i → ki

- Soma silabi na maneno.

  ki ja na → kijana  ja mi i → jamii  ku o ga → kuoga  ku ka ta → kukata

- **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

  Tunga sentensi tatu ukitumia **huyu** katika umoja na **hawa** katika wingi.

**Kusoma hadithi**

**Waweru**



Waweru ni kijana safi. Kijana huyo ni mfano mwema katika jamii. Huzingatia usafi kila wakati. Yeye hunyoa nywele na kukata kucha zake. Rafiki zake Alimlim na Nafula hupenda kucheza naye. Wamefuata mfano mwema kutoka kwa Waweru. Wao hufua nguo na kuzipiga pasi. Pia huoga mara mbili na kusugua meno kila siku.

Mali ya Serikali ya Kenya  116

Kipindi cha 116 na 117 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 117**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  K k

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  hu zingatia → huzingatia  hu nyoa → hunyoa

  hu penda → hupenda  wa me iga → wameiga

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Usafi wa mwili**



117  Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** k

**U:** Endelea na herufi j, l na m.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 116.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /j/ /o/ silabi ni jo

**U:** Endelea na silabi ma, i.

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 116.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** ki ja na - kijana

**U:** Endelea na maneno jamii, kuoga, kukata

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 116.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **hunyoa nywele, kusugua, meno.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Kijana mtanashati anaitwaje? *(Waweru)*

**T:** Kijana mtanashati hufanya nini kila wakati? *(Huzingatia usafi)*

**U:** Je, wewe hufanya nini kuweka nywele yako safi? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 116.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi akamilishe vifungu vifuatavyo akitumia **huyu** au **hawa.**

**Kwa mfano:** Mwanafunzi huyu

1. Walimu __________  2. Msichana __________
3. Mbuzi __________  4. Mtoto __________
5. Madaktari __________

Tarehe: ____________________ Muda: ____________________ Idadi: ____________________

# Kipindi cha 117: Usafi wa mwili 3

Kipindi cha 116 na 117 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 116**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

k j l m

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

j o → **jo** m a → **ma** i → **i** k i → **ki**

- Soma silabi na maneno.

ki ja na → **kijana** ja mi i → **jamii** ku o ga → **kuoga** ku ka ta → **kukata**

- **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Tunga sentensi tatu ukitumia **huyu** katika umoja na **hawa** katika wingi.

**Kusoma hadithi**

**Waweru**



Waweru ni kijana safi. Kijana huyo ni mfano mwema katika jamii. Huzingatia usafi kila wakati. Yeye hunyoa nywele na kukata kucha zake. Rafiki zake Alimlim na Nafula hupenda kucheza naye. Wamefuata mfano mwema kutoka kwa Waweru. Wao hufua nguo na kuzipiga pasi. Pia huoga mara mbili na kusugua meno kila siku.

Mali ya Serikali ya Kenya 116

Kipindi cha 116 na 117 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 117**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

K k

- Soma sehemu za neno na neno lote.

hu zingatia → **huzingatia** hu nyoa → **hunyoa**

hu penda → **hupenda** wa me iga → **wameiga**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Usafi wa mwili**



117 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** K
**U:** Endelea na herufi k.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 117**.

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo useme neno lote upesi.
**N/T/U:** hu zingatia - huzingatia
**U:** Endelea na maneno hunyoa, hupenda, wameiga
Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 117.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 116**.

## Hadithi ya mwalimu

**Usafi wa mwili**

Usafi ni muhimu kwetu. Sharti tuweke miili yetu safi. Ukiwa mchafu, utapata magonjwa mengi.
Kila asubuhi mimi huoga. Jioni, mimi hucheza na marafiki zangu. Baada ya kula chakula cha jioni mimi husugua meno ili kuondoa mabaki ya chakula. Kila mara, mimi hunawa mikono. Ni muhimu kunawa kabla ya kula na baada ya kutoka msalani. Mimi huzikata kucha zangu zinapokuwa ndefu. Kucha ndefu huweka uchafu.
Ni muhimu kunyoa nywele ili ziwe fupi, nadhifu na za kupendeza. Shuleni, marafiki zangu hukataa kucheza na wanafunzi wachafu. Sote tunafaa kuzingatia usafi wa mili yetu.

Funza maana ya maneno haya: **huoga, huzikata kucha, kunyoa nywele.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Mimi hufanya nini ninapotoka msalani? *(Hunawa mikono.)*

**T:** Marafiki zangu shuleni hukataa kucheza na wanafunzi gani? *(Wanafunzi wachafu)*

**U:** Kwa nini mtoto akiwa mchafu hutorokwa na wengine? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Zoezi

Mwanafunzi aandike sentensi akitumia **huyu** na **hawa**.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi zifuatazo na amsomee mlezi wake.

1. Kuku huyu ni wetu.
2. Ng'ombe hawa wamekula nyasi.
3. Vifaranga hawa ni wengi.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 118: Usafi wa mwili 3

Kipindi cha 118 na 119 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 118**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **m** **k** **l**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  j i → **ji** k o → **ko** k a → **ka** j u → **ju**

- Soma silabi na maneno.

  ki ta nu ka → **kitanuka** ki nywa → **kinywa** u na fi ki ri → **unafikiri** m re mbo → **mrembo**

- **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

  Tunga sentensi nne ukitumia **hawa** katika wingi.

**Kusoma hadithi**

**Sarafina**



Sarafina ni msichana safi. Nywele zake ni ndefu na safi. Sarafina hupenda kusoma pamoja na rafiki zake Hawa na Wendi. Hawa hapendi kuoga. Sarafina humshauri aoge la sivyo mwili utanuka fe! Wendi naye hapendi kusugua meno. Sarafina humshauri ayasugue la sivyo kinywa kitanuka fe! Je, unafikiri Hawa na Wendi watafanya wanavyoshauriwa?

Mali ya Serikali ya Kenya 118

Kipindi cha 118 na 119 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 119**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **M** **K** **L**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  wa na vyo shauriwa → **wanavyoshauriwa** hu m shauri → **humshauri**

  a ya sugue → **ayasugue** ki ta nuka → **kitanuka**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kasiti**



119 Hakiluzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** m
**U:** Endelea na herufi k na l.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 118.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:**/j/ /i/ silabi ni ji
**U:** Endelea na ko, ka
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 118.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.
**N/T/U:** ki ta nu ka - kitanuka
**U:** Endelea na maneno kinywa, unafikiri, mrembo
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 118.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kuchana nywele**, **kuoga**, **kusugua meno.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Nywele za Sarafina ziko vipi? *(Ndefu na safi)*

**T:** taja marafiki wa Sarafina. *(Hawa na Wendi)*

**U:** Je, usipooga ni nini kitafanyika? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**
**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 118.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentenzi akitumia maneno haya:

1. kuoga
2. rafiki
3. safi
4. meno
5. anapenda

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 118 na 119 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 118**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

m k l

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

j i → **ji** k o → **ko** k a → **ka** j u → **ju**

Soma silabi na maneno.

ki ta nu ka → **kitanuka** ki nywa → **kinywa** u na fi ki ri → **unafikiri** m re mbo → **mrembo**

**Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Tunga sentensi nne ukitumia **hawa** katika wingi.

**Kusoma hadithi**

**Sarafina**



Sarafina ni msichana safi. Nywele zake ni ndefu na safi. Sarafina hupenda kusoma pamoja na rafiki zake Hawa na Wendi. Hawa hapendi kuoga. Sarafina humshauri aoge la sivyo mwili utanuka fe! Wendi naye hapendi kusugua meno. Sarafina humshauri ayasugue la sivyo kinywa kitanuka fe! Je, unafikiri Hawa na Wendi watafanya wanavyoshauriwa?

Mali ya Serikali ya Kenya 118

Kipindi cha 118 na 119 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 119**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

M K L

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa na vyo shauriwa → **wanavyoshauriwa** hu m shauri → **humshauri**

a ya sugue → **ayasugue** ki ta nuka → **kitanuka**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kasiti**



119 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** M

**U:** Endelea na K, L

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 119**.

## Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno uunganishe sehemu hizo useme neno lote kwa upesi.

**N/T/U:** wa na vyo shauriwa - wanavyoshauriwa

**U:** Endelea na humshauri, ayasugue

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 119.**

## Wakati wa kusoma

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 118.**

## Hadithi ya mwalimu

**Kasiti**

Kasiti alikuwa mwanafunzi katika shule ya Bongo. Alikuwa mchafu. Hakusugua meno wala kuchana nywele zake. Kucha zake zilikuwa ndefu na chafu. Nywele zake zilijaa chawa. Miguu yake ilikuwa imeliwa na funza. Hakuna aliyetaka kucheza naye. Kasiti alikosa furaha wakati wote.

Siku moja mwalimu Dora alimwita Kasiti. Alimwuliza kwa nini alikuwa mchafu. Kasiti alimwambia kuwa aliogopa maji. Pia, alikuwa ametoroka nyumbani. Mwalimu aliwaita wazazi wa Kasiti. Walimpeleka nyumbani, wakamwosha na kumtibu. Kasiti alinyolewa na kukatwa kucha. Alivaa nguo safi. Kasiti alipokuja shuleni mwalimu Dora alifurahi na kumpongeza. Mwalimu aliwaeleza wanafunzi umuhimu wa usafi wa mwili.

Funza maana ya maneno haya: **hakusugua meno, kucha, kuchana nywele.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## Maswali

**U:** Kasiti alikuwa mwanafunzi katika shule gani? *(Bongo)*

**T:** Ni mambo gani yaliyoonyesha kuwa Kasiti alikuwa mchafu? *(Hakusugua meno wala kuchana nywele zake.)*

**U:** Mtoto akitoroka nyumbani hupata shida gani? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Zoezi

Mwanafunzi ajaze mapengo akitumia maneno haya safi, ndefu na kuoga yalivyotumika kwenye hadithi.

1. Yeye ni msichana ____________________ (safi).
2. Nywele zake ni safi na ________________ (ndefu).
3. Hawa ni mrembo lakini hapendi ________ (kuoga).

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno yafuatayo:

1. kucha 2. nywele

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 120: Usafi wa mwili 3

**Kipindi cha** 120 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 120**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**M m**      **K k**

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ma ji - maji**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| li | ma | ki | i | ko |
| ji | ju | a | ka | ni |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi zifuatazo.

1. **Huyu** ananyoa nywele.
2. **Hawa** wananyoa nywele.
3. **Huyu** anachana nywele.
4. **Hawa** wanachana nywele.
5. Aliyepaka uso mafuta ni **huyu**.
6. Waliopaka nyuso mafuta ni **hawa**.
7. Aliyeninyoa ni **huyu**.
8. Waliotunyoa ni **hawa**.
9. Waliotusuka nywele ni **hawa**.

**Zoezi: Kuandika**

Tunga sentensi tatu ukitumia **huyu** na **hawa**.

Mali ya Serikali ya Kenya

120

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** M

**U:** Endelea na herufi m, K, k.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 120**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'ma ji' kuandika neno 'maji'. Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mpe mwanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 120.**

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 120.**

## Kuandika maneno

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 120** katika daftari lake.

## Kuandika

Mwanafunzi atunge sentensi nne akitumia **huyu** na **hawa**.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Bata _______ ni mzuri. | Bata _______ ni wazuri. |
| 2. Mdudu _______ ni mkali. | Wadudu ______ ni wakali. |
| 3. Kuku _______ ni mdogo. | Kuku ______ ni wadogo. |
| 4. Nyoka _______ ni mrefu. | Nyoka ______ ni warefu. |

## Zoezi

Mwanafunzi ahamishe wenzake kuhusu usafi wa mwili.

Tarehe: ____________________________ Muda: ___________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 121: Usafi wa mwili 3

Kipindi cha 121 na 122 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 121**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **ng'** **n**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  ng' o → **ng'o** ng' a → **ng'a** n o → **no** n a → **na**

- Soma silabi na maneno.

  Ti ng'a → **Ting'a** Mu ng'a ro → **Mung'aro**

- **Sarufi: *Jaza mapengo ukitumia 'huyu', 'hawa'***

1. Mwanafunzi __________ anapanda basi.
2. Walimu __________ ni wa shule yetu.
3. Wakulima _________ ni hodari.

**Kusoma hadithi**

**Mung'aro**



Mung'aro alihamia shule ya Ting'a. Babu yake alimnunulia viatu na sare mpya ya shule. Nyanya yake alihakikisha kuwa anaoga na kuvaa nguo safi kila siku. Alimsaidia kupiga viatu rangi, kuchana nywele, kukata kucha na kufuta kamasi. Mung'aro aling'ang'ana kubaki safi mchana kutwa. Mwishoni mwa mwaka huo, Mung'aro alipata tuzo la kijana safi.

121 Hakiuzwi

Kipindi cha 121 na 122 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 122**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **NG'** **ng'** **N** **n**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  a li m nunulia → **alimnunulia** a li hakikisha → **alihakikisha**

  a li m saidia → **alimsaidia** a li ng'ang'ana → **aling'ang'ana**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Nguo zetu**



Mali ya Serikali ya Kenya 122

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** ng'
**U:** Endelea na herufi ng', N, n.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 121**.

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:** /ng'/ /o/ silabi ni ng'o
**U:** Endelea na ng'a, no
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa 121.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.
**N/T/U:** ng'a ng'ana - ng'ang'ana
**U:** Endelea na neno ting'a
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 121**.

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **anaoga**, **alikata kucha, kufuta kamasi.**

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Mung'aro alihamia wapi? *(Shule ya Ting'a)*

**T:** Babu alimununulia Mung'aro nini? *(Viatu na sare ya shule)*

**U:** Unafikiria ni kwa nini nyanya yake Mung'aro alihakikisha anaoga? *(Hakiki majibu ya wanafunzi)*

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**
**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa 121.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi tano akitumia **huyu.**

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 121 na 122 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 121**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **ng'** **n**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  ng' o — **ng'o** ng' a — **ng'a** n o — **no** n a — **na**

- Soma silabi na maneno.

  Ti ng'a — **Ting'a** Mu ng'a ro — **Mung'aro**

- **Sarufi: Jaza mapengo ukitumia 'huyu', 'hawa'**

1. Mwanafunzi __________ anapanda basi.
2. Walimu __________ ni wa shule yetu.
3. Wakulima _________ ni hodari.

**Kusoma hadithi**

**Mung'aro**



Mung'aro alihamia shule ya Ting'a. Babu yake alimnunulia viatu na sare mpya ya shule. Nyanya yake alihakikisha kuwa anaoga na kuvaa nguo safi kila siku. Alimsaidia kupiga viatu rangi, kuchana nywele, kukata kucha na kufuta kamasi. Mung'aro aling'ang'ana kubaki safi mchana kutwa. Mwishoni mwa mwaka huo, Mung'aro alipata tuzo la kijana safi.

121

Kipindi cha 121 na 122 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 122**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **NG'** **ng'** **N** **n**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  a li m nunulia — **alimnunulia** a li hakikisha — **alihakikisha**

  a li m saidia — **alimsaidia** a li ng'ang'ana — **aling'ang'ana**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Nguo zetu**



Mali ya Serikali ya Kenya 122

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** NG'
**U:** Endelea na herufi ng', N, n.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 122.**

## Kusoma maneno marefu

Soma sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.
**N/T/U:** a li m nunulia - alimnunulia
**U:** Endelea na maneno alihakikisha, alimsaidia
Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 122.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 121.**

## Hadithi ya mwalimu

**Nguo zetu**

Nguo hutumiwa na watu kwa kuvaa. Nguo hutusaidia kuficha uchi wetu. Pia hutusaidia wakati wa baridi na jua kali. Kuna nguo za wasichana na wavulana. Wasichana huvaa rinda. Wavulana nao huvaa shati, fulana pamoja na kaptura. Kofia nayo huvaliwa kichwani. Siku hizi wasichana wanapenda kuvaa suruali ndefu. Wakati wa baridi watu huvaa sweta kuepuka kushikwa na mafua. Wakati huu ni vizuri kuwa na hanchifu. Hanchifu ni kitambaa cha kufuta kamasi wakati wa baridi. Usiitumie nguo yako kufutia kamasi. Nguo zikivaliwa huwa chafu na haziwezi kuvaliwa tena. Nguo chafu zikivaliwa huweza kuleta magonjwa. Ni vizuri kuosha nguo chafu kuepuka magonjwa.

Funza maana ya maneno haya: **rinda, shati, kofia.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Kwa nini watu huvaa nguo? *(Kuficha uchi)*
**T:** Hanchifu hutumiwa kufanya nini? *(Kufuta kamasi)*
**U:** Wewe unapenda kuvaa nguo gani? *(Kubali jibu lolote sahihi.)*

## Zoezi

Wanafunzi wajaze mapengo wakitumia **huyu** au **hawa**.

1. ____________ ni baba yangu. (Huyu)
2. ____________ ni mababu zetu. (Hawa)
3. ____________ ni mwalimu wangu. (Huyu)
4. ____________ ni madaktari wetu. (Hawa)

## Kazi ya ziada

Nakili vifungu vifuatavyo kisha umsomee mlezi wako.

1. alikata kucha
2. kufuta kamasi
3. nywele ilinyolewa
4. wanakijiji

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 123: Usafi wa mwili 3

Kipindi cha 123 na 124 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 123**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**p** **o**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| p o | p a | n o | ng' o |
| **po** | **pa** | **no** | **ng'o** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| pa mbo | pi gwa | hu m pa |
| **pambo** | **pigwa** | **humpa** |

**Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Tumia **huyu** au **hawa** kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Ndama ____ ni wangu. | Ndama ____ ni wetu. |
| 2. Nyati ____ ni mweusi. | Nyati ____ ni weusi. |
| 3. Duma ____ ni mdogo. | Duma ____ ni wadogo. |

**Kusoma hadithi**

**Mwalimu Esipisu**



Esipisu ni mwalimu wa darasa la kwanza shuleni Pambo. Kila asubuhi yeye huwakagua wanafunzi wake kuhakikisha wako safi. Mwalimu Esipisu huangalia ikiwa nywele zao zimenyolewa, viatu vimepigwa rangi, na kucha zimekatwa. Yeye huwaelezea wanafunzi umuhimu wa kuwa safi.

123 Hakiuzwi

Kipindi cha 123 na 124 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 124**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**P** **O**

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu wa kagua | ku hakikisha |
| **huwakagua** | **kuhakikisha** |
| vi me pigwa | hu wa elezea |
| **vimepigwa** | **huwaelezea** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Usafi wa mikono yetu**



Mali ya Serikali ya Kenya 124

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** p

**U:** Endelea na herufi o.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 123.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /p/ /o/ silabi ni po

**U:** Endelea na silabi pa, no

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa 123.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** pa mbo - pambo

**U:** Endelea na neno pigwa

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 123.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **safi, vimepigwa rangi, zimenyolewa**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Mwalimu Esipisu alikuwa mwalimu wa darasa gani? *(Darasa la kwanza)*

**T:** Kila asubuhi Mwalimu Esipisu alifanya nini? *(Hukagua wanafunzi wake)*

**U:** Wewe hufanya nini kuweka kucha zako safi? *(Kubali jibu lolote sahihi)*

### Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 123.**

**Majibu**

1. huyu/hawa 2. huyu/hawa
3. huyu/hawa 4. huyu/hawa

### Kazi ya ziada

Nakili vifungu vifuatavyo kwenye daftari lako kisha utamsomea mlezi wako.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Paka huyu | Paka hawa |
| 2. Ng'ombe huyu | Ng'ombe hawa |
| 3. Nguruwe huyu | Nguruwe huyu |
| 4. Mbuzi huyu | Mbuzi hawa |

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 123 na 124 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 123**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **p** **o**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

  | p o | p a | n o | ng' o |
  |---|---|---|---|
  | **po** | **pa** | **no** | **ng'o** |

- Soma silabi na maneno.

  | pa mbo | pi gwa | hu m pa |
  |---|---|---|
  | **pambo** | **pigwa** | **humpa** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Tumia **huyu** au **hawa** kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo.

| | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| **1.** | Ndama ___ ni wangu. | Ndama ___ ni wetu. |
| **2.** | Nyati ___ ni mweusi. | Nyati ___ ni weusi. |
| **3.** | Duma ___ ni mdogo. | Duma ___ ni wadogo. |

**Kusoma hadithi**

**Mwalimu Esipisu**



Esipisu ni mwalimu wa darasa la kwanza shuleni Pambo. Kila asubuhi yeye huwakagua wanafunzi wake kuhakikisha wako safi. Mwalimu Esipisu huangalia ikiwa nywele zao zimenyolewa, viatu vimepigwa rangi, na kucha zimekatwa. Yeye huwaelezea wanafunzi umuhimu wa kuwa safi.

123

Kipindi cha 123 na 124 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 124**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

  **P** **O**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

  | hu wa kagua | ku hakikisha |
  |---|---|
  | **huwakagua** | **kuhakikisha** |
  | vi me pigwa | hu wa elezea |
  | **vimepigwa** | **huwaelezea** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Usafi wa mikono yetu**



Mali ya Serikali ya Kenya

124

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** P

**U:** Endelea na herufi O.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 124**.

### Kusoma maneno marefu

Soma sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo useme neno lote kwa upesi.

**N/T/U:** hu wa kagua - huwakagua

**U:** Endelea na kuhakikisha, vimepigwa

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 124**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 123**.

### Hadithi ya mwalimu

**Usafi wa mikono yetu.**

Kila binadamu ana mikono miwili. Mikono hutumika kufanya kazi mbalimbali kama kulima, kuosha vyombo, kufua nguo na kuandika. Ni vizuri kuweka mikono yetu safi. Hakikisha kucha ni fupi. Kucha ndefu hubeba uchafu. Kucha chafu huleta magonjwa. Baada ya kufanya kazi mikono huwa chafu na huchoka. Mikono pia huwa chafu mtu anapoenda msalani. Hivyo basi ni vyema kunawa mikono vizuri kwa maji na sabuni. Unapoiosha hakikisha unasugua vizuri katikati ya vidole ili kuondoa uchafu wote. Tulinde mikono yetu kila wakati.

Funza maana ya maneno haya: **uchafu, kucha**. Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Binadamu ana mikono mingapi? *(Miwili)*

**T:** Kucha ndefu zinafaa kufanyiwa nini? *(Kukatwa)*

**U:** Ni wakati gani mwingine unafaa kuiosha mikono yako? *(Kubali jibu lolote sahihi)*

### Zoezi

Andika vifungu hivi ubaoni kisha mwanafunzi anakili katika daftari lake kwa hati nadhifu.

1. Bata huyu
2. Dubu hawa
3. Kuku huyu
4. Watoto hawa

### Kazi ya ziada

Wanafunzi waandike sentensi **nne** wakitumia **hawa**.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 125: Usafi wa mwili 3

Kipindi cha 125 **Usafi wa mwili 3**

**Kipindi 125**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng'** **n** **p** **o**

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: nyo a - nyoa**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| po | nya | a | ni | pa |
| nyo | o | nyu | ng'o | ka |

**Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Soma sentensi zifuatazo katika vikundi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu** ni mzee. | **Hawa** ni wazee. |
| 2. **Huyu** ni mkulima. | **Hawa** ni wakulima. |
| 3. **Huyu** ni mvuvi. | **Hawa** ni wavuvi. |
| 4. **Huyu** ni mjomba wangu. | **Hawa** ni wajomba wetu. |
| 5. Mkulima **huyu** ni hodari. | Wakulima **hawa** ni hodari. |
| 6. Daktari **huyu** ni mpole. | Madaktari **hawa** ni wapole. |

**Zoezi: Kuandika**

Jaza mapengo kwa jibu sahihi. (nawa mikono, futa kamasi, kata kucha)

1. Mtoto ali_______ kwenye pua yake.
2. Baada ya kutoka msalani ali_______.
3. Mwanafunzi ali_______ zake ndefu za vidole.

125 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ng'

**U:** Endelea na herufi n, p, o.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 125**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi zote pamoja na mwanafunzi. Tumia silabi 'nyo' na 'a' kuandika neno 'nyoa'. Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mpe mwanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 125.**

## Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

Wanafunzi wasomeane sentensi kwenye **ukurasa wa 125**.

## Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **kuosha, kunawa**

Hakikisha wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya zoezi.

## Kuandika

**T:** Rejelea njia mbalimbali za kudumisha usafi wa mwili pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 125** kwenye daftari lake.

**Majibu**

1. futa kamasi
2. nawa mikono
3. kata kucha

## Kazi ya ziada

**T:** Rejelea mambo muhimu kuhusu usafi wa mwili.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 125.**

## Kazi ya nyongeza

Wanafunzi wajadiliane kuhusu utuzaji wa mwili uongoni mwa wenzake kulinda usiri wa mwili wakiwa katika vikundi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 126: Vyakula vya kiasili 2

Kipindi cha 126 na 127 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 126**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh** **th**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| sh a | sh e | th a | th e |
|---|---|---|---|
| **sha** | **she** | **tha** | **the** |

● Soma silabi na maneno.

| sha mba ni | sha ha da | tha ma ni | the lu ji |
|---|---|---|---|
| **shambani** | **shahada** | **thamani** | **theluji** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi hizi.

1. Chakula **changu** kimeiva.
2. Tunda **langu** limeoza.
3. Mboga **zetu** zimepaliliwa.

**Kusoma hadithi**

**Shamba la Babu**



Babu yangu ni mkulima hodari. Ana shamba la thamani kubwa. Mle shambani amepanda mihogo, viazi, mahindi na maharagwe. Pia ana maembe, machungwa, mapapai na mapera.
Amepanda pia kunde, mchicha na pamba. Pamba shambani huonekana nyeupe kama theluji. Wazazi wetu hutupeleka kumtembelea. Sisi hufurahia kula mboga na matunda na humshukuru kwa bidii yake.

Mali ya Serikali ya Kenya 126

Kipindi cha 126 na 127 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 127**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH sh** **TH th**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu tu peleka | ku m tembelea |
|---|---|
| **hutupeleka** | **kumtembelea** |
| hu furahia | ku m shukuru |
| **hufurahia** | **kumshukuru** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mjomba Noti**



127 Hakiluzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** sh
**U:** Endelea na herufi th.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 126.**

## ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.
**N/T/U:** /sh/ /a/ silabi ni sha
**U:** Endelea na silabi she, tha
Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 126.**

## ★ Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.
**N/T/U:** sha mba ni - shambani
**U:** Endelea na maneno shahada, theluji
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 126.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **maharagwe, mapaipai, kunde**

## Kabla ya kusoma

Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## ? Maswali

**N:** Ni nani mkulima hodari? *(Babu)*

**T:** Taja aina ya vyakula ambavyo vimepandwa shambani? *(Mihogo, viazi, mahindi na maharagwe)*

**U:** Umewahi kuona mimea gani? *(Kubali jibu sahihi)*

## ◆ Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Kiazi **changu** - Viazi **vyetu.**

## Zoezi

Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 126.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno yafuatayo.

1. Matunda
2. Machungwa
3. Viazi
4. Mboga
5. Shamba

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 127: Vyakula vya kiasili 2

Kipindi cha 126 na 127 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 126**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**sh** **th**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| sh a | sh e | th a | th e |
|---|---|---|---|
| **sha** | **she** | **tha** | **the** |

● Soma silabi na maneno.

| sha mba ni | sha ha da | tha ma ni | the lu ji |
|---|---|---|---|
| **shambani** | **shahada** | **thamani** | **theluji** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi hizi.

1. Chakula **changu** kimeiva.
2. Tunda **langu** limeoza.
3. Mboga **zetu** zimepaliliwa.

**Kusoma hadithi**

**Shamba la Babu**



Babu yangu ni mkulima hodari. Ana shamba la thamani kubwa. Mle shambani amepanda mihogo, viazi, mahindi na maharagwe. Pia ana maembe, machungwa, mapapai na mapera. Amepanda pia kunde, mchicha na pamba. Pamba shambani huonekana nyeupe kama theluji. Wazazi wetu hutupeleka kumtembelea. Sisi hufurahia kula mboga na matunda na humshukuru kwa bidii yake.

Mali ya Serikali ya Kenya

126

Kipindi cha 126 na 127 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 127**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**SH sh** **TH th**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu tu peleka | ku m tembelea |
|---|---|
| **hutupeleka** | **kumtembelea** |
| hu furahia | ku m shukuru |
| **hufurahia** | **kumshukuru** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Mjomba Noti**



127

Hakiuzwi

## ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** SH
**U:** Endelea na herufi sh, TH, th.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 127**.

## Kusoma maneno marefu

Soma sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo zote usome neno kwa upesi.
**N/T/U:** hu tu pelekea - hutupelekea
**U:** Endelea na maneno kumtembelea, hufurahia
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 127.**

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 126**.

## Hadithi ya mwalimu

**Mjomba Noti**

Mimi na dadangu Mueni tulikuwa tukicheza nyuma ya nyumba yetu. Mara tukasikia honi ya gari. Pii! Pii! Tulitoka mbio kwenda kufungua lango kuu. Lo! Mjomba Noti alikuwa ametutembelea. Tulimkaribisha kwa furaha. Mjomba aliandaliwa chai kwa mkate. Alipomaliza kuinywa, alituambia twende kwenye gari lake kuchukua zawadi alizotuletea.
Tulibeba gunia ambalo lilikuwa zito kwelikweli. Mama alimshukuru mjomba. "Kieti! Njoo uone alicholeta mjomba," mama aliniita. Mjomba alikuwa ametuletea mihogo, viazi vitamu, mahindi, maharagwe na matunda. Pia alikuwa ameleta unga wa wimbi. Tuliketi na mjomba wetu akitueleza umuhimu wa vyakula vyetu vya kiasili. Alisema vyakula hivi vinafanya tuwe na afya nzuri.

Funza maana ya maneno haya: **mihogo, viazi vitamu, mahindi.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## ? Maswali

**N:** Watoto walikuwa wakifanya nini waliposikia honi? *(Wakicheza nyuma ya nyumba)*
**T:** Taja vyakula alivyoleta mjomba. *(Mihogo, viazi vitamu, mahindi, maharagwe na matunda)*
**U:** Unafikiri ni kwa nini mjomba alileta vyakula vya kiasili? *(Kubali jibu lolote sahihi.)*

## Zoezi

Mweleze mwanafunzi aandike maneno yafuatayo katika kitabu chake.

| | | |
|---|---|---|
| 1. Maharagwe | 2. Mapaipai | 3. Kunde |
| 4. Matunda | 5. Vyakula | |

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi anakili majina ya matunda **embe, ndizi, chungwa, paipai** kisha achore picha za matunda hayo.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 128: Vyakula vya kiasili 2

Kipindi cha 128 na 129 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 128**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**r** **s**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| s o | s i | r a | r i |
|---|---|---|---|
| **so** | **si** | **ra** | **ri** |

- Soma silabi na maneno.

| so ko | ki a si li | ra fi ki | vi zu ri |
|---|---|---|---|
| **soko** | **kiasili** | **rafiki** | **vizuri** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Jaza mapengo kwa kuchagua jibu sahihi.

1. Tunda _____ ni tamu. (langu, yetu)
2. Viti _____ vimevunjika. (chetu, vyetu)
3. Mwalimu _____ amefika. (wangu, yetu)

**Kusoma hadithi**

**Siku ya soko Sori**



Jumatano ni siku ya soko kule Sori. Mama yangu huuza vyakula vya kiasili vifuatavyo: maharagwe, mahindi na njugu. Rafiki yake Sara humuuzia mihogo na viazi. Baba yangu naye huuza mboga na matunda. Yeye pia huuza ndizi, maembe, machungwa na tufaha. Kaka yangu huwasaidia kuuza. Vyakula wanavyouza vina madini muhimu kwa mwili.



Kipindi cha 128 na 129 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 129**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**R** **S**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu mu uzia | hu wa saidia |
|---|---|
| **humuuzia** | **huwasaidia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vyakula vyetu**





### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** r

**U:** Endelea na herufi s.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 128.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /s/ /o/ silabi ni so

**U:** Endelea na silabi si, ra

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 128.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** so ko - soko

**U:** Endelea na maneno kiasili, rafiki

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 128.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **mihogo, tufaha na njugu.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Soko la Sori huwa siku gani? *(Jumatano)*

**T:** Baba huuza nini? *(Mboga na matunda)*

**U:** Nini huuzwa katika Soko lililo karibu na shule yenu? *(Kubali jibu lolote sahihi.)*

### Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Chakula **changu** - Vyakula **vyetu.**

### Zoezi

Mwanafunzi ajaze mapengo kwa kuchagua jibu sahihi kwenye **ukurasa wa 128.**

**Majibu**

1. langu
2. vyetu
3. wangu

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike majina ya vyakula anavyovijua.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 129: Vyakula vya kiasili 2

Kipindi cha 128 na 129 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 128**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**r** **s**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| s o | s i | r a | r i |
|---|---|---|---|
| **so** | **si** | **ra** | **ri** |

● Soma silabi na maneno.

| so ko | ki a si li | ra fi ki | vi zu ri |
|---|---|---|---|
| **soko** | **kiasili** | **rafiki** | **vizuri** |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Jaza mapengo kwa kuchagua jibu sahihi.

1. Tunda _____ ni tamu. (langu, yetu)
2. Viti _____ vimevunjika. (chetu, vyetu)
3. Mwalimu _____ amefika. (wangu, yetu)

**Kusoma hadithi**

**Siku ya soko Sori**



Jumatano ni siku ya soko kule Sori. Mama yangu huuza vyakula vya kiasili vifuatavyo: maharagwe, mahindi na njugu. Rafiki yake Sara humuuzia mihogo na viazi. Baba yangu naye huuza mboga na matunda. Yeye pia huuza ndizi, maembe, machungwa na tufaha. Kaka yangu huwasaidia kuuza. Vyakula wanavyouza vina madini muhimu kwa mwili.

Mali ya Serikali ya Kenya

128

Kipindi cha 128 na 129 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 129**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**R** **S**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu mu uzia | hu wa saidia |
|---|---|
| **humuuzia** | **huwasaidia** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vyakula vyetu**



129

Hakiuzwi

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** R

**U:** Endelea na herufi S.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 129**.

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** hu mu uzia - humuuzia

**U:** Endelea na maneno husaidia, huwasaidia

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 129**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 128**.

### Hadithi ya mwalimu

**Vyakula vyetu**

Jina langu ni Wekesa. Rafiki yangu ni Chelimo. Wazazi wetu ni wazuri. Wao hutupa vyakula vingi. Baba husema, "Kuleni vyakula mbalimbali ili afya yenu iwe nzuri." Asubuhi tunapoamka, sisi hula mihogo au viazi vitamu kwa chai. Sisi hufurahia kula mapera, machungwa, ndizi na maembe. Wakati wa mchana tukiwa shuleni, wapishi wetu hutupatia pure. Sichale ni mwanafunzi darasani mwetu. Yeye hali vyakula hivi. Kila mara yeye huwa mgonjwa. Alipopelekwa hospitalini daktari alimwambia ale vyakula kama vile kunde na mchicha. Sichale alipofuata maagizo ya daktari aliimarika.

Funza maana ya maneno haya: **pure, kunde, mchicha.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Rafiki yake Wekesa aliitwa nani? *(Chelimo)*

**T:** Ni vyakula vipi vilivyotajwa? *(Mihogo, viazi vitamu)*

**U:** Kwa nini ni muhimu kula vyakula vilivyotajwa? *(Kubali jibu sahihi.)*

### Zoezi

Mweleze mwanafunzi aandike sentensi tatu akitumia –**angu** na –**etu.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi anakili sentensi zifuatazo kisha amsomee mlezi/mzazi nyumbani.

1. Maziwa yangu yamechemka.
2. Wali wangu umeiva.
3. Njugu zetu ni tamu.
4. Mboga zetu zimekauka.
5. Mhogo wangu umeisha.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 130: Vyakula vya kiasili 2

**Kipindi cha 130 — Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 130**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**r** **s** **sh** **th**

Jedwali la silabi

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ndi zi – ndizi**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ndi | vi | a | wi | ma |
| i | mbi | hi | zi | pa |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Jaza mapengo kwa usahihi kwa kutumia **-angu** na **-etu**.

1. Ndizi _______ zimeharibika. (zetu, langu)
2. Mihogo _______ imepikwa. (letu, yetu)
3. Embe ______ limeiva. (langu, zangu)
4. Muwa _____ni mtamu. (zetu, wangu)
5. Viazi _______ ni vikubwa. (chetu, vyetu)
6. Hindi _______ limeiva. (langu, zetu)
7. Maharagwe _____ yamepikwa. (yetu, wetu)
8. Matunda ______ yanaliwa. (yetu, zetu)

**Zoezi: Kuandika**

Chora maumbo ya vyakula hivi.

1. mayai
2. muhogo
3. ndizi

Mali ya Serikali ya Kenya

130

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** r

**U:** Endelea na herufi s, sh, th.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 130**.

## Jedwali la Silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'ndi' na 'zi' kuandika neno ndizi. Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mpe mwanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 130.**

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Muhogo **wangu** - Mihogo **yetu.**

Mwanafunzi ajaze mapengo kwa usahihi kwa kutumia **-angu** na **-etu** kwenye **ukurasa wa 130.**

## Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **vyakula, mkate**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya zoezi.

## Kuandika

**T:** Rejelea mambo muhimu kuhusu vyakula vya kiasili.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 130.**

**Majibu**

1. langu
2. yetu
3. langu

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ahamasishe wengine katika jamii kuhusu umuhimu wa vyakula vya kiasilia.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 131 na 132 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 131**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**v** **u** **w**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

v a → **va**  v e → **ve**  v i → **vi**  v u → **vu**

● Soma silabi na maneno.

vi a zi → **viazi**  wi mbi → **wimbi**  wa za zi → **wazazi**  m ta ma → **mtama**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Tunga sentensi sahihi ukitumia **-angu** na **-etu** pamoja na maneno haya.

**1.** Chakula **2.** Tunda **3.** Mboga

**Kusoma hadithi**

**Lishe bora**



Madaktari huwashauri watu kuzingatia lishe bora. Kuna vyakula mbalimbali vinavyochangia lishe bora. Baadhi ya vyakula hivi ni mboga za kienyeji, wimbi na mtama. Vingine vinavyochangia ni mahindi na maharagwe. Mimi na kaka yangu hufurahia kula kunde, viazi na mbaazi. Wazazi wetu hutuhimiza kuvitumia vyakula hivi. Wao husema vyakula hivi hutukinga dhidi ya magonjwa mbalimbali.

131 Hakiuzwi

Kipindi cha 131 na 132 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 132**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**V v** **U u** **W w**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

hu wa shauri → **huwashauri**  vi na vyo changia → **vinavyochangia**

hu furahia → **hufurahia**  hu tu himiza → **hutuhimiza**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kiro apona**



Mali ya Serikali ya Kenya 132

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** V

**U:** Endelea na herufi u na w.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 131**.

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /v/ /a/ silabi ni va

**U:** Endelea na ve, vi, vu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 131.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.

**N/T/U:** vi a zi - viazi

**U:** Endelea na maneno wimbi, wazazi

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 131**.

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **kunde, wimbi, mtama.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Je, madaktari huwashauri watu kufanya nini? *(Kuzingatia lishe bora)*

**T:** Ni vyakula gani vya kienyeji vilivyotajwa kwenye hadithi? *(Mboga za kienyeji, wimbi na mtama)*

**U:**Taja aina mbili za mboga za kienyeji. *(Kubali jibu lolote sahihi.)*

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Tunda **langu** - Matunda **yetu**.

## Zoezi

Mwelekeze mwanafunzi kufanya zoezi kwenye **ukurasa wa 131.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike majina ya matunda mbalimbali anayoyajua.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 132: Vyakula vya kiasili 2

Kipindi cha 131 na 132 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 131**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**v** **u** **w**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| v a | v e | v i | v u |
|---|---|---|---|
| **va** | **ve** | **vi** | **vu** |

- Soma silabi na maneno.

| vi a zi | wi mbi | wa za zi | m ta ma |
|---|---|---|---|
| **viazi** | **wimbi** | **wazazi** | **mtama** |

- **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Tunga sentensi sahihi ukitumia **-angu** na **-etu** pamoja na maneno haya.

**1.** Chakula **2.** Tunda **3.** Mboga

**Kusoma hadithi**

**Lishe bora**



Madaktari huwashauri watu kuzingatia lishe bora. Kuna vyakula mbalimbali vinavyochangia lishe bora. Baadhi ya vyakula hivi ni mboga za kienyeji, wimbi na mtama. Vingine vinavyochangia ni mahindi na maharagwe. Mimi na kaka yangu hufurahia kula kunde, viazi na mbaazi. Wazazi wetu hutuhimiza kuvitumia vyakula hivi. Wao husema vyakula hivi hutukinga dhidi ya magonjwa mbalimbali.

131 Hakiuzwi

Kipindi cha 131 na 132 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 132**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**V v** **U u** **W w**

- Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu wa shauri | vi na vyo changia |
|---|---|
| **huwashauri** | **vinavyochangia** |
| hu furahia | hu tu himiza |
| **hufurahia** | **hutuhimiza** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Kiro apona**



Mali ya Serikali ya Kenya 132

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** V
**U:** Endelea na herufi v, U, u, W, w.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 132.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.
**N/T/U:** hu wa shauri - huwashauri
**U:** Endelea na vinavyochangia, hufurahia
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 132.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 131.**

### Hadithi ya mwalimu

**Kiro apona**

Kiro alikuwa msichana wa miaka saba. Nyumba yao ilikuwa karibu na barabara kuu. Alibaki nyumbani huku wenzake wakienda shuleni. Alikuwa mnyonge. Mwili wake haukuwa na afya nzuri. Nywele zake zilikuwa zimebadili rangi. Wazazi wake hawakujua tatizo alilokuwa nalo. Walisikitika.
Daktari Bora aliwatembelea. Akawashauri wampeleke hospitalini. Kiro alipelekwa hospitali ya Bora afya. Baada ya kupimwa, mama yake alishauriwa ampe Kiro vyakula kama mboga, matunda, maharagwe na samaki. Alielezwa ugonjwa ulitokana na ukosefu wa lishe bora. Mama Kiro alimshukuru daktari. Alifuata ushauri wake. Mwishowe aliweza kuenda shuleni na kusoma kwa bidii. Afya ya Kiro ikaanza kuwa nzuri.

Funza maneno haya: **mboga, matunda, samaki.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Kwa nini Kiro hakuwa anaenda shuleni? *(Alikuwa mnyonge na mwili wake haukuwa na afya)*
**T:** Daktari Bora alimshauri mamaye Kiro ampe vyakula gani? *(Vyakula kama mboga, matunda, maharagwe na samaki)*
**U:** Kwa nini Kiro alifurahi? *(Alianza kwenda shuleni, afya yake iliimarika)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike sentensi tano akitumia **yangu** au **yetu.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi tano akitumia **yangu** au **yetu.**

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 133: Vyakula vya kiasili 2

Kipindi cha 133 na 134 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 133**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**w** **y** **u**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

w e → **we**   w o → **wo**   w u → **wu**

● Soma silabi na maneno.

wa za zi → **wazazi**   wi mbi → **wimbi**   ki to we o → **kitoweo**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-etu'**

Soma vifungu hivi.

1. Kiti **chetu** 2. Vyombo **vyetu** 3. Vitumbua **vyetu**

**Kusoma hadithi**

**Vyakula vitamu**



Mama yangu ni mpishi hodari. Kila asubuhi yeye hututayarishia kiamshakinywa. Yaya wetu Sudi humsaidia kuandaa meza.

Barua ni ndugu yangu mdogo. Yeye hupenda maziwa, mihogo na mayai. Mimi ninapenda maziwa na viazi vitamu. Ninapenda pia zambarau na mapera. Mama na baba yetu hupenda kitoweo cha sungura. Sisi wote humshukuru mama kwa upishi bora.

133 Hakiuzwi

Kipindi cha 133 na 134 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 134**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**R** **S**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.


hu tu tayarishia → **hututayarishia**   ku andaa → **kuandaa**

hu m saidia → **humsaidia**   hu m shukuru → **humshukuru**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vyakula ni afya**



Mali ya Serikali ya Kenya 134

### ■ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** w

**U:** Endelea na herufi y na u.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 133.**

### ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /w/ /e/ we

**U:** Endelea na wo, wu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 133.**

### ★ Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja ili kulisoma neno.

**N/T/U:** wa za zi - wazazi

**U:** Endelea na wimbi, kitoweo

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 133.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **mihogo, viazi vitamu, mapera**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Kila asubuhi mama hufanya nini? *(Hututayarishia kiamsha kinywa)*

**T:** Barua anapenda nini? *(Mihogo, mayai na maziwa)*

**U:** Maziwa yana umuhimu gani mwilini? *(Husaidia kwa ujenzi wa mwili)*

### ◆ Sarufi

**Matumizi ya –angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Maharagwe **yangu** - Maharagwe **yetu.**


### Zoezi

Mwanafunzi asome vifungu kwenye **ukurasa wa 133.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi nne akitumia **yangu.**

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Kipindi cha 133 na 134 Vyakula vya kiasili 2

Kipindi 133

Taja jina la herufi na utamke sauti.

w y u

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

w e — **we** w o — **wo** w u — **wu**

Soma silabi na maneno.

wa za zi — **wazazi** wi mbi — **wimbi** ki to we o — **kitoweo**

**Sarufi: Matumizi ya '-etu'**

Soma vifungu hivi.

1. Kiti **chetu** 2. Vyombo **vyetu** 3. Vitumbua **vyetu**

**Kusoma hadithi**

**Vyakula vitamu**

Mama yangu ni mpishi hodari. Kila asubuhi yeye hututayarishia kiamshakinywa. Yaya wetu Sudi humsaidia kuandaa meza.

Barua ni ndugu yangu mdogo. Yeye hupenda maziwa, mihogo na mayai. Mimi ninapenda maziwa na viazi vitamu. Ninapenda pia zambarau na mapera. Mama na baba yetu hupenda kitoweo cha sungura. Sisi wote humshukuru mama kwa upishi bora.

133 Hakiuzwi


Kipindi cha 133 na 134 Vyakula vya kiasili 2

Kipindi 134

Taja jina la herufi na utamke sauti.

R S

Soma sehemu za neno na neno lote.

hu tu tayarishia — **hututayarishia** ku andaa — **kuandaa**

hu m saidia — **humsaidia** hu m shukuru — **humshukuru**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vyakula ni afya**

Mali ya Serikali ya Kenya 134

### ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** R
**U:** Endelea na herufi S.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 134**.

### Kusoma maneno marefu

Soma sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.
**N/T:** hu tu tayarishia - hututayarishia
**U:** Endelea na maneno kuandaa, humsaidia.
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 134**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 133**.

### Hadithi ya mwalimu

**Vyakula ni afya**

Mwalimu wetu Bwana Wema aliingia darasani. Baada ya kutusalimia alisema, "Leo tutajifunza kuhusu vyakula na afya." Akatuambia kuwa afya ni hali ya mwili kuwa bila magonjwa. Alisema kuwa vyakula, huzuia magonjwa. Miili yetu huwa na nguvu tukila vyakula kama vile mihogo, viazi vitamu na mahindi.
Mwalimu pia alisema kuwa hatutayapata magonjwa ya kufura tumbo na mwili kukosa nguvu tukila maharagwe na njugu. "Matunda na mboga yatatukinga dhidi ya magonjwa."
Niliporudi nyumbani kwetu, nilimweleza mama yangu alivyotufunza mwalimu. Baadaye, tukala na kufurahia chakula chetu.

Funza maana ya maneno haya: **njugu, viazi vitamu, maharagwe.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### ? Maswali

**N:** Mwalimu Wema aliwafunza wanafunzi kuhusu nini? *(Vyakula na afya)*
**T:** Taja vyakula ambavyo huleta nguvu mwilini? *(Mihogo, viazi vitamu na mahindi)*
**U:** Je, wewe unapenda vyakula gani? *(Kubali jibu sahihi)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike vifungu vifuatavyo kwa wingi.

| | Umoja | Wingi | |
|---|---|---|---|
| 1. | Kitabu changu | ______________ | (Vitabu vyetu) |
| 2. | Embe langu | ______________ | (Maembe yetu) |
| 3. | Kalamu yangu | ______________ | (Kalamu zetu) |

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi akamilishe vifungu vifuatavyo akitumia **-angu**.

1. vikapu 2. kikombe 3. ng'ombe
4. meza 5. vifyekeo

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 135: Vyakula vya kiasili 2

Kipindi cha 135 **Vyakula vya kiasili 2**

**Kipindi 135**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Ww** **Yy** **Vv**

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: vi a zi - viazi**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| vi | mu | ya | ta | zi | wa |
| ga | ma | a | mbo | i | wi |

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-etu'**

Kamilisha vifungu hivi ukitumia **-etu**.

**Kwa mfano: Mwalimu wetu**

1. Maembe ______ etu
2. Vyakula ______ etu
3. Mtoto ______ etu
4. Miwa _____etu.
5. Viazi _______ etu.
6. Mahindi _______ etu.
7. Maharagwe _____ etu.
8. Matunda ______ etu.

**Zoezi: Kuandika**

Tunga sentensi tatu ukitumia **-angu** na **-etu**.

135 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** w

**U:** Endelea na herufi w, V, v, w, y, Y

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 135**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi zote. Tumia silabi 'vi', 'a' na 'zi' kuandika neno 'viazi'. Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno halisi kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 135**.

## Sarufi

Mwanafunzi akamilishe vifungu kwenye **ukurasa wa 135** akitutumia **-etu**.

**Majibu**

1. yetu 2. vyetu 3. wetu

## Kuandika maneno

**N/T/U**: Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **paipai**, **kunde**. Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya zoezi.

## Kuandika

**T: -angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani.

**U:** Tunga sentensi nne ukitumia **-angu** na **-etu**.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi achore paipai, embe na mapera na kupaka michoro hiyo rangi.

## Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi aeleze jinsi ya kutayarisha vyakula vya kiasili kabla ya kuvila.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha | 136 na 137 | **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 136**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**dh** **d** **j** **l**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| dh a | d e | j i | l o |
|---|---|---|---|
| **dha** | **de** | **ji** | **lo** |

● Soma silabi na maneno.

| m che zo | hu wa fu nza | ku ru ka | na dhi fu |
|---|---|---|---|
| **mchezo** | **huwafunza** | **kuruka** | **nadhifu** |

♦ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma vifungu vifuatavyo.

| | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| 1. | Darasa **langu** | Madarasa **yetu** |
| 2. | Kamba **yangu** | Kamba **zetu** |
| 3. | Kiranja **wangu** | Viranja **wetu** |

**Kusoma hadithi**



**Karimi**

Karimi ni msichana nadhifu. Yeye husoma katika gredi ya kwanza shuleni Leleji. Mwalimu wake wa darasa ni Bi. Khadija. Bi. Khadija huwafunza wanafunzi wake vizuri. Kiranja wa darasa la Karimi ni mvulana. Jina lake ni Adhoch. Karimi anapenda mchezo wa kikapu. Rafiki yake Adhiambo pia hupenda mchezo huo.

Mali ya Serikali ya Kenya 136

Kipindi cha | 136 na 137 | **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 137**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**DH dh** **M m** **K k**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu penda | hu wa funza |
|---|---|
| **hupenda** | **huwafunza** |
| hu soma | a na penda |
| **husoma** | **anapenda** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Lelei Matano**



137 Hakiuzwi

## ■ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** dh

**U:** Endelea na herufi dh, M, m, K, k.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 136.**

## ● Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T:** /dh/ /e/ dhe

**U:** Endelea na silabi de, ji

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 136.**

## ★ Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T:** m che zo - mchezo

**U:** Endelea na maneno huwafunza, nadhifu

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 136.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **mvulana, gredi.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## ? Maswali

**N:** Karimi alikuwa mwanafunzi wa shule ipi? *(Shuleni Leleji)*

**T:** Amina alipenda kucheza mchezo upi? *(Mchezo wa kuruka kamba)*

**U:** Je, wewe hupenda kucheza mchezo upi? *(Mpira wa miguu, wanafunzi wataje michezo mbalimbali wanayoipenda.)*

## ♦ Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Mwalimu **wangu** - Walimu **yetu.**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 136.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi anakili sentensi hizi kisha umsomee **mzazi/mlezi** nyumbani.

1. Msichana wangu ni mrefu.
2. Darasa letu ni kubwa.
3. Mwalimu wetu ni mrefu.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

Kipindi cha 136 na 137 **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 136**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**dh** **d** **j** **l**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| dh a | d e | j i | l o |
|---|---|---|---|
| **dha** | **de** | **ji** | **lo** |

Soma silabi na maneno.

| m che zo | hu wa fu nza | ku ru ka | na dhi fu |
|---|---|---|---|
| **mchezo** | **huwafunza** | **kuruka** | **nadhifu** |

**Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma vifungu vifuatavyo.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Darasa **langu** | Madarasa **yetu** |
| 2. | Kamba **yangu** | Kamba **zetu** |
| 3. | Kiranja **wangu** | Viranja **wetu** |

**Kusoma hadithi**

**Karimi**



Karimi ni msichana nadhifu. Yeye husoma katika gredi ya kwanza shuleni Leleji. Mwalimu wake wa darasa ni Bi. Khadija. Bi. Khadija huwafunza wanafunzi wake vizuri. Kiranja wa darasa la Karimi ni mvulana. Jina lake ni Adhoch. Karimi anapenda mchezo wa kikapu. Rafiki yake Adhiambo pia hupenda mchezo huo.

Mali ya Serikali ya Kenya 136

Kipindi cha 136 na 137 **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 137**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**DH dh** **M m** **K k**

Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu penda | hu wa funza |
|---|---|
| **hupenda** | **huwafunza** |
| hu soma | a na penda |
| **husoma** | **anapenda** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Lelei Matano**



137 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** DH

**U:** Endelea na herufi dh, M, m, K, k.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 137**.

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U: hu penda - hupenda**

**U:** Endelea na husoma, huwafunza.

Wanafunzi wasomeane **maneno waliyojifunza vitabuni** mwao kwenye **ukurasa wa 137**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 136**.

### Hadithi ya mwalimu

**Lelei Matano**

Mimi ni Lelei Matano. Mimi ni msichana. Nilizaliwa miaka sita iliyopita kijijini Kinga. Mimi ndiye kitinda mimba katika familia yetu. Nina kaka mmoja na dada wawili. Wazazi wangu ni Bwana na Bi. Wanjala Simeo. Rafiki yangu naye anaitwa Salma Njeri. Mimi husomea shule ya msingi ya Maji Mazuri. Niko katika gredi ya kwanza. Mwalimu wangu wa darasa anaitwa Bwana Keplimo Yegon. Bwana Yegon ni mwalimu mzuri. Nakumbuka muhula uliopita sikuweza kufanya hesabu za kuongeza. Mwalimu Yegon aliniita na kunitia moyo. "Lelei usife moyo. Fanya mazoezi ya hesabu ya kuongeza kila siku na unapopata tatizo njoo nitakusaidia." Nikayafuata mashauri ya mwalimu. Sasa hivi mimi ni mwanafunzi bora darasani mwetu katika hesabu.

Darasani mimi husoma kwa bidii ili nifaulu maishani. Mimi husaidiana na wanafunzi wenzangu kuhakikisha tunamaliza kazi ya mwalimu. Tukiwa shuleni mimi na Salma hucheza pamoja na wanafunzi wengine. Tufikapo nyumbani sisi huwasaidia wazazi wetu kufanya kazi za nyumbani kama vile kwenda mtoni na kuosha vyombo. Ninasoma kwa bidii niwe mkulima hodari nchini mwetu.

Funza maana ya maneno haya: **kaka, gredi, dada.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Lelei alizaliwa lini? *(Miaka sita iliyopita)*

**T:** Lelei ana dada wangapi? *(Wawili)*

**U:** Je, unaishi na nani nyumbani? *(Baba, mama, dada, babu)*

### Zoezi

Mwelekeze mwanafunzi kuandika sentensi akitumia –**angu na –etu.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike wingi wa vifungu hivi.

1. Mvulana wangu ________________ (Wavulana wetu)
2. Kiranja wangu ________________ (Viranja wetu)
3. Mtoto wangu ________________ (Watoto wetu)

Tarehe: ____________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

# Kipindi cha 138: Mimi na wenzangu 3

Kipindi cha 138 na 139 **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 138**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Gh** **b** **ch** **k**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

gh e → **ghe** ch i → **chi** k a → **ka** b o → **bo**

● Soma silabi na maneno.

gho ro fa → **ghorofa** wa li li ma → **walilima** gha la → **ghala** wa li cho ta → **walichota**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mavuno **yangu** ni mengi. | 1. Mavuno **yetu** ni mengi. |
| 2. Kisima **changu** kimekauka. | 2. Visima **vyetu** vimekauka. |
| 3. Ghala **langu** limejaa. | 3. Maghala **yetu** yamejaa. |

**Kusoma hadithi**

**Chura na Chui**



Chura na Chui walikuwa marafiki wa dhati. Hakuna kilichowatenganisha. Walikuwa na umri wa miaka saba. Walifanya kazi pamoja. Walichota maji kwenye kisima pamoja. Walilima na kuvuna pamoja. Walihifadhi mavuno yao kwenye ghala la ghorofa pamoja. Waliuza nafaka sokoni pamoja. Walikula na kunywa pamoja. Walinunuliana zawadi za thamani na kuishi raha mstarehe.

Mali ya Serikali ya Kenya 138

Kipindi cha 138 na 139 **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 139**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**f** **g** **m**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

ki li cho wa tenganisha → **kilichowatenganisha** wa li chota → **walichota**

wa li lima → **walilima** wa li nunuliana → **walinunuliana**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Siku ya kwanza shuleni**



139 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** gh

**U:** Endelea na herufi b, ch na k.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 138.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /gh/ /e/ silabi ni ghe

**U:** Endela na silabi chi, ka

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa 138.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** gho ro fa - ghorofa

**U:** Endelea na walilima, ghala

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 138.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **marafiki, umri, miaka.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Chui na chura walikuwa na umri wa miaka ngapi? *(Saba)*

**T:** Chui na chura walihifadhi nafaka yao wapi? *(Ghala)*

**U:** Wewe hufanya nini na rafiki zako? *(Kucheza, kusoma hadithi.)*

## Sarufi

**Matumizi ya –angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani. Kwa mfano: Mpira **wangu** - Mipira **yetu.**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 138.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi anakili sentensi hizi kwa hati nadhifu. Baadaye awasomee wazazi/walezi nyumbani.

1. Chui alikuwa na umri wa miaka saba.
2. Walihifadhi mavuno yao kwenye ghala la ghorofa.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 139: Mimi na wenzangu 3

**Kipindi cha 138 na 139** | **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 138**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Gh** **b** **ch** **k**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

gh e → **ghe**, ch i → **chi**, k a → **ka**, b o → **bo**

● Soma silabi na maneno.

gho ro fa → **ghorofa**, wa li li ma → **walilima**, gha la → **ghala**, wa li cho ta → **walichota**

◆ **Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mavuno **yangu** ni mengi. | 1. Mavuno **yetu** ni mengi. |
| 2. Kisima **changu** kimekauka. | 2. Visima **vyetu** vimekauka. |
| 3. Ghala **langu** limejaa. | 3. Maghala **yetu** yamejaa. |

**Kusoma hadithi**

**Chura na Chui**



Chura na Chui walikuwa marafiki wa dhati. Hakuna kilichowatenganisha. Walikuwa na umri wa miaka saba. Walifanya kazi pamoja. Walichota maji kwenye kisima pamoja. Walilima na kuvuna pamoja. Walihifadhi mavuno yao kwenye ghala la ghorofa pamoja. Waliuza nafaka sokoni pamoja. Walikula na kunywa pamoja. Walinunuliana zawadi za thamani na kuishi raha mstarehe.

Mali ya Serikali ya Kenya

138

**Kipindi cha 138 na 139** | **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 139**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**f** **g** **m**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

ki li cho wa tenganisha → **kilichowatenganisha**, wa li chota → **walichota**

wa li lima → **walilima**, wa li nunuliana → **walinunuliana**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Siku ya kwanza shuleni**



139

Hakiuzwi

## ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** f

**U:** Endelea na herufi g na m.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 139**.

## Kusoma maneno marefu

Soma sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo kwa upesi.

**N/T/U:** ki li cho wa tenganisha – kilichowatenganisha

**U:** Endelea na maneno: walichota, walilima. Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 139**.

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 138**.

## Hadithi ya mwalimu

**Siku ya kwanza shuleni**

Jina langu ni Shira, wiki iliyopita nilienda shuleni. Ilikuwa mara yangu ya kwanza kuingia shuleni. Nilikuwa nimefikisha umri wa kwenda shuleni. Nilikutana na wanafunzi wengi. Walikuwa wasichana na wavulana. Sikujua kuzungumzia lugha ya Kiswahili. Nilifahamu tu lugha ya mama. Nilikutana na rafiki yangu Mika. Yeye pia alikuwa amefika shuleni kwa mara ya kwanza. Kengele ilipolia tuliingia darasani. Mwalimu alifika na kutusalimia "Hamjambo watoto?" Wengi wetu hatukujibu, kwa sababu hatukujua Kiswahili. Alituambia tuwe tukitumia Kiswahili. Alitufunza umuhimu wa Kiswahili. Alituambia kuwa atatufundisha jinsi ya kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Alituambia kuwa Kiswahili ni lugha ambayo ingetusaidia kuelewana. Alisema kuwa akituuliza "Hamjambo?" tunajibu "Hatujambo mwalimu." Mwalimu alitusalimia tena na tukamjibu. Akatuahidi kuendelea kutufunza zaidi jinsi ya kuwasiliana katika kipindi kingine cha Kiswahili.

Funza maana ya maneno haya: **shuleni, hamjambo.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## ? Maswali

**N:** Jina la rafiki aliyekutana na shira shuleni ni nani? *(Mika)*

**T:** Kengele ilipolia wanafunzi waliingia wapi? *(Darasani)*

**U:** Siku yako ya kwanza shuleni ulifanya nini? *(Wanafunzi wataje)*

## Zoezi

Soma maneno haya mara mbili huku mwanafunzi akiyaandika katika daftari lake.

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ghorofa | 2. Dhati | 3. Marafiki |
| 4. Umri | 5. Walihifadhi | 6. Thamani |

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi ukitumia maneno haya:

1. chui 2. chura 3. kisima 4. zawadi 5. sokoni

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 140: Mimi na wenzangu 3

Kipindi cha 140 **Mimi na wenzangu 3**

**Kipindi 140**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**Ww** **Yy** **Vv**

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ra fi ki – rafiki**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ja | ya | to | fi | ra |
| ki | mi | ka | we | a |

**Sarufi: Matumizi ya '-angu', '-etu'**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mbwa **wangu** anabweka. | 1. Mbwa **wetu** wanabweka. |
| 2. Paka **wangu** anakunywa maziwa. | 2. Paka **wetu** wanakunywa maziwa. |
| 3. Mbuzi **wangu** amenunuliwa. | 3. Mbuzi **wetu** wamenunuliwa. |
| 4. Sungura **wangu** anapenda karoti. | 4. Sungura **wetu** wanapenda karoti. |
| 5. Punda **wangu** hunibebea mzigo kila siku. | 5. Punda **wetu** hutubebea mizigo kila siku. |

**Zoezi: Kuandika**

Andika sentensi nne kuhusu hadithi uliyoisoma leo.

Mali ya Serikali ya Kenya 140

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** W

**U:** Endelea na herufi w, Y, y, V na v.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 140**.

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U**: Soma silabi. Tumia silabi 'ra', 'fi' na 'ki' kuandika neno 'rafiki'. Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Wanafunzi waunde maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 140**.

## Sarufi

**Matumizi ya -angu na -etu**

**-angu** na **-etu** hutumiwa kuonyesha kitu ni cha nani.

Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 140.**

## Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **msichana**, **thamani**.

Hakikisha mwanafunzi anaandika kwa hati nadhifu anapofanya mazoezi ya kuandika.

## Kuandika

**T:** Rejelea mambo muhimu katika hadithi uliyoisoma leo.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 140**.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike majina matano ya marafiki wake.

## Kazi ya nyongeza

Wanafunzi wajizatiti kuwatumbua wenzao shuleni na kijijini.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Kipindi cha 141 na 142 **Tarakimu 3**

**Kipindi 141**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**t** **s** **th** **ny**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

t i — **ti**
s e — **se**
th u — **thu**
ny o — **nyo**

● Soma silabi na maneno.

si ku — **siku**
sa ba — **saba**
sa ba bu — **sababu**
so ma — **soma**

◆ **Sarufi: Idadi**

Soma vifungu hivi.

1. Mtoto **mmoja**
2. Ndege **mmoja**
3. Kitabu **kimoja**
4. Watoto **wawili**
5. Ndege **kumi**
6. Vitabu **vitatu**

**Kusoma hadithi**

**Lokeno**



Lokeno huamka asubuhi na mapema. Yeye hujitayarisha kwenda shuleni. Saa moja inapofika, yeye hupata kiamshakinywa, kisha hukimbia kwenda shuleni. Saa mbili Lokeno na wenzake hupanga foleni kwenda paredi. Saa tatu Lokeno husoma somo la hesabu. Wao huhesabu moja hadi kumi. Saa nne Lokeno hucheza na marafiki zake. Saa saba Lokeno hurudi nyumbani. Yeye huwasaidia wazazi wake kufanya kazi za nyumbani.

141 Hakiuzwi

Kipindi cha 141 na 142 **Tarakimu 3**

**Kipindi 142**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**t T** **s S**


■ Soma sehemu za neno na neno lote.

hu ji tayarisha — **hujitayarisha**
hu kimbia — **hukimbia**
hu hesabu — **huhesabu**
hu rudi — **hurudi**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vifaranga wa ajabu**



Mali ya Serikali ya Kenya 142

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** t

**U:** Endelea na herufi s, th na ny.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 141.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /t/ /i/ ti

**U:** Endelea na se, thu

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 141.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** si ku - siku

**U:** Endelea na maneno saba, sababu

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 141.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **moja, mbili, nne.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Lokeno hufanya nini saa moja inapofika? *(Hupata kiamsha kinywa)*

**T:** Taja vitu ambavyo Lokeno hufanya kila siku. *(Kupata kiamsha kinywa, kuenda paredi, kusoma hesabu, kuenda nyumbani)*

**U:** Je, wewe hutoka shuleni saa ngapi? *(Saa sita )*

### Sarufi

**Umoja na wingi**

Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: **Mtoto** - **Watoto.**

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 141.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aambatanishe nambari na maneno kwa kuonyesha nambari husika.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ____________

# Kipindi cha 142: Tarakimu 3

Kipindi cha 141 na 142 **Tarakimu 3**

**Kipindi 141**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**t** **s** **th** **ny**

- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| t i | s e | th u | ny o |
| **ti** | **se** | **thu** | **nyo** |

- Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| si ku | sa ba | sa ba bu | so ma |
| **siku** | **saba** | **sababu** | **soma** |

**Sarufi: Idadi**

Soma vifungu hivi.

1. Mtoto **mmoja**
2. Ndege **mmoja**
3. Kitabu **kimoja**
4. Watoto **wawili**
5. Ndege **kumi**
6. Vitabu **vitatu**

**Kusoma hadithi**

**Lokeno**



Lokeno huamka asubuhi na mapema. Yeye hujitayarisha kwenda shuleni. Saa moja inapofika, yeye hupata kiamshakinywa, kisha hukimbia kwenda shuleni. Saa mbili Lokeno na wenzake hupanga foleni kwenda paredi. Saa tatu Lokeno husoma somo la hesabu. Wao huhesabu moja hadi kumi. Saa nne Lokeno hucheza na marafiki zake. Saa saba Lokeno hurudi nyumbani. Yeye huwasaidia wazazi wake kufanya kazi za nyumbani.

141 Hakiuzwi

Kipindi cha 141 na 142 **Tarakimu 3**

**Kipindi 142**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.

**t T** **s S**


- Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu ji tayarisha | hu kimbia |
| **hujitayarisha** | **hukimbia** |
| hu hesabu | hu rudi |
| **huhesabu** | **hurudi** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Vifaranga wa ajabu**



Mali ya Serikali ya Kenya 142

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** T
**U:** Endelea na herufi t, S, s
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 142.**

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.
**N/T:** hu ji tayarisha- hujitayarisha
**U:** Endelea na maneno hukimbia, hurudi, huhesabu.
Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 142.**

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 141.**

### Hadithi ya mwalimu

**Vifaranga wa ajabu**

Ushindi alinunuliwa kuku na jogoo. Kila siku aliwalisha mahindi na chakula. Baada ya miezi miwili, kuku alianza kutaga mayai. Ushindi alifurahia. Kuku aliyaatamia au kuyalalia mayai.
Kila siku alishinda akiangalia ikiwa kuku wake ameangua vifaranga. Baada ya wiki tatu kuku wake aliangua vifaranga saba. "Huzuni iliyoje! Nia yangu ilikuwa vifaranga kumi," Ushindi akamwambia baba yake. "Usijali mwanangu, hali hii ni ya kawaida," Baba alimwambia. Vifaranga walikua wakawa wakubwa. Kuku wake alitaga mayai mengine tena. Alipata mayai manane baada ya siku nane. Alifurahi sana na kumshukuru baba kwa zawadi ya faida.

Funza maana ya maneno haya: **kutaga**, **vifaranga**, **ameangua**. Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Baada ya miezi miwili kuku alifanya nini? *(Alitaga mayai)*

**T:** Ushindi alitarajia kuku wake aangue vifaranga wangapi? *(Kumi)*

**U:** Baba alimwambia nini ushindi? *(Kuwa asijali hio ni kawaida)*

### Zoezi

Katika vikundi wanafunzi wapange kadi za majina ya nambari moja hadi kumi kwa utaratibu.

### Kazi ya ziada

Jaza mapengo.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. Mwanafunzi | __________ (Wanafunzi) |
| 2. ___________ | Watoto (Mtoto) |
| 3. Msichana | ___________ (Wasichana) |

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 143: Tarakimu 3

Kipindi cha 143 na 144 | Tarakimu 3

**Kipindi 143**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng** **v** **w**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ng e | ng i | ng o | ng u | v e | w a |
|---|---|---|---|---|---|
| **nge** | **ngi** | **ngo** | **ngu** | **ve** | **wa** |

● Soma silabi na maneno.

| u nga | nga o | ngo ma | ngi ri |
|---|---|---|---|
| **unga** | **ngao** | **ngoma** | **ngiri** |

◆ **Sarufi: Idadi**

Andika vifungu vifuatavyo kwenye daftari lako.

1. Mti **mmoja**
2. Ndege **mmoja**
3. Kiti **kimoja**
4. Miti **miwili**
5. Ndege **kumi**
6. Viti **vitatu**

**Kusoma hadithi**

**Wimbo wa kuhesabu**



Moja mbili tatu, nne tano sita, saba nane tisa, habari ya shuleni. Kuna mtoto mmoja aliyepotea na tukimpata tumrudishe shule.

Rafiki yangu njoo, twende shuleni leo.

Moja mbili tatu, nne tano sita, saba nane tisa, habari ya shuleni.

Watoto wawili waliopotea na tukiwapata tuwarudishe shule. Marafiki zangu njooni, twende shuleni leo.

143 Hakiuzwi

Kipindi cha 143 na 144 | Tarakimu 3

**Kipindi 144**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**f** **g** **m**

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li ye potea | tu ki m pata | tu m rudishe |
|---|---|---|
| **aliyepotea** | **tukimpata** | **tumrudishe** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Wasafiri sita**



Mali ya Serikali ya Kenya 144

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ng

**U:** Endelea na herufi v na w.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 143.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /ng/ /e/ silabi ni nge

**U:** Endelea na silabi ngu, ngo, ve, ngi

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 143.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** u nga - unga

**U:** Endelea na maneno ngao, ngoma.

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 143.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **tisa, nane.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri

## Maswali

**N:** Ni namba gani huja baada ya sita? *(Saba)*

**T:** Wakimpata mtoto watamfanya nini? *(Watamrudisha shule)*

**U:** Umuhimu wa kwenda shule ni nini? *(Kuelimika, kujua kuhesabu)*

## Sarufi

**Umoja na wingi**

Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: **Mtu - Watu.**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 143.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike sentensi zifuatazo kwenye daftari yake kisha amsomee mzazi au mlezi wake.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Mtoto mmoja | Watoto wawili |
| 2. | Ndege mmoja | Ndege kumi |
| 3. | Kitabu moja | Vitabu tatu |
| 4. | Mwanafuzi mmoja | Wanafunzi tisa |
| 5. | Ubao mmoja | Mbao mbili |

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: _____________

# Kipindi cha 144: Tarakimu 3

Kipindi cha 143 na 144 — **Tarakimu 3**

**Kipindi 143**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng** **v** **w**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| ng e | ng i | ng o | ng u | v e | w a |
|---|---|---|---|---|---|
| **nge** | **ngi** | **ngo** | **ngu** | **ve** | **wa** |

Soma silabi na maneno.

| u nga | nga o | ngo ma | ngi ri |
|---|---|---|---|
| **unga** | **ngao** | **ngoma** | **ngiri** |

**Sarufi: Idadi**

Andika vifungu vifuatavyo kwenye daftari lako.

1. Mti **mmoja**
2. Ndege **mmoja**
3. Kiti **kimoja**
4. Miti **miwili**
5. Ndege **kumi**
6. Viti **vitatu**

**Kusoma hadithi**

**Wimbo wa kuhesabu**



Moja mbili tatu, nne tano sita, saba nane tisa, habari ya shuleni. Kuna mtoto mmoja aliyepotea na tukimpata tumrudishe shule.

Rafiki yangu njoo, twende shuleni leo.

Moja mbili tatu, nne tano sita, saba nane tisa, habari ya shuleni.

Watoto wawili waliopotea na tukiwapata tuwarudishe shule. Marafiki zangu njooni, twende shuleni leo.

143

Hakiuzwi

Kipindi cha 143 na 144 — **Tarakimu 3**

**Kipindi 144**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**f** **g** **m**

Soma sehemu za neno na neno lote.

| a li ye potea | tu ki m pata | tu m rudishe |
|---|---|---|
| **aliyepotea** | **tukimpata** | **tumrudishe** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Wasafiri sita**



Mali ya Serikali ya Kenya

144

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** f

**U:** Endelea na herufi g na m.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 144**.

## Kusoma maneno marefu

Soma sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** a li ye potea- aliyepotea

**U:** Endelea na neno tukimpata

Mwanafunzi asome maneno kwenye **ukurasa wa 144**.

## Wakati wa kusoma

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 143**.

## Hadithi ya mwalimu

**Wasafiri sita**

Wasafiri sita walisafiri kwa muda mrefu. Wakafika ukingoni mwa mto.

Mara mvulana alitokea na mashua. Walimwomba awavushe mto ng'ambo ya pili. Walipokuwa wakivuka, mawimbi makali yalitokea. Mashua ikazama. Wale wasafiri waliogelea hadi ng'ambo ya pili. "Mmoja, wawili, watatu, wanne, watano," alihesabu msafiri wa kwanza. Alisema, "Mmoja wetu ametoweka, Idadi yetu ni watu watano. Wapi mtu wa sita?"

Mvulana alisema, "Hebu kwanza niwahesabu tena kabla sijaanza kumtafuta mwenzenu aliyepotea."

Aliwahesabu, na kupata wote sita. Alisema, "Nimempata msafiri aliyepotea." Wasafiri walicheka.

Yule msafiri wa kwanza alikuwa amesahau kujihesabu!

Funza maana ya maneno haya: **ukingoni, ng'ambo, ametoweka.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## Maswali

1. Wasafiri walikuwa wangapi? *(Sita)*
2. Mvulana alitokea na nini? *(Mashua)*
3. Je, ukitaka kusafiri wewe hutumia nini? *(Kubali jibu sahihi.)*

## Zoezi

Waongoze wanafunzi watoe muhtasari wa matukio yaliyosimuliwa kwenye hadithi.

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike kwa nambari.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| moja | mbili | tatu | nne | tano |
| sita | saba | nane | tisa | kumi |

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 145: Tarakimu 3

Kipindi cha 145 **Tarakimu 3**

**Kipindi 145**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

**ng** **th** **ny**

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: ti sa - tisa**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| re | si | na | ti | he |
| nga | nya | ta | pa | sa |

**Sarufi: Umoja na wingi**

Soma sentensi zifuatazo.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Ki**azi kimepikwa. | 1. **Vi**azi vimepikwa. |
| 2. **M**toto amekula. | 2. **Wa**toto wamekula. |
| 3. **Mwa**nafunzi amefika. | 3. **Wa**nafunzi wamefika. |
| 4. **Ma**shua imebeba mtu. | 4. **Ma**shua zimebeba watu. |
| 5. **M**to umefurika. | 5. **Mi**to imefurika. |
| 6. **Sa**maki anaishi majini. | 6. **Sa**maki wanaishi majini. |
| 7. **Ku**ku ana kifaranga. | 7. **Ku**ku wana vifaranga. |
| 8. **M**toto amerudi shuleni. | 8. **Wa**toto wamerudi shuleni. |

**Zoezi: Kuandika**

Andika nambari moja hadi kumi kwa maneno.

145 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ng

**U:** Endelea na herufi th na ny.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 145.**

## Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'ti' na 'sa' kuandika neno 'tisa'. Soma neno pamoja na mwanafunzi.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 145.**

## Sarufi

**Umoja na wingi**

Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: **M**toto - **Wa**toto.

Mwanafunzi asome sentensi kwenye **ukurasa wa 145.**

## Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **jumla, idadi.**

Hakikisha mwanafunzi anaandika kwa hati nadhifu anapofanya mazoezi ya kuandika.

## Kuandika

Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika sentensi za sarufi kwenye **ukurasa wa 145.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike aya ndogo kuhusu walichokisoma darasani.

## Kazi ya nyongeza

Andika nambari moja hadi kumi.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 146: Marejeleo

Kipindi cha 146 na 147 **Marejeleo 3**

**Kipindi 146**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch f g

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

ch a → cha    f i → fi    g o → go

● Soma silabi na maneno.

cha ku la → **chakula**    fu ra ha → **furaha**    fa ra si → **farasi**    go go → **gogo**

◆ **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu** ni mtu mzuri. | 1. **Hawa** ni watu wazuri. |
| 2. **Huyu** ni mbuzi mzuri. | 2. **Hawa** ni mbuzi wazuri |
| 3. **Huyu** ni mnyama mbaya. | 3. **Hawa** ni wanyama wabaya. |

**Kusoma hadithi**

**Harusi kijijini**



Anasi alienda kijijini kuhudhuria harusi ya dada yake. Bwana harusi alivaa kanzu na kilemba cheupe. Bi. harusi alivaa nguo ndefu nyeupe.

Vyakula kama magimbi, keki, pilau na chapati vilipikwa. Matunda kama zambarau, mapera, mapapai na machenza yaliliwa. Juisi ya parachichi ilikuwa tamu. Harusi ilikuwa ya kukata na shoka. Anasi alifurahia harusi.

Mali ya Serikali ya Kenya 146

Kipindi cha 146 na 147 **Marejeleo 3**

**Kipindi 147**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

CH ch    F f    G g

▬ Soma sehemu za neno na neno lote.

a li enda → **alienda**    i li fanyika → **ilifanyika**

vi li pikwa → **vilipikwa**    a li furahia → **alifurahia**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Shule yangu**




147 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ch

**U:** Endelea na herufi f na g.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 146.**

### Kusoma silabi

Tamka kila sauti. Unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /ch/ /a/ silabi ni cha

**U:** Endelea na silabi fi, go

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa 146.**

### Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** cha ku la - chakula

**U:** Endelea na maneno furaha, farasi

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 146.**

### Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **magimbi, parachichi.**

### Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

### Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Nani alikuwa anaolewa? *(Dadake Anasi)*

**T:** Bwana harusi alivaa nini? *(Kanzu na kilemba cheupe)*

**U:** Ni chakula kipi kinapikwa wakati wa harusi kwenu? *(Nyama, pilau, chapati)*

### Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

### Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 146.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike maneno yafuatayo kisha amsomee mzazi/mlezi nyumbani.

1. machenza 2. magimbi 3. parachichi
4. zambarau 5. paipai

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 146 na 147 **Marejeleo 3**

**Kipindi 146**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  ch f g
- Tamka sauti ya herufi na usome silabi.
  ch a → **cha**; f i → **fi**; g o → **go**
- Soma silabi na maneno.
  cha ku la → **chakula**; fu ra ha → **furaha**; fa ra si → **farasi**; go go → **gogo**
- **Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **Huyu** ni mtu mzuri. | 1. **Hawa** ni watu wazuri. |
| 2. **Huyu** ni mbuzi mzuri. | 2. **Hawa** ni mbuzi wazuri |
| 3. **Huyu** ni mnyama mbaya. | 3. **Hawa** ni wanyama wabaya. |

**Kusoma hadithi**

**Harusi kijijini**



Anasi alienda kijijini kuhudhuria harusi ya dada yake. Bwana harusi alivaa kanzu na kilemba cheupe. Bi. harusi alivaa nguo ndefu nyeupe.
Vyakula kama magimbi, keki, pilau na chapati vilipikwa. Matunda kama zambarau, mapera, mapapai na machenza yaliliwa. Juisi ya parachichi ilikuwa tamu. Harusi ilikuwa ya kukata na shoka. Anasi alifurahia harusi.

Mali ya Serikali ya Kenya 146

Kipindi cha 146 na 147 **Marejeleo 3**

**Kipindi 147**

- Taja jina la herufi na utamke sauti.
  CH ch F f G g
- Soma sehemu za neno na neno lote.
  a li enda → **alienda**; i li fanyika → **ilifanyika**
  vi li pikwa → **vilipikwa**; a li furahia → **alifurahia**

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Shule yangu**




147 Hakiuzwi

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.
**N/T/U:** CH
**U:** Endelea na herufi ch, F, f, G, g.
Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 147**.

### Kusoma maneno marefu

Tamka sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.
**N/T/U:** a li enda - alienda
**U:** Endelea na maneno ilifanyika, vilipikwa, alifurahia
Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 147**.

### Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 146.**

### Hadithi ya mwalimu

**Shule yangu**
Shule yangu inaitwa Bondeni. Mimi ni mwanafunzi katika darasa la kwanza. Darasa letu lina madawati, vitabu, kalamu na vifutio. Sisi husoma Hesabu, Kiingereza, Kiswahili na masomo mengine.
Somo nilipendalo ni Kiswahili. Wiki iliyopita tulisoma kuhusu sehemu za mwili. Sehemu hizi ni macho, pua, mdomo, mikono na miguu. Mwalimu hutushauri tuwe safi. Yeye husema, "Kila mwanafunzi akate kucha zilizo ndefu, achane nywele, aoge na kufua nguo."
Jana mwalimu alitufunza kuhusu umuhimu wa vyakula vya kiasili kwa afya yetu. Vyakula hivi ni kama mihogo, viazi, mahindi na maharagwe. Kila siku tunapokuwa shuleni tunazungumza Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa. Ninaipenda lugha yangu ya taifa.

Funza maana ya maneno haya: **kalamu, vitabu, vifutio.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

### Maswali

**N:** Taja vitu vinavyopatikana katika darasa? *(Madawati, kalamu, vitabu)*

**T:** Yeye anapenda somo gani? *(Kiswahili)*

**U:** Taja vitu vinavyopatikana katika darasa lako. *(Kubali jibu lolote sahihi)*

### Zoezi

Mwanafunzi aandike wingi wa sentensi zifuatazo.
1. Ngo'mbe aliyenona. (Ng'ombe walionona)
2. Nguruwe aliyenona. (Nguruwe walionona)
3. Kuku aliyekonda. (Kuku waliokonda)

### Kazi ya ziada

Mwafunzi atunge sentensi akitumia **huyu** na **hawa**.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Kipindi cha 148 na 149 **Marejeleo 3**

**Kipindi 148**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

l v i

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| l o | v u | l a | v i |
|---|---|---|---|
| **lo** | **vu** | **la** | **vi** |

● Soma silabi na maneno.

| lo ri | pi la u | vu a | m vu a |
|---|---|---|---|
| **lori** | **pilau** | **vua** | **mvua** |

◆ **Sarufi: Andika kwa wingi**

1. Ninaimba 2. Ninachora 3. Ninaruka

**Kusoma hadithi**

**Familia ya Lochita**



Lochita aliishi na wazazi wake Batei. Wazazi hao walimpenda sana. Wakati wa likizo, Lochita aliwatembelea shangazi na mjomba. Aliwanunulia binamu zake kalamu na vifutio. Shangazi alimwambia Lochita abaki ili watembelee mbuga ya wanyama. Mbugani waliona wanyama wengi. Waliona simba, ndovu na chui. Lochita alipiga picha ili awaonyeshe wazazi wake.

Mali ya Serikali ya Kenya 148

Kipindi cha 148 na 149 **Marejeleo 3**

**Kipindi 149**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

L V I

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li m penda | a li wa nunulia |
|---|---|
| **walimpenda** | **aliwanunulia** |
| wa tembelee | a wa onyeshe |
| **watembelee** | **awaonyeshe** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Aisha, Shiko na Shumila wazawadiwa**



149 Hakiuzwi

## Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** l

**U:** Endelea na herufi v na i.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 148.**

## Kusoma silabi

Tamka kila sauti kisha unganisha sauti na usome silabi.

**N/T/U:** /l/ /o/ lo

**U:** Endelea na vu, la

Mwanafunzi asome silabi kwenye **ukurasa wa 148.**

## Kusoma maneno kutumia silabi

Soma kila silabi katika neno. Soma silabi zote kwa pamoja kulisoma neno.

**N/T/U:** lo ri - lori

**U:** Endelea na pilau, vuma

Wanafunzi wasomeane maneno waliyojifunza vitabuni mwao kwenye **ukurasa wa 148.**

## Msamiati

Funza maana ya maneno haya: **shangazi, binamu, mjomba.**

## Kabla ya kusoma

**N/T/U:** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri.

## Hadithi ya mwanafunzi

**N/T/U:** Soma hadithi. Hakiki utabiri.

## Maswali

**N:** Lochita na wazazi wake waliishi wapi? *(Batei)*

**T:** Wakati wa likizo Lochita aliwatembelea akina nani? *(Shangazi na mjomba)*

**U:** Je, unafanya nini wakati wa likizo? *(Kutembelea nyanya na babu, kusafiri)*

## Sarufi

**Umoja na wingi**

Eleza **umoja** na **wingi** wa majina. Sisitiza sehemu za neno zinazobadilika. Kwa mfano: **Kisu - Visu.**

## Zoezi

Mwanafunzi afanye zoezi kwenye **ukurasa wa 148.**

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno yafuatayo.

1. shangazi 2. mjomba 3. binamu

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 149: Marejeleo

Kipindi cha 148 na 149 **Marejeleo 3**

**Kipindi 148**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**l** **v** **i**

● Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| l o | v u | l a | v i |
|---|---|---|---|
| **lo** | **vu** | **la** | **vi** |

● Soma silabi na maneno.

| lo ri | pi la u | vu a | m vu a |
|---|---|---|---|
| **lori** | **pilau** | **vua** | **mvua** |

◆ **Sarufi: Andika kwa wingi**

1. Ninaimba 2. Ninachora 3. Ninaruka

**Kusoma hadithi**

**Familia ya Lochita**



Lochita aliishi na wazazi wake Batei. Wazazi hao walimpenda sana. Wakati wa likizo, Lochita aliwatembelea shangazi na mjomba. Aliwanunulia binamu zake kalamu na vifutio. Shangazi alimwambia Lochita abaki ili watembelee mbuga ya wanyama. Mbugani waliona wanyama wengi. Waliona simba, ndovu na chui. Lochita alipiga picha ili awaonyeshe wazazi wake.

Mali ya Serikali ya Kenya 148

Kipindi cha 148 na 149 **Marejeleo 3**

**Kipindi 149**

■ Taja jina la herufi na utamke sauti.

**L** **V** **I**

■ Soma sehemu za neno na neno lote.

| wa li m penda | a li wa nunulia |
|---|---|
| **walimpenda** | **aliwanunulia** |
| wa tembelee | a wa onyeshe |
| **watembelee** | **awaonyeshe** |

**Hadithi ya mwalimu**

Tazama picha. Sikiliza hadithi.

**Aisha, Shiko na Shumila wazawadiwa**



149 Hakiuzwi

## ▲ Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** L

**U:** Endelea na herufi V na I.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 149**.

## Kusoma maneno marefu

Soma sehemu za neno kisha uunganishe sehemu hizo usome neno kwa upesi.

**N/T/U:** wa li m penda- walimpenda

**U:** Endelea na maneno aliwanunuli, awatembelee, awaonyeshe

Soma maneno kwenye **ukurasa wa 149**.

## Hadithi ya mwanafunzi

**U:** Somea mwenzako hadithi kwenye **ukurasa wa 148**.

## Hadithi ya mwalimu

**Aisha, Shiko na Shumila wazawadiwa**

Ilikuwa Alhamisi, siku moja kabla ya siku ya michezo ya kuigiza. Shuleni Imara, wanafunzi waliambiwa waje mapema kufanya usafi. Aisha alifika asubuhi na mapema. Alisimama dirishani na kutazama Shumila akikariri shairi. Mara Shiko alitokea. Walishikana mikono kwa furaha. Shiko alisema, "Hujambo Aisha?" Aisha alijibu, "Sijambo. U hali gani Shiko?" "Njema," Shiko akajibu. Shumila alisikia kelele, akashtuka. Mara aliwaona Shiko na Aisha. Wote walisema, "Samahani Shumila, hatukukusudia kupiga kelele." Shumila na wasichana hawa wawili walipanga madawati na kufagia karibu na mkorosho. Baadaye waliungana na Shumila darasani kukariri shairi. Siku ya michezo ya kuigiza ilipofika, walishinda na kupewa nishani na shada la maua.

Funza maana ya maneno haya: **dirishani, madawati.** Soma kichwa cha hadithi. Jadili picha. Mwanafunzi atoe utabiri. Soma hadithi mwanafunzi asikize huku akitazama picha. Hakiki utabiri.

## ? Maswali

**N:** Kwa nini wanafunzi waliambiwa wakuje shuleni mapema? *(Kufanya usafi)*

**T:** Aisha alimtazama shumila akifanya nini? *(Akikariri shairi)*

**U:** Shiko, Aisha na shumila walifanya usafi gani? *(Walipanga madawati na kufagia karibu na mkorosho)*

## Zoezi

Mwanafunzi aandike wingi wa maneno yafuatayo.

1. kikombe 2. kitabu 3. kikapu
4. kifyekeo 5. kijiko

**Majibu**

1. vikombe 2. vitabu 3. vikapu 4. vifyekeo 5. vijiko

## Kazi ya ziada

Mwanafunzi ajaze mapengo akitumia huyu au hawa.

1. Wadudu __________ni wengi.
2. Nguruwe __________ni mnono.
3. Mtoto __________ ni mtiifu.

Tarehe: ______________________ Muda: ________________ Idadi: ______________

# Kipindi cha 150: Marejeleo

Kipindi cha 150 **Marejeleo 3**

**Kipindi 150**

Taja jina la herufi na utamke sauti.

ch f g l v i

Jedwali la silabi

Tumia silabi zilizo kwenye jedwali kuunda maneno.

**Kwa mfano: bi na mu - binamu**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| chi | na | ra | ti | ka |
| bi | pa | cha | mu | vu |

**Sarufi: Matumizi ya 'huyu', 'hawa'**

Jaza mapengo ukitumia **'huyu'**, **'hawa'**.

1. Nguruwe __________ ni mnono.
2. Mtoto __________ ni mtiifu.
3. Wanafunzi __________ wamechelewa.
4. Simba ________ ni mkali.
5. _______ni mgeni.
6. _______ni wazazi wake.
7. Wasichana _______ walipewa zawadi.
8. _______ walitembelea mbuga ya wanyama.

**Zoezi: Kuandika**

Tunga sentensi ukitumia vifungu hivi.

1. Kunawa mikono
2. Kunawa miguu
3. Kufuta kamasi

Mali ya Serikali ya Kenya 150

### Ufahamu wa herufi

Taja jina la herufi na utamke sauti yake.

**N/T/U:** ch

**U:** Endelea na herufi f, g, v, l na i.

Mwanafunzi ataje majina ya herufi na atamke sauti zake kwenye **ukurasa wa 150**.

### Jedwali la silabi

Chora jedwali la silabi.

**N/T/U:** Soma silabi. Tumia silabi 'bi', 'na' na 'mu' kuandika neno 'binamu'. Soma neno pamoja na wanafunzi.

**U:** Mwanafunzi aunde maneno halisi kwa kutumia jedwali la silabi kwenye **ukurasa wa 150**.

### Sarufi

**Matumizi ya huyu na hawa**

**Huyu** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria mtu mmoja. **Hawa** hutumiwa tunapozungumzia na kuashiria watu wengi.

Mwanafunzi afanye zoezi la sarufi kwenye **ukurasa wa 150.**

### Kuandika maneno

**U:** Soma maneno haya mara mbili huku mwanafunzi akiyaandika kwenye daftari lake: **binamu, mjomba**

Hakikisha anaandika kwa hati nadhifu anapofanya zoezi.

### Kuandika

**T:** Rejelea mambo muhimu kuhusu usafi wa mwili.

**U:** Mwanafunzi afanye zoezi la kuandika kwenye **ukurasa wa 150.**

### Kazi ya ziada

Mwanafunzi aandike aya fupi kuhusu kile alichosoma katika hadithi.

### Kazi ya nyongeza

Mwanafunzi atunge sentensi akitumia maneno haya:

1. kunawa mikono
2. kunawa miguu
3. kufuta kamasi
4. mihogo

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

JAMHURI YA KENYA
Mali ya
Serikali ya Kenya
HAKIUZWI

# Kiswahili 1

## Mazoezi ya Lugha

### Mwongozo wa Mwalimu

Mwongozo huu wa mwalimu wa gredi ya 1 umetayarishwa kwa kurejelea pakubwa mbinu za utafiti ili kumsaidia mwalimu anapofundisha kuwasaidia wanafunzi kukuza ujuzi wao katika lugha ya Kiswahili. **Mwongozo huu umeshughulikia uhusiano na maadili, uhusiano na masuala mutambuko, sehemu nne za ujifunzaji lugha – kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika, vilevile mada zote na maadili yaliyojadiliwa katika mtaala.** Mwongozo huu unamwezesha mwalimu kuwapa wanafunzi wa gredi ya 1 mbinu tofauti za kusoma, kujifundisha na kujitathmini na hivyo basi kuakifia malengo lengwa kwa kurejelea sehemu husika za kipindi/somo.

Mwongozo huu unarejelea yaliyojiri wakati wa muda wa majaribio ya Tusome. Tusome imedhaminiwa na USAID na kutekelezwa na Wizara ya Elimu. Malengo ya kitabu hiki ni kuwa wanafunzi watakaokamilisha vipindi na masomo kwenye vitabu vya wanafunzi watakuwa wamejikimu na ujuzi wa kuweza kusoma katika gredi ya 1. Pia, wanafunzi wataweza kusoma kwa ufasaha na kuelewa wanachokisoma na kuandika. Hivyo, wanafunzi wakimaliza masomo ya gredi ya 1 watakuwa na uwezo wa kusoma na kujifunza kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya ujifunzaji katika gredi za juu.

Vipengele muhimu vilivyopewa kipao mbele kwenye mwongozo huu wa gredi ya 1 ni:

- Shughuli za ufundishaji ambazo ni za kufurahisha wakati wa kufundisha mada zilizomo kwenye mtaala KICD.
- Mpangilio maalum wa shughuli za ufundishaji zilizopangwa kwa mtiririko na msambao ufaao kwa kurejelea utafiti uliofanywa katika kufunza na kujifunza Kiswahili.
- Nakala za kitabu cha mwanafunzi kenye mwongozo huu ili kumwenzesha mwalimu kufanya marejeleo ya moja kwa moja na kwa urahisi anapofundisha.
- Hadithi tamu zinazolandana na tamaduni na umri wa mwanafunzi zitakazo msaaidia pakubwa katika kukuza ujuzi wake wa kusoma.
- Maelekezo yaliyopangwa vizuri kumwongoza mwalimu katika kuutumia mwongozo kwa urahisi.
- Hadithi zilizoandikwa za kiwango cha mwanafunzi na rahisi kusoma ambazo zitamwenzesha mwanafunzi kusoma na kuelewa hadithi husika.
- Hadithi za mwalimu ambazo zinalenga kukuza msamiati na ujuzi wa kusikiliza wa mwanafunzi.

Mwongozo huu umetayarishwa na wataalamu wenye tajriba kubwa kutoka Wizara ya Elimu, Tume ya Huduma ya Walimu, Taasisi ya Masomo Maalumu ya Kenya, na Taasisi ya usimamizi wa Elimu nchini Kenya.

USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa U.S. Agency for International Development (USAID) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.

ISBN 978-9966-110-09-1

© 2018